

BUNGE LA TANZANIA

MAJADILIANO YA BUNGE

MKUTANO WA KUMI NA MOJA

Kikao cha Kumi na Tatu – Tarehe 19 Aprili, 2018

(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)

D U A

Spika (Mhe. Job Y. Ndugai) Alisoma Dua

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge tukae. Tunaendelea Waheshimiwa Wabunge na Mkutano wa Kumi na Moja, Kikao cha leo ni cha Kumi na Tatu. Katibu.

NDG. STEPHEN KAGAIGAI – KATIBU WA BUNGE:

HATI ZA KUWASILISHA MEZANI

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:-

Hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto kwa mwaka wa fedha 2018/2019.

MHE. PETER J. SERUKAMBA - MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA HUDUMA NA MAENDELEO YA JAMII:-

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii kuhusu Utekelezaji wa Bajeti na Majukumu ya Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto kwa mwaka wa fedha 2017/2018 pamoja

na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2018/2019.

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Peter Serukamba, maoni ya Kambi ya Upinzani siyaoni, Katibu tunaendelea.

NDG. STEPHEN KAGAIGAI – KATIBU WA BUNGE:

MASWALI KWA WAZIRI MKUU

SPIKA: Maswali kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu, Mheshimiwa Waziri Mkuu karibu tafadhali. *(Makofi)*

Swali la kwanza litaulizwa na Mheshimiwa Hussein Nassor Amar (CCM), Mbunge wa Jimbo la Nyang'hwale.

MHE. HUSSEIN N. AMAR: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi hii adimu ya kuweza kumuuliza swali Mheshimiwa Naibu Waziri.

MBUNGE FULANI: Waziri Mkuu.

SPIKA: Inabidi uombe radhi bwana. *(Kicheko)*

MHE. HUSSEIN N. AMAR: Naomba radhi, ni Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa tumepata bahati kubwa kutoka kwa Mwenyezi Mungu, mvua nyingi zimenyesha nchini kwetu na miundombinu takribani asilimia zaidi ya 75 imeharibika. Je, Serikali imejipanga vipi kuweza kuirejesha miundombinu hii katika hali yake?

SPIKA: Ahsante sana kwa swali hilo. Mheshimiwa Waziri Mkuu, majibu tafadhali.

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Hussein Amar, Mbunge wa Nyang'hwale, kama ifuatavyo:-

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba katika kipindi hiki tumeendelea kupata mvua nyingi sana karibu nchi yote na mvua hizi zimeleta maafa makubwa pamoja na kwamba kwa upande wa kilimo tunapata faida. Nianze kwa kutoa pole kwa Watanzania wenzetu wote waliopata maafa, wako wenzetu wametangulia mbele za haki kutokana na mvua hizi kuwa nyingi na wako watu wameathirika kwa kuharibika kwa miundombinu yao. Wale wote ambao wametangulia mbele ya haki tuendeleo kuwaombea, Mwenyezi Mungu aweze kuweka roho zao mahali pema lakini tuwape pole wale wote ambao wamepata athari ya kuharibika kwa miundombinu hii.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Mbunge anataka kujua ni namna gani Serikali imejipanga kurejesha miundombinu iliyoharibika. Kwa kuwa mvua hizi zinaendelea na kila mkoa tunazo Kamati za Maafa na miundombinu hiyo iliyoharibika sehemu kubwa ni barabara na miundombinu mingine ambayo ni ya Serikali na ya watu binafsi. Kamati ya Maafa itafanya tathmini ya kujua ni miundombinu ipi imeharibika kwa kiasi gani na ile ambayo ipo upande wa Serikali kama kutakuwa kuna barabara, shule na maeneo mengine taratibu za kawaida za matengenezo zitafanywa. Yale maeneo ya watu binafsi, Kamati zile za Maafa kadiri zitakavyoweza kutathmini zinaweza kufanya maamuzi ya namna ya kusaidia kurudisha miundombinu hiyo, lakini Kamati zile za Maafa ndiyo zitafanya kazi mikoani na kule wilayani.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nataka nimhakikishie tu kwamba miundombinu ambayo inazungumzwa sasa kama ambavyo tumeshuhudia barabara zetu nyingi zimeharibika, kwa kuwa mkoani kuna chombo kinachoshughulika barabara kinaitwa *TANROADS* na Wilayani tuna *TARURA*, vyombo vyote hivi sasa baada ya tathmini hiyo vinaweza kufanya maamuzi ya kurejesha miundombinu hiyo. Ahsante sana. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante. Tunaendelea na Mheshimiwa Upendo Furaha Pendeza wa Viti Maalum - CHADEMA, swali.

MHE. UPENDO F. PENEZA: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipatia fursa hii kumuuliza Waziri Mkuu swali.

Mheshimiwa Spika, katika tamko la kisera la Sera ya Elimu, Serikali imesema itaondoa vikwazo vyote vinavyozuia wanafunzi kupata elimu. Moja ya sababu inayofanya watoto wa kike wanakosa fursa hii ya kupata elimu ni pamoja na wao kuwa katika kipindi cha hedhi na kukosa taulo za kujihifadhi.

Mheshimiwa Spika, tunashukuru Serikali kupitia Naibu Waziri wa TAMISEMI imesema kwamba asilimia kumi ya pesa zinazotolewa kwa ajili ya *capitation fund*, zile shilingi 10,000 ama shilingi 20,000 zitumike kwa ajili ya kuwanunulia watoto wetu *sanitary pads* ama taulo za kujihifadhi. Hata hivyo, kiasi hicho ni kidogo ukizingatia kwamba kiasi hicho kimepangwa tangu miaka kumi iliyopita kipindi dola moja ikiwa ni shilingi 1,000 na sasa dola moja ni *almost* shilingi 2,200.

Mheshimiwa Spika, kwa nini sasa Serikali ilsilete pendekezo kupitia *Finance Bill* ya kuondoa kodi ambazo zipo kwenye *sanitary pads* ili kuhakikisha kwamba bei ya taulo za kujihifadhi kipindi cha hedhi zinashuka kwa hiyo hata hiyo asilimia kumi itakayotolewa kidogo itaweza kusaidia kwa sababu pedi zitapatikana katika bei rafiki? Ahsante sana. *(Makofi)*

SPIKA: Ahsante sana, kwa hiyo swali lako *specifically* ni?

MHE. UPENDO F. PENEZA: Mheshimiwa Spika, swali langu *specifically* ni kwamba...

SPIKA: *Straight.*

MHE. UPENDO F. PENEZA: Namuuliza Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa nini sasa Serikali isilete pendekezo katika *Finance Bill* ya kuondoa kodi zote ambazo zipo kwenye taulo za kujihifadhi kipindi cha hedhi? Ahsante. *(Makofi)*

SPIKA: Ahsante. Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Waziri Mkuu.

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Spika, naomba nijibu swali la Mheshimiwa Peneza, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inao utaratibu wake katika kuondoa kodi kwenye bidhaa zote ambazo zinaleta tija pale ambapo zinatumiwa na jamii yetu huku ndani ikiwemo na jambo ambalo ametaka kupata ufafanuzi. Kwa kuwa Serikali imeanza na kutenga fedha kwa ajili ya kutoa huduma hiyo kama ambavyo ameeleza na kama ambavyo Naibu Waziri ameeleza, kama alieleza, basi sasa Naibu Waziri anaweza kuona sasa umuhimu kutokana na ombi lako kuwa Serikali sasa itoe pendekezo la kuweza kuingiza kwenye *Finance Bill* kuona namna ya kuondoa kodi ili hivi vifaa viweze kupatikana kwa bei nafuu. Kwa kuwa Wizara ya Fedha bado haijawasilisha na kwa kuwa Naibu Waziri naye amesikia, watakaa pamoja kuona umuhimu wa jambo hilo na kukushirikisha ili kuweza kuona namna nzuri ya kupunguza bei ya vifaa hivyo ili viweze kutumiwa na walengwa ambao tumewalenga zaidi. Ahsante. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante. Tunaendelea na Mheshimiwa Vedastus Mathayo Manyinyi, Mbunge wa CCM, Jimbo la Musoma Mjini.

MHE. VEDASTUS M. MANYINYI: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi na mimi kumuuliza swali Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Spika, kama tunavyofahamu ni kwamba Serikali iliamua kujitoa kwenye biashara na hivyo ikaacha sekta binafsi waweze kuendesha biashara na hii ni katika kuboresha tija. Hata hivyo, kama tunavyofahamu baadhi ya biashara zilizokuwa zinafanywa na Serikali ilikuwa ni pamoja na viwanda mbalimbali vya nguo kama *MUTEX*, *MWATEX* na Sungura.

Mheshimiwa Spika, swali langu ni kwamba katika Serikali kuachia yapo mafao ya wale watumishi ambayo

hayajalipwa hadi leo. Nikiwa *specific*, bahati nzuri Mheshimiwa Waziri Mkuu ulibahatika kuja Musoma, uliweza kuona mfano wa watumishi wa Kiwanda cha *MUTEX* toka wakati huo mpaka leo hawajalipwa hayo mafao yao. Kwa bahati nzuri uliahidi kwamba wangeweza kulipwa kwa wakati muafaka.

Sasa nini kauli ya Serikali kuhakikisha kwamba hawa watu wanaweza kulipwa mafao yao mara moja ili waweze kuendelea na maisha yao maana wametaabika kwa muda mrefu?

SPIKA: Ahsante sana. Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Waziri Mkuu tafadhali.

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mathayo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, upo ukweli kwamba Tanzania tuna viwanda vingi na vingine vilikuwa viwanda vya muda mrefu, vipo viwanda ambavyo kwa sasa havifanyi kazi kabisa. Serikali kwa dhamira ya kujenga uchumi kwenda uchumi wa kati kupitia viwanda, tumeendelea kufanya tathmini ya kutosha kwenye sekta hii.

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Wizara ya Viwanda imeunda timu ya kufanya mapitio kwenye viwanda vyote tulivyokuwa tumebinafsisha na viwanda vyote ambavyo Serikali tulikuwa tunavihudumia lakini vyote havifanyi kazi ili kwanza tuweze kuvitambua ni vingapi na tulivibinafsisha kwa ajili ya nini ili tuweze kufanya maamuzi. Maamuzi hayo ni kwamba viwanda vyote ambavyo tumebinafsisha na havifanyi kazi tunataka tuvirushe Serikalini ili tuweze kutafuta wawekezaji wenye uwezo wa kuviendesha viwanda hivi, vile ambavyo vimebinafsishwa hata hivi pia tulivyonavyo sasa.

Mheshimiwa Spika, malengo ya kuwekeza tunataka kwanza tupate mtaji, teknolojia lakini pia tuweze kutoa ajira za kutosha na wakati mwingine pia hata kuhakikisha kwamba uzalishaji wa sekta hiyo unaendelea vizuri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, swali la Mheshimiwa anataka kujua hatma ya viwanda vile vilivyokufa vilivyokuwa na watumishi na watumishi wale hawajalipwa mishahara yao. Ni kweli baada ya tathmini hiyo, tutabaini uwepo wa watumishi eneo hilo wangapi na madeni yao yakoje na baada ya kuwa tumepata mwekezaji kwa malengo niliyoyataja, sasa tunaweza tukaanza kulipa pia watumishi ambao wanadai Serikali kupitia viwanda hivyo. Viwanda ambavyo pia vimekuwa na wawekezaji ambapo wameshindwa kuviendesha vitakaporudishwa Serikalini tutatafuta njia nzuri ya kisheria ya kuweza kuwalipa watumishi hawa.

Mheshimiwa Spika, natambua nimekwenda Mkoani Mara na nilikutana na kundi la wafanyakazi wa Kiwanda cha *MUTEX* na Mheshimiwa Mbunge akiwemo na tuliwahakikishia kwamba Serikali inaendelea na utaratibu ambao nimeueleza hapa wa tathmini ili tuweze kujua ni watumishi wangapi, wanadai kiasi gani halafu tuandae utaratibu wa kuwalipa. Nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge na watumishi wote wa *MUTEX* kwamba tunaendelea na kukamilisha tathmini hiyo chini ya Wizara ya Viwanda na baada ya tathmini hiyo itatuwezesha kujua na kuweka sasa mpango wa kuwalipa watumishi hao. Ahsante sana. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante. Sasa ni zamu ya Mbunge wa Karagwe, Mheshimiwa Innocent Lugha Bashungwa, uliza swali lako.

MHE. INNOCENT L. BASHUNGWA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kipekee ili niweze kumuuliza swali Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi, tumeona Serikali ya Awamu ya Tano ikiweka jitihada kubwa sana katika kuhakikisha angalau kila wilaya inapata vituo vya afya visivyopungua viwili au zaidi lakini kwenye mafanikio hapakosi changamoto. Je, nini mkakati wa Serikali kuhakikisha vituo hivi vya tiba nchini vinapata wauguzi wa kutosha? Ahsante sana. (*Makofi*)

SPIKA: Mheshimiwa Waziri Mkuu, majibu ya swali hilo, tafadhali.

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Bashungwa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nikiri kwamba Serikali imeendelea na jitihada kubwa sana ya kuimarisha sekta ya afya na miongoni mwa mkakati mkubwa tulionao kwenye sekta ya afya ni ujenzi wa vituo vya afya kwenye ngazi ya Wilaya ili kuimairisha utoaji huduma ya afya kwenye ngazi ya vituo vya afya kupunguza msongamano mkubwa kwenye hospitali zetu za wilaya na mkoani. Kama ambavyo mmekuwa mkipata taarifa mbalimbali kutoka kwenye hotuba yangu, hotuba ya TAMISEMI lakini pia Wizara ya Afya kwamba mkakati huu umepelekea Mheshimiwa Rais kuruhusu kutumia fedha kwa ajili ya ujenzi wa vituo hivi na msimu huu tumetoa shilingi zisizopungua shilingi bilioni 160 ili kujenga au kuimarisha kwa kukarabati vituo vya afya kwenye ngazi ya Wilaya. Tumepata bahati kila Wilaya tumepata vituo siyo chini ya viwili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, fedha hizi kwenye vituo vile vya afya, moja zinafanya kazi ya au kukarabati kituo cha afya kilichopo au kujenga kituo kipya cha afya kulingana na mahitaji ya kila Wilaya. Nimeshuhudia kazi nzuri zilizofanywa kwenye eneo hili na malengo ya Serikali ya ujenzi wa vituo hivi ni kuhakikisha kwamba kwenye vituo vya afya huduma zifuatazo zinapatikana, kama ambavyo tumeeleza kwenye taarifa zetu mbalimbali. Kwanza tunajenga chumba cha kupimia magonjwa (*laboratory*) lakini tunajenga pia chumba cha upasuaji (*theatre*) na wodi ya akina mama na mtoto (*maternity ward*). Malengo yetu kwenye maeneo haya ni kwamba huduma zote za vipimo, huduma za mama na mtoto pamoja na upasuaji zipatikane kwenye ngazi ya kata ili kupunguza mzigo mkubwa kwenye Hospitali za Wilaya na Mkoa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, tunajenga pia nyumba ya mganga mkuu wa kituo cha afya, lakini pia tunajenga nyumba ya kutunzia miili ya wenzetu waliotangulia mbele za

haki na ikiwezekana sasa tujenge pia hata na wodi mbili: moja ya akina mama magonjwa mchanganyiko na nyingine ya wanaume magonjwa mchanganyiko. Jitihada hizi za Serikali zitaendelea kuhakikisha kwamba tunaimarisha huduma ya sekta ya afya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, viko vituo vya afya ambavyo Mheshimiwa Mbunge ameomba apate ufafanuzi kutoka Serikalini vilivyochakaa. Kwa kuwa fedha hizi zinapopelekwa kwenye Halmashauri ya Wilaya na Halmashauri ya wilaya hufanya maamuzi ya namna ya kuzitumia kwa ama kukarabati kituo ama kujenga kituo kipya, basi wakati mwingine fedha hizi zitumike kukarabati vituo vilivyochakaa. Kama vituo vilivyochakaa ni vingi kwa utaratibu huu huu wa Wizara ya Afya na Wizara ya TAMISEMI, wataendelea tena kuona umuhimu wa kutenga fedha. Kwa kuwa sasa tuko kwenye bajeti, muendeleo kupitisha bajeti zetu ili tufukie azma ya kutoa huduma ya kuimarisha vituo vya afya vilivyochakaa na hivi vipya ambavyo vinajengwa ili tuendeleo kutoa huduma ya afya vizuri zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. *(Makofi)*

SPIKA: Ahsante sana. Tunaendelea na Mbunge wa Babati Vijijini, Mheshimiwa Jitu Soni, uliza swali lako tafadhali.

MBUNGE FULANI: Hayupo.

SPIKA: Mheshimiwa Soni hayupo, ahsante sana. Tunaendelea na Mbunge wa Viti Maalum - CHADEMA, Mheshimiwa Aida Jospeh Khenani. Ndugu zangu wa CUF msione kimya, hakuna jina hapa hata moja. Mheshimiwa Aida, uliza swali lako.

MHE. AIDA J. KHENANI: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niweze kumuuliza swali Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Spika, Serikali ilihamasiha wananchi kulima kilimo cha kisasa na kilimo chenye tija. Wananchi

wakaitika wito huo wakalima kilimo cha kisasa na wakazalisha kwa wingi wakiwemo wakulima wa zao la mahindi. Mpaka hivi sasa ninavyozungumza hali ni mbaya kwa wakulima hawa. Nini mkakati wa Serikali kuhusu kuandaa soko la uhakika la ndani na nje ya nchi ili wakulima hawa waweze kuuza mazao yao wapate tija kwa mazao waliyozalisha? (*Makofi*)

SPIKA: Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Waziri Mkuu, tafadhali.

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Aida Joseph Khenani, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, upo ukweli kwamba wakulima wetu nchini kote wamelima mazao mengi sana yakiwemo haya ya biashara na chakula na zao la mahindi ambalo Mheshimiwa Mbunge amelisema likiwemo. Serikali imefanya jitihada za kuhakikisha kwamba tunaboresha sekta ya kilimo kwa kuhakikisha kwamba pembejeo zinapatikana ingawa nazo hazipatikani za kutosha kwa sababu kuna ongezeko la kilimo lakini Serikali imeendelea kufanya jitihada za kuhakikisha kwamba tunapata mbegu nzuri, mbolea na madawa ili kuwezesha wakulima kuweza kufanya kazi yao vizuri nao waweze kuzalisha mazao mengi zaidi. Pia tumeimarisha pia kilimo cha kitaalam ambacho sasa kinaelekea kuzalisha mahindi mengi kama Mheshimiwa Mbunge alivyosema kwa kutoa maelekezo kila halmashauri na idara za kilimo, maafisa kilimo wote waliojaa pale wilayani waondoke na waende kwenye kata kusimamia kilimo bora na kusimamia sekta zote mpaka masoko yake. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, sasa Serikali imejipanga vipi kuhakikisha kwamba mkulima akishalima mahindi anapata soko la ndani na nje ya nchi. Tumepita katika kipindi ambacho tumekuwa tukijifunza kila mwaka na tumekuwa tunafanya maamuzi mbalimbali ya namna ya kupata masoko ya mazao haya, mahindi yakiwemo. Tathmini hii ilikuwa inatulenga kwanza Taifa lenyewe ndani tuwe na chakula cha

kutosha, lakini pia tuweze kuwa na ziada ambayo mkulima atakuwa huru kuweza kuiuza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mtakumbuka mwaka jana tulizua mahindi yasiende nje lakini tupeleke unga. Ilikuwa inalenga tu kuleta thamani ya zao letu ili tunapopeleka nje tuwe tumesha-*process* kuwezesha pia hata viwanda vya ndani kupata mapato. Bado suala la masoko tumellacha wazi, kama uzalishaji utakuwa mzuri na tuna ziada tutatoa vibali vya kuruhusu kuuza nje au hata watu wa nje waje kununua ndani kwa sababu ndiyo mtaji wetu na namna ambayo tunaweza kupata mapato zaidi ili wakulima waweze kupata fedha za kutosha waweze kuendelea na kilimo chao.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, pale ambapo tunaona kutakuwa na tatizo la chakula tumezalisha nchini, hata kama tuna ziada kidogo, lakini majirani hawajalima vizuri, hiyo sasa tutalazimika kufanya maamuzi ambayo yataweza kulinda usalama wa chakula ndani ili Taifa lisikubwe na njaa kwa kuruhusu chakula chote kutoka nje. Nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, kwa namna ambavyo tumeona hali ya hewa mwaka huu na maeneo mengi tuliyopita tumeona mazao, mahindi yamelimwa sana, tuna uhakika mwaka huu tutakuwa na mazao ya kutosha na kwa hiyo tutashirikiana na wananchi kutafuta masoko ya kutosha ndani na nje ya nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, upande wa Serikali, mimi Jumamosi, keshokutwa nazindua ujenzi wa maghala ya kisasa (vihenge vya kuhifadhia mazao yetu). Sasa Serikali itakuwa na uwezo wa kukusanya chakula tunachozalisha na kuweka ile akiba ya kitaifa kwenye vihenge vile ili tuweze kuona akiba tuliyonayo inayotutosha na ile ziada sasa tunaweza kuwaruhusu wakulima kuweza kuuza nje.

Kwa hiyo, tutafungua masoko kuwawezesha wakulima kuuza ndani na nje ya nchi. Nataka nitumie nafasi hii kutoa wito kwa Watanzania kutumia vizuri mvua zinazoendelea kunyesha kwa kulima mazao zaidi ya chakula na biashara na Serikali tuko pamoja nao katika kutafuta

masoko ya ndani baada ya kuwa tumezalisha vizuri ili tuweze kupata tija ya kutosha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, namsihi Mheshimiwa Mbunge, tuendeleo kutoa ushirikiano kuwahamasisha Watanzania walime kwa sababu kwenye masoko tumejipanga vizuri kwa haya mazao ambayo yanahitaji kutafuta masoko yakiwemo mazao ya biashara kama vile pamba ambayo mwaka huu imezalishwa kwa wingi sana, kahawa, chai, korosho lakini pia na tumbaku na mazao mengine kama katani. Tumeanza kuiona katani inaleta mafanikio mazuri, tumeanza kuona mazao mengine mengi ambayo yanaleta fedha nchini, tutaendelea kufungua milango kutafuta masoko yake. Ahsante sana kwa swali lako. *(Makofi)*

SPIKA: Mheshimiwa Abdallah Mtolea, CUF swali fupi.

MHE. ABDALLAH A. MTOLEA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi asubuhi ya leo niweze kumuuliza swali Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa niaba ya Watanzania wote.

Mheshimiwa Spika, imekuwa ni kawaida sana kila zinaponyesha mvua hasa mvua kubwa katika Jiji la Dar es Salaam, haijalishi zimenyesha kwa mfululizo siku ngapi, lakini hata ikinyesha siku moja inaleta madhara makubwa sana kwa makazi ya watu kuharibika, miundombinu ya Serikali kuharibika na watu kupoteza maisha. Mvua zinazoendelea kunyesha sasa hivi tayari watu 12 wameshapoteza maisha yao.

Mheshimiwa Spika, tunaamini tatizo kubwa linalosababisha maafa hayo kuwa makubwa ni miundombinu ya kusafirisha maji ya mvua kuwa mibovu au kutokuwepo. Mimi siamini katika kampeni labda za kuwahamisha watu wanaokaa kwenye maeneo labda ni ya bondeni kwa sababu yako maeneo hata Serikali yenyewe imejenga mabondeni, lakini mimi naamini...

SPIKA: Sasa swali.

MHE. ABDALLAH A. MTOLEA: Naamini katika kutengeneza miundombinu mizuri ili maji yaondoke lakini kuwa na vitengo mahususi vya uokoaji wakati matatizo yanapotokea.

Mheshimiwa Spika, sasa nataka kujua Serikali ina mpango gani kuhakikisha kwamba madhara haya ambayo yanatokana na mvua Jijini Dar es Salaam yataadhibitiwa? *(Makofi)*

SPIKA: Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Waziri Mkuu, tafadhali.

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Spika, naomba nijibu swali la Mheshimiwa Abdallah Mtolea, Mbunge wa Temeke, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, swali hili linafanana sana na swali lililopita la kunyesha kwa mvua nyingi ingawa limetaka lizungumzie zaidi Jiji la Dar es Salaam. Kwanza hatuwezi kuzuia kunyesha kwa mvua na tutaendelea kuzipokea hizi mvua kwa sababu pia zinatuletea tija ingawa zinatuletea madhara. Nilianza kutoa pole pia kwa wote waliofikwa na maafa kutokana na mvua hizi ambazo zinaendelea kunyesha na hasa Jijini Dar es Salaam ambako mpaka jana jioni tulipata taarifa kwamba Watanzania wenzetu 12 wamepoteza maisha kwa sababu ya mafuriko. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa mkakati wa kuboresha miundombinu ya kusafirisha maji kwa maana ya kuwa na mifereji mikubwa ya kutosha kuweza kusafirisha maji, Jiji la Dar es Salaam kupitia manispaa zake, lakini Serikali kupitia Wizara zake; Ofisi ya Makamu wa Rais, Mazingira na Ofisi ya Rais kupitia TAMISEMI, hizi zote zinayo mipango ya kuboresha miundombinu kwenye miji yetu, makao makuu ya mikoa na maeneo yote ambayo yanakaliwa na watu wengi sana ikiwemo ya Dar es Salaam. Tunayo miradi sasa tunaendelea nayo ambayo inalenga kuboresha miundombinu ya mifereji

na Mheshimiwa Makamba alipokuwa anatoa hotuba yake hapa alieleza mkakati wa kulijenga upya Bonde la Msimbazi ambalo sehemu kubwa ndilo linaloleta madhara makubwa. TAMISEMI nao walipokuwa wanatoa hotuba yao hapa wameeleza mkakati kupitia Mradi wa *DMPU*, kitu kama hicho, upo mradi pale ambao unafanya kazi ya kuboresha miundombinu ya barabara lakini pia na mifereji kuhakikisha kwamba maeneo yote yanayopitiwa na maji mengi yanaimarishwa kwenye manispaa zote zilizo Mkoani Dar es Salaam. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunapopata mvua nyingi za kutosha na maji kufurika mpaka maeneo ambayo ni rasmi kwa kuishi ndiyo tunapata tatizo kubwa kwa sababu hatuwezi kuzuia mvua. Nataka niendeleo kutumia nafasi hii kuwasih Wabunge wenzangu, mara kadhaa tumeshuhudia mvua hizi zinapoleta madhara kwa wale walioko mabondeni, pamoja na Serikali kuwaambia waondoke mabondeni, tumekuwa tukiingilia sana utendaji kwa kuingiza siasa za kuwataka watu wabaki, watu wanawaonea huruma, watu wanashindwa kutoka kwenye mabonde kwa sababu ya utetezi unaotoka kwa watu wenye mapenzi yao binafsi, lakini baadaye tunapata madhara ya aina hii ambayo sasa tunakuja kuanza kuulizana namna ya kufanya kazi. *(Makofi)*

Nitoe wito kama ambavyo tumeendelea kutoa wito na Waheshimiwa Wabunge kupitia Bunge hili, tuendeleo kuwasih Watanzania na kuwataka wote waliopo mabondeni wahame kwa sababu mvua hizi zinapokuja wanapata madhara makubwa na hatimaye sasa hata katika kuokoa inakuwa shida. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ni vizuri sasa tukashirikiana. Serikali kwa upande wake tunaandaa fedha ili kuhakikisha kwamba miundombinu ile ya mabonde inaboreshwa ili maji yaweze kupita kwa ulaini, lakini wale wote walioko kwenye mabonde na yale maeneo yote yaliyokatanzwa watu waanze kuondoka sasa ili wasipate madhara kama haya pindi mvua nyingi zinapojitokeza.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali tunaendelea kujipanga vizuri kuhakikisha kwamba tunaboresha mifereji maeneo yote; Mwananyamala na maeneo mengine, Ubungo kule, tumeona huku maeneo ya Ilala, maeneo yote haya mpaka kule Vingunguti ambako jana Mheshimiwa Mbunge alitaka ufafanuzi wa Serikali namna ambavyo inafanya kazi. Kwa hiyo, tutashirikiana kuhakikisha kwamba tunasafisha maeneo haya na kuboresha zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. *(Makofi)*

SPIKA: Swali la mwisho kwa siku ya leo, Mheshimiwa Jaku Hashim Ayoub, Mbunge wa Baraza la Wawakilishi.

MHE. JAKU HASHIM AYOUB: Mheshimiwa Spika, nami nakushukuru kwa kunipa fursa hii na vilevile niendeleo kumpa pole na kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa majukumu yake mazito ya kutumikia wananchi wa Tanzania, ikiwemo Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, juzi tumepitisha bajeti ya Wizara ya Mazingira na Muungano na kilio kikubwa cha Wabunge kutoka Zanzibar ilikuwa katika Bandari ya Dar es Salaam, wafanyabiashara wadogo wadogo wamekuwa wakipata usumbufu mkubwa sana au adhabu au mateso, naweza kuthubutu kusema hivyo. Kuna watu wanathubutu kuvunja *televitions* zao, wengine vyerehani vyao na mizigo mingine kuisamehe kutokana na usumbufu huo.

Mheshimiwa Spika, Zanzibar ukiacha karafuu uchumi wake wa pili ni biashara na mtoto akizaliwa haendi mbio moja kwa moja, hutambaa akikweta akapata mguu mpaka akakamata kiambaza akaweza kuchanganya kwenda mwendo. Hebu tusaidie suala hili, tulichangia sana hapa kwa hisia tofauti lakini jawabu halikuja vizuri kupitia kwa Waziri wetu mchapakazi, Mheshimiwa January Makamba na aendeleo kuudumisha Muungano huu, lini utakaa na Afisa wa *TRA* angalau kupunguza makali yale?

Narudia tena, Mheshimiwa Waziri Mkuu, Wajumbe wengi kutoka Zanzibar tumechangia suala hili kwa hisia tofauti...

SPIKA: Mheshimiwa Jaku, swali lako hasa ni lipi sasa?

MHE. JAKU HASHIM AYOUB: Mheshimiwa Spika, lini atakaa na Afisa *TRA* au kufanya ziara ya kushtukiza kwenda kuona mwenyewe pale bila kuuziwa mbuzi kwenye gunia?

SPIKA: Mheshimiwa Waziri Mkuu.

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Spika, samahani, naomba alirudie lile swali lake niweze kulijibu vizuri, sijasikia vizuri.

MHE. JAKU HASHIM AYOUB: Mheshimiwa Spika, ahsante sana, naomba nizungumze kidogo kidogo au niende na swali moja kwa moja. Juzi...

SPIKA: Nafikiri ulichokizungumza ni kama ushauri fulani hivi.

MHE. JAKU HASHIM AYOUB: Si ushauri Mheshimiwa.

SPIKA: Kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu kuufanyia kazi.

MHE. JAKU HASHIM AYOUB: Mheshimiwa Spika, si ushauri, hili suala limekuwa ni la muda mrefu na linataka kufanyiwa kazi maana yake ushauri unaweza ukafanyiwa kazi au usifanyiwe kazi, hiki kilio kimekuwa cha muda mrefu kwa Wazanzibari. Lini tatizo hili litaondoka ili wananchi wa Zanzibar waweze kufanya biashara zao ikiwa yeye ni Waziri Mkuu?

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Jaku. Katika maswali ya kisera, swali linalosema lini ni gumu sana, linakuwa siyo swali, maana yake sasa kwenye sera lini, kwani kuna sera ya kusumbua wananchi wa Zanzibar?

MHE. JAKU HASHIM AYOUB: Mheshimiwa Spika, ni usumbufu na mateso.

SPIKA: Ahsante Mheshimiwa Jaku. Mheshimiwa Waziri Mkuu labda kama una cha kusema chochote kile sijui, tafadhali.

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Spika, naomba nijibu swali na kupokea ushauri wa Mheshimiwa Jaku juu ya namna hawa wafanyabiashara au abiria kutoka Zanzibar au abiria kutoka Bara kwenda Zanzibar wanaopata usumbufu bandarini kupitia chombo chetu cha *TRA*.

Mheshimiwa Spika, lakini nataka niseme siyo *TRA* pekee wanaofanya kazi hiyo bandarini. Waheshimiwa Wabunge wote na Watanzania mnajua sasa hivi tuko kwenye mapambano ya dawa za kulevya ambayo tunayafanya kwa pamoja Bara na Visiwani katika kuhakikisha kwamba hatutoi nafasi ya wasafirishaji, watumiaji na wazalishaji. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, pale bandarini kuna watu wengi, siyo tu Wazanzibari wanaokuja Bara, wako wananchi wengine wa mataifa mengine wanatumia njia hizi kuwa ni vipito vya kupita na vitu ambavyo si rasmi. Kwa hiyo, unapooona kunakuwa na upekuzi wa aina hiyo ambayo unadhani inaweza kutuvurugia Muungano, hapana, upekuzi huu unalenga hasa katika kubaini vitu vingine ambavyo havitakiwi kuingia Bara au kuingia Zanzibar na ni wajibu wetu kulinda maeneo yote mawili, Bara na Zanzibar. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, abiria wote, nataka niwahakikishie kama ambavyo Mheshimiwa Makamba ameeleza kwamba sasa tunataka tuimarishe kupata mitambo ya kubaini vitu vyote ambavyo haviruhusiwi kupita, tutakapopata mitambo hii tukaiweka kwenye mipaka yetu au maeneo yote ya bandari, viwanja vya ndege na vituo vya mabasi, usumbufu huu utakuwa umeondoka.

Kwa sasa kwa kuwa tuna mazoezi hayo mengi ikiwemo na kuhakikisha kwamba haturuhusu madawa ya kulevya kupita, tutalazimika tu kuwasihi waridhie tuone kwenye mizigo yetu kuna nini, lakini hatulengi kuzuia bidhaa yoyote kutoka mahali pengine kwenda mahali pengine. Kwa

hiyo, jambo hili naomba niliweke wazi kwamba Serikali inaendelea na utaratibu wa kutafuta mitambo itakayoweza kusaidia kubaini vile ambavyo hatuvihitaji vipite kwenda moja ya pande zetu kwa lengo la kulinda usalama tulionao. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. (Makofi)

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Waziri Mkuu. Muda umeshaisha, tunakushukuru sana kwa kujibu maswali kwa ufasaha mkubwa. Ahsante sana Mheshimiwa Waziri Mkuu na wauliza maswali wote wamemalizika. (Makofi)

Sasa tunaendelea na maswali mengine, Katibu.

NDG. STEPHEN KAGAIGAI – KATIBU WA BUNGE:

MASWALI NA MAJIBU

SPIKA: Maswali ya kawaida, swali la kwanza litaelekezwa Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala Bora, linaulizwa na Mheshimiwa Mwalimu Kasuku Samson Bilago, Mbunge wa Buyungu.

Na. 104

Wanufaika wa Mfuko wa TASAF

MHE. KASUKU S. BILAGO aliuliza:-

Kaya zinazonufaika na Mfuko wa TASAF kwa vigezo vya umaskini baada ya kukidhi vigezo zimeanza kupata wakati mgumu na usumbufu mkubwa ikiwa mmoja wa wanakaya ni kiongozi wa Serikali ya Kijiji. Mfano baba wa kaya ndiye anakidhi vigezo vya kunufaika na mafao ya TASAF huku mama akiwa Mjumbe wa Serikali ya Kijiji, matokeo yake anaondolewa kuwa mnufaika na kuamuliwa kurudisha fedha yote aliyokwishanufaika nayo.

(a) Je, kuwa Mjumbe wa Kijiji kunaondoa umaskini wa kaya?

(b) Je, kaya maskini inapataje uwezo wa kurudisha fedha walizotumia?

(c) Je, ni kwa nini Serikali isiangalie upya vigezo vya wanufaika wa *TASAF* kwa kushirikisha wadau wengi?

SPIKA: Majibu ya swali hilo, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala Bora, Mheshimiwa Kepteni Mkuchika.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA alijibu:-

Mheshimiwa Spika, leo mimi nimeamka vizuri, nimefurahi sana, ndiyo maana niliwahi kuja. Nataka nichukue nafasi hii kuwapongeza vijana wangu wa Yanga... *(Makofi/Kicheko)*

SPIKA: Mheshimiwa Waziri, unakiuka utaratibu. *(Kicheko)*

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA: Tuliowatuma wakatuwakilisha kule Ethiopia, wamevuka, wanasonga mbele, ndiyo timu peke yake ya wakubwa nchi hii inayoshiriki mashindano ya kimataifa. *(Makofi/Kicheko)*

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tarehe 29 Aprili, 2018 inakuja! *(Makofi/Kicheko)*

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA: Mheshimiwa Spika, tunazidi kuwaombea wasonge mbele wapate mafanikio, wabebe vizuri bendera ya nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya utangulizi huo mzuri tu, naomba sasa kuchukua nafasi hii kujibu swali la Mheshimiwa

Kasuku Samson Bilago, Mbunge wa Buyungu, kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, mpango wa kunusuru kaya maskini una kanuni na taratibu zake za uendeshaji. Taratibu za uendeshaji wa mpango huu ziko bayana kwamba katika utambuzi wa kaya maskini, viongozi wa vijiji, mitaa, shehia hawaruhusiwi kutambuliwa kama walengwa. Hii iliwekwa hivyo ili kuondoa ukinzani wa kimaslahi kwani wao ndiyo wasimamizi wa shughuli zote za mpango katika maeneo yao. Ni kweli kwamba kuwa Mjumbe wa Serikali ya Kijiji hakuondoi umaskini wa kaya yake, hata hivyo, kanuni za mpango zinaruhusu iwapo kaya ya mjumbe inakidhi vigezo vingine vyote vya umaskini lakini anayo hiyari ya kuacha uongozi na kuchagua kuwa mlengwa.

(b) Mheshimiwa Spika, kaya ambazo zilitakiwa kurejesha fedha zilizopokelewa ni zile za wafanyabiashara, watumishi, viongozi na watu wenye uwezo ambao hawakustahili kupokea fedha hizi. Nakiri kwamba katika kuziondoa kaya hizo zilikuwepo zilizoondolewa kwa makosa kwa sababu tu zilikuwa zimeanza kuonyesha mafanikio na kujiimarisha kiuchumi chini ya mpango huu nazo zikatakiwa kurejesha fedha. Hali hii imeleta usumbufu mkubwa kwa kaya hizo.

Naomba kutoa wito kwa watendaji katika halmashauri na vijiji kuacha kuzidai fedha kaya ambazo zilinufaika kwa kutambuliwa kuwa ni kaya maskini na zikatolewa kwa makosa. (*Makofi*)

(c) Mheshimiwa Spika, yapo mambo mengi mazuri tuliyojifunza katika kipindi cha kwanza cha awamu ya tatu ya *TASAF*. Aidha, tumekutana pia na changamoto ambazo zitazingatiwa katika kipindi hiki ambapo tupo katika mchakato wa maandalizi ya kipindi cha pili cha awamu ya tatu ya *TASAF*. Ushauri wa Mheshimiwa Mbunge kuhusu kuwashirikisha wadau wengi zaidi ili kupata maoni yao katika kubainisha vigezo vya kuwapata wanufaika wa *TASAF* utazingatiwa.

SPIKA: Hii *TASAF* ina maswali mengi sana, Mwalimu Bilago swali la nyongeza tafadhali.

MHE. KASUKU S. BILAGO: Mheshimiwa Spika, ahsante pamoja na majibu yaliyotolewa kwa swali hili, nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, swali la kwanza, kumekuwa na upotoshaji mkubwa sana kuhusu *TASAF* kwamba ni fedha zinazotolewa na Chama cha Mapinduzi. Hata Ndugu Polepole alipokuja jimboni kwangu aliwaambia wanufaika wa *TASAF* ni kwamba ni fedha zinazotolewa na Chama cha Mapinduzi. Naomba kauli ya Serikali kuhusu kuzuia upotoshaji huu unaofanywa na Ndugu Polepole pamoja na wenzake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali la pili, kuna vijiji 12 katika Jimbo la Buyungu havinufaiki na *TASAF* kama Vijiji vya Juhudi, Kewe, Rusenga, Kikulazo, Kihomoka, Ruhuru, Njomlote, Yakiobe, Kiniha, Muhange ya Juu, Nyanzige na Nkuba. Ni lini vijiji hivi vitaingia kwenye mfumo wa *TASAF*? Ahsante. *(Makofi)*

SPIKA: Napata taabu sana na swali lako la kwanza, kama fedha hizi zinatolewa na Serikali ya CCM, sasa Ndugu Polepole amekosea nini? Mheshimiwa Waziri majibu tafadhali. *(Makofi)*

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA: Mheshimiwa Spika, la kwanza, sikuwepo Buyungu wala Kigoma kusikia nini alisema Katibu Mwenezi wa CCM, lakini ametaka kujua fedha hizi zinatolewa na CCM au zinatolewa na Serikali? Majibu dhahiri wazi kwamba fedha hizi ni mkopo umekopwa na Serikali ya Tanzania utalipwa na Serikali ya Tanzania unachangiwa na Serikali ya Tanzania, lakini muhimu hiyo Serikali ya Tanzania iliyoweka mipango yote hii inaongozwa na CCM. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali lake la pili kwamba viko vijiji 12 katika jimbo lake ambavyo haviko katika mpango.

Napenda kuchukua nafasi hii kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba mpango wa *TASAF* mpaka sasa kwa Tanzania nzima tumefikia maeneo na watu asilimia 70, hatujafika maeneo yaliyobaki asilimia 30. Maandalizi tunayofanya sasa awamu itakayokuja kuhakikisha kwamba tunamaliza asilimia 30 iliyobaki na tukifanya hivyo hapa shaka vijiji vyake 12 vilivyobaki vitakuwa vimeingia katika mpango wa *TASAF*.

SPIKA: Kwa sababu ya muda Waheshimiwa, tunaendelea Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), swali linaulizwa na Mheshimiwa na Hawa Abdulrahman Ghasia, Mbunge wa Mtwara Vijijini, kwa niaba yake Mheshimiwa Jerome Bwanausi nimekuona.

Na. 105

**Kukarabati Mifereji na Matuta Kwenye
Kingo za Bahari-Mikindani**

MHE. JEROME D. BWANAUSI (K.n.y. MHE. HAWA A. GHASIA) aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kukarabati mifereji ya maji na matuta ambayo yalijengwa zaidi ya miaka 50 iliyopita katika Mji wa Mikindani ili kupunguza athari ya maji ya bahari kwenye mitaa na makazi ya watu hasa kipindi cha mvua kali?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO NA MAZINGIRA): alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira) sasa naomba kujibu swali la Mheshimiwa Hawa Abdulrahman Ghasia, Mbunge wa Mtwara Vijijini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali imeweka mipango ya ukarabati wa mifereji ya maji ya mvua na matuta katika Halmashauri ya Manispaa ya Mtwara Mikindani. Halmashauri ya Manispaa ya Mtwara Mikindani imekuwa ikifanya ukarabati

wa mifereji ya maji ya mvua inayoingia baharini katika mji wa Mikindani kila mara mahitaji yanapojitokeza kwa kutumia fedha za mapato ya ndani na Serikali Kuu.

Mheshimiwa Spika, kwa mwaka wa fedha 2017/2018 Halmashauri imetuma kiasi cha shilingi milioni tatu kutoka mapato ya ndani ya Halmashauri katika kufanya ukarabati wa mfereji uliopo Kata ya Magengeni. Aidha, kiasi cha shilingi milioni 37 zilitumika kufanya ukarabati wa mfereji katika Kata ya Mtonya, Magengeni na Mitengo kupitia fedha za Mfuko wa TASAF.

Mheshimiwa Spika, kwa kutambua umuhimu wa ukarabati wa mifereji na matuta, Halmashauri ya Manispaa ya Mtwara Mikindani imeendelea kutenga fedha kwa ajili ya ukarabati huo. Hivyo, kwa mwaka wa fedha 2018/2019 Halmashauri imetenga kiasi cha fedha shilingi milioni 50 kutoka mapato ya ndani kwa ajili ya kufanya ukarabati wa mifereji kata za Mtonya, Magengeni na Kisungule.

SPIKA: Mheshimiwa Jerome Bwanausi, nimekuona swali la nyongeza.

MHE. JEROME D. BWANAUSI: Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, tatizo lililoko Mikindani ni kubwa na halmashauri haina uwezo wa kumudu tatizo hilo. Wale waliotembelea Mikindani na wanaopita pale watakubaliana na mimi kabisa. Je, Serikali haioni sasa jukumu hili likabebwa na Serikali Kuu kuisaidia Halmashauri ya Mikindani kwa sababu matuta haya yalijengwa miaka 50 iliyopita na sasa ukarabati wake unahitaji fedha nyingi? Hilo ni swali la kwanza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini swali langu la pili, tatizo lililopo Mikindani linafafana na tatizo lililopo Masasi. Mji wa Masasi umezungukwa na milima na hivyo kuleta athari kubwa sana ya maji kutoka milimani kuingia pale mji. Je, Mheshimiwa Waziri yuko tayari kutembelea Masasi na Mikindani kwenda kujionea hali halisi ili Serikali iingilie kati? *(Makofi)*

SPIKA: Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Mheshimiwa January Makamba, majibu tafadhali.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO NA MAZINGIRA): Mheshimiwa Spika, kwanza nitatembelea Mikindani na Masasi baada ya Bunge hili ili kwenda kujionea hali halisi ya anayozungumza Mheshimiwa Mbunge. Kabla sijatembelea, nitatuma wataalam wa Ofisi ya Makamu wa Rais waende Miji wa Mikindani mapema wakatazame haya aliyouliza Mheshimiwa Ghasia na aliyozungumza Mheshimiwa Bwanausi na baada ya hapo tutafanya tathmini tuone nini kinahitajika kufanyika. *(Makofi)*

SPIKA: Ahsante sana. Tunaendelea na Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, swali linaulizwa na Mheshimiwa Hassan Elias Masala, Mbunge wa Nachingwea, Mheshimiwa Masala, tafadhali.

Na. 106

Migogoro ya Mipaka katika Kambi za Jeshi Nachingwea

MHE. HASSAN E. MASALA aliuliza:-

Je, ni nini kauli ya Serikali katika kushughulikia tatizo la migogoro ya mipaka katika Kambi za JKT Nachingwea na Kikosi Namba 41 Majimaji na vijiji vinavyozunguka Kambi hizo?

WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Hassan Elias Masala, Mbunge wa Nachingwea, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu inatambua kuwepo kwa migogoro katika maeneo mbalimbali kati ya Kambi za Jeshi na vijiji jirani au maeneo yaliyotwaliwa na Jeshi kwa maslahi mapana ya nchi yetu.

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Spika, Kambi ya 41 KJ (Majimaji) ilipimwa mwaka 2005, wananchi waliokuwepo wakati wa upimaji idadi yao walikuwa 61. Katika Kambi ya 843 KJ ya JKT iliyopo Nachingwea mwaka 2009 Halmashauri ya Wilaya ya Nachingwea ilichukua jukumu la kuainisha mipaka kati ya Kambi hiyo na Kijiji cha Mkukwe. Wananchi waliokuwa ndani ya Kambi wakati wa kubaini mipaka hiyo walikuwa ni kaya tisa.

Mheshimiwa Spika, mwaka huu wa fedha 2018/2019 Wizara yangu imetenga bajeti kwa ajili ya uthamini na kulipa fidia kwa wananchi wanaostahili. Baada ya uthamini, wananchi wenye stahiki ya malipo watalipwa fidia zao kwa mujibu wa sheria na kanuni za fidia za ardhi zilizopo.

SPIKA: Mheshimiwa Mbunge wa Nachingwea, swali la nyongeza.

MHE. HASSAN E. MASALA: Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu ya Mheshimiwa Waziri, naomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, pamoja na wananchi hao ambao Mheshimiwa Waziri anakiri kwamba hawajalipwa fidia na anakiri kwamba wakati maeneo haya vikosi wanayatwaa hawajalipwa chochote bado vikosi vyetu vimeendelea kuwafukuza wananchi hawa wasifanye shughuli zozote ikiwemo kuokota korosho zao kwa wale ambao walishapanda mikorosho.

Naomba kupata kauli ya Serikali juu hatma ya watu hawa wakati wanaendelea kutengewa hii bajeti ambayo Mheshimiwa Waziri ameisema ili waweze kuendelea kufanya shughuli zao? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, swali la pili Mheshimiwa Waziri naomba kupata *commitment* ya Serikali kwa sababu tatizo ni la muda mrefu na Tume nyingi zimeshaundwa na tayari zilishaleta majibu ya kukiri kwamba kuna tatizo.

Ni lini Serikali sasa itaenda kufanya hili zoezi ili tatizo hili liondoke na wananchi wale waweze kujua hatma yao?
(Makofi)

SPIKA: Majibu ya swali hilo, Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, Mheshimiwa Dkt. Hussein Mwinyi, tafathali.

WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:
Mheshimiwa Spika, lazima tukiri kwamba tatizo kubwa limekuwa ni upungufu wa bajeti na kwa maana hiyo kupelekea wananchi wanaostahili kulipwa fidia kuchelewa. Hata hivyo, kulikuwa kuna maamuzi ya makusudi ya kuzuia wananchi kufanya shughuli za kibinadamu katika makambi haya. Sababu kubwa ya maamuzi hayo ni kwamba katika baadhi makambi haya kuna silaha na kuna milipuko ambayo inaweza kuleta athari kwa wananchi na ndiyo sababu wakakatazwa kufanya shughuli za kibinadamu.

Lakini ukiacha tatizo hilo, wapo wananchi ambao wakipewa ruhusa ya kufanya hivyo basi wanafanya maendelezo makubwa, wengine wanajenga hata nyumba ambayo inapelekea uthamini na fidia zao kuwa kubwa mno. Hizo ndiyo sababu zilizopelekea wakazuiwa kufanya shughuli zote za kibinadamu ili kwanza wasidhurike lakini pili wasiendelee maeneo hayo kwa sababu yatapelekea fidia kuongezeka.

Mheshimiwa Spika, kuhusu *commitment* ya Serikali kwamba ni lini zoezi hili litakamilika, nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba tutakapokuwa tumepokea fedha hizi kutoka kwenye bajeti yetu jukumu hili litafanyika mara moja ili tuondokane na tatizo hili la muda mrefu.
(Makofi)

SPIKA: Ahsante. Tunaendelea na Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika ya Mashariki, swali linaulizwa na Mheshimiwa na Ally Saleh Ally, Mbunge wa Malindi, Mheshimiwa Ally Saleh hayupo Mheshimiwa Masoud kwa niaba yake.

Na. 107

Tanzania Kupanua Uwanda wa Kidiplomasia

MHE. MASOUD ABDALLAH SALIM (K.n.y. MHE. ALLY SALEH ALLY) aliuliza:-

Tanzania inaonekana kupanua uwanda wake wa kidiplomasia kwa kuanzisha Balozi mpya maeneo kadhaa, lakini pia kumekuwa na malalamiko ya makazi ya Wanabalozi wa nchi hii huko ughaibuni.

(a) Je, Serikali haioni haja ya kuwekeza katika eneo hili kwa kujenga ofisi ambazo pia zinaweza kuwa kibiashara?

(b) Kama hilo linafanyika, je, limefanyika wapi na wapi hadi sasa?

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa ruhusa yako na kwa niaba ya Wziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Ally Saleh Ally, Mbunge wa Malindi, lenye vipengele (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kuwa Tanzania imeendelea kufungua Balozi zake mpya katika nchi mbalimbali duniani ili kuimarisha mahusiano na kunufaika na fursa mbalimbali za kiuchumi zilizopo katika nchi hizo. Kwa mwaka wa fedha 2016/2017 jumla ya Balozi mpya sita zimefunguliwa katika nchi za Sudan, Algeria, Israel, Korea Kusini, Qatar na Uturuki.

Mheshimiwa Spika, halikadhalika Serikali inatambua umuhimu wa kuendelea kujenga majengo ya ofisi na makazi ya watumishi Balozini na imekuwa ikitekeleza jukumu hilo kwa kutumia fedha za bajeti ya maendeleo zinazopangwa kwa kila kipindi cha mwaka wa fedha. Hadi hivi sasa Serikali inamiki jumla ya majengo 106 yalipo katika nchi mbalimbali

ambayo yanatumika kama makazi ya watumishi na ofisi za Balozi zetu.

Mheshimiwa Spika, vilevile Serikali inatambua kuwa na majengo ya vitega uchumi katika Balozi zetu ni muhimu ili kuwezesha kupatikana kwa fedha zitakazokuwa zikumika kuziendesha Balozi hizo na hatimaye kuipunguzia mzigo Serikali. Kwa mfano, Serikali inamiliki majengo ya Ofisi ambayo pia yanatumika kama kitega uchumi katika Balozi zetu za Tanzania Maputo, Msumbiji; New York, Marekani na Paris, Ufaransa. Aidha, Serikali imeanza kushirikiana na Mifuko ya Hifadhi ya Jamii na taasisi za fedha zilizopo nchini kwa ajili kujenga majengo ya vitega uchumi katika viwanja vya Serikali vilivyopo Abuja, Nigeria na Lusaka, Zambia.

Mheshimiwa Spika, kupitia mpango wa Wizara ya miaka 15 wa ujenzi, ununuzi, ukarabati wa majengo ya ofisi na makazi ya watumishi Balozi ulioanza kutekelezwa mnamo mwaka wa fedha 2002/2003, Wizara imefanikiwa kutekeleza miradi mbalimbali kwenye Balozi zetu kama vile kufanikisha ujenzi wa jengo la ofisi ya Ubalozzi New Delhi, India; ununuzi wa jengo la Ofisi ya Ubalozzi Washington D.C, Marekani; ununuzi wa jengo la ofisi ya Ubalozzi New York, Marekani; ununuzi wa jengo la ofisi ya makazi ya Balozi Paris, Ufaransa; ukarabati wa jengo la makazi ya Balozi Nairobi, Kenya; ukarabati wa makazi ya ya Balozi wa Tanzania Tokyo, Japan; na ukarabati wa jengo la ghorofa tisa la ofisi na makazi lililopo Ubalozzi wa Tanzania Maputo, Msumbiji ambalo litatumika kama ofisi ya Ubalozzi na kitega uchumi cha Serikali nchini humo.

Mheshimiwa Spika, hivi sasa Wizara imeandaa mpango mwingine wa miaka 15 wa ujenzi, ununuzi, ukarabati wa majengo ya ofisi na makazi ya watumishi Balozi ulioanza kutekelezwa mwaka huu wa fedha 2017/2018. Baadhi ya miradi inayotekelezwa ni ukarabati wa jengo la ofisi na makazi ya watumishi kwenye Balozi za Tanzania Harare, Zimbabwe; Kampala, Uganda; Beijing, China; Pretoria, Afrika Kusini; Cairo, Misri; ukarabati wa nyumba za Ubalozzi wa Tanzania Lilongwe, Malawi; Kinshasa,

DRC; ukarabati wa jengo la zamani la ofisi ya Ubalazi lilipo Washington DC; ujenzi wa makazi ya Balazi wa Tanzania Addis Ababa, Ethiopia na ujenzi wa ofisi ya Ubalazi wa Tanzania Muscat, Oman.

SPIKA: Mheshimiwa Masoud, swali la nyongeza.

MHE. MASOUD ABDALLAH SALIM: Mheshimiwa Spika, nakushukuru na nina maswali mawili ya nyongeza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, katika majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri ameeleza majengo ambayo yatajengwa katika nchi mbalimbali na ukarabati ambao utafanyika katika nchi mbalimbali katika Balazi hizo. Hata hivyo, Mheshimiwa Naibu Waziri atakumbuka kwamba katika jambo kubwa ambalo linatupa aibu nje ya nchi ni viwanja ambavyo tumepewa na wenzetu walioko nje na hasa nchini Uingereza ambapo imetishia usalama wetu na inaonekana kwamba sisi kama Watanzania hatukuwa na fadhila nzuri ya kupewa vile viwanja na tunatishiwa hata kupelekwa Mahakamani au kunyang'anywa viwanja vile ambavyo viko Uingereza na Sweden.

Je, Mheshimiwa Naibu Waziri anawaambia nini Watanzania kuepukana na aibu hii ya viwanja tulivyopewa kule Uingereza ambavyo vimekuwa ni pori/kichaka na tunatishiwa kunyang'anywa sambambana majengo ya kule Sweden ambayo hayaendelezwi? Hilo ni swali la kwanza.

Mheshimiwa Spika, swali la pili, Mheshimiwa Naibu Waziri ameeleza hapa suala zima la mikakati ya kibiashara, lakini moja ya mkakati mkubwa katika suala zima la biashara ni diplomasia ya kiuchumi (*economic diplomacy*). Hata hivyo, inaonekana Serikali haina mkakati na dhamira iliyo nzuri kuelekea kwenye *economic diplomacy*. Nini mkakati husika wa nchi ambazo amezitaja wa kuelekea kwenye diplomasia ya kiuchumi ili nchi yetu ipate manufaa zaidi?

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante. Majibu ya maswali hayo Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki. Viwanja visivyojengwa ni pamoja na Abuja na Nairobi. *(Makofi)*

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI: Mheshimiwa Spika, kuhusu viwanja vyetu 11 vilivyoko nje ya nchi nimesema kwamba tumeweka mkakati na mkakati huu Mheshimiwa Masoud kama Mjumbe wa Kamati ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama anaufahamu. Mkakati huu ulianza mwaka 2002/2003 na ukaisha 2017. Katika jibu langu la msingi nimesema kwamba katika mkakati huo tumeainisha viwanja vyetu vyote na kuvitengenezea utaratibu wa kuhakikisha kwamba tunavijenga ili kuweza kuweka vitega uchumi. Hilo ndiyo jibu langu kwa swali lako la kwanza.

Mheshimiwa Spika, lakini swali la pili kwamba Serikali ina mkakati gani wa kutekeleza diplomasia ya uchumi, nataka tu nimweleze kwamba moja ya majukumu makuu ya Mabalizi wetu tunapowateua kwenda nje ya nchi pamoja na watumishi ambao tunawapeleka katika Balozi zetu ni kuhakikisha kwamba wanatekeleza diplomasia ya uchumi kwa kuhakikisha kwanza wanajenga mahusiano mazuri baina yetu na nchi hizo zilizoko nje ya nchini lakini pili waweze kutangaza na kutafuta fursa mbalimbali za kijamii, kiuchumi na za uwekezaji na wanapimwa kwa mambo hayo ili kuhakikisha kwamba sisi tunafaidika na uwepo wao nje ya nchi.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Abuja kama nilivyosema kwenye jibu langu la msingi kwamba iko katika mpango na tayari mazungumzo yanaendelea na Mheshimiwa Masoud anajua.

MHE. MASOUD ABDALLAH SALIM: Uingereza?

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI: Uingereza nimeshajibu.

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri, Mheshimiwa Masoud anakusumbua tu. *(Kicheko)*

Tunaendelea na Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, swali la mwisho kwa siku ya leo linaulizwa na Mheshimiwa Andrew John Chenge, Mbunge wa Bariadi, uliza swali lako tafadhali.

Na.108

Kurejesha Eneo la Gereza la Matongo kwa Wananchi

MHE. ANDREW J. CHENGE aliuliza:-

Katika miaka ya 1980 wanakijiji wa Kijiji cha Mwanchumu, Salaliya na Matongo walitoa maeneo yao kwa Serikali ili yatumike kwa shughuli za kilimo zilizokusudiwa na Gereza la Matongo lakini kwa sasa maeneo hayo hayatumiwi na Magereza kikamilifu.

Je, Serikali ipo tayari kurejesha eneo hilo ambalo halitumiki kikamilifu kwa wananchi wa vijiji hivyo?

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Andrew John Chenge, Mbunge wa Bariadi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Gereza la Matongo liko Mkoani Simiyu katika Wilaya ya Bariadi na lina ukubwa wa hekari 2472.62. Gereza hili lilianzishwa mwaka 1975 kwa kuchukua eneo lililokuwa la Mbunge wa zamani wa eneo hilo, Marehemu Edward Ng'wani ambapo alifidiwa eneo hilo kwa kupewa eneo lingine na Serikali. Aidha, wananchi wa Vijiji vya Mwanchumu, Salaliya kwa asili ni wahamiaji kutoka maeneo mengine na siyo wenyeji wa Matongo.

Mheshimiwa Spika, ikumbukwe kuwa Serikali iko kwenye mpango wa kuboresha kilimo kupitia Jeshi la

Magereza kwa kuliwezesha kuzalisha chakula cha kutosheleza kulisha wafungwa na mahabusu. Eneo la Gereza la Matongo lipo kwenye orodha ya maeneo yaliyopewa kipaumbele katika kilimo cha mahindi, alizeti, pamba, ufugaji wa nyuki na mifugo pamoja na upandaji wa miti na uhifadhi wa mazingira.

Mheshimiwa Spika, Serikali ilitwa eneo hilo ili kuwezesha Magereza kuendeleza shughuli za urekebishaji wafungwa kwa kutumia kilimo cha ufugaji ambapo mazao mbalimbali ya kilimo hustawi. Kwa sasa eneo hilo limeshapimwa na taratibu za kufuatilia upatikanaji wa hati unaendelea.

Mheshimiwa Spika, kutokana na eneo hilo kuwa kwenye mpango mkakati wa Jeshi la Magereza wa kujitosheleza kwa chakula na shughuli nyingine, Serikali haina mpango wa kulirejesha eneo hilo kwa vijiji tajwa.

SPIKA: Mheshimiwa Chenge, swali la nyongeza, tafadhali.

MHE. ANDREW J. CHENGE: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, Gereza la Matongo ni miongoni mwa Magereza yaliyoanzishwa na Serikali katikati ya miaka 1970 kwa lengo hilo hilo ambalo Waziri amesema katika jibu lake, lakini zaidi ya miaka 40 ukifika pale Matongo hakuna cha maana kinachoendelea. Mheshimiwa Naibu Waziri katika majibu yake anasema Gereza hili limo kwenye mpango wa kuboresha kilimo, ni lini mpango huu mahsusni kwa Gereza la Matongo utanza kutekelezwa na Serikali? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, swali la pili, Mheshimiwa Naibu Waziri katika majibu yake ametambua mazao yanayolimwa katika eneo hilo likiwepo eneo lenyewe la Matongo. Je, yuko tayari na ikiwezekana kushirikiana na Mbunge wa eneo hilo kutafuta mwekezaji ili kuanzisha kiwanda ili kuongeza

thamani ya mazao yatakayolimwa na Magereza lakini pia kusaidia soko kwa wananchi ambao wanazunguka eneo hilo? Ahsante. (Makofi)

SPIKA: Majibu ya maswali hayo, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, *Engineer* Hamad Masauhi, tafadhali.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:

Mheshimiwa Spika, swali lake la kwanza nimeshamjibu katika majibu yangu ya msingi, naomba tu nichukue fursa hii kufafanua. Nimesema kwamba tuna mkakati wa kuhakikisha kwamba Jeshi la Magereza linajitosheleza kwa chakula. Kwa sasa hivi Jeshi la Magereza linajitosheleza kwa chakula kwa asilimia 30, malengo yetu ni kuhakikisha kwamba tunafikia asilimia 70.

Mheshimiwa Spika, mkakati huu utatekelezwa baada ya kuhakikisha kwamba tumepata fedha za kutosha kuwekeza. Katika bajeti ya maendeleo ya mwaka huu tunatarajia kupata takribani shilingi bilioni 3 ambazo zitatumika katika moja ya mikakati ya kuimarisha kilimo pamoja na kujitosheleza katika Magereza yetu. Pia tuna mpango vilevile kupitia jitihada za Mheshimiwa Waziri Mkuu kupata matrekta 50 kwa kuanzia ambayo tutayapeleka katika Magereza ikiwemo Gereza hili la Matongo ili kuweza kusaidia kuimarisha kilimo katika maeneo hayo. Kwa hiyo, nimwombe Mheshimiwa Mbunge aendelee kuvuta subira lakini ni jambo ambalo tayari liko katika hatua nzuri za utekelezaji.

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na swali lake la pili kwamba kama Serikali iko tayari kushirikiana na mwekezaji kuwekeza. Ndiyo mikakati ya Serikali ya Awamu ya Tano kuhakikisha kwamba nchi yetu inafikia uchumi wa kati kupitia viwanda. Kwa hiyo, nina uhakika kabisa Mheshimiwa Mbunge akiweza kuwasiliana na mamlaka husika kwa maana ya Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji atapata mwongozo na msaada mzuri wa kuweza kusaidia jitihada za Serikali za kuimarisha viwanda katika nchi yetu. Sisi kama

Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi pale ambapo tunaweza kutoa mchango wetu kwa namna yoyote ile tutakuwa tayari kushirikiana naye.

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri. Waheshimiwa kipindi cha maswali wakati huu bajeti ni saa moja tu, kwa hiyo, muda wetu umekwisha tunaendelea na ratiba nyingine.

Wageni waliopo katika Jukwaa la Spika ni 36 wa Mheshimiwa Ummu Mwalimu, Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto ambao ni viongozi wa Wizara na wadau wa maendeleo wa sekta ya afya kutoka ndani na nje ya nchi ambao ni pamoja na Katibu Mkuu, Idara Kuu ya Maendeleo ya Jamii, Ndugu Sihaba Nkinga, ahsante sana Katibu Mkuu; Kaimu Katibu Mkuu, Idara Kuu ya Afya, Muhammad Kambi, karibu sana na Naibu Katibu Mkuu, Afya upande wa TAMISEMI, Ndugu Zainabu Chaula, ahsante sana. (Makofi)

Pia wapo wadau wa maendeleo ya sekta ya afya kutoka ndani na nje ya nchi ni pamoja na wanaotoka *Irish Embassy*, Balozi Paul Sherlock, karibu kule mliko; *UNICEF-Tanzania*, Mbelwa Gabagambi; Mwakilishi wa *Irish Embassy*, Bronagh Carr; mwakilishi wa *Irish Embassy*, Oliva Kinabo; mwakilishi wa *WHO*, Adielle Onyeza; mwakilishi wa *WHO*, Leticia Rweyemamu; mwakilishi wa *World Bank*, Chicho Suzuki; mwakilishi wa *USAID*, Godfrey Nyombi; mwakilishi wa *GTZ*, Erick Msoffe; mwakilishi wa *UN-Women*, Rachel Boma; mwakilishi wa *JSI*, Anthony Mwendamaka; mwakilishi wa *HelpAge International*, Smart Daniel; mwakilishi wa *Measure Evaluation-Tanzania*, Willis Odek na mwakilishi wa *REPSI*, Edwin Mapalala. (Makofi)

Pia tunaye Katibu wa Baraza la *NGO's* Ndugu Ismail Suleiman; mwakilishi wa *GUGA-Tanzania Child Right Forums*, Erick Shemweta; mwakilishi wa Shirika la *Institutional for Inclusive Development*, Victoria Lihuru; mwakilishi wa *SIKIKI*, Atuswege Mwanganele; mwakilishi wa *PRINMAT*, Kezia Kaposi na mwakilishi wa *PRINMAT*, Novest Matee. (Makofi)

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

Wageni wa Waheshimiwa Wabunge ni wageni saba wa Mheshimiwa Jumaa Aweso, Naibu Waziri wa Maji na Umwagiliaji ambao ni watumishi wa Halmashauri ya Wilaya ya Pangani, Mkoani Tanga. Karibuni sana wageni wetu kutoka kule Pangani, Tanga. *(Makofi)*

Pia tuna wageni watatu wa Mheshimiwa Stella Ikupa Alex, Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu, Walemavu ambao ni mdogo wake ameambatana na watoto wake. Wako wapi wageni wa Mheshimiwa Stella Ikupa? Wale pale, karibuni sana sana. Mtoto wa Mheshimiwa Stella Ikupa nyoosha mkono, yuko pale dogo, karibuni sana. *(Kicheko/Makofi)*

Mgeni wa Mheshimiwa Stanslaus Nyongo, Naibu Waziri wa Madini ambaye ni bibi mzaa mama, Mwalimu mstaafu, Casta George Budodi kutoka Wilayani Maswa, Mkoa wa Shinyanga. Bibi karibu sana hapa mjengoni. *(Makofi)*

Wageni wanne wa Mheshimiwa Hassan Masala kutoka Jimboni kwake Nachingwea Mkoani Lindi. Karibuni sana. *(Makofi)*

Wageni 24 wa Mheshimiwa Richard Ndassa ambao ni wanafunzi wa *UDOM*wanaotoka Wilaya ya Kwimba. Wale pale, karibuni sana hapa Dodoma. Wasukuma mmejaa kweli Dodoma, itabidi tuanzishe kodi maalum kwa ajili ya ninyi peke yenu. *(Makofi/Kicheko)*

Wageni wawili wa Mheshimiwa Musa Ntimizi ambao ni viongozi wa CCM Wilaya ya Uyui, Mkoa wa Tabora, karibuni sana. *(Makofi)*

Wageni wa Mheshimiwa Joseph Kasheku Musukuma ambao ni Mheshimiwa Elias Simon Kisome, Diwani wa Kata ya Busanda, Mkoa wa Geita. Karibu sana Mheshimiwa Diwani. *(Makofi)*

Wageni watano wa Mheshimiwa Marium Ditopile ambao ni wasanii kutoka Dar es Salaam. Wageni hawa ni pamoja na Papii Nguza maarufu Papii Kocha lakini pia yupo

Nguza Viking (Babu Seya) na pia yuko Francis Nguza. Ahsante sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa kesho tarehe 20 Aprili, 2018 kutakuwa na shughuli maalum ya *Viking Night* pale *Royal Village* saa 2.00 usiku. Itaratibiwa na Mheshimiwa Mariam Ditopile, kwa hiyo, mnakaribishwa sana na tiketi anazo Mheshimiwa Mariam Ditopile. *(Makofi)*

Wageni saba wa Mheshimiwa Peter Serukamba ambao ni wadau wa afya wa Taasisi ya SIKIKA na NACOPHA kutoka Jijini Dar es Salaam. Karibuni sana. Pia wawakilishi 12 wa Maspika wa Mabunge ya Vyuo Vikuu Tanzania. Karibuni sana Wawakilishi wa Maspika wenzangu katika vyuo vikuu. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, huo ndiyo mwisho wa matangazo ya wageni wetu, kipekee nimtambulishie Mheshimiwa Mwamoto, naomba usimame. Naomba tu Bungeni hapa tumtambue pamoja na sifa alizonazo kwamba yeye ndiyo Balozi wa Watu wenye Ulemavu wa Macho. Kwa hiyo, kuanzia leo muwe mnamuita Mheshimiwa Balozi Mwamoto. *(Makofi/Kicheko)*

MWONGOZO WA SPIKA

MHE. GEORGE M. LUBELEJE: Mwongozo wa Spika.

SPIKA: Jamani hatuwezi kuwa na miongozo mingi namna hii, halafu wengine Mwongozo kila siku haiwezekani. Haya tuendelee, Katibu uwe unanitajia majina halafu mimi niwe naandika huku.

NDG. JOSHUA CHAMWELA - KATIBU MEZANI: Mheshimiwa Lubeleje, Mheshimiwa Kangi Lugola, Mheshimiwa Aida Khenani, Mheshimiwa Mussa Mbarouk, Mheshimiwa Esther Matiko na Mheshimiwa Godbless Lema.

SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Kangi Lugola, tafadhali.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO NA MAZINGIRA): Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Naomba Mwongozo wako kwa Kanuni ya 68(7).

Mheshimiwa Spika, humu ndani kuanzia jana na leo imejirudia, kumekuwa na upotoshaji juu ya shughuli ambazo Mheshimiwa Polepole ambaye ni Katibu wa Itikadi na Uenezi wa CCM anazozifanya.

Mheshimiwa Spika, jana Mheshimiwa Godbless Lema alimtuhumu Mheshimiwa Polepole kwamba ameagiza Jeshi la Polisi kumkamata Mheshimiwa Zitto Kabwe kwa kile kinachosemakana ambacho ni dhahiri kwamba anapotosha ripoti ya CAG kwa wananchi na leo Mheshimiwa Bilago, rafiki yangu amerudia tena kwamba anapotosha juu ya fedha za TASAF.

Mheshimiwa Spika, Ilani yetu ya CCM ambayo ninayo hapa katika utangulizi wake Ibara ya kwanza inasema, Ilani ya CCM ni kwa ajili ya uchaguzi Mkuu wa mwaka 2015 wa kuwachangua Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Rais wa Zanzibar, Wabunge, Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi na Madiwani, imeandaliwa ikiwa ni mkataba kati ya CCM na wananchi, huu ni mkataba.

Pia Ibara ya 4 inasema, katika miaka mitano ijayo 2015-2020, CCM ikiwa madarakani itazielekeza Serikali zake kutumia nguvu zake zote kuendelea kupambana na changamoto kubwa nne:-

(i) kuondoa umaskini;

(ii) kupunguza tatizo la ajira;

(iii) kuendeleza vita dhidi ya rushwa na ubadhirifu wa mali ya umma; na

(iv) kuendelea kudumisha amani, ulinzi na usalama wa maisha ya wananchi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, upotoshaji juu ya ripoti ya CAG unalenga kuvunja amani na usalama katika nchi yetu na kitendo cha kupotosha wananchi kwamba fedha za TASAF za Serikali ya CCM ndio ajenda kubwa ya Polepole ya kupambana na umaskini.

Sasa nilikuwa naomba Mwongozo wako chama madhubuti kinazaa Serikali makini na Serikali yenye upako, sasa katika mazingira haya na kwa kuwa upande wa wenzetu hawana uelewa juu ya mkataba huu ambao ni ilani; na kwa kuwa Wabunge tunapokuja hapa huwa tunapewa mkoba ambao una Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania una Kanuni za Kudumu za Bunge; kwa nini ilani hii kiti usielekeze kwamba katika mkoba ule kuwe na mkataba huu wa CCM ambapo Wabunge wote watakuwa nao ili waweze kujua kazi za Mheshimiwa Polepole ambazo anazifanya katika kusimamia Serikali ya CCM na ataendelea kutoa maagizo kwa Serikali yake Serikali, Serikali yenye upako ili iendeleo kuyafanya haya ambayo ni mkataba wa wananchi.

Mheshimiwa Spika, naomba Mwongozo wako juu ya mkataba huu kwa nini wenzetu wasiwekewe kwenye mkoba? (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante sana Kangi Lugola tunaendelea Mheshimiwa Aida Khenan.

MHE. AIDA J. KHENANI: Mheshimiwa Spika, nakushukuru na nasimama kwa Kanuni ya 68(7) na kwa ajili ya kuokoa muda sitaweze kuisoma.

Mheshimiwa Spika, ninaomba Mwongozo wako kipindi nauliza swali kwa Waziri Mkuu amejibu vizuri, lakini nilikuwa naomba Mwongozo wa kiti chako kwa kuwa Serikali ilitamka hapa ndani ya Bunge kuweka zuio kwa wakulima kuuza mazao yao nje ya nchi wakati haijafanya tathmini ni kiasi gani kimezalishwa na kiasi gani kinahitajika kwenye Taifa matokeo yake ikaleta shida kubwa kwa wakulima mpaka hivi nazungumza mazao yao yaani mahindi yameoza na wamekata tamaa ya kuendelea tena na kilimo hiki.

Mheshimiwa Spika, Waziri anapozungumza hajasema sasa kwa sababu wao walitamka kama Serikali ni kitu gani wanakwenda kukifanya kwa wakulima hawa ambao wao walilima lakini Serikali ikawaaambia wasiuze ikazuia na badala yake haikununua yenyewe Serikali. Naomba Mwongozo wako kwa nini Serikali isitoe utaratibu mzuri kwa wakulima hao. *(Makofi)*

SPIKA: Hilo nilimalize kabisa Mwongozo wangu ni kwamba Wizara ya Kilimo watakapokuja hapa kwenye bajeti yao pamoja na mambo mengine watatoa ufafanuzi wa hilo. Mheshimiwa Mussa Mbarouk. *(Makofi)*

MHE. MUSSA B. MBAROUK:Mheshimiwa Spika, wakati nikijibiwa namba 107 la Ally Saleh, lililoulizwa na Mheshimiwa Masoud, Naibu Waziri wa Mambo ya Nje alisema kwamba katika viwanja ambavyo tumepewa katika baadhi ya nchi vinaendelea kujengwa sasa ipo taarifa kwamba tulipewa kiwanja cha *low density* na Serikali ya Oman lakini tukashindwa kujenga kwa taratibu za Oman tulinyang'anywa kiwanja kile wakapewa nchi ya India na sisi tukapewa kiwanja kingine sasa nilitaka kujua ujenzi anaosema Naibu Waziri ni kiwanja kilekile tulirudishiwa au tumepata kiwanja kingine? Nataka aliambie Taifa tujue nini kinachoendelea.

SPIKA: Hilo nalo nalielekeza wakati Wizara ya Mambo ya Nje itakapokuja na bajeti yake hapa ni moja ya jambo ambalo watapaswa kulifafanua pia habari za viwanja kujengwa. Mheshimiwa Lubeleje George Malima.

MHE. GEORGE M. LUBELEJE: Mheshimiwa Spika, Mwongozo wa Spika kanuni ya 64(7) swali namba 104 ninataka maelezo ya kina ya Mheshimiwa Waziri kuhusu *TASAF* kwa sababu kuna kaya maskini ziliandikishwa, lakini wamerejesha zile fedha na leo Mheshimiwa Waziri ametoa kauli kwamba wazirejeshe zile fedha.

Mheshimiwa Spika, je, wale ambao wamesharejesha zile fedha watarudishiwa? Ahsante.

SPIKA: Mheshimiwa Kepteni Mkuchika sijui kama umempata Mheshimiwa Lubeleje kama una la kusema kwa kifupi sana.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA ABORA: Mheshimiwa Spika, nimempata somo yangu George kwa sababu haya masuala ni ya mtu mmoja mmoja mimi ninaomba tu wapiga kura wake ambayo yamewasibu hayo aniletee tutawatafuta tupate ukweli ili tuweze kuchukua hatua vinginevyo si rahisi kutoa jibu la jumla kwa wote mpaka tumejua tatizo la kila mmoja wao.

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Esther Matiko Mbunge wa Tarime Mjini.

MHE. ESTHER N. MATIKO: Mheshimiwa Spika, nakushukuru na naomba Mwongozo wangu kwa Kanuni ya 68(7) nikisoma pamoja na Kanuni ya 64(1)(g) ambayo inasema Mbunge hatatumia lugha ya kuudhi au inayodhalilisha watu wengine.

Mheshimiwa Spika, jana wakati Waziri wa Katiba na Sheria ambaye ni Mbunge wa Kuteuliwa anahitimisha hoja yake aliweza kutumia lugha ya kuudhi na kudhalilisha. Kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Ibara ya 66(1) imeyatamka bayana wajumbe wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ikianza kwa ruhusa yako kwa kusema wajumbe wa kwanza kabisa ni Wabunge walichaguliwa kuwakilisha majimbo ya uchaguzi ambayo mimi mmoja wapo nimechaguliwa kuwakilisha jimbo la uchaguzi la Tarime mjini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, (b) yake inasema Wabunge wanawake wa idadi isiyopungua asilimia 30 ya Wabunge wote waliotajwa katika ibara husika; (c) Wabunge watano waliochaguliwa na Baraza la Wawakilishi kutoka miongoni mwa Wajumbe wake angalau wawili kati yao wanawake; (d) Mwanasheria Mkuu wa Serikali; (e) Wabunge wasiozidi 10 walioteuliwa na Rais kutoka miongoni mwao wenye sifa

zilizotajwa katika Ibara wamezianisha pale ku-serve muda kati yao walau watano wawe wanawake na Mheshimiwa Kabudi katika kundi hili; (f) Spika iwapo hatakuwa miongoni mwa Wabunge waliochaguliwa.

Mheshimiwa Spika, kwa nini mmeamua ku-*refer* hiyo; jana wakati Mheshimiwa Kabudi anahitimisha hoja yake kwanza kabisa alianza kwa kuwadhalilisha Wabunge wa Viti Maalum ambao wamekuja huku kwa *affirmative action*, akasema kwamba ni kama *favor*, kama wasingekuwepo hawakutakiwa kuwepo na kungekuwa na Wabunge wachache sana Bungeni. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hakuishia hapo akaendelea zaidi kwa kuonesha jinsi gani Waziri wa Katiba na Sheria anakiuka Katiba ambayo pia naye anaisimamia, akatamka kwamba mimi Mbunge wa Tarime Mjini ambaye nimechaguliwa na wananchi na nikamzidi mgombea wa CCM kwa zaidi ya kura 6,000 kwamba nimekuja kwa ajali.

Sasa sijui walionichagua walikuwa na ajali kichwani mwao kwamba wamenichagua kwa bahati mbaya, haya maneno sio tu kwamba yanadhalilisha wanawake wa majimbo, lakini zaidi ameweka taharuki kwa wananchi Tarime na nafikiri unawafahamu vizuri kwamba uamuzi walioufanya Mheshimiwa Kabudi anaona kwamba ilikuwa ni ajali. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nilikuwa nataka Mwongozo wako, ni kwa nini Mawaziri tena wa Katiba na Sheria anavunja Katiba, zaidi waziwazi kabisa kwa kudhalilisha jinsia ya wanawake? Naomba mwongozo wako *either* kwanza kabisa afute haya maneno na atutake radhi wanawake wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania awatake radhi wananchi wa Jimbo la Tarime mjini ambao walinichagua kwa kura nyingi sana na wanajivunia kuwa mwakilishi wao, hawajutii. (*Makofi*)

SPIKA: Mheshimiwa Esther Matiko sikuwepo, sikusikia lakini taarifa nilizonazo ni kwamba Mheshimiwa Chenge

alilitolea *ruling* hili jambo jana. Kwa hiyo tunaendelea Mheshimiwa Godbless Lema. (*Makofi*)

MHE. GODBLESS J. LEMA: Mheshimiwa Spika, tunaendelea na vikao vya Bunge la Bajeti na wakati tunaendelea na vikao hivi Mbunge mwenzetu yuko bado hospitalini Ubelgij na Ofisi ya Spika bado imeendelea kukataa kumlipia matibabu yake na haki zote za msingi ambazo ana-*qualify* kama wewe ambao tunafahamu Mungu amekusaidia umerudi hivi karibuni kutoka India ulipokuwa matibabu na *checkup*, lakini Serikali imegharamikia kila kitu chako.

Mheshimiwa Spika, leo Mbunge bado yuko hospitali Serikali haijaona wajibu na Wabunge tuko kwenye *comfort zone* kabisa *as if* kama hapo *Chief Whip* bado yuko hapo. Inawezekana jambo hilo halijatokea jana, lakini makusudi ya kutafuta upendo wa Mungu naomba vilevile ulitolee Mwongozo wako kwa nini wewe Serikali ina wajibu wa kugharamikia matibabu yako, lakini Mbunge aliyepigwa risasi Dodoma Serikali inashindwa kuwajibikia mambo hayo? (*Makofi*)

SPIKA: Mheshimiwa Jenista.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, VIJANA, AJIRA NA WENYE ULEMAVU: Mheshimiwa Spika, naomba Mwongozo, lakini ni Mwongozo unaohusu pia utaratibu. Kanuni ya 68(7) ambayo imekuwa ikitumika kuomba Mwongozo na ninaomba leo nisome. Inasema kwamba; "Halikadhalika Mbunge anaweza kusimama wakati wowote ambapo hakuna Mbunge mwingine anayesema na kuomba Mwongozo wa Spika kuhusu jambo ambalo limetokea Bungeni mapema."

Mheshimiwa Spika, nitarudia; "...kuhusu jambo ambalo limetokea Bungeni mapema ili Spika atoe ufafanuzi kama jambo hilo linaruhusiwa au hariruhiswi kwa mujibu wa Kanuni na taratibu za Bunge na majibu ya Spika yatatolewa papo hapo au baadaye kadri atakavyoona inafaa."

Mheshimiwa Spika, naomba kuomba Mwongozo wako kwa sababu kwa kadri tunavyoendelea na shughuli za Bunge imekuwa sasa ni mazoea fulani kila siku baada ya maswali Waheshimiwa Wabunge wamekuwa wakisimama kuomba miongozo kwa mambo haya ambayo hayapo kwa mujibu wa Kanuni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, na kiti chako kimekuwa kikiruhusu miongozo hiyo lakini nafikiri leo unisaidie Mwongozo wa Kiti kama miongozo hii ambayo sasa imekuwa ni utaratibu ndani ya Bunge huko kwa mujibu wa Kanuni tulizojiwekea. Naomba Mwongozo wako. *(Makofi)*

SPIKA: Nianze na hili la mwisho Wabunge walio wengi wamezingatia Kanuni hiyo Mheshimiwa Mussa Mborouk ameulizia kuhusu viwanja ambavyo haviyajengwa sambamba na swali ambalo lilikuwa kwa Wizara ya Mambo ya Nje ambalo aliuliza Mheshimiwa Masoud; Mheshimiwa Lubeleje aliuliza swali la *TASAF* sambamba na swali la leo la *TASAF* ambalo lilikuwa limeulizwa; Mheshimiwa Kangi Lugola aliuliza swali la linaloendana na swali la Mwalimu Bilago kuhusiana na masuala ya Mheshimiwa Polepole ambao linaendana na swali la leo na Mheshimiwa Aida Khenani aliuliza swali la wakulima ambalo linaendana na swali ambalo Mheshimiwa Waziri Mkuu alijibu kuhusiana na maswali ya wakulima na kadhalika. *(Makofi)*

Kwa hiyo, ambaye amekwenda kushoto zaidi ni Mheshimiwa Lema peke yake, kwa hiyo kwa kuwa ni mtu mmoja tu hatuwezi kusema kwamba kiti hiki sasa kinaruhusu mambo kinyume na utaratibu. *(Makofi)*

Lakini swali lake yeye japo ni mmoja ninalazimika kulipa nafasi kidogo kwa sababu kanituhumu mimi mwenyewe, kwa hiyo, nikitumia Kanuni kulizima lile swali nitaonekana sijatenda haki. Lakini nakushukuru sana Mheshimiwa Waziri wa Nchi kwa kutukumbusha mimi na wenzangu huenda jambo limekuwa likijitokeza wakati mwingine na mimi mwenyewe nakuwa sipo hapa, kwa hiyo nakushukuru sana kutukumbusha kwa hilo, hapana lazima

kukumbushana ndio wajibu hapa Bungeni hata sisi hapa mezani tunakosea lazima tukumbushwe. *(Makofi)*

Kwa hiyo, nianze na hoja ya Mheshimiwa Kangi Lugola yeye amependekeza kwa kweli kuna umuhimu kwamba je, kuna umuhimu wa Wabunge kupewa nakala ya Ilani ya Chama cha Mapinduzi ya 2015/2020 kwa sababu inaelekea kuna wengine ambao yaani wako wana *unaware* kabisa mimi nakubaliana na wewe Mheshimiwa Kange Lugola kabisa asilimia mia moja. *(Makofi)*

Kwa hiyo, Katibu angalia uwezekano wa kupatikana kwa nakala hizo kwa wakati muafaka na kama nakala hizo ni chache basi uhakikishe upande huo wa kushoto zimetosha kwanza ili waweze kuelewa Chama Tawala kimeahidi nini, isilete mkanganyiko. *(Makofi)*

Mengine yote tumejibu limebakia la Mheshimiwa Godbless Lema. Mheshimiwa Lema swali lako ni zuri, bahati mbaya tu unaliweka moja kwa moja ukinilinganisha na mimi mwenyewe na hili mmekuwa mkilifanya huko mara kadhaa. Nisikitike kidogo ukiwa unajenga hoja ijenge tu hoja isimame yenyewe kwa sababu hakuna asiyestahili au anayestahili sana, hayupo. Kwa hiyo, ukimjengea mtu hoja unamjengea mtu hoja yeye mwenyewe hata kama ni mwananchi hapati mshahara unamjengea tu hoja yeye mwenyewe kwa nini mwananchi wangu hajapata mshahara jamani, sio kwa nini hajapata mshahara wakati wewe Waziri mshahara unapata. Sasa kidogo si namna nzuri sana. *(Makofi)*

Nirudie tena kwamba nimekuwa sipendi sana swali hili kwa sababu mwenzetu yupo hospitalini, lakini kila mnavyonichokoza basi inabidi niwe nafunguka kidogo kidogo. Kuna aina mbili za namna ya matibabu ya Wabunge na wananchi wa Tanzania wote. Namna moja ni njia ya umma ya kufuata utaratibu wa umma ambao na sisi Wabunge tunahusika, sisi Wabunge tunayo kadi ile ya *NHIF*, ya matibabu. Kadi ile ni ya matumizi ya ndani ya nchi tu, ni bima ya afya ya hapa ndani ya nchi. Kadi ile sio bima ya afya ya kutibiwa popote duniani. *NHIF* haitibu watu nje ya

nchi, sisi ni Wabunge tunapaswa kulijua hilo, kwa wote!
Including mwenzetu aliyeko hospitali.

Utaratibu wetu katika nchi hii ni kwamba anaenda kutibiwa nje na hasa *specifically* Wabunge sasa lazima sisi Bunge ili *cheque* itoke hapa ili Mhasibu wa Bunge aandike *cheque* ni lazima pawepo na barua yenye kibali cha Hospitali ya Muhimbili kwamba mgonjwa huyu anahitajika rufaa tena wao watasema rufaa wapi, na pili awe na kibali cha Katibu Mkuu Wizara ya Afya au niseme cha Wizara ya Afya.

Cha tatu, ni suala la utaratibu pia kwa ninyi Wabunge *specifically* kwa kutibiwa nje lazima Spika nipate barua ya kibali ya Mheshimiwa Rais mwenyewe, nikishapata hivi vitatu ndipo Mhasibu wa Bunge anaweza kuandika *cheque* kwa Mbunge yeyote yule kwenda kutibiwa nje ya nchi.

Wakati Mheshimiwa Rais anafungua hili Bunge alikuja hapa alisimama hapa akaelezea jinsi ambavyo haridhishwi na utaratibu uliokuwepo kabla ambapo watu walikuwa wanaenda nje huko hovyohovyoko akaahidi Serikali yake katika miaka mitano inayokuja moja ya jambo atakalofanya ni *control* ya safari za nje za hovyoko. Kwa hiyo, huo ndio utaratibu, Mhasibu wa Bunge hawezi, Katibu wa Bunge hawezi akatoa pesa yoyote bila vibali hivyo vitatu. (*Makofi*)

Kwa hiyo, Mbunge yeyote ambaye anatibiwa huko nje na ni wengi tumesema sisi huwa hatuna tabia ya kutaja majina, lakini mkitaka siku moja mimi nitakuja na orodha hata iwe miaka mitano ya Wabunge wote ambao wametibiwa nje, wote hao kwa awamu hii wameenda kwa utaratibu huo, wote wana kibali cha Muhimbili, wana kibali cha Wizara ya Afya na wana kibali cha Mheshimiwa Rais vinginevyo *cheque* haindikwi.

Sasa Spika anaandikaje *cheque* kwa jambo hili la Mheshimiwa Tundu Lissu wakati utaratibu wake Mheshimiwa Lema wewe hukuwepo siku ile, wenzako walikuwepo walipoamua kwamba anapelekwa Nairobi walijua na walioamua mambo hayo ni pande mbili, aliyekuwepo akidai

kwamba ni mwakilishi wa familia, alikuwepo pale na mimi nikimuona na walikuwepo viongozi wako wa Kambi. Mheshimiwa Kiongozi wa Upinzani na Mheshimiwa Msigwa ambao wote wawili ni Wajumbe wa Tume ya Huduma za Bunge ambayo ndiyo inashughulia matibabu ya Wabunge, wote wawili. (*Makofi*)

Uamuzi wa kwenda Nairobi ulikuwa ni uamuzi wa rufaa binafsi na ndiyo maana nikasema kuna aina mbili, kuna aina ya umma na kuna aina ya pili sasa ya matibabu binafsi na hii ya matibabu binafsi wako Wabunge wengi tu hapa ambao wanaenda kwenye matibabu binafsi, wengi tu sina haja ya kuwataja majina lakini wengi tu. Naweza nikamtaja mmoja kwa sababu ni mtani wangu Mheshimiwa Charles Kitwanga, hata leo sijui yuko hapa au hayuko. Hata leo ameniandikia, mara ya mwisho alienda kutibiwa Ujerumani, ananiaga tu bwana mimi naenda zangu Ujerumani kwa tiba anaenda!

Yupo mtani wangu mwingine Mbunge wa hapa Mwadui, Mwadui panaitwaje lile jimbo lile, Jimbo ambalo Mgodu wa Mwadui upo, eeh Kishapu, Mbunge wa Kishapu! Alikuwa anatibiwa *South Africa* hapo amekaa karibu miezi miwili yeye mwenyewe ananitaarifu tu Mheshimiwa mimi naenda zangu *South Africa* anaenda, kwa sababu hajashughulika na haya mambo ya vibali anaenda yeye mwenyewe. Kwa hiyo, ni kuchagua *public route* au *private route*. Ninyi mlischagua *private route*! (*Makofi*)

Kwa hiyo, Mheshimiwa Lema, wewe niletee tu hiyo barua ya Wizara ya Afya na ya Muhimbili ikiwezekana lakini ya Rais inaweza kukusaidia kufanya kazi yake. Mambo mengine yote yatakuwa yamenyooka. Kwa hiyo, hii ya fulani, fulani ni mambo ambayo hayana maana wala hakuna yeyote anayebaguliwa na asimame hapa mtu yeyote ambaye aliwahi kwenda kwa utaratibu huo halafu akakosa kutibiwa na fedha za umma.

Mheshimiwa James hapa amerudi juzi tu kutoka matibabu. Kwa hiyo, hilo...

Mheshimiwa Heche ni vizuri ukamsikiliza mtu ukamuelewa, utaratibu ni utaratibu! Utaratibu ni kwa watu wote, hauna *exception!* (Makofi)

Kwa hiyo, tunawashukuru hata hivyo Wajerumani ambao wanamtibu Mheshimiwa Lissu kule Ubelgiji aliko kwa sababu hilo jambo aliniambia Balozi wa Ujerumani yeye mwenyewe. Kwa hiyo, tunashukuru pia kwa msaada huo ambao tunaupata. (Makofi)

Katibu tuendelee!

NDG. STEPHEN KAGAIGAI – KATIBU WA BUNGE:

HOJA ZA SERIKALI

Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019

SPIKA: Ahsante sana. Sasa Waheshimiwa nimpishe Mheshimiwa Zungu aje aendelee na shughuli.

Hapa Mwenyekiti (Mhe. Mussa A. Zungu) Alikalia kiti

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri wa Afya. (Makofi)

WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO: Mheshimiwa Mwenyekiti, kufuatia taarifa iliyowasilishwa na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii ndani ya Bunge lako tukufu ambayo imechambua bajeti ya Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, ninaomba sasa kutoa hoja kwamba Bunge lako likubali kupokea na kujadili taarifa ya utekelezaji wa kazi za Wizara kwa Mwaka 2017/2018 na vipaumbele vya Wizara kwa mwaka 2018/2019. Aidha, ninaliomba Bunge lako tukufu likubali kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Kawaida pamoja na Mpango wa Maendeleo wa Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto kwa mwaka 2018/2019.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kusimama mbele ya Bunge lako tukufu na kuwasilisha hotuba yangu siku ya leo.

Aidha, ninapenda kutumia fursa hii kwa heshima na unyenyekevu mkubwa kumshukuru kwa dhati Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa uongozi wake imara kwa nchi yetu na maelekezo yake ambayo yamekuwa dira sahihi katika utendaji wangu na katika kuimarisha huduma za afya na...

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri, ngoja kidogo.

Waheshimiwa Wabunge mnaotoka nje mtoke kwa nidhamu, kuna zogo kubwa sana na *Hansard* haipokei taarifa ya Mheshimiwa Waziri.

WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO: Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, ninampongeza Mheshimiwa Rais kwa kuendelea kuipa kioaumbele sekta ya afya ikiwemo kutoa msukumo mkubwa katiak uanzishwaji wa viwanda vya ndani vya dawa, vifaa na vifaatiba. Msukumo huu utaboresha huduma za afya kwa Watanzania kama nyenzo muhimu ili kufikia uchumi wa kati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa Mheshimiwa Mama Samia Suluhu Hassan, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuwa mstari wa mbele katika jitihada za kuboresha huduma za afya kwa Watanzania hasa katika mapambano dhidi ya ugonjwa wa kifua kikuu, afya ya mama na mtoto, magonjwa yasiyo ya kuambukiza pamoja na afya ya vijana. Wizara yangu itaendelea kutumia ushawishi, nasaha na uzoefu wake ili kuhakikisha Watanzania wanakuwa na afya njema na tunajenga jamii ya Watanzania yenye afya bora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kuchukua fursa hii kumshukuru Mheshimiwa Kassim Majaliwa, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa uongozi wake mahiri

unaosaidia kuleta tija na ufanisi katika utendaji na kuimarisha huduma zinazotolewa katika sekta ya afya. Aidha, ninampongeza kwa hotuba yake aliyoiwasilisha kwenye Bunge lako tukufu ambayo imetoa dira ya jinsi Serikali itakavyotekelza majukumu yake katika mwaka 2018/2019.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kumpongeza Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Naibu Spika na Wenyeviti wa Bunge kwa kusimamia vyema mijadala ndani ya Bunge. Aidha, kipekee ninapenda kuishukuru Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii chini ya uongozi mahiri wa Mwenyekiti Mheshimiwa Peter Serukamba na Makamu Mwenyekiti Mheshimiwa Juma Nkamia kwa ushauri na maelekezo waliyoyotoa wakati wa maandalizi ya bajeti hii.

Aidha, ninawashukuru Waheshimiwa Wbaunge wote kwa ushirikiano mzuri ambao wananipatia kwa maoni na ushauri katika kuboresha huduma za afya na maendeleo ya jamii. Ninawaahidi Waheshimiwa Wabunge wote kwamba Wizara yangu itazingatia ushauri wenu na kuendelea kuwapa ushirikiano katika kutekelza majukumu na kazi zetu za kuwatumikia wananchi ndani na nje ya Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninatoa pole kwa Watanzania wote waliopoteza ndugu, jamaa na marafiki zao kutokana na sababu mbalimbali ikiwa ni pamoja na magonjwa, ajali na majanga. Aidha, ninatoa pole kwa wagonjwa na majeruhi wa ajali waliopo hospitalini na majumbani pamoja na wahanga wa vitendo vya ukatili na unyanyasaji wa kijinsia. Ninamuomba Mwenyezi Mungu awaponye haraka ili waweze kuendelea na ujenzi wa Tanzania ya viwanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, ninapenda sasa kutoa maelezo kuhusu utekelezaji wa shughuli za Wizara kwa mwaka 2017/2018, vipaumbele vya Wizara kwa mwaka 2018/2019 pamoja na maombi ya fedha ambazo zitaiwezesha Wizara yangu kutekeleza majukumu yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kutekeleza majukumu yake, Wizara imeendelea kuzingatia sera, mipango mikakati pamoja na makubaliano ya Kitaifa na Kimataifa yenye lengo la kuimarisha utoaji wa huduma za afya ndhini, maendeleo ya wanawake na jinsia, haki, ulinzi na ustawi wa watoto na wazee.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2017/2018, kupitia Idara Kuu ya Afya Wizara yangu ilipanga kutekeleza afua mbalimbali zenye lengo la kuboresha utoaji wa huduma za afya kama nilivyoainisha katika aya ya 11 ya hotuba yangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kupitia Idara Kuu ya Maendeleo ya Jamii kazi zilizopangwa kutekelezwa kwa mwaka 2017/2018 nimeziainisha katika hotuba yangu aya ya 12.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa mapato na mtumizi, Fungu 52 - Afya hadi kufikia mwezi Machi 2018, Wizara pamoja na Taasisi zake imefanikiwa kukusanya kiasi cha shilingi bilioni 162.8 sawa na asilimia 72 ya lengo la mwaka. Katika mwaka wa fedha 2017/2018, Wizara iliidhinishwa na Bunge lako tukufu kupokea na kutumia jumla ya shilingi bilioni 1,077. Kati ya fedha hizo shilingi bilioni 785.8 sawa na asilimia 72.9 kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi kufikia Machi, 2018 Wizara imepokea jumla ya shilingi bilioni 617.5 sawa na asilimia 57 ya bajeti iliyoidhinishwa kwa ajili ya utekelezaji wa majukumu yake. Kwa upande wa miradi ya maendeleo hadi kufikia Machi, 2018 kiasi cha shilingi bilioni 400.7 kilipokelewa sawa na asilimia 51 ya fedha zilizoidhinishwa kutekeleza miradi ya maendeleo. Aidha, Wizara ilipokea kiasi cha shilingi bilioni 82.5 na kuzipeleka Ofisi ya Rais, TAMISEMI kwa ajili ya kukarabati vituo vya afya 139 ili viweze kutoa huduma za uzazi za dharura ikiwemo upasuaji wa kumtoa mtoto. Kati ya fedha hizo shilingi bilioni 63, tumezipata kutoka Benki ya Dunia na shilingi bilioni 19.5 tumezipata ikiwa ni

mchango wa Serikali ya Denmark na Mfuko wa Afya ya Pamoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa Idara Kuu ya Maendeleo ya Jamii - Fungu 53, Wizara ilitarajia kukusanya kiasi cha shilingi bilioni 2.1 kutoka vyanzo vilivyobainishwa. Hadi kufikia tarehe 31 Machi, 2018 jumla ya shilingi bilioni 1.7 sawa na asilimia 84 zilikusanywa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa mapokeo ya fedha, Wizara ilitengewa shilingi bilioni 37.9 na hadi kufikia tarehe 31 Machi jumla ya shilingi bilioni 18.3 sawa na asilimia 48 zilipokelewa. Kati ya fedha hizo, shilingi billion 1 sawa na asilimia 40 ni fedha za miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa nieleze utekelezaji wa majukumu wa kazi mbalimbali ambazo zimetokelezwa na Wizara kwa kipindi cha Julai, 2017 hadi Machi, 2018 kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa Idara Kuu ya Afya, tumetekeleza kazi mbalimbali lakini nitataja kazi chache za kipaumbele.

Kwa upande wa huduma za kinga, Wizara ilisimamia shughuli za utoaji wa chanjo kwa watoto ili kuhakikisha malengo yaliyowekwa Kitaifa na Kimataifa yanafikiwa. Takwimu za Januari hadi Desemba, 2017 zinaonesha kuwa asilimia 101.2 ya watoto wote waliolengwa nchini walipatiwa chanjo zote muhimu ili kuwakinga na magonjwa. Mnamo mwezi Desemba, 2017 nafurahi kulitaarifu Bunge lako tukufu kwamba Serikali ya Tanzania ilipongezwa na Shirika la Afya Duniani na wadau wa Kimataifa wa chanjo kwa kufikia kiwango cha juu cha chanjo kwa asilimia 97 kwa takwimu za mwaka 2016. Lengo la mkakati wa dunia kupitia Shirika la Afya Duniani ni nchi kufikia kiwango cha uchanjaji wa asilimia 90. Mikakati ya Wizara imeiwezesha nchi yetu kufikia kiwango cha asilimia 97 ambapo inakuwa nchi ya tatu Barani Afrika ikitanguliwa na Zambia yenye kiwango cha asilimia 99 ikifuatiwa na Rwanda yenye asilimia 98.

Mheshimiwa Mwenyekiti, saratani ya mlangowa kizazi ndiyo inaongoza nchini kwa kuwa na idadi kubwa ya wagonjwa na pia kusababisha vifo vya wanawake wengi. Kwa mujibu wa takwimu za Taasisi ya Saratani *Ocean Road* za mwaka 2016/2017 asilimia 32.8 ya wagonjwa wa saratani nchini ni wa saratani ya mlango wa kizazi ikifuatiwa na saratani ya matiti yenye asilimia 12.9.

Mheshimiwa Mwenyekiti, habari njema, saratani ya malngo wa kizazi inazuilika kwa kuwapatia chanjo wasichana wenye umri wa miaka tisa hadi miaka 14. Katika kukabiliiana na saratani hiyo, Serikali imeanza kutoa chanjo ya saratani ya mlango wa kizazi (*HPV Vaccine*) ambapo kwa mwaka 2018 tumeanza kuwachanja wasichana wenye umri wa miaka 14 ambapo hadi Desemba tunalenga kuwafikia wasichana 616,734 wa umri huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutumia Bunge lako tukufu kusema kwamba chanjo hii ni salama na inatumika katika nchi mbalimbali za Afrika ikiwemo Rwanda, Uganda, Afrika Kusini, Zambia na Lesotho. Kupitia Bunge lako tukufu nawasihi wazazi na walezi wenye watoto kuhakikisha binti zetu wanapata chanjo hiyo muhimu ili kuwakinga dhidi ya ugonjwa wa saratani ya mlango wa kizazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa afya na usafi wa mazingira, tumeendelea kuratibu utekelezaji wa Sheria ya Afya ya Jamii pamoja na kuendesha kampeni ya Taifa ya usafi wa mazingira inayotekelezwa katika Halmashauri zote nchini, shughuli zilizotekelezwa zimeainishwa katika aya ya 22 mpaka 24 ya hotuba yangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee nitambue na kuzipongeza Halmashauri zilizofanya vizuri katika masuala ya afya na usafi wa mzingira. Kwa upande wa Halmashauri za Miji ni Halmashauri ya Mji wa Njombe, Halmashauri ya Kahama na Halmashauri ya Tunduma. Kwa upande wa Halmashauri za Majiji ni Halmashauri ya Moshi, Halmashauri ya Arusha na Halmashauri ya Iringa. Kwa upande wa Halmashauri za Wilaya ni Halmashauri ya Wilaya ya Meru,

Halmashauri ya Wilaya ya Njombe na Halmashauri ya Wilaya ya Makete.

Mheshimiwa Menyekiti, Wizara yangu imetoa zawadi ya gari jipya aina ya Nissan kwa Halmashauri ya Meru kwa kufanya vizuri katika kampeni hii lakini pia tumetoa trekta la kubebea taka kwa Halmashauri ya Mji wa Njombe kwa kuchukua nafasi ya pili. Tumetoa pikipiki kwa vijiji vitatu vilivyofanya vizuri. Kijiji cha Kanikele katika Halmashauri ya Wilaya ya Njombe, Kijiji cha Nambala katika Halmashauri ya Meru DC na kijiji cha Lihalalo katika Halmashauri ya Njombe DC.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie fursa hii kutoa rai kwa viongozi wote wa mkoa kulfanya suala la afya na usafi wa mzingira ikiwemo kupambana na ugonjwa wa kipindupindu kuwa ni ajenda ya kudumu katika vipaumbele vyao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa afya ya uzazi, mama na mtoto Wizara imeendelea kutekeleza mpango mkakati wa miaka mitano wa mwaka 2016 hadi 2020 unaolenga kuboresha afya ya uzazi, mama, watoto vijana pamoja na kupunguza vifo vitokanvyo na uzazi kufikia 292 kwa kila vizazi hai 100,000 ifikapo mwaka 2020.

Katika kutekeleza mkakati huu Wizara imezingatia maeneo makuu matatu ambayo ni huduma ya uzazi wa mpango, huduma wakati wa ujauzito na huduma wakati wa kujifungua. Kwa upande wa huduma za uzazi wa mpango Wizara imenunua na kusambaza dawa za uzazi wa mpango katika vituo vya kutolea huduma za afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia, Wizara inaendelea kuhakikisha kwamba huduma kwa wanawake wajawazito zinapatikana sambamba na kuelimisha wajawazito kuhudhuria kliniki. Kulingana na taarifa tulizozipokea kutoka vituo vya kutolea huduma za afya hadi kufikia mwezi Februari, 2018 asilimia 81 ya wajawazito walihudhuria kliniki angalau mara moja. Lengo letu ni kufikisha asilimia 70 ya

wajawazito wanaohudhuria kliniki angalau mara nne katika kipindi cha ujauzito wao ifikapo mwaka 2020.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie Bunge lako tukufu kuwahimiza wanawake wajawazito wote kuhudhuria kliniki kama inavyoshauriwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara kwa kushirikiana na wadau imeendelea kuhamasisha na kuhimiza wajawazito kujifungulia katika vituo vya kutolea huduma za afya. Muelekeo wa takwimu za hadi mwezi Machi 2018 inaonesha kwamba kuna ongezeko la wajawazito wanaojifungulia katika vituo vya afya kufikia asilimia 68.5 kutoka asilimia 64 mwaka 2015/2016. Napenda kutoa wito kwa wanawake wajawazito wote nchini wajifungulie kwenye vituo vya kutolea huduma za afya ili kupunguza vifo na changamoto za uzazi kwa mama na mtoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara kwa kushirikiana na wadau wa maendeleo imeendelea kuboresha miundombinu ya kutoa huduma za afya katika ngazi ya vituo vya afya ili viweze kutoa huduma za uzazi za dharura ikiwemo upasuaji wa kumtoa mtoto tumboni pia mama mjamzito anapojhitajika. Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais TAMISEMI inaboresha vituo vya afya takriban 208 ili kuwezesha kutoa huduma za simo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maboresho yanahusu ujenzi wa vyumba vya upasuaji, wodi za akina mama wajawazito, vyumba vya maabara na nyumba za watumishi. Kukamilika kwa maboresho hayo kutaongeza idadi ya vituo vya afya vya Serikali vinavyotoa huduma za upasuaji wa dharura kufikia asilimia 53.7 kutoka asilimia 21 mwezi Juni, 2016. Haya ni mafanikio makubwa sana kwa upande wetu sekta ya afya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeendelea pia kusogeza huduma za kupima na matibabu ya mabadiliko ya awali ya saratani ya mlango wa kizazi na saratani ya matiti ambapo tumeanzisha vituo vipya 100 vya uchunguzi na tiba ya

mabadiliko ya awali ya saratani ya mlango wa kizazi katika mikoa ya Mbeya, Mwanza, Songwe, Geita, Dodoma, Singida, Manyara, Arudha, Tanga, Lindi, Mtwara, simiyu, Mara na Ruvuma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa udhibiti wa udhibiti wa ugonjwa wa UKIMWI, hadi kufikia Desemba, 2017 watu wapatao milioni 5.1 walipimwa VVU na kupewa majibu ya hali zao za afya ambapo watu 145,000 sawa na asilimia 2.8 kati yao waligundulika kuwa na maambukizi ya VVU na kuanzishiwa dawa za kufubaza Virusi vya UKIMWI.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, takwimu za hadi Desemba zinaonesha kuwa jumla ya watu wanaoishi na VVU wapatao 565,000 walikuwa wanatumia dawa za kufubaza VVU ikiwa ni sawa na asilimia 69 ya watu milioni 1.4 wanaokadiriwa kuishi na virusi vya UKIMWI. Wizara imeendelea na kazi za kuzuia maambukizi ya VVU kutoka kwa mama kwenda kwa mtoto ambapo jumla ya akina mama wajawazito milioni 1.9 sawa na asilimia 98.7 walipatiwa huduma za ushauri nasaha na upimaji wa VVU. Kati ya akina mama hao akina mama 79,242 sawa na asilimia nne waligundulika kuwa wanaishi na VVU.

Mheshimiwa Mwenyekiti, habari njema akina mama 79,240 sawa na asilimia 99.9 ya wenye maambukizi ya VVU walipatiwa dawa kwa ajili ya kufubaza virusi vya UKIMWI. Hivi sasa maambukizi ya VVU kutoka kwa mama kwenda kwa mtoto ni asilimia 4.9 kutoka asilimia 12 mwaka 2011.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeendelea na jitahada za kudhibiti ugonjwa wa kifua kikuu na ukoma ambapo tumenunua na kusambaza dawa za kifua kikuu na ukoma, lakini kubwa tumezindua matumizi ya dawa mpya ya kifua kikuu kwa watoto. Dawa hizi mpya ni za mseto ulioboreshwa zina ladha nzuri ya matunda, zinayeyuka kwa urahisi zikiwekwa kwenye maji na hivyo hazihitaji kukatwakatwa ili kupata dozi sahihi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeongeza pia wigo wa upatikanaji wa huduma za ugunduzi wa kifua kikuu kwa kutumia vipimo vya vina saba ambapo tumenunua na kusambaza mashine za *genexpert* 189 ikilinganishwa na mashine 66 zilizosambazwa mwaka 2015. Mashine hizi zimesambazwa katika hospitali zote za rufaa za kanda, mikoa, wilaya na baadhi ya vituo vikubwa vya afya. Teknolojia ya mashine hizi inatuwezesha kupata majibu ya *TB* ndani ya masaa mawili badala ya kusubiri kwa zaidi ya saa 24 kama ilivyo kwa njia za kawaida za hadubini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kudhihirisha azma ya Serikali kushirikiana na sekta binafsi katika mapambano dhidi ya ugonjwa wa kifua kikuu ili kuongeza wagonjwa wanaogundulika kutoka asilimia 40 hadi 70. Wizara imenunua mashine za *genexpert* tano na kuzipatia hospitali binafsi za Aga Khan, Hebert Kairuki, Regency Medical Center, TMJ na Hindu Mandal kila mashine yenye thamani ya shilingi milioni 38. Tumeanza na hospitali hizi kwa kuwa zina viwango vikubwa vya wagonjwa wanaohudumiwa na pia kwa kuzingatia kwamba walikuwa tayari kushirikiana na Serikali katika kutoa huduma za kifua kikuu bure na hivyo kuwezesha malengo ya Serikali ya Awamu ya Tano ya kuhakikisha tunawafikia wananchi wote wanaogua ugonjwa wa kifua kikuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na jitihada hizi mchango wa sekta binafsi katika kuibua wagonjwa wa kifua kikuu umeonekana kumekuwa na ongezeko la wagonjwa wanaoibuliwa na sekta binafsi kutoka wagonjwa 3,476 hadi kufikia wagonjwa 7,281 katika mwaka 2017. Nitumie fursa hii kuwashukuru kwa dhiti na kuwapongeza sekta binafsi kwa kushiriki katika kutokomeza kifua kikuu nchini kwetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, malaria imeendelea kuwa sababu ya vifo vya Watanzania wengi ambapo kwa takwimu za Januari hadi Desemba jumla ya watu milioni 5.5 waliugua ugonjwa wa malaria, kati yao wagonjwa 4,421 walifariki kutokana na ugonjwa wa malaria. Wizara yangu imeendelea kutekeleza shughuli mbalimbali za udhibiti wa malaria ikiwa

ni pamoja na kununua dawa, vifaa na kuvisambaza katika vituo vya kutolea huduma za afya. Pia tumesambaza jumla ya vyandarua milioni 4.7 kwa jamii bila malipo kupitia wanafunzi shuleni na kupitia kliniki za wajawazito na watoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeendelea kutekeleza afua za kudhibiti magonjwa yaliyokuwa hayapewi kipaumbele ambapo nimeainisha katika hotuba yangu aya ya 48 na 49. Habari njema ni kwamba Halmashauri 93 zimefanikiwa kupunguza kiwango cha maambukizi ya ugonjwa wa matende na mabusha na hivyo tumeziondoa kwenye orodha ya Halmashauri zenye maambukizi makubwa. Haya ni mafanikio makubwa kwa sababu watazania takribani milioni 20.4 wanaoishi katika Halmashauri sasa hawapo tena katika hatari ya kupata maambukizi ya magonjwa ya matende na mabusha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa huduma za lise tumeendelea kushirikiana na wadau kutekeleza hatua mbalimbali ikiwemo kutoa matone ya nyongeza ya vitamini A kwa watoto na dawa za minyoo kwa watoto. Pia tumeendelea kuongeza idadi ya hospitali zinazotoa matibabu ya utapiamlo, kuboresha miundombinu za hospitali kwenye wodi za kulaza wagonjwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeendelea kuelimisha na kuhamasisha jamii kupenda na kutunza afya zao pamoja na kufanya uchunguzi wa afya mara kwa mara. Kwa upande wa huduma za tiba ningependa kujikita katika maeneo makubwa matatu. Eneo la kwanza ni usajili na usimamizi wa vituo vya kutolea huduma ambapo Wizara imeendelea kusajili na kusimamia vituo vya kutoa huduma za afya na hadi kufikia Machi, 2018 vituo vya kutolea huduma za afya vimeongezeka kutoka 7,284 hadi kufikia 7,437.

Aidha, katika kipindi hiki pia tumeendelea na kazi ya kuimarisha huduma za matibabu ya kibingwa na lengo ni kuboresha huduma hizi ili kuhakikisha Watanzania wanapata matibabu ya kibingwa, lakini kubwa ni kupunguza idadi ya wagonjwa wanaopewa rufaa ya matibabu nje ya nchi. Hadi

kufikia mwezi Juni, 2018 idadi ya wagonjwa waliopewa rufaa ya matibabu nje ya nchi ilipungua na kufikia wagonjwa 103 kilinganishwa na wagonjwa 304 mwaka 2017.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mafanikio haya ni kutokana na maboresho makubwa yaliyofanyika katika hospitali zetu, Hospitali ya Taifa Muhimbili, Taasisi ya Mifupa, Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete, Taasisi ya Saratani ya *Ocean Road* na Hospitali ya Benjamin Mkapa. Hospitali zetu 10 ikiwemo Hospitali ya Kibong'oto na hospitali za rufaa za kanda ya Mbeya, KCMC na Bugando zimehudumia wagonjwa takribani milioni moja na elfu tisini na mchanganuo nimeuonesha katika kiambatanisho namba mbili cha hotuba yangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa Hospitali ya Taifa ya Muhimbili kazi kubwa ambayo ilifanyika ni ukarabati wa jengo la kutolea huduma za upandikazaji wa figo na ununuzi wa vifaa kwa ajili ya huduma za upandikazi wa figo ambayo mgonjwa mmoja aliweza kupata huduma hii mwezi Novemba, 2017.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nirekebishe hotuba yangu kwamba nilisema wagonjwa watano wamepangwa kupatiwa huduma hii mwishoni mwa mwezi Aprili, 2018 lakini nitumie Bunge lako tukufu kuliarifu kwamba, jana Hospitali yetu ya Taifa Muhimbili imeweza kupandikiza figo kwa wagonjwa wanne na haya ni mafanikio makubwa katika nchi yetu na tunategemea sasa kila mwezi tutapandikiza figo wagonjwa watano kila mwaka. Hatua hii imepunguza gharama za kupandikiza figo kwa mgonjwa mmoja nje ya nchi kutoka wastani wa shilingi milioni 100 hadi milioni 20. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hospitali yetu ya Muhimbili pia imeanzisha huduma za upandikazaji wa vifaa vya kusaidia kusikia kwa lugha ya kitaalam *cochlea implants*, ambapo hadi kufikia Machi, 2018 watoto 11 walipata huduma ya kuwekewa vifaa vya usikivu. Huduma hii sasa inatolewa kwa wastani wa shilingi milioni 36 kulinganisha na shilingi milioni 80

hadi milioni 100 ambapo zingetumika endapo mgonjwa angepelekwa nje ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba pia nifanye marekebisho katika aya ya 58 ya hotuba yangu watoto waliofanyiwa upandikizaji wa vifaa vya kusikia sasa hivi ni 11 badala ya watoto sita. Taasisi ya Mifupa Muhimbili Moi imeendelea kufanya kazi ya upasuaji wa mifupa na mishipa ya fahamu ikiwepo upasuaji wa mgongo kwa njia ya matundu kwa kushirikiana na madaktari wa Hospitali ya BLK India. Lengo ni kujenga uwezo wa ndani na hivyo kupunguza rufaa za wagonjwa. Pia tumekamilisha ujenzi wa Jengo la Moi Awamu ya III kwa gharama ya shilingi bilioni 16.5.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Taasisi ya Moyo ya Jayaka Kikwete imeendelea kufanya kazi kubwa na nzuri kwa ajili ya Watanzania ambapo sasa huduma kwa wagonjwa wenye matatizo ya moyo zinapatikana nchini. Hivi sasa taasisi ina uwezo wa kutoa huduma za upasuaji za ubingwa wa hali ya juu kwa asilimia 85 kwa huduma ambazo hapo awali zilikuwa zikipatikana nje ya nchi. Tunawapongeza sana kwa kuendelea kuwa taasisi ya mfano katika Afrika Mashariki na Afrika ya Kati na hiyo imewezesha sasa wagonjwa wanaopelekwa nje ya nchi kwa ajili ya matibabu ya moyo kupungua kutoka wagonjwa 43 hadi wagonjwa 12 mwaka 2018. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, taasisi yetu ya Saratani ya *Ocean Road* imeendelea kuboresha huduma kwa wagonjwa wa saratani hasa kwa kutoa tiba ya mionzi, kwa kutibu wagonjwa 70 kutoka wagonjwa 30 kwa siku. Lakini taasisi inakamilisha kufunga mashine za tiba mpya na za kisasa za mionzi aina ya *Linear Accelerator* na *CT Simulator* ambazo zimenunuliwa kwa gharama ya shilingi bilioni 5.5. Mashine hizi zitaiwezesha *Ocean Road* sasa kutoa huduma za matibabu ya mionzi na kupunguza muda wa wagonjwa kusubiri tiba kutoka wiki sita hadi kufikia wiki mbili na hivyo kuongeza ufanisi katika matibabu ya saratani. Pia *Ocean Road* imeanzisha huduma za wodi binafsi ambayo ina vitanda vinne vya *VIP* hatua hii ni kutaka kuhakikisha

wagonjwa wenye uwezo wa kulipia wanapata huduma bila tatizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Hospitali yetu ya Benjamin Mkapa - Dodoma imeendelea kutoa huduma za matibabu ya kibingwa ambapo na wenyewe tarehe 22 Machi kwa kushirikiana na *TOKUSHIKAI Medical Group* kutoka Japan ilifanikiwa kufanya upandikizaji figo kwa mara ya kwanza kwa mgonjwa mmoja mwenye umri wa miaka 51; hali ya mgonjwa inaendelea vizuri na amepewa ruhusa ya kurudi nyumbani. Pia Benjamin Mkapa wameanzisha huduma za chumba cha wagonjwa mahututi na upatikanaji wa dawa ni asilimia 95.2.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Hospitali ya Mirembe imeendelea kutoa huduma kwa wagonjwa wa afya ya akili ambapo pia hali ya upatikanaji wa dawa imefikia asilimia 90. Hospitali ya Rufaa ya magonjwa ya Kifua Kikuu Kibong'oto imeendelea kutoa huduma za utambuzi na matibabu ya kifua kikuu, kifua kikuu sugu, VVU na magonjwa mengine ambapo pia imeweza kutoa elimu kwa wataalam 239 kutoka mikoa mbalimbali kwa ajili ya kuwajengea uwezo wa kuanzisha matibabu ya kifua kikuu sugu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Hospitali yetu ya Rufaa Kanda ya Nyanda za Juu Kusini Mbeya imeendelea kuboresha huduma zake ikiwemo kuongeza miundombinu ya kutolea huduma za afya kama nilivyoainisha katika aya ya 82 ya hotuba yangu. Upatikanaji wa dawa katika hospitali hii ni kwa kiwango cha asilimia 95.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Hospitali ya Rufaa ya Kanda ya Ziwa imeendelea kutoa huduma za kibingwa kwa wagonjwa kutoka mikoa nane ya Kanda ya Magharibi na Kanda ya Ziwa ambayo ni Mwanza, Geita, Mara, Kagera, Simiyu, Kigoma, Shinyanga na Tabora. Hospitali ilifanya upasuaji katika magonjwa mbalimbali ikiwemo magonjwa ya saratani, saratani ya tumbo, saratani ya pua lakini pia imetoa huduma za matibabu ya mionzi kwa wagonjwa wa saratani ya mlango wa kizazi.

Vilevile hospitali imenunua mashine mbili za vipimo vya moyo na mashine ya *CT Scan* kwa gharama ya shilingi bilioni 1.7.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Hospitali ya Rufaa ya Kanda ya Kaskazini - KCMC imeendelea kuboresha na kutoa huduma kwa wananchi wa mikoa ya Kilimanjaro, Arusha, Manyara na Tanga ambapo hospitali imeweza kuwahudumia wagonjwa zaidi ya 1,100 wa saratani ambapo wagonjwa 47 walipewa huduma shufaa. Uendeshaji wa hospitali za rufaa za mikoa ulikuwa ukisimamiwa na kuratibiwa na Ofisi ya Rais TAMISEMI. Hata hivyo Mheshimiwa Rais Dkt. John Pombe Magufuli alitoa maelekezo tarehe 25 Novemba, 2017 ambapo sasa usimamizi na uendeshaji wa hospitali hii upo chini ya Wizara ya Afya. Hospitali za rufaa za mikoa zilizopo ni 28 na katika kipindi cha kutoa taarifa hii jumla ya wagonjwa milioni 1.6 walihudumiwa katika hospitali zetu za rufaa 28.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara imeweka mikakati ya muda mfupi, muda wa kati na muda mrefu ili kuhakikisha kwamba huduma za kibingwa za upasuaji (*general surgery*), magonjwa ya wanawake na watoto, magonjwa ya watoto. Magonjwa ya ndani, magonjwa ya kinywa na meno na radiolojia zinatolewa katika hospitali zetu zote za rufaa za mikoa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeendelea na jitihada za kudhibiti magonjwa yasiyo ya kuambukiza kwa sababu utafiti wa viashiria vya magonjwa yasiyo ya kuambukizwa uliofanywa na wataalamu unaonesha kwamba asilimia 26 ya wananchi ni wanene kupita kiasi; asilimia 29 ya wananchi wanalehemu nyingi mwilini; asilimia 33.8 ya wananchi wana mafuta mengi mwilini; asilimia 9.1 wana kisukari na asilimia 25.9 wana shinikizo kubwa la damu. Utafiti pia ulionyesha kwamba asilimia 25 ya wananchi waliohojiwa hawajishughulishi na shughuli mbalimbali ikiwemo kufanya mazoezi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mapambano dhidi ya magonjwa yasiyo ambukiza yamejikita katika kinga kuliko tiba

kwa kutumia kauli mbiu ya “Afya yangu mtaji wangu” ambayo ilizinduliwa na Mheshimiwa Makamu wa Rais Mama Samia Suluhu Hassan, lengo ni kuhimiza wananchi kufanya mazoezi mara kwa mara kupima afya na kujiepusha na visababishi vinavyosababisha magonjwa yasiyo ya kuambukiza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie fursa hii kulipongeza Bunge lako tukufu kwa kuanzisha Jukwaa la Waheshimiwa Wabunge wa kupambana na magonjwa yasiyo ya kuambukiza na tunaamini kwamba mtaenda kutoa elimu kwa wananchi ya kujikinga na kuwaelimisha juu ya magonjwa yasiyo ya kuambukiza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, upatikanji wa damu salama wizara kupitia mpango wa Taifa wa damu salama umeendelea kukusanya kuhifadhi na kusambaza damu salama katika vituo vya kutolea huduma za afya ambapo zimekusanywa jumla ya chupa 233,000 sawa na asilimia 101 ya lengo la makusanyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie Bunge lako tukufu kuwashukuru wananchi wote wanaojitolea kuchangia damu, aidha, nitoe rai kwa watazania kuchangia damu mara kwa mara ili kuokoa maisha ya wananchi hasa wanawake wajawazito na watoto wa umri wa chini ya miaka mitano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, upatikanaji wa dawa, vifaa na vifaa tiba umeendelea kuimarika hadi kufikia asilimia 81 katika dawa muhimu 135. Pia hali ya upatikanaji wa dawa katika vituo vya kutolea huduma za afya ni asilimia 92 na dawa za ARVs zinapatikana kwa asilimia 92 hadi asilimia 100.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumetekeleza pia agizo la Mheshimiwa Rais la kuhimiza uzalishaji wa ndani wa dawa ambapo tulifanya kikao na wadau takribani 430 na wawekezaji 38 wamejitokeza na kuonesha nia ya kuwekeza katika uzalishaji wa dripu, uzalishaji wa bomba za sindano, uzalishaji wa dawa na uzalishaji wa pamba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeendelea pia kuhakiki ubora wa huduma za afya katika vituo vya kutolea huduma za afya katika kipindi cha Julai, 2017 hadi Machi, 2018 wizara ilifanya zoezi la tathmini ya mara ya pili ya kutoa nyota kulingana na ubora kwa vituo vya kutolea huduma za afya katika mkoa 14. Matokeo yanaonyesha vituo 180 sawa na asilimia 4.7 vilipata nyota sifuri kulinganisha na vituo 1244 sawa na asilimia 33 ambapo vilipata nyota sifuri mwaka 2016. Mwaka 2017 vituo 749 sawa na asilimia 19.4 vilipata nyota tatu kulinganisha na vituo 62 sawa na asilimia mbili vilivyopata nyota tatu mwaka 2016. Matokeo haya yanaonyesha kazi nzuri ya Mheshimiwa Rais Dkt. John Pombe Magufuli ya kuwekeza katika huduma za afya na hivyo kuimarika kwa ubora wa huduma za afya katika vituo vya afya na zahanati na hospitali za wilaya ambako ndiko wananchi wetu wengi wanapata huduma za afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, rasilimali watu katika sekta ya afya; tumeendelea kusimamia ubora wa mafunzo ya kada za afya zisizo katika kiwango cha shahada. Pia tumetoa ufadhili wa mafunzo ya kibingwa kwa watumishi wa afya ikiwemo watumishi 376 ambao wanalipiwa na Wizara katika ngazi ya shahada ya uzamili hususani Madaktari Bingwa katika fani za kipaumbele za upasuaji magonjwa ya wanawake na wazazi, magonjwa ya watoto, magonjwa ya ndani na radiolojia. Pia tulipata kibali cha ajira kutoka Ofisi ya Rais, Utumishi ambapo watumishi 3,152 walijajiwa na kusambazwa katika Hospitali za Wizara ya Afya na Vituo vya Afya vya Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeendelea kuboresha mazingira ya kazi kwa watumishi wa afya ambapo katika kipindi hiki nyumba 30 za watumishi wa afya zimejengwa katika Mkoa wa Manyara, Halmashauri za Kiteto nyumba 10, Simanjiro nyumba 10 na Hanang nyumba 10. Na umekamilisha mradi ambao ulikuwa unafadhiliwa wa *Global Fund* wa kujenga nyumba 480.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bila fedha hakuna utoaji bora wa huduma za afya, hivyo Serikali ipo katika hatua za

kuhakikisha inafikia malengo ya afya kwa wote (*Universal Health Coverage*) ambapo kila mwananchi atakuwa na uhakika wa upatikanaji wa huduma bora za afya bila kuwa na kikwazo cha fedha. Lengo letu ifikapo 2020 asilimia 70 ya wananchi wote wawe wamejiunga na mifuko ya Bima ya Afya. Hivi sasa ni asilimia 32 tu ya Watanzania ambao wako katika mfumo wa bima ya afya na hivyo kupata changamoto za kupata huduma bora za matibabu. Nitoe rai kwa Waheshimiwa Wabunge wenzangu kwa nafasi zenu na ushawishi mkubwa mlionao katika jamii tunayoishi kuendelea kuwashawishi wananchi umuhimu wa kujiunga na kuchangia katika Mfuko wa Bima ya Afya ili waweze kupata huduma za matibabi bila kikwazo cha fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais - TAMISEMI imeanza utekelezaji wa azimio la kupeleka fedha moja kwa moja katika vituo vya kutolea huduma za afya (*direct health facility financing*) badala ya kuzipeleka kwenye Halmashauri. Jumla shilingi bilioni 45.7 zimepokelewa na kupelekwa katika vituo 5170. Hatua imechangia kuboresha upatikanaji wa fedha katika vituo kwa wakati na kusaidia vituo kupanga mikakati ya kuboresha huduma na kuleta ufanisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimezungumzia pia teknolojia ya Habari na Mawasiliano, ikiwemo uzinduzi wa Mpango wa Uwekezaji katika Habari, Mawasiliano na Teknolojia (*Digital Health Investment Recommendation Roadmap*) ambao tumeshirikiana na taasisi ya *Bill and Melinda Gates Foundation* kwa ajili ya kuboresha taarifa za huduma za afya pamoja na umuhimu wakukusanya taarifa na matumizi sahihi ya taarifa ya afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utekelezaji wa majukumu ya taasisi zilizo chini ya Idara Kuu ya Afya; nimezungumza kuhusu utendaji wa Bohari Kuu ya Dawa na kubwa ni kuanza utekelezaji wa kununua dawa kutoka moja kwa moja kwa wazalishaji na hatua hii imepunguza bei ya dawa kwa wastani wa 40%, lakini Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya umeendelea kutekeleza mikakati mbalimbali ili kuongeza

wigo wa wanufaika wa Bima ya Afya nchini na tumeonesha kazi zilizofanyika katika hotuba yangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mamlaka ya Chakula na Dawa imeendelea na kazi ya kudhibiti ubora, ufanisi wa dawa, chakula na vifaa tiba vinavyoingizwa na kuzalishwa ndani ya nchi, lakini mamlaka imeendelea na utoaji wa elimu kwa umma kwa makundi mbalimbali kuhusu madhara ya dawa, vipodozi hatarishi na usalama wa chakula pamoja na jumbe fupi zilizorushwa kupitia redio/luninga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkemia Mkuu wa Serikali ameendelea kuhakikisha kwamba, anafanya kazi zake kwa kuzingatia sheria, lakini tumeingia mkataba wa kununua mitambo na vifaa vya maabara vyenye thamani ya bilioni 1.4, ili kuweza kuhakikisha kazi inayofanywa na mkemia inaleta matokeo yanayotarajiwa. Taasisi ya Chakula na Lishe imeendelea kutekeleza majukumu mbalimbali katika kuimarisha utoaji wa huduma za lishe nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara yangu kupitia Taasisi ya Uchunguzi wa Magonjwa ya Binadamu – *NIMR*, imeendelea kutekeleza majukumu yake ya utafiti. Tafiti zilizofanyika ikiwemo majaribio ya chanjo ya UKIMWI, tiba mbadala, afya ya mama na mtoto, malaria na *TB* na matokeo ya tafiti hizi yamesaidia Wizara yangu kuandaa afua mbalimbali za kuboresha huduma za afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nieleze sasa kazi kubwa zilizofanywa chini ya Idara Kuu ya Maendeleo ya Jamii; kazi kubwa zilizofanywa ni pamoja na uwezesaji wanawake kiuchumi ambapo Wizara iliendelea kuratibu na kusimamia Mfuko wa Maendeleo ya Wanawake katika kipindi cha Julai hadi Disemba Halmashauri 170 zimechangia bilioni 7.9 ikilinganishwa na bilioni 8.9 zilizochangiwa mwaka 2016/2017. Na ninaomba nirekebishe hotuba yangu, aya ya 16, badala ya Halmashauri 130 isomeke Halmashauri 170.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara kwa kushirikiana na wadau wakiwemo *SIDO*, Mfuko wa Fursa Sawa kwa Wote

na Baraza la Taifa, iliwezesha ushiriki wa wanawake katika Maonesho ya Biashara ya Kimataifa, wanawake wajasiriamali 1,185 lakini kupitia Benki ya Wanawake tumeendelea kutoa mikopo kwa wajasiriamali 6,237 mikopo yenye thamani ya jumla ya shilingi bilioni 10.1. Kwa upande wa maendeleo ya jamii tumeendelea kuamsha ari ya wananchi kushiriki katika miradi ya maendeleo na kazi zimefanyika katika mikoa 11 ambayo nimeiainisha katika hotuba yangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara imeendelea kusimamia na kuratibu uzalishaji wa wataalam wa maendeleo ya jamii kutoka katika vyojo nane vya maendeleo ya jamii ya Buhare, Mlale, Misungwi, Lungemba, Mabugai, Ruaha, Uyole na Monduli ambapo wanafunzi 1,588 walidahiliwa ikilinganishwa na wanafunzi 3,248. Kwa upande wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali Wizara yangu imeendelea na kazi ya kusajili Mashirika Yasiyo ya Kiserikali ambapo mashirika 192 yalisajiliwa na mashirika 4,868 yalifanyiwa uhakiki na kuchukua hatua kwa ajili ya kuboresha uratibu na usimamizi mzuri katika masuala ya uwezi, taarifa za pesa na uwajibikaji kwa jamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa haki na maendeleo ya mtoto, ukatili dhidi ya watoto bado ni tatizo kubwa katika nchi yetu. Takwimu za Jeshi la Polisi za mwaka 2016 zinaonesha kwamba matukio ya ukatili dhidi ya watoto yalikuwa 13,457 ikilinganishwa na matukio 10,551 mwaka 2016. Katika kukabiliana na tatizo hili, Wizara kwa kushirikiana na wadau tunaendelea kutekeleza mpango kazi wa Taifa wa kutokomeza ukatili dhidi ya wanawake na watoto, hasa kwa kutoa elimu kuhusu athari za mila na desturi zenye madhara kwa watoto, ikiwemo ukeketaji, mimba na ndoa za utotoni kwa makundi mbalimbali ya jamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara imeendelea kusimamia utoaji wa huduma za malezi, makuzi na maendeleo ya awali ya watoto walio chini ya umri wa miaka mitano ambapo vituo vya kulelea watoto mchana 139 vilisajiliwa, lakini tumeendelea kuzalisha wataalam wa malezi, makuzi na maendeleo ya awali ya mtoto katika

Chuo cha Ustawi wa Jamii Kisangala. Kwa upande wa huduma za ustawi kwa watoto, Wizara imeendelea kuhakikisha upatikanaji wa huduma za msingi ikiwemo, malazi, matunzo na ulinzi kwa watoto walio katika mazingira hatarishi 6,132 katika makao ya watoto 157 yanayoendeshwa na taasisi za dini, mashirika ya watu binafsi na Serikali. Pia tumetoa leseni 14 za usajili wa makao ya watoto, lengo la Serikali ni kuhakikisha watu wote ambao wanatoa huduma za makazi ya watoto walio katika mazingira hatarishi, basi wanajisajili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeendelea pia kutoa huduma kwa watoto walio katika mkinzano na sheria katika mahabusu tano za watoto za Mbeya, Moshi, Tanga, Arusha na Dar es Salaam, lakini pia watoto walio katika mkinzano na sheria waliweza kupata huduma za msingi iliwemo chakula, malazi, ikiwa ni pamoja na msaada wa kisheria. Wizara kwa kushirikiana na Wizara ya Katiba na Sheria imewachepusha watoto 126 kutoka katika mfumo rasmi wa haki jinai kwa kuwarekebisha tabia na kuwaunganisha na familia zao ikilinganishwa na watoto 72.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeendelea pia kusimamia upatikanaji wa huduma za msingi kwa wazee wasiojiweza katika makazi yetu 17 yanayomilikiwa na Serikali, lakini kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais, TAMISEMI tumewezesha wazee 506,000 kupata vitambulisho vya matibabu bure katika kipindi hiki ikilinganishwa na wazee 74,000 waliopata vitambulisho vya matibabu bure mwaka 2016/2017.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeendelea kupitia Baraza la Usuluhishi wa Ndoa lililopo chini ya usimamizi wa Kamishna wa Ustawi wa Jamii na Ofisi za Ustawi wa Jamii tumeendelea kutoa huduma za usuluhishi wa migogoro ya ndoa na mashauri ya matunzo kwa watoto.

Katika kipindi cha Julai, 2017 hadi Machi, 2018 jumla ya mashauri ya migogoro ya ndoa 13,382 yalipokelewa na kufanyiwa usuluhishi ikilinganishwa na mashauri ya migogoro ya ndoa 4,400.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia Wizara imeendelea kufanyia kazi mashauri ya matunzo kwa watoto, mashauri ya matunzo kwa watoto 11,815 yalipokelewa. Kati ya mashauri haya 4,900 yalihu matunzo ya watoto walio ndani ya migogoro ya ndoa na 5,708 watoto waliozaliwa nje ya ndoa. Kati ya mashauri yaliyopokelewa mashauri 10,600 yalikalika kuwezesha huduma kwa watoto na mashauri 1,142 yalipewa rufaa kwenda mahakamani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa kazi zilizotekelezwa chini ya Idara Kuu ya Maendeleo ya Jamii, Taasisi za Idara Kuu ya Maendeleo ya Jamii ni Taasisi ya Maendeleo ya Jamii Tengeru ambayo ilidahili jumla ya wanafunzi 1,167 lakini pia, taasisi imefanya tafiti katika maeneo mbalimbali kuhusu ustawi na maendeleo ya jamii. Taasisi ya Ustawi wa Jamii Kijitonyama imeendelea kutoa mafunzo katika ngazi ya cheti, diploma na stahhada.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuseme hayo, sasa niseme, kama nilivyosema kazi zilizotekelezwa ni nyingi na zipo katika hotuba yangu, lakini kwa sababu ya muda niruhusu nizungumzie vipaumbele vya Wizara kwa mwaka 2018/2019. Kwa upande wa Idara Kuu ya Afya tumejiwekea vipaumbele vikubwa vifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kuimarisha huduma za chanjo kwa watoto ili kuendelea kubaki katika viwango vya juu vya utoaji wa huduma za chanjo, ili kuwaepusha watoto na magonjwa yanayoweza kuepukika kwa chanjo; pili, kuimarisha huduma za kinga dhidi ya magonjwa yanayotokana na kutizingatia kanuni za usafi na usafi wa mazingira, kama magonjwa ya kuhara, kuhara damu na kipindupindu kwa kuongeza uhamasishaji na usimamizi wa usafi na usafi wa mazingira; tatu, kuimarisha huduma za kinga dhidi ya magonjwa yasiyo ya kuambukiza kama magonjwa ya moyo, kisukari na saratani; nne, kuimarisha huduma za afya ya uzazi na mtoto, ili kupunguza vifo vya wanawake na watoto vinavyotokana na uzazi; tano kupunguza maambukizi ya malaria, TB na VVU UKIMWI; sita, kuimarisha upatikanaji wa damu salama ikiwa ni pamoja na ujenzi wa

vituo vya kukusanyia damu; saba, kuimarisha upatikanaji wa dawa vifaa na vifaa tiba; nane, kuimarisha huduma za matibabu ya kibingwa nchini katika hospitali zetu za rufaa na mikoa, hospitali za rufaa za kanda, hospitali maalum na hospitali za kitaifa na tisa, kuimarisha ubora wa huduma za afya zinazotolewa katika vituo vya afya vinavyomilikiwa na Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumi, ni kuboresha vyuo vya mafunzo, kuimarisha mifumo ya habari, takwimu na teknolojia ili kurahisisha upatikanaji wa takwimu sahihi katika sekta ya afya. Kipaumbele kingine ni kuimarisha mfumo wa ugharamiaji wa huduma za afya kwa kuongeza idadi ya Watanzania ambao wana bima za afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kutekeleza vipaumbele hivi nimeeleza katika hotuba yangu kuanzia aya ya 199 mpaka 205 kazi kubwa zitakazotekelezwa, lakini nitaje kazi chache; kwanza ni kununua na kusambaza chanjo za watoto, ikiwemo chanjo ya kuwakinga wasichana na saratani ya mlango wa kizazi ambapo tumetenga shilingi bilioni 30. Lakini kuongeza wigo na kasi ya uibuaji wa matibabu kwa wagonjwa wa kifua kikuu katika mikoa yote nchini ambapo tumetenga fedha za ndani bilioni tano; kukarabati na kujenga wodi maalum kwa ajili ya watoto wachanga katika hospitali za rufaa za mikoa saba ya Dar es Salaam, Katavi, Geita, Rukwa, Kilimanjaro, Iringa na Kigoma, ambapo tumetenga shilingi milioni 900; kupanua wodi za wazazi na kutenga vyumba vya wagonjwa mahututi wanaotokana na uzazi na mnaweza mkauliza kwa nini, kwa sababu, ndio kipaumbele cha Waziri wa Afya. Kwa hiyo, katika hospitali zetu za rufaa za mikoa tutakuwa na vyumba vya wagonjwa mahututi wanaotokana na uzazi katika hospitali za rufaa za mikoa ya Mbeya, Shinyanga, Morogoro, Pwani na Kigoma ambapo tumetenga shilingi bilioni moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kuimarisha upatikanaji wa damu salama kwa kujenga vituo vya kukusanyia damu katika mikoa 12 ya Manyara, Katavi, Rukwa, Ruvuma, Njombe, Tanga, Arusha, Pwani, Singida, Songwe, Geita,

Simiyu, ambapo tumetenga shilingi bilioni 4.3. Lakini pia kununua dawa zamalaria kwa ajili ya akinamama wajawazito na kununua dawa za kuokoa maisha ya wamama wajawazito, ambapo tumetenga shilingi bilioni 8.5. Kununua na kusambaza vitanda vitanda, magodoro, mashuka na vitanda vya kuzalia, ambapo tumetenga shilingi bilioni 4.9 kuimarisha hali ya upatikanaji wa dawa kwa kununua na kusambaza katika vituo vyote vya Serikali ambapo tumetenga shilingi bilioni 270.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuendelea na huduma za kupandikiza figo katika Hospitali ya Taifa ya Muhimbili na Hospitali ya Benjamin Mkapa ambapo, tumetenga jumla ya shilingi bilioni 20; kuendelea kutoa huduma za matibabu ya kibingwa ikiwemo upandikizaji wa vifaa vya kusaidia kusikia kwa kuweka *cochlea implant* katika Hospitali ya Taifa Muhimbili, kuimarisha matibabu ya moyo katika Taasisi ya Moyo ya *JKCI* na upasuaji wa mifupa katika Taasisi ya Moi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kununua na kusimika vifaa vya kisasa vya uchunguzi wa matibabu ya saratani (*pet scan*) katika taasisi ya saratani ya *Ocean Road* ambapo tumetenga kiasi cha shilingi bilioni 14.5. lakini tutaendelea kumaliza jengo katika hospitali ya rufaa ya kanda ya Mbeya, ikiwemo kusimika *X-Ray Machine*, ambapo tumetenga shilingi bilioni tano; kununua *ambulance* 27 kwa ajili nya kuimarisha mfumo wa rufaa nchini, kufanya ukarabati katika hospitali za rufaa za mikoa, ambapo tumetenga shilingi bilioni 20; kuendelea na ujenzi wa hospitali za rufaa za mikoa ambayo haina hospitali hizo ambayo ni Mikoa ya Simiyu, Geita, Katavi, songwe, Mara, Njombe ambapo tumetenga shilingi bilioni 10 na kufanyia ukarabati vyuo vya afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa Idara Kuu ya Maendeleo ya Jamii tumepanga kutekeleza vipaumbele vifuatavyo; kukuza usawa wa jinsia na uwezeshaji wanawake kiuchumi, kuimarisha upatikanaji wa haki na huduma za ustawi wa jamii kwa wazee na watoto, kuwezesha utekelezaji wa Mpango wa Taifa wa Kutokomeza Ukatili dhidi ya wanawake na watoto, kuboresha mazingira ya kufundishia

na kujifunzia katika Taasisi ya Maendeleo ya Jamii Tengeru na Taasisi ya Ustawi wa Jamii Kijitonyama, kuboresha makazi ya wazee, makao ya Taifa ya watoto na mahabusu za watoto na shule za maadisho. Kuweka mazingira wezeshi, ili mashirika yasiyo ya kiserikali kuchangia katika kuleta maendeleo ya Taifa na pia kuamsha ari ya wananchi kushiriki katika shughuli za maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi zitakazotekelezwa nimeonesha katika aya ya 206 mpaka 213 ya hotuba yangu, kwa upande wa kukuza usawa wa jinsia na uwezesaji wanawake kiuchumi tumetenga milioni 416. Ukarabati wa majengo katika vyuo vya maendeleo ya jamii vya Uyole, Mlale na Misungwi tumetenga milioni 550, kukarabati makazi ya wazee, Bukumbi, Mwazange na Misufini ambapo tumetenga milioni 450, kukamilisha ujenzi wa mahabusu ya watoto Mtwara ambapo kiasi cha shilingi milioni 500 kimetengwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuimarisha ulinzi wa mtoto ambapo shilingi bilioni 1.8 zimetengwa; kuimarisha hali ya upatikanaji wa huduma za msingi kwa wazee wasiojiweza na watoto walio katika mazingira hatarishi na watoto walio katika mkinzano na sheria ambapo kiasi cha shilingi bilioni moja kimetengwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuwasilisha vipaumbele vya Wizara napenda kuchukua fursa hii ya kipekee kuzishukuru nchi wahisani za Denmark, Canada, Ireland, Uswis na Korea Kusini pamoja na mashirika ya maendeleo ya kimataifa ya *UNICEF* na Benki ya Dunia kwa kutoa misaada katika Mfuko wa Pamoja wa Afya ambao umesaidia kwa kiasi kikubwa kuboresha huduma za afya. Pia shukrani ziende kwa Shirika la Afya Duniani (*WHO*), *Global Vaccine Alliance (GAVI)* na *Global Fund* kwa mchango wao katika kutekeleza mikakati ya sekta ya afya.

Aidha, napenda kuzishukuru nchi za China, Cuba, Hispania, India, Italia, Japan, Marekani, Misri, Sweden, Uingereza, Ujerumani na Ufaransa ambazo zimeendelea kusaidia sekta ya afya kwa njia mbalimbali. Nayashukuru

mashirika ya kimataifa na yasiyo ya kimataifa yanayofanya kazi pamoja na Wizara yangu pamoja na wadau wa maendeleo.

Katika utendaji wa kazi zangu nimepata ushrikiano mkubwa kutoka kwa viongozi na wafanyakazi wa Wizara ya Afya. Napenda kumshukuru Mheshimiwa Dkt. Faustine Ndugulile, Naibu Waziri kwa ushrikiano anaonipa katika kutekeleza majukumu yangu. Nawashukuru sana Dkt. Mpoki Ulisubisya - Katibu Mkuu Afya na Bibi Sihaba Nkinga - Katibu Mkuu Maendeleo ya Jamii kwa mchango wao. Namshukuru sana Profesa Mohamed Bakari Kambi, Mganga Mkuu wa Serikali kwa kunilea vyema na mimi naonekana kama *bush doctor* siku hizi, lakini nawashukuru sana Makamishna, Wakurugenzi na Wakuu wote wa Vitengo vya Wizara. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee na kwa unyenyekevu mkubwa namshukuru Mkurugenzi wa Hospitali ya Taifa Muhimbili, Profesa Lawrance Museru, Mkurugenzi wa Hospitali ya Moyo ya Jakaya Kikwete, Profesa Mohamed Janabi na Mkurugenzi wa Taasisi ya Mifupa Muhimbili (*MOI*) Dkt. Respicious Boniface kwa kazi nzuri, pamoja na Dkt. Julius Mwaisalage wa Taasisi ya Saratani ya *Ocean Road*. Pia nawashukuru Wakurugenzi wa Hospitali za Kibong'oto, Mkurugenzi wa Hospitali ya Afya ya Akili Mirembe, Mkurugenzi wa Hospitali ya Rufaa Kanda Mbeya, *KCMC* na Mkurugenzi wa Rufaa ya Kanda ya Bugando na Mkurugenzi wa Benjamin Mkapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru, anasema sijamtaja, nimemshukuru Katibu Mkuu Mawendeleo ya Jamii; nawashukuru Taasisi zote na Waganga Wakuu wa Mikoa na Wilaya, Waganga Wafawidhi wa Hospitali, Vituo vya Afya na Zahanati na Wakuu wa Mafunzo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, natoa shukrani kwa sekta zote ambazo tunashirikiana nazo katika kutoa huduma za afya, maendeleo ya jamii na ustawi wa jamii. Nawaasa waendeleo kuzingatia misingi ya huduma bora na kufanya kazi kwa bidii. Nawapenda sana watoa huduma wote wa

afya, madaktari, wauguzi, wafamasia, wataalam wa maabara na wote ambao waafanya kazi kwa uadilifu na kujituma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie fursa hii kipekee kuishukuru kwa dhati familia yangu, akiwemo mume wangu Paschal Richard kwa upendo na uvumilivu na kunitia moyo katika kutekeleza majukumu yangu ya kitaifa. Aidha, napenda kuwashukuru wananchi wote wa Mkoa wa Tanga kwa ushirikiano wanaoendelea kunipatia katika kuuendeleza mkoa wetu. Naahidi kwamba nitaendelea kuwatumikia Wana-Tanga kwa akili na nguvu zangu zote ili kuleta maendeleo katika Mkoa wetu wa Tanga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa niombe fedha; kwa upende wa Fungu 52 – Idara Kuu ya Afya; Wizara imekadiria kukusanya mapato ya shilingi bilioni 240,042,508,157; kati ya fedha hizo shilingi 220,267,010,057 zitakusanywa katika mashirika na taasisi zilizo chini ya Wizara na shilingi 19,775,498,100 ni kutoka makao makuu. Kwa upande wa Matumizi ya Kawaida kwa mwaka 2018/2019 Wizara inakadiria kutumia kiasi cha shilingi 304,473,476,000 kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida, kati ya fedha hizo, shilingi 88,465,756,000 zitatumika kwa ajili ya Matumizi Mengineyo na shilingi 216,007,720,000 zitatumika kwa ajili ya mishahara ya watumishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa Miradi ya Maendeleo, Fungu 52; Wizara inakadiria kutumia shilingi 561,759,999,000 kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo; kati ya hizo, fedha za ndani ni shilingi 184,959,999,000 na fedha za nje ni shilingi 376,800,000,000. Jumla ya Makadirio ya Bajeti kwa mwaka 2018/2019 kwa Fungu 52 ni shilingi 866,233,475,000.

Kwa upande wa Fungu 53 – Idara Kuu ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto; Mapato Wizara kwa mwaka 2018/2019 inakadiria kukusanya shilingi 3,090,796,000 kutokana na ada za wanafunzi kutoka vyuo nane vya Maendeleo ya Jamii na Chuo cha Ustawi wa Jamii Kisangara na ada ya usajili wa mashirika yasiyo ya Kiserikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, matumizi kwa mwaka 2018 kwa Fungu 53 inakadiriwa kuwa shilingi 32,140,649,000. Kati ya makadirio haya, matumizi ya kawaida ni shilingi 27,226,800,000 na miradi ya maendeleo ni shilingi 4,913,845,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, matumizi ya kawaida katika mwaka 2018 Fungu 53 Wizara inakadiriwa kutumia kiasi cha shilingi 27,226,804,000. Kati ya fedha hizo shilingi 15,116,962,000 ni mishahara ya watumishi na shilingi 12,109,842,000 ni matumizi mengineyo. Kwa upande wa miradi ya maendeleo Wizara inakadiriwa kutumia shilingi 4,913,845,000 kwa ajili ya miradi ya maendeleo. Kati ya fedha hizo shilingi 1,500,000,000 ni fedha za ndani na shilingi 3,413,845,000 ni fedha za nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jumla kuu ya fedha inayoombwa kwa Fungu 53 kwa mwaka 2018/2019 ni shilingi 32,140,649,000. Jumla kuu ya fedha ambayo ninaomba kwa heshima na taadhima Bunge lako Tukufu lipitishwe kwa ajili ya mafungu yote mawili kwa mwaka 2018/2019 ni shilingi 898,374,124,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hotuba yangu inapatikana katika tovuti za Wizara ya Afya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto kama tulivyoonesha katika kitabu changu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naomba kutoa hoja. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante na hongera kwa kazi nzuri unayoifanya wewe na Naibu wako. Hoja imeungwa mkono.

HOTUBA YA WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO, MHE. UMMY A. MWALIMU (MB), KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA FEDHA KWA MWAKA 2018/2019 - KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI

A: UTANGULIZI

1. **Mheshimiwa Spika**, kufuatia taarifa iliyowasilishwa na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma na

Maendeleo ya Jamii ndani ya Bunge lako Tukufu, ambayo imechambua Bajeti ya Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, ninaomba kutoa hoja kwamba sasa Bunge lako likubali kupokea na kujadili Taarifa ya Utekelezaji wa Kazi za Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto kwa mwaka 2017/18 na Vipaumbele vya Wizara kwa mwaka 2018/19. Aidha, ninaliomba Bunge lako Tukufu likubali kupitisha Makadirio na Mapato ya Matumizi ya Kawaida pamoja na Mpango wa Maendeleo ya Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto kwa mwaka 2018/19.

2. Mheshimiwa Spika, kwanza napenda kumshukuru Mwenyenzi Mungu kwa kuniwezesha kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu na kuwasilisha hotuba yangu siku ya leo. Aidha, ninapenda kutumia fursa hii kwa heshima na unyenyekevu mkubwa kumshukuru kwa dhati **Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli**, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa uongozi wake imara kwa nchi yetu na maelekezo yake ambayo yamekuwa dira sahihi katika utendaji wangu na katika kuimarisha huduma za Afya na Maendeleo ya jamii nchini.

Aidha, ninampongeza Mheshimiwa Rais kwa kuendelea kuipa kipaumbele Sekta ya Afya kwa kutoa msukumo mkubwa katika uanzishwaji wa viwanda vya kutengeneza Dawa, Vifaa, Vifaa Tiba na Vitendanishi hapa nchini. Msukumo huo utaboresha huduma za afya kwa watanzania kama nyenzo muhimu ili kufikia Uchumi wa Kati.

3. Mheshimiwa Spika, ninapenda kutoa shukrani za dhati kwa **Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan**, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuwa mstari wa mbele katika jitihada za kuboresha huduma za afya kwa Watanzania hasa katika mapambano dhidi ya Kifua Kikuu, Afya ya Mama na Mtoto, magonjwa yasiyo ya kuambukiza pamoja na Afya ya Vijana. Wizara yangu itaendelea kutumia ushauri, nasaha, ushawishi na uzoefu wake ili kuhakikisha watanzania wanaweza kujikinga na maradhi na kujenga jamii ya Watanzania wenye Afya Bora.

4. *Mheshimiwa Spika*, ninaomba kuchukua fursa hii kumshukuru **Mheshimiwa Majaliwa Kassim Majaliwa (Mb)**, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa uongozi wake mahiri unaosaidia kuleta tija na ufanisi katika utendaji na kuimarisha huduma zinazotolewa katika Sekta ya Afya. Aidha, ninampongeza kwa hotuba yake aliyoiwasilisha kwenye Bunge lako tukufu ambayo imetoa dira ya jinsi Serikali itakavyotekeleza majukumu yake katika mwaka 2018/19.

5. *Mheshimiwa Spika*, ninapenda kukupongeza wewe binafsi kwa kuendelea kutekeleza majukumu yako kwa weledi katika kuliongoza Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Aidha, ninampongeza **Mheshimiwa Dkt. Tulia Ackson (Mb)** katika utekelezaji wa majukumu yake. Vilevile, nitumie fursa hii kuwapongeza Wenyeviti wa Bunge kwa kusimamia vyema mijadala ndani ya Bunge.

6. *Mheshimiwa Spika*, ninapenda kumshukuru **Mheshimiwa Selemeni Jaffo (Mb)** Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, kwa ushirikiano wake ulioniwezesha kusimamia na kuboresha utoaji wa huduma za afya ngazi ya msingi. Pia, ninawashukuru Mawaziri wa Wizara nyingine zote ambazo ushirikiano wao na Wizara yangu umechangia katika utoaji wa huduma za afya na maendeleo ya jamii.

7. *Mheshimiwa Spika*, kipekee ninapenda kuishukuru Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii, chini ya Mwenyekiti wake **Mheshimiwa Peter Serukamba (Mb)**, na Makamu Mwenyekiti, **Mheshimiwa Juma Nkamia (Mb)** kwa ushauri na maelekezo waliyoyotoa wakati wa maandalizi ya Bajeti hii. Aidha ninawashukuru Waheshimiwa Wabunge wote kwa ushirikiano mzuri wanaonipatia ikiwemo kutoa ushauri na maoni mbalimbali yenye lengo la kuboresha huduma za afya na maendeleo ya jamii nchini. Ninawaahidi kwamba, Wizara yangu itazingatia ushauri wao na kuendelea kuwapa ushirikiano katika kutekeleza majukumu na kazi zetu za kuwatumikia wananchi ndani na nje ya Bunge.

8. Mheshimiwa Spika, ninatoa pole kwa watazania wote, waliopoteza ndugu, jamaa na marafiki zao kutokana na sababu mbalimbali ikiwa ni pamoja na magonjwa, ajali na majanga. Aidha, ninatoa pole kwa wagonjwa na majeruhi wa ajali waliopo hospitalini na majumbani pamoja na wahanga wa vitendo vya ukatili na unyanyasaji wa kijinsia. Ninamuomba Mwenyezi Mungu awaponye haraka ili waweze kuendelea na ujenzi wa Tanzania ya Viwanda.

9. Mheshimiwa Spika, Baada ya kusema hayo, ninapenda sasa kutoa maelezo kuhusu utekelezaji wa shughuli za Wizara kwa mwaka 2017/18, Vipambebe vya Wizara kwa mwaka 2018/19 pamoja na maombi ya fedha ambazo zitaiwezesha Wizara yangu kutekeleza majukumu yake.

B: MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA BAJETI NA MPANGO WA MAENDELEO KWA MWAKA WA FEDHA 2017/18

10. Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza majukumu yake, Wizara imeendelea kuzingatia Sera, Mipango Mikakati pamoja na makubaliano ya Kitaifa na Kimataifa yenye lengo la kuimarisha utoaji wa huduma za afya nchini. Maeneo haya ya vipambebe yameainishwa katika Dira ya Taifa ya Maendeleo (2025), Mpango wa Maendeleo wa Muda wa Kati 2016/17 – 2020/21, Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi (CCM) ya 2015-2020, na Malengo ya Maendeleo Endelevu (SDG's 2030). Aidha, Wizara imezingatia vipambebe vilivyoainishwa katika Sera ya Afya (2007) na Mpango Mkakati wa IV wa Sekta ya Afya (2015 – 2020); Sera ya Maendeleo ya Jamii (1996); Sera ya Maendeleo ya Wanawake na Jinsia (2000); Sera ya Taifa ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali (2001); Sera ya Wazee (2003); na Sera ya Maendeleo ya Mtoto (2008); Mkataba wa Kimataifa wa Kuondoa Aina Zote za Ubaguzi Dhidi ya Wanawake (1979); na Mkataba wa Haki za Mtoto (1989)

11. Mheshimiwa Spika, Katika mwaka wa fedha 2017/18, kupitia **Fungu 52**, Wizara yangu kwa kushirikiana na Wizara nyingine, Idara na Taasisi za serikali, Wakala wa Serikali na Wadau wa Maendeleo ilipanga kutekeleza afua mbalimbali

zenye lengo la kuboresha utoaji huduma za Afya katika maeneo yafuatayo;

a) Kuimarisha Huduma za Kinga, Tiba, na kuongeza usawa katika kutoa huduma za afya,

b) Kuimarisha huduma za afya ya uzazi na mtoto ili kupunguza vifo vya wanawake wajawazito na watoto,

c) Kuimarisha upatikanaji wa dawa, vifaa, vifaa tiba, vitendanishi na chanjo katika vituo vya kutolea huduma za afya,

d) Kuimarisha miundombinu kwenye vyuo vya mafunzo ya afya kwa lengo la kuongeza udahili na upatikanaji wa rasilimali watu,

e) Kuimarisha matibabu ya kibingwa nchini kwa kuendeleza ujenzi, upanuzi, ukarabati wa miundombinu na kufunga mitambo ya kisasa ya kutolea huduma za afya katika Hospitali ya Taifa Muhimbili, Taasisi ya Mifupa Muhimbili (MOI), Taasisi ya Moyo Jakaya Kikwete (JKCI), Hospitali ya Benjamini Mkapa - Dodoma, Taasisi ya Saratani Ocean Road, Hospitali Maalum za Mirembe na Kibong'oto; pia Hospitali za Rufaa za Kanda; Kanda ya ziwa (Bugando), Kanda ya Kaskazini (KCMC), Hospitali ya Rufaa ya Nyanda za Juu Kusini (Mbeya) na Kanda ya Kusini (Mtwara),

f) Kuimarisha mazingira ya ubia na ushirikiano kati ya Serikali na Sekta binafsi (PPP) katika utoaji wa huduma za afya,

g) Kuimarisha huduma za lishe na upatikanaji wake katika jamii na vituo vya kutolea Huduma za Afya,

h) Uimarishaji wa matumizi ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) katika kuboresha huduma za afya.

i) Kuhamasisha wananchi kujiunga na Mifuko ya Bima za Afya kwa lengo la kuhakikisha wananchi wote wanapata huduma za afya zenye uhakika.

12. Mheshimiwa Spika, kupitia **Fungu 53**, Idara Kuu ya Maendeleo ya Jamii, Wizara ilipanga kutekeleza kazi zifuatazo:

a) Kuratibu utekelezaji na ufuatiliaji wa Mpango wa Taifa wa Kutokomeza Ukatili Dhidi ya Wanawake na Watoto wa mwaka 2017/18 – 2021/22, kwa kutoa elimu kwa jamii na watoa huduma kwa waathirika wa ukatili kwa wanawake na watoto, uimarishaji wa Kamati za Ulinzi wa Wanawake na Watoto; Kuendeleza kampeni ya kukomesha ndoa za utotoni na mimba za utotoni katika mikoa yenye kiwango kikubwa cha ukatili ya Katavi, Shinyanga, Mara, Dodoma, Singida, Simiyu na Geita;

b) kuimarisha upatikanaji wa haki, maendeleo na ustawi watoto ikiwemo kwa watoto walio katika mkinzano wa Sheria;

c) Kuwezesha wazee wasiojiweza na watoto walio katika mazingira hatarishi kupata huduma za msingi;

d) Kuhamasisha jamii kushiriki katika shughuli za kujiletea maendeleo kwa kuzingatia rasilimali walizonazo;

e) kuelimisha jamii hususan wanawake na katika ngazi ya Halmashauri kujunga na VICOBA na SACCOS kwa ajili ya kuwawesha kiuchumi;

f) Kuwezesha utoaji wa huduma za ustawi wa jamii katika makazi ya wazee, Makao ya Taifa ya Watoto Kurasini, mahabusu za watoto na Shule ya Maadilisho; na

g) Kuboresha mazingira ya kujifunzia na kufundishia katika vyuo na Taasisi za maendeleo na ustawi wa jamii.

Mapato na Matumizi ya Fedha – Fungu 52

13. Mheshimiwa Spika, Wizara yangu kupitia **Fungu 52** (Afya), hukusanya mapato yake kupitia huduma za tiba zitolewazo na hospitali zilizo chini yake, tozo za huduma

katika Taasisi mbalimbali, Bodi na Mabaraza, ada za uchangiaji wa gharama za mafunzo, marejesho ya masurufu, malipo ya ununuzi wa vitabu vya maombi ya zabuni, pamoja na makusanyo yatokanayo na utoaji wa huduma katika Taasisi na Mashirika yaliyo chini ya Wizara. Hadi kufikia mwezi Machi 2018, Wizara pamoja na Taasisi zake imefanikiwa kukusanya kiasi cha Shilingi **162,891,572,942** sawa na **asilimia 72** ya lengo la mwaka la kukusanya kiasi cha Shilingi **227,041,160,573** kutoka kwenye vyanzo mbalimbali vya mapato. Mafanikio haya yametokana na utaratibu wa kulipia huduma kupitia benki, uhamasishaji kuhusu kulipa maduhuli ya serikali, uhibititi wa makusanyo, kuongezeka kwa ari ya utendaji kazi, uboreshwaji wa huduma za Bima na Kuimarishwa kwa mfumo wa malipo kwa njia ya Ki-elektroniki.

14. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2017/2018 Wizara iliidhinishiwa na Bunge lako Tukufu kupokea na kutumia jumla ya **Shilingi 1,077,701,892,000**. Kati ya fedha hizo kiasi cha **Shilingi 291,895,940,000** sawa na **asilimia 27** ya bajeti yote ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida, na shilingi ni **Shilingi 785, 805, 952,000** sawa na **asilimia 72.9** kwa ajili ya utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo.

15. Mheshimiwa Spika, Hadi kufikia Machi 2018, Wizara imepokea jumla ya **Shilingi 617,507,623,167** sawa na **asilimia 57** ya bajeti iliyoidhinishwa ya **Shilingi 1,077,701,892,000** kwa ajili ya utekelezaji wa majukumu ya Wizara. Aidha fedha zilizopokelewa kwa ajili ya matumizi ya kawaida katika kipindi cha Julai hadi Machi, 2018 ni **Shilingi 216,736,325,825,824** sawa na **asilimia 74** ya fedha zote zilizotengwa kwa ajili ya matumizi ya kawaida kwa mwaka. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 68,814,900,939** zilitumika katika Matumizi Mengineyo (OC) ikiwa ni sawa na **asilimia 73.3** ya kiasi kilichotengwa na **shilingi 147,921,424,885** zilitumika kulipia mishahara (Fungu 52) sawa na **asilimia 65** ya kiasi cha fedha kilichotengwa. Aidha, Wizara imepokea kiasi cha shilingi 22,500,000,000 kwa ajili ya kulipa madeni ya wazabuni na matibabu nje ya nchi.

Kwa upande wa **Miradi ya Maendeleo**, hadi kufikia Machi, 2018 kiasi cha **Shilingi 400,771,297,343** kilipokelewa, sawa na **asilimia 51** ya fedha zilizoidhinishwa kutekeleza Miradi ya Maendeleo. Kati ya fedha hizo, kiasi cha **Shilingi 79,756,079,206** ni fedha za ndani sawa **asilimia 24** ya fedha iliyoidhinishwa. Fedha za nje zilizopokelewa ni **Shilingi 321,015,218,137.12** sawa na **asilimia 71** ya fedha zilizoidhinishwa. Aidha Wizara ilipokea kiasi cha **Shilingi 82,515,009,463.82** na kuzipeleka **OR-TAMISEMI** kwa ajili ya ukarabati wa vituo vya kutolea huduma za afya ili viweze kutoa huduma za dharura ikiwa ni pamoja na upasuaji wa akina akinamama wajawazito (CEmONC) ili kumtoa mtoto tumboni pindi wanapokabiliwa na uzazi pingamizi. Kati ya fedha hizo **Shilingi 63,015,009,462.82** ni kutoka Benki ya Dunia na **shilingi 19,500,000,000.00** kutoka Mfuko wa Afya wa Pamoja (Health Basket Fund).

Mapato na Matumizi - Fungu 53

16. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2017/18, Wizara kupitia Fungu 53 (Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto), ilitarajia kukusanya kiasi cha **Shilingi 2,101,874,000** kutokana na ada za wanafunzi kutoka katika Vyuo nane vya Maendeleo ya Jamii vya Buhare, Uyole, Rungemba, Mlale, Misungwi, Ruaha, Mabughai na Monduli; uuzaji nyaraka za zabuni na ada mbalimbali za Mashirika Yasiyo ya Kiserikali. Hadi kufikia tarehe 31 Machi, 2018 jumla ya **Shilingi 1,775,466,155** sawa na **asilimia 84** zilikusanywa.

17. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2017/18, Wizara kupitia Fungu 53 ilitengewa jumla ya **Shilingi 37,909,880,000**. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 19,142,252,240** ni bajeti ya Mishahara, **Shilingi 16,161,349,760** ni Matumizi Mengineyo na **Shilingi 2,606,278,000** ni kwa Miradi ya Maendeleo. Hadi kufikia tarehe 31 Machi, 2018, jumla ya **Shilingi 18,352,527,400** sawa na **asilimia 48** zilipokelewa. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 8,848,331,727** sawa na **asilimia 55** ni Matumizi Mengineyo; **Shilingi 8,470,927,127** sawa na **asilimia 44** ni Mishahara ya Idara pamoja na Taasisi zilizo chini ya Wizara; na **Shilingi 1,033,268,546** sawa na **asilimia 40** fedha za Miradi ya Maendeleo.

18. Mheshimiwa Spika, Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara kwa kipindi cha Julai 2017 hadi Machi 2018 ulikuwa kama ifuatavyo:

**UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU CHINI YA IDARA KUU YA AFYA
HUDUMA ZA KINGA
Chanjo**

19. Mheshimiwa Spika, Katika kipindi cha Mwaka 2017/2018, Wizara ilitibu ununuzi wa chanjo Rota; dozi **2,383,700** kwa ajili ya kuinga ugonjwa wa kuhara kwa watoto; PCV 13 dozi **1,000,000** kwa ajili ya kuinga watoto dhidi ya ugonjwa wa Nimonia; chanjo za Surua Rubella dozi **3,326,200** kwa ajili ya kuinga watoto dhidi ya ugonjwa wa Surua na Rubella; BoPV zilinunuliwa dozi **3,966,000** kwa ajili ya kuinga ugonjwa wa kupooza (Polio), pentavalenti dozi **1,179,000** kwa ajili ya kuinga Donda Koo, Kifaduro, Pepopunda, Homa ya Ini, na Mafua ya Influenza dozi **2,000,000** kwa ajili ya kuinga ugonjwa wa Pepo Punda, BCG dozi **2,000** za kuinga watoto dhidi ya ugonjwa wa Kifua Kikuu na dozi **999,600** kwa ajili ya kuinga ugonjwa wa ulemavu wa ghafla.

Vile vile Wizara ilisimamia shughuli za utoaji wa chanjo kwa watoto ili kuhakikisha kuwa malengo yaliyowekwa kitaifa na kimataifa yanafikiwa. Takwimu za Januari hadi Desemba 2017 zinaonyesha kuwa **asilimia 101.2** ya Watoto waliolengwa nchini walipatiwa chanjo zote muhimu ili kuwakinga na magonjwa. **Mnamo mwezi Desemba 2017, Serikali ya Tanzania ilipongezwa kwa kufikia kiwango cha juu cha chanjo kwa asilimia 97 ya uchanjaji watoto kwa chanjo ya pentavalent kwa takwimu za mwaka 2016.** Lengo la Mkakati wa Dunia kupitia Shirika la Afya Duniani ni nchi kufikia kiwango cha uchanjaji wa **asilimia 90.** Shirika la Afya Duniani na wadau wameipongeza Serikali ya Tanzania kwa kufikia kiwango hicho ambapo inakuwa nchi ya Tatu barani Afrika ikitanguliwa na **Zambia** yenye kiwango cha **asilimia 99** ikifuatiwa na **Rwanda** yenye **asilimia 98.** Taarifa ya Wataalam wa Chanjo ulimwenguni (GNAP Assessment Report 2017) ilibainisha kwamba wastani wa kiwango cha uchanjaji barani Afrika ni **asilimia 74** na kiwango cha uchanjaji cha Dunia ni

asilimia 86. Kwa hali hiyo Tanzania ni moja ya nchi iliyopata mafanikio makubwa katika eneo hili kwa kufikia kiwango kilicho juu ya wastani wa bara la Afrika na cha Dunia.

20. Mheshimiwa Spika, saratani ya mlango wa kizazi ndio inayoongoza nchini kwa kuwa na idadi kubwa ya wagonjwa na pia kusababisha vifo vya wanawake wengi. Kwa mujibu wa takwimu za Taasisi ya Saratani Ocean Road za mwaka 2017/18, **asilimia 32.8** ya wagonjwa wa saratani nchini ni wa saratani ya mlango wa kizazi ikifuatiwa na saratani ya matiti yenye **asilimia 12.9**. Saratani nyingine ni *Kaposi Sarcoma* (11.9%), saratani ya koo (10.9%), saratani ya kichwa na shingo (7.5%), saratani ya matezi (5.4%), saratani ya damu (4.7%), saratani ya kibofu cha mkojo (3.0%), saratani ya ngozi (2.6%) na saratani ya tezi dume (2.1%).

21. Mheshimiwa Spika, kwa bahati nzuri, saratani ya mlango wa kizazi inazuilika kwa kuwapatia chanjo wasichana kuanzia miaka 9 hadi 14. Katika kukabiliana na saratani hiyo, mwaka 2017/18 Serikali imeanza kutoa chanjo ya saratani ya mlango wa kizazi (HPV Vaccine). Kutokana na upatikanaji wa dozi kutoka kwa wazalishaji, kwa mwaka 2018 chanjo hiyo imeanza kutolewa kwa wasichana wenye miaka 14, ambapo, hadi Desemba 2018, Wizara imelenga kuwafikia wasichana **616,734** wa umri huo. Chanjo hiyo ni salama na inatumika katika nchi mbalimbali za Afrika ikiwemo **Rwanda, Uganda, Afrika ya Kusini, Zambia** na **Lesotho**. Kupitia Bunge lako Tukufu, nawasihi wazazi na walezi wenye watoto kuhakikisha binti zetu wanapata chanjo hiyo muhimu ili kuwakinga dhini ya saratani ya mlango wa kizazi.

Afya na Usafi wa Mazingira

22. Mheshimiwa Spika, Wizara imeendelea kuratibu utekelezaji wa Kampeni ya Taifa ya Usafi wa Mazingira inayotekelezwa katika Halmashauri zote nchini. Kupitia Kampeni hii idadi ya kaya zenye vyoo bora imeongezeka kutoka **1,996,413** Juni 2017 hadi **2,414,094** Desemba, 2017. Katika kipindi hicho, kaya zenye sehemu maalum za kunawa mikono zimeongezeka kutoka **611,257** hadi **1,056,604**. Kwa

upande wa Vituo vya Tiba, jumla ya Vituo **277** vilijenga au kukarabati vyoo kwa kiwango cha ubora unaotakiwa. Aidha, Wizara iliendesha Mashindano ya Taifa ya Usafi wa Mazingira katika Halmashauri 184 ambapo Washindi wa kwanza, wa pili, na watatu walizawadiwa kama ifuatavyo: **Kundi la Majiji na Manispaa** washindi ni Halmashauri ya Manispaa ya Moshi, jiji la Arusha na Manispaa ya Iringa; **Halmashauri za Miji**, washindi ni; Mji wa Njombe, Kahama na Tunduma; na upande wa Halmashauri za Wilaya washindi ni **Halmashauri ya Wilaya** ya Meru, Njombe na Makete ambapo pia vijiji vya Kanikele-Njombe DC, Nambala-Meru DC na Lyalalo-Njombe DC viliibuka washindi. Katika Kundi la Hospitali, washindi ni Arusha Lutheran Medical Center, St. Francis Hospital-Ikara na Mt. Meru Hospital ya Arusha. Kwa kundi la Hoteli za Kitalii washindi watatu wa juu ni Hyatt Regency Dar es Salaam, Kilimanjaro Hotel, Mount Meru Hotel na Adden Palace Hotel-Mwanza. **Wizara ilitoa zawadi ya gari jipya aina ya NISSAN kwa Halmashauri ya Wilaya ya Meru, Trekta la kubeba taka kwa Halmashauri ya Mji wa Njombe na zawadi ya Pikipiki kwa Halmashauri na Vijiji vilivyoibuka washindi.** Nitumie fursa hii kuzipongeza Halmashauri zilizofanya vizuri na kuzitaka Halmashauri nyingine kuongeza jitihada katika utekelezaji wa Sheria ya Afya ya Jamii ya 2009 kupitia kada ya Maafisa Afya ngazi ya Kata hadi Tarafa.

23. Mheshimiwa Spika, Katika kudhibiti magonjwa ya mlipuko hususani Kipindupindu, Wizara kwa kushirikiana na wadau pamoja na vyombo vya habari imetekeleza afua mbalimbali ikiwa ni pamoja na; kuandaa mpango wa miaka 3 (2018-2020) wa kudhibiti Ugonjwa wa Kipindupindu nchini, sambamba na kufuatilia hali ya ugonjwa wa kipindupindu nchi nzima. Wizara yangu ilituma timu za wataalam za kukabiliana na ugonjwa huo (Rapid Response Teams) katika mikoa ya Kigoma, Tanga, Iringa, Mbeya, Dar es Salaam, Ruvuma na Songwe ili kudhibiti ugonjwa wa Kipindupindu. Wizara ilitoa matamko 9 kwa jamii kupitia Vyombo vya Habari 13 (Luninga, Radio na mikutano ya waandishi wa habari) kuhusu hali ya ugonjwa wa kipindupindu nchini na mikakati ya kuudhibiti.

24. Mheshimiwa Spika, Wizara imesambaza vidonge vya kutakasa maji (aqua tabs) **milioni 6.72**, na pia jumla ya tani 50 za *chlorine granules* zimesambazwa katika Mamlaka za Maji katika Mikoa 19 ambayo ni Kigoma, Katavi, Mwanza, Rukwa, Iringa, Ruvuma, Mbeya, Songwe, Kilimanjaro, Dar es Salaam, Morogoro, Dodoma, Arusha, Mara, Singida, Tanga, Geita, Simiyu na Pwani ili kutibu vyanzo vya maji. Aidha maji katika *Water bowzers* 64 katika miji ya Dar es Salaam na Morogoro yametibiwa kwa kutumia *jumbo aqua tabs* makasha 132 ya vidonge 6 kila moja. Mafunzo yametoledwa kwa wauza maji ya magari wapatao 213 katika mikoa ya Mwanza, Mara, Dodoma, Morogoro na Dar es Salaam. Pia jumla ya visima virefu (Boreholes) 18 vimechimbwa katika mikoa ya Dodoma, Morogoro, Mara na Mwanza. Wizara imesambaza jumla ya pakiti za *Oral Rehydration Salt (ORS)* **milioni 7.36** pamoja na dawa na vifaa tiba kwa ajili ya kudhibiti kipindupindu katika Mikoa 9 ya Dar es Salaam, Pwani, Manyara, Arusha, Geita, Mara, Morogoro, Dodoma na Mwanza.

25. Mheshimiwa Spika, Hali ya ugonjwa wa Kipindupindu nchini inaendelea kudhibitiwa. Katika kipindi cha Julai 2017 hadi Machi 2018 jumla ya wagonjwa wa kipindupindu 4,508 na vifo 92 viliripotiwa katika Mikoa ya Songwe, Dodoma, Ruvuma na Mbeya. Nitoe rai kwa viongozi katika mikoa yote nchini kulifanya suala la kupambana na ugonjwa wa kipindupindu kuwa ni agenda ya kudumu katika vipaumbele vyao.

26. Mheshimiwa Spika, Wizara pia imeendelea kutoa huduma ya chanjo ya homa ya manjano katika vituo 20 vikiwemo vituo vya Afya Bandari, Mipakani, Viwanja vya Ndege na Mnazi Mmoja kwa wasafiri wanaokwenda kwenye nchi zenye maambukizi ya ugonjwa huo. Jumla ya dozi **14,000** za chanjo na vyeti **22,000** viliagizwa na kusambazwa kwenye vituo vya afya mipakani Uwanja wa Ndege wa Kimataifa Mwalimu Julius Nyerere, Bandari ya Dar es Salaam, Uwanja wa Ndege wa Kimataifa Kilimanjaro, Uwanja wa Ndege Songwe, Tunduma, Kasumulu, Mtambaswala, Rusumo, Namanga, Uwanja wa Ndege Mwanza, Kigoma, Mtukula,

Tarakea, Holili, Horohoro, Bandari ya Tanga, Bandari Kavu Isaka, Sirari na Hospitali ya Mnazi Mmoja, Dar es Salaam.

Afya ya Uzazi, Mama na Mtoto

27. **Mheshimiwa Spika**, Katika kuimarisha huduma za Afya ya Uzazi, Mama na Mtoto nchini, Wizara imeendelea kutekeleza Mpango Mkakati wa miaka 5 wa mwaka 2016 hadi 2020 unaolenga kuboresha afya ya uzazi, mama, watoto na vijana pamoja na kupunguza vifo vitokanavyo na uzazi kufikia 292 kwa kila vizazi hai 100,000 ifikapo mwaka 2020. Katika kutekeleza mkakati huo, Wizara imezingatia maeneo makuu matatu ambayo ni: **huduma ya uzazi wa mpango, huduma wakati wa ujauzito na huduma wakati wa kujifungua**. Lengo ni kuhakikisha upatikanaji wa huduma bora, inayofikiwa kwa wanawake wote, kabla ya ujauzito, wakati wa ujauzito, na wakati wa kujifungua hadi wiki sita baada ya kujifungua, kama muhimili muhimu wa kupunguza vifo vitokanavyo na uzazi na watoto chini ya miaka mitano.

28. **Mheshimiwa Spika**, **huduma za uzazi wa mpango** ni muhimu katika kuimarisha afya ya mama na mtoto pamoja na kupunguza vifo vitokanavyo na uzazi. Katika kipindi cha Julai 2017 hadi Machi 2018, Wizara imenunua na kusambaza dawa za uzazi wa mpango katika vituo vya huduma za afya nchini ikiwa ni pamoja na: Depo-provera vichupa **2,986,853**; dawa ya kidonge yenye kichocheo kimoja (Microval) mizunguko **19,357**; Vipandikizi **227,976**; Vitanzi **61,599**; dawa ya dharura (emergency contraceptives) **28,953**; Vipandikizi vya Jadelle **209,050**; Microgynon mizunguko **1,500,000**; Kondomu za Kiume **6,902,646**; na kondomu za kike **61,599**. Aidha jumla ya **wateja 519,817** walifikwa na huduma ya uzazi wa Mpango kupitia utaratibu wa mkoba (out reach services) na **424,595** walipata huduma kutoka katika vituo vya kutolea huduma za afya.

29. **Mheshimiwa Spika**, upatikanaji wa huduma ya afya wakati wa ujauzito ni afua muhimu katika kupunguza vifo vitokanavyo na uzazi, kwani matatizo mengi yanaweza kuzuilika, kugundulika na kutibiwa kama wanawake wajawazito watahudhuria kliniki ya wajawazito na kupimwa

na wahudumu wenye ujuzi ndani ya **wiki 12 tangu wanapokuwa wamejigundua kuwa wanaujauzito**. Katika kipindi cha Julai 2017/18, Wizara iliendelea kuhakikisha kwamba huduma kwa wanawake wajawazito zinapatikana sambamba na kuelimisha wajawazito kuhudhuria kliniki. Kulingana na TDHS 2015/16, asilimia 51 ya wanawake wajawazito walihudhuria angalau mara 4 ikiwa ni kiwango cha chini cha mahudhurio kinachotakiwa. Aidha, kulingana na taarifa kutoka vituo vya kutolea huduma ya afya, hadi kufikia mwezi Februari 2018 asilimia 81.7 walihudhuria angalau mara moja. Lengo ni kufikisha asilimia 70 ya wanawake wajawazito kuhudhuria kliniki angalau mara 4 katika kipindi cha ujauzito ifikapo mwaka 2020. **Nitumie fursa hii kuwahimiza wajawazito wote kuhudhuria kliniki kama inavyoshauriwa.**

30. Mheshimiwa Spika, upatikanaji wa **huduma bora wakati wa kujifungua** ikiwemo huduma ya dharura wakati wa kujifungua hadi wiki sita baada ya kujifungua, ni muhimu sana ili kuepuka vifo vitokanavyo na uzazi. Huduma kwa matatizo haya hupatikana tu kwenye vituo vya kutolea huduma za afya na kutolewa na watoa huduma wenye ujuzi. Katika mwaka 2017/18, Wizara kwa kushirikiana na wadau imeendelea kuhamasisha na kuhimiza wanawake wajawazito kujifungulia kwenye vituo vya kutolea huduma. Mwelekeo ni kwamba Idadi ya akinamama wanaojifungulia katika vituo vya kutolea huduma inaendelea kuongezeka hadi kufikia asilimia **68.5 mwezi Februari 2018 katoka asilimia 64 mwaka 2015/16**. Napenda kutoa wito kwa wanawake wajawazito wote nchini, wajifungulie kwenye vituo vya kutolea huduma ya afya ili kupunguza vifo na changamoto za uzazi kwa mama na mtoto.

31. Mheshimiwa Spika, katika kuboresha huduma za afya ya Uzazi na Watoto, dawa za sindano aina ya Oxytocin (kwa ajili ya kuzuia mama mjamzito kutokwa na damu nyingi baada ya kujifungua) vichupa **1,141,208** na Magnesium Sulphate (dawa ya kuzuia kifafa cha mimba) vichupa **76,219**; Fefol (dawa ya kuongeza wingi wa damu) vidonge **55,888,500**; Vidonge vya Amoxicillin myeyuko **4,086,946** na Zinc/

ORS **1,084780** (dawa ya kuzuia kuharisha) vilinunuliwa na kusambazwa kwenye vituo vya kutolea huduma ya afya katika Halmashauri mbalimbali nchini. Hatua hii imeokoa maisha ya wanawake wajaawazito ambao walipata matatizo ya kutokwa na damu nyingi au kifafa cha mimba wakati na baada ya kujifungua. Nitumie fursa hii kumshukuru sana Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kuhakikisha fedha za uzazi salama zinapatikana kwa wakati.

32. Mheshimiwa Spika, kupunguza **vifo vya watoto chini ya miaka mitano** ni moja ya kipaumbele cha Wizara. Kulingana na **Mpango Mkakati wa Afya ya Uzazi na Mtoto wa 2016-2020**, Serikali imedhamiria kuwa ifikapo 2020 vifo vya watoto wa chini ya mwezi mmoja vipungue kutoka 21 hadi 16 katika kila vizazi hai 1,000; vifo vya watoto wa chini ya umri wa mwaka mmoja kutoka 45 hadi 25 katika kila vizazi hai 1,000 na vifo vya watoto wa chini ya umri wa miaka mitano kutoka 54 hadi 40 katika kila vizazi hai. Katika kipindi cha Julai 2017 hadi Machi 2018. Wizara ili wajengea uwezo watoa huduma ya afya Katika kuwahudumia watoto wagonjwa kwa njia jumuishi (Integrated Management Child Illness-IMCI). Mafunzo haya yalitolewa kwa watoa huduma **1,342** katika mikoa ya Mwanza, Geita na Mara. Aidha watoa huduma 296 kutoka katika mikoa ya Mtwara, Lindi, Ruvuma, Rukwa na Katavi walijengewa uwezo jinsi ya kutoa huduma ya dharura kwa mtoto mgonjwa sana.

33. Mheshimiwa Spika, Wizara kwa kushirikiana na Wadau wa Maendeleo imeendelea kuboresha miundombinu ya kutolea huduma za afya katika ngazi ya Vituo vya Afya ili viweze kutoa huduma za dharura za upasuaji ikiwa ni pamoja na upasuaji wa kutoa mtoto tumboni (CEmONC) pindi mama mjamzito anapohitajika. Wizara kwa kushirikiana na OR-TAMISEMI inaboresha vituo vya afya takribani 208 (kama ilivyoainishwa katika hotuba ya Ofisi ya Rais – TAMISEMI) ili kuviwezesha kutoa huduma za CEmONC. Hadi Machi 2018, maboresho ya vituo hivyo yalikuwa yapo katika hatua mbalimbali za ukamilishwaji. Maboresho haya yanahusu ujenzi wa vyumba vya upasuaji (Theatres), wodi ya wakinamama

wajawazito (Martenity/Labour wards), vyumba vya maabara na nyumba za watumishi. Kukamilika kwa maboresho haya kutaongeza idadi ya vituo vinavyomilikiwa na Serikali vyenye uwezo wa kutoa huduma hiyo ya CEmONC kufikia 283 kati ya Vituo vya Afya 527. Hii itakuwa sawa na asilimia 53.7 ya vituo vya afya vya umma vitakavyoweza kutoa huduma za upasuaji wa dharura kutoka asilimia 21 mwezi Juni 2016.

34. Mheshimiwa Spika, Wizara kwa kushirikiana na wadau wa maendeleo imeandaa mpango wa **mafunzo ya kuwajengea uwezo watumishi** wa sekta ya afya ili kuboresha huduma za Upasuaji wa Dharura. Jumla ya watumishi 200 kutoka katika Halmashauri 96 wanatarajiwa kujiunga na mafunzo ya mwaka mmoja ya utoaji wa dawa ya usingizi (Anaesthesia) mwezi Mei, 2018. Aidha, Wizara yangu imejiwekea mkakati maalumu wa kuboresha huduma kwenye vituo vilivyokarabatiwa kwa kutekeleza yafuatayo: Kutoa kipaumbele cha ajira hususani katika vituo vyenye uhaba mkubwa, kutawanya watumishi kutoka kwenye maeneo yenye watumishi wengi kuhamishiwa kwenye maeneo yenye upungufu mkubwa pamoja na kuandaa program maalumu ya wataalamu (madaktari bingwa) kutembelea vituo kwa ajili ya kuwajengea uwezo wa kutoa huduma bora na salama za upasuaji kwa wajawazito. Wizara imeendelea kushirikiana na Wadau katika kutoa **Elimu ya Uzazi Salama** kwa jamii kupitia njia mbalimbali za mawasiliano ikiwemo Runinga, Redio na ujumbe kwa njia ya simu. Takriban jumla ya wajawazito **952,484** wamefikwa kwa kutumia ujumbe kwa njia ya simu kuwahamasisha kujifungulia katika vituo vya kutolea huduma za afya pamoja na kuwaelimisha umuhimu wa kuhudhuria kliniki katika kipindi chote cha ujauzito na baada ya kujifungua hadi mtoto anapotimiza miaka mitano. Lengo ni kufikia wajawazito **1,800,000** kwa mwaka.

35. Mheshimiwa Spika, Wizara imeendelea na juhudi za kudhibiti saratani za via vya uzazi (Reproductive cancers) ikiwemo saratani ya mlango wa kizazi, saratani ya matiti na saratani ya Tezidume. Aidha, katika kuhakikisha upatikanaji wa huduma za kupima na matibabu ya Mabadiliko ya awali

ya Saratani ya Mlango wa kizazi na saratani ya matiti ambazo ndizo zinazoongoza nchini, Wizara kwa kushirikiana na wadau imeanzisha **vituo vipya 100 vya uchunguzi na tiba ya mabadiliko ya awali ya saratani ya mlango wa kizazi** katika mikoa ya Mbeya, Mwanza, Songwe, Geita, Dodoma, Singida, Manyara, Arusha, Tanga, Lindi, Mtwara, Simiyu, Mara na Ruvuma. Vilevile, Wizara ilinunua na kusambaza **mashine 100 za cryotherapy**, 9 za LEEP na mitungi 173 kwa ajili ya matibabu ya dalili za awali za Saratani ya mlango wa kizazi. Pia, watoa huduma 186 kutoka mikoa iliyotajwa hapo juu, walipata mafunzo ya uchunguzi na matibabu ya mabadiliko ya awali ya saratani ya mlango wa kizazi, na madaktari 18 walipatiwa mafunzo ya namna ya kutoa matibabu kwa kutumia mashine za LEEP.

36. Mheshimiwa Spika, Wizara yangu imeanzisha kampeni ya uchunguzi wa saratani ya mlango wa kizazi na saratani ya matiti, ambapo kila kituo kinachotoa huduma kimeagizwa kutenga siku maalum kila mwezi kwa ajili ya kuwafanyia wanawake uchunguzi wa saratani hizo pamoja na utoaji huduma za matibabu katika halmashauri zote nchini. Kila kituo (Hospitali na Kituo cha Afya) kimepangiwa lengo maalum ili kuwezesha kufikiwa kwa wanawake **3,000,000**, ifikapo mwezi Desemba 2018.

Udhibiti wa UKIMWI

37. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha Julai 2017 hadi Desemba 2017, jumla ya watu wapatao **5,164,297** walipimwa VVU na kupewa majibu ya hali zao za afya, ambapo watu **145,104** (sawa na asilimia **2.8**) kati yao waligundulika kuwa na maambukizi na kuanzishiwa dawa za kufubaza virusi vya UKIMWI. Aidha, takwimu za hadi Desemba, 2017 zinaonesha kuwa jumla ya watu wanaoishi na VVU wapatao **965,081** walikuwa wanatumia dawa za kufubaza VVU, ikiwa ni sawa na **asilimia 69** ya watu **1,400,000** wanaokadiriwa kuishi na virusi vya UKIMWI nchini na kati yao watoto walikuwa **55,304** ambao ni sawa na **asilimia 5.7**. Kutokana na takwimu hizo Tanzania tumebakiza **asilimia 21** kufikia lengo la dunia la **asilimia 90** ya watu wanaoishi na virusi vya UKIMWI

kuanzishiwa dawa za kufubaza VVU ifikapo mwaka 2020. Wizara imeweka mikakati mbalimbali ili kufikia lengo hilo.

38. Mheshimiwa Spika, Wizara yangu ilifunga mashine mpya 5 zenye uwezo mkubwa wa kupima sampuli nyingi kwa siku na kubainisha wingi wa virusi vya UKIMWI (HIV Viral Load) na utambuzi wa maambukizi kwa watoto waliozaliwa na wakina mama wanaoishi na VVU (HIV Early Infant Diagnosis). Mashine tatu (3) zimefungwa katika Maabara ya Hospitali ya Temeke, Mashine moja imefungwa katika maabara ya Hospitali ya Rufaa ya Kanda Mbeya na moja imefungwa katika Maabara ya hospitali ya Bugando, Mwanza.

39. Mheshimiwa Spika, Huduma za kuzuia maambukizi ya VVU kutoka kwa mama kwenda kwa mtoto (PMTCT), zimeendelea kutolewa, ambapo, jumla ya akina mama wajawazito **1,967,260** sawa na asilimia **98.7%** ya akina mama **1,993,639** walipatiwa huduma za ushauri nasaha na upimaji wa VVU. Kati yao akina mama **79,242** sawa na asilimia **4** waligundulika kuwa wanaishi na VVU. Akina mama **79,240** sawa na asilimia **99.9** ya akina mama wenye maambukizi ya VVU walipatiwa dawa (ARV) kwa ajili ya kufubaza virusi vya UKIMWI. Aidha jumla ya Watoto **72,960** sawa na asilimia **92** walipata kipimo cha awali cha utambuzi wa maambukizi ya VVU ambapo watoto **2,918** sawa na asilimia **4** walikutwa na maambukizi. Kiwango hicho cha maambukizi kinaashiria kuendelea kupungua kwa maambukizi ya VVU kutoka kwa mama kwenda kwa mtoto, na hivyo kuiwezesha nchi kufikia malengo ya Kimataifa ya kutokomeza kabisa maambukizi ya VVU kwa watoto. Hivi sasa, maambukizi ya VVU kutoka kwa mama kwenda kwa mtoto ni **asilimia 4.9** kutoka asilimia **12 mwaka 2011**.

Huduma za Udhhibiti wa Kifua Kikuu na Ukoma

40. Mheshimiwa Spika, Wizara imeendelea na mkakati wake wa Udhhibiti wa ugonjwa wa Kifua Kikuu na Ukoma ambapo katika kipindi cha Julai hadi Machi 2017, Serikali ilinunua na kusambaza dawa za Kifua Kikuu na Ukoma. Katika kuhakikisha Serikali inaboresha matibabu ya ugonjwa wa

Kifua Kikuu kwa watoto, mwezi Machi 2018, Wizara yangu ilizindua matumizi ya **dawa mpya za kifua kikuu kwa watoto**. Dawa hizi mpya ni za mseto (RHZ/RH) ulioboreshwa, zina ladha nzuri ya matunda, zinayeyuka kwa urahisi zikiwekwa kwenye maji na hivyo hazihitaji kukatwakatwa ili kupata dozi sahihi.

41. Mheshimiwa Spika, Wizara yangu imeongeza wigo wa upatikanaji wa **huduma za ugunduzi wa ugonjwa wa kifua kikuu kwa kutumia vipimo vya vinasaba (gene-xpert)** katika wilaya zote nchini ili kuongeza kazi ya kuwagundua wagonjwa wengi wa TB na kuwatibu. Kwa mwaka 2017/18, Serikali kwa kushirikiana na Wadau wa Maendeleo ilinunua na kusambaza mashine za “genexpert” 189 ikilinganishwa na mashine 66 zilizokuwepo mwaka 2015. Vilevile, Wizara imepokea jumla ya vitendanishi (Catridges) boksi 3,675 ambazo zitatumika katika ugunduzi wa ugonjwa wa kifua kikuu kwa kutumia vipimo vya vinasaba (gene-xpert). **Teknolojia ya mashine hizi inatuwezesha kupata majibu ndani ya masaa 2 badala ya kusubiri kwa zaidi ya masaa 24** kama ilivyo kwa njia za kawaida za hadubini (Microscopes). Aidha, mashine hizi zina uwezo wa kupima usugu wa dawa za kifua kikuu wakati huo huo wa upimaji wa makohozi, na hivyo kugundua kifua kikuu sugu kwa urahisi zaidi. Mashine hizi zimesambazwa kwenye hospitali zote za rufaa za kanda, mikoa, wilaya na baadhi ya vituo vikubwa vya afya.

42. Mheshimiwa Spika, Katika kudhihirisha nia ya serikali ya kushirikiana na Sekta binafsi katika mapambano dhidi ya ugonjwa wa kifua kikuu hasa kuongeza idadi ya wagonjwa wa TB wanaogunduliwa kutoka **asilimia 40** hadi **asilimia 70** mwaka 2020, Wizara yangu imekabidhi mashine za gene-xpert tano (5) kwa hospitali binafsi za jijini Dar es Salaam. Hospitali zilizopokea mashine hizi ni Aga Khan, Hubert Kairuki, Regency Medical Center, TMJ na Hindul Mandal. Mashine hizo kila moja ina thamani ya **Shilingi milioni 38**. Tumeanza na hospitali hizi zenye viwango vikubwa vya wagonjwa wanaohudumiwa na pia kwa kuzingatia utayari wa hospitali hizi katika kutoa huduma za kifua kikuu sanjari na malengo ya Serikali yetu ya

awamu ya tano ya Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli, Rais wa jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika kuhakikisha huduma za afya zinawafikia wananchi wote. Kadhalika, ushirikishwaji huu wa Sekta Binafsi katika kutambua wagonjwa wa kifua kikuu umeonesha **ongezeko la wagonjwa wa TB wanaoibuliwa na sekta binafsi kutoka wagonjwa 3,476 mnamo mwaka 2014 hadi wagonjwa 7,281 katika mwaka 2017 ambao ni sawa na 10.4%** waligunduliwa na sekta binafsi. Nitumie fursa hii kuwashukuru na kuwapongeza sekta binafsi kwa ushiriki wao katika kutokomeza TB nchini.

43. Mheshimiwa Spika, Wizara yangu imeendelea kuongeza wigo wa **huduma za matibabu ya wagonjwa wa kifua kikuu sugu nchini**. Katika kipindi cha mwaka 2017 hadi Machi 2018 Wizara iliongeza vituo 41 na kufanya jumla ya vitu vinvavyotoa huduma hiyo kufikia vituo 63 ikilingalishwa na kituo kimoja cha hospitali Maalum ya Kibong'oto mwaka 2015. Mafanikio haya yamewawezesha wagonjwa wa kifua kikuu sugu kutibiwa katika hospitali za karibu wakitokea majumbani kwao badala ya kutegemea Hospitali Maalum ya Kibong'oto, ambako pia walikuwa wanakaa kwa muda mrefu. Mikoa yenye vituo hivyo vilivyoweza kuanzisha matibabu ya wagonjwa chini ya ugatuzi ni Dar es salaam, Kagera, Geita, Mtwara, Lindi, Mbeya, Pwani, Morogoro, Tanga, Unguja, Tabora, Kigoma, Mwanza, Arusha, Rukwa na Simiyu. Vile vile, Wizara imeanzisha matibabu ya muda mfupi **kwa wagonjwa wa kifua kikuu sugu kufupisha tiba hiyo kutoka miezi ishirini ya hapo awali mpaka miezi tisa kwa wagonjwa wanoakidhi vigezo.**

44. Mheshimiwa Spika, Katika kushughulikia madhara yatokanayo na Kifua Kikuu cha mapafu (Pulmonary TB) pamoja na magonjwa mengine sugu ya mapafu (Chronic Lung Diseases), Wizara yangu imezindua kituo cha kisasa cha huduma za afya mahala pa kazi yaani *Occupational Health Services Centre* kwenye hospitali maalum ya Kibong'oto.

45. Mheshimiwa Spika, kwa upande wa **ugonjwa wa Ukoma**, Wizara ilifanya uchunguzi wa vimelea vya Ukoma katika ngazi ya jamii kwenye Wilaya 6 zenye maambukizi

makubwa katika mikoa ya Geita (Chato), Lindi (Liwale), Mtwara (Nanyumbu), Morogoro (Kilombero) na Tanga (Mkinga na Muheza). Katika zoezi hilo takriban watu **500** wamefanyiwa uchunguzi, ambapo watu **54** sawa na asilimia **10.8** waligundulika kuwa na vimelea vya ugonjwa wa ukoma na kuanzishiwa matibabu, takriban watu **300** wamepatiwa tiba kinga.

Udhibiti wa Malaria

46. Mheshimiwa Spika, Malaria imeendelea kuwa sababu ya vifo vya wananchi wengi ambapo kwa takwimu za Januari – Desemba 2017, jumla ya wagonjwa **5,592,844** wameugua ugonjwa huu, kati yao wagonjwa **4,421** walifariki kutokana na ugonjwa wa Malaria. Katika kuendeleza juhudi za kupunguza maambukizi ya malaria nchini; Wizara yangu imeendelea kutekeleza shughuli mbalimbali za udhibiti wa malaria. Katika kipindi cha Julai 2017 hadi Machi, 2018, Wizara kwa kushirikiana na wadau imenunua **Dawa mseto (Alu)** jumla ya **dozi 12,916,050**, vitepe vya **mRDT 21,428,725**, **vidonge vya SP dozi 6,899,700** kwa ajili ya tiba-kinga kwa wajawazito na dawa ya sindano ya **Artesunate vichupa 1,668,464** kwa ajili ya matibabu ya malaria kali na kusambazwa katika vituo vya huduma za afya kupitia Bohari ya Dawa nchini (MSD). Ili kuendelea kuwakinga wananchi dhidi ya malaria, na hasa kulenga makundi maalum; wajawazito na watoto chini ya mwaka mmoja, Serikali imesambaza jumla ya **vyandarua 4,726,763** kwa jamii bila malipo kupitia wanafunzi shuleni na kupitia kliniki za wajawazito na watoto (Chandarua Kliniki).

47. Mheshimiwa Spika, Katika kutekeleza Agizo la Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. John Pombe Magufuli, kuhusu Afua ya kuangamiza viluwiluwi vya mbu katika mazalia (larviciding), Wizara kwa kushirikiana na OR-TAMISEMI imeratibu zoezi la usambazaji wa viuadudu vya **kibailojia (biolarviciding)** jumla ya **lita 236,420** katika Halmashauri zote nchini, na Halmashauri zipo katika hatua mbalimbali za utekelezaji wa afua katika maeneo yao. Kutokana na juhudi kubwa za Serikali kwa kushirikiana na wadau wake, katika kutekeleza mikakati ya udhibiti

Iliyopendekezwa na WHO, kiwango cha maambukizi ya malaria kimepungua kwa takriban **asilimia 50** kutoka **asilimia 14.8** mwaka 2016 hadi **asilimia 7.3** mwaka 2017. Katika kutambua juhudi hizi kubwa na kipaumbele cha Serikali yetu katika kudhibiti malaria, **Shirika la Afya Duniani limetoa tuzo kwa Wizara yangu kwa kuthamini mchango wa Serikali yetu na mafanikio yaliyopatikana katika kudhibiti malaria nchini.**

Udhibiti wa Magonjwa Yaliyokuwa Hayapewi Kipaumbele

48. Mheshimiwa Spika, Wizara yangu kwa kushirikiana na wadau, imeendelea na juhudi za kudhibiti na kutokomeza magonjwa yaliyokuwa hayapewi kipaumbele (matende, mabusha, usubi, kichocho, minyoo ya tumbo na trachoma) kwa njia ya kingatiba kupitia ugawaji wa dawa kwenye jamii zenye kiwango kikubwa cha maambukizi katika Halmashauri zote 185 za hapa nchini. Aidha, hadi kufikia Machi 2018 Serikali imetoa **dozi takribani 52,537,325** kwa watu wapatao **24,373,159**. Kati yao, watu **12,669,612** walipatiwa Kingatiba ya magonjwa wa Matende na Mabusha, watu **4,894,307** walipewa kingatiba ya Ugonjwa wa Usubi, watu **6,917,303** walipewa kingatiba ya Kichocho, watu **22,041,327** walipewa kingatiba ya Minyoo ya Tumbo, na watu wapatao **3,536,764** walipewa kingatiba dhidi ya ugonjwa wa trachoma.

49. Mheshimiwa Spika, Katika kupunguza madhara yatokanayo na magonjwa haya, Wizara kwa kushirikiana na Wadau ilitoa huduma ya upasuaji wa mabusha kwa wagonjwa wapatao **1,639** kutoka mikoa ya Dar es Salaam, Tanga, Pwani na Lindi. Pia, takribani wagonjwa **6,535** walipatiwa huduma ya kurekebishiwa kope katika mikoa ya Tanga, Ruvuma, Arusha, Manyara, Mtwara, Lindi, Pwani na Dodoma.

50. Mheshimiwa Spika, Kutokana na utekelezaji wa afua mbalimbali za kudhibiti magonjwa yaliyokuwa hayapewi kipaumbele, jumla ya **Halmashauri 93 zimefanikiwa kupunguza kiwango cha maambukizi** ya ugonjwa wa matende na mabusha na **hivyo kuondolewa kwenye orodha**

ya Halmashauri zenye maambukizi makubwa zinazoshiriki katika zoezi la Kingatiba kulingana na vigezo vya Shirika la Afya Duniani (WHO). **Kiambatisho Na. 1** kinaainisha Halmashauri zilizofanikiwa kupunguza Maambukizi Makubwa ya ugonjwa wa Matende na Mabusha. Haya ni mafanikio makubwa kwani Watanzania wapatao **20,446,532** wanaoishi katika halmashauri hizi hawapo tena katika hatari ya maambukizi ya magonjwa haya.

Huduma za Lishe

51. Mheshimiwa Spika, Katika kupambana na utapiamlo nchini, Wizara yangu kwa kushirikiana na wadau wa Lishe imetoa matone ya nyongeza ya vitamin A kwa watoto wa kati ya miezi sita na miaka mitano sambamba na dawa za minyoo kwa watoto wa umri kati ya mwaka mmoja na miaka mitano. Matone hayo ya vitamini A hutolewa kwa awamu mbili yaani mwezi Juni 2017 na Desemba 2017. Jumla ya watoto **7,824,360** sawa na asilimia **93** walipatiwa matone ya vitamini A kwa mwezi Juni, 2017 na watoto **6,837,920** sawa na asilimia **92** walipatiwa dawa za minyoo. Kwa mwezi Desemba 2017, jumla ya watoto **8,007,114** sawa na asilimia **93** walipatiwa matone ya vitamini A na watoto **6,977,047** sawa na asilimia **92** walipatiwa dawa za minyoo.

52. Mheshimiwa Spika, Wizara yangu kwa kushirikiana na asasi mbalimbali za Serikali na zisizo za kiserikali inaendelea kutoa virutubishi muhimu vya madini na vitamini kwa ukuaji wa mwili na akili kupitiaurutubishaji wa unga wa ngano, unga wa mahindi na mafuta ya alizeti. Jumla ya mikoa 16 yenye Halmashauri 59 imefikiwa kupitiaurutubishaji wa unga wa ngano, unga wa mahindi na mafuta ya alizeti sawa na asilimia 31. Aidha, asilimia 82 ya kaya zote nchini zinatumiachumvi iliyoongezwa madini joto na hivyo kuziepusha dhidi ya ugonjwa wa Goita. Vile vile, mikoa inayotekelezaurutubishaji wa chakula kwa kutumia virutubishi nyongeza kwenye chakula cha kawaida kwa watoto wenye umri wa miezi 6 hadi 59 katika ngazi ya jamii (Home Food Fortification) imeongezeka na kufikia 16.

53. Mheshimiwa Spika, Wizara yangu imendelea kutoa huduma za matibabu ya utapiamlo mkali kwa watoto, kupitia uboreshaji wa Hospitali kwa kuzijengea miundombinu kwenye wodi za kulaza watoto, kuimarisha mfumo wa upatikanaji wa chakula dawa na vifaa vya kupimia hali ya Lishe pamoja na kujengea uwezo wa watoa huduma. Aidha, Hospitali zinazotoa matibabu ya utapiamlo mkali zimeongezeka na kufikia 32. Lengo la Serikali ni kuhakikisha Hospitali zote za Mikoa na Wilaya zinatoa huduma za matibabu ya utapiamlo mkali.

Elimu ya Afya kwa Umma

54. Mheshimiwa Spika, Wizara iliendelea kuelimisha na kuhamasisha jamii kutunza afya zao dhidi ya magonjwa, kufanya uchunguzi wa afya mara kwa mara na kujenga tabia inayozingatia kanuni za afya. Katika kutoa elimu hiyo, Wizara ilitayarisha na kusambaza vipeperushi, majarida, mabango na Makala mbalimbali zilizokuwa na ujumbe wa kuelimisha jamii kuhusu magonjwa ya kuambukiza na yale yasiyo ya kuambukiza. Elimu hiyo ilitolewa maeneo mbalimbali ikiwa ni pamoja na Shuleni, makundi ya vijana, vijijini, mijini kwa kupitia njia mbalimbali za mawasiliano kama vile radio na Televisheni, pamoja na mitandao ya kijamii kama *Twitter, WhatsApp na face book*. Wizara kupitia mpango wa Elimu ya Afya kwa Umma imeandaa mkakati wa mawasiliano utakaowezesha namna ya kuwasiliana kwa haraka wakati wa majanga na milipuko ya magonjwa, tayari timu za mikoa ya mipakani zimeelimishwa juu ya mkakati huo. Aidha, Wizara imekamilisha **ujenzi wa studio ya radio na televisheni** ambavyo vimeanza kurekodi vipindi vitakavyorushwa nchi nzima kwa ajili ya kuelimisha jamii ya Watanzania kuhusu masuala mbalimbali ya afya.

Udhibiti wa Magonjwa Yasiyo ya Kuambukiza Nchini

Mheshimiwa Spika, Wizara iliandaa miongozo ya udhibiti wa magonjwa yasiyo ya kuambukiza. Miongozo hiyo ni pamoja na Mwongozo wa kitaifa wa usafishaji figo (Dialysis) na Mwongozo wa mafunzo ya huduma za dawa ya kuzuia

athari zitokanazo na kuacha matumizi ya dawa za kulevya (*Methadone*). Aidha, kazi nyingine iliyotekelezwa ni kuendesha kampeni za uhamasishaji wa kufanya mazoezi kwa kila Mtanzania mara kwa mara kama moja ya mkakati wa kujikinga na magonjwa yasiyo ya kuambukiza. Aidha, Wizara kwa kushirikiana na *International Centre for Eye Health* imeandaa mpango wa kuimarisha huduma za macho kwa watu wanaoishi na ugonjwa wa Kisukari zinazotolewa katika Hospitali ya Taifa Muhimbili na Hospitali za Rufaa za Kanda za KCMC and Mbeya.

HUDUMA YA TIBA

Usajili na Usimamizi wa Vituo vya kutolea huduma za Afya

55. *Mheshimiwa Spika*, Wizara imeendelea kusimamia upatikanaji wa huduma za afya kupitia vituo vya kutolea huduma nchini vikiwemo vya Serikali, binafsi na mashirika ya dini. Hadi kufika Machi 2018, huduma za afya zimeendelea kutolewa katika vituo vya kutolea huduma za afya **7,437** ikilinganishwa na vituo **7,284** mwezi Juni 2017. Aidha, katika kipindi cha Julai 2017 hadi Machi 2018, jumla ya Vituo binafsi 153 vya kutolea huduma za Afya vilisajiliwa.

Uimarishaji wa Huduma za Matibabu ya Kibingwa

Mheshimiwa Spika, Katika mwaka 2017/18, moja ya jukumu la kipaumbele kwa Wizara ilikuwa ni kuendelea kuboresha na kuimarisha huduma za matibabu ya kibingwa yatolewayo nchini. Maboresho hayo, yanalenga katika kupunguza idadi ya wagonjwa wanaopewa rufaa ya Matibabu nje ya nchi ili kupunguza gharama kubwa kwa Serikali katika kupeleka wagonjwa nje ya nchi.

Hadi kufikia mwezi Machi 2018, idadi ya Wagonjwa waliopewa rufaa ya Matibabu nje ya nchi ilipungua na kufikia Wagonjwa **103** ikilinganishwa na wagonjwa **304** mwaka 2016/17. Mafanikio haya ni kutokana na maboresho yaliyofanyika katika Hospitali zilizo chini ya Wizara ambapo kwa hivi sasa zimeongezewa uwezo wa kutoa huduma za Kibingwa

ambazo awali hazikuwa zikitolewa hapa nchini na hivyo kulazimu wagonjwa kupatiwa rufaa nje ya nchi. Katika kipindi cha Julai 2017 hadi Machi 2018, Hospitali za Rufaa za Kanda, Hospitali Maalum na Hospitali ya Taifa ya Muhimbili zilihudumia jumla ya wagonjwa **1,090,863** ambapo wagonjwa wa kulazwa walikuwa **230,403** na wagonjwa wa nje walikuwa **860,460**. Mchanganuo wa idadi ya wagonjwa kwa kila Hospitali umeoneshwa katika **Kiambatisho Namba 2**.

Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH)

56. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2017/18, Hospitali ya Taifa ya Muhimbili ilihudumia jumla ya wagonjwa **333,611**. Kati ya hao wagonjwa **37,226** walikuwa wa kulazwa na Wagonjwa **296,385** walikuwa ni wa nje. Aidha Hospitali kwa kushirikiana na Serikali ya Scotland ilifanya ukarabati wa vyumba viwili vya upasuaji wa Watoto na hivyo kuongeza upatikanaji wa huduma za upasuaji kwa Watoto kufikia **Watoto hamsini (50)** kwa wiki kutoka **watoto 12** kwa wiki hapo awali.

57. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2017/18, Hospitali ilifanya ukarabati wa jengo la kutolea huduma za upandikizaji wa Figo na ununuzi wa vifaa Tiba kwa ajili **huduma za upandikizaji wa figo** iliyoanza kutolewa Mwezi Novemba 2017 ambapo Mgonjwa mmoja (1) alipatiwa huduma hiyo na kwa sasa wagonjwa watano (5) wamepangwa kupatiwa huduma hii mwishoni mwa Mwezi Aprili 2018. **Hatua hii imepunguza gharama za kupandikiza figo kwa mgonjwa mmoja nje ya nchi kutoka wastani wa shilingi milioni mia 100 hadi milioni 20.**

58. Mheshimiwa Spika, Hospitali imeanzisha **huduma za upandikizaji wa vifaa vya kusaidia kusikia (Cochlea implant)**, hadi kufikia mwezi Machi 2018, wagonjwa sita (6) walipata huduma ya kuwekewa vifaa vya usikivu. Huduma ya kupandikiza vifaa vya kusaidia kusikia inatolewa kwa wastani wa **shilingi milioni 36 kulinganisha na shilingi milioni**

80 hadi 100 ambazo zingetumika endapo mgonjwa angepelekwa nje ya nchi.

59. Mheshimiwa Spika, Hospitali ya Taifa ya Muhimbili imeanza ujenzi wa jengo maalum kwa wagonjwa wanaolipia (private wing) ambapo eneo lenye ukubwa wa mita za mraba 5,400 kwa ajili ya ujenzi huo limetengwa. Jumla ya **Shilingi bilioni 4** zimeshatolewa na Serikali kwa ajili ya kuanza ujenzi wa Jengo hili. Aidha, katika kuboresha utoaji wa huduma za kibingwa, Hospitali ya Taifa Muhimbili imekamilisha miradi mbalimbali ambayo ilikuwa imeanza katika kipindi cha Mwaka wa Fedha 2016/17 kwa kutumia fedha zake za ndani. Miradi hii inajumuisha kukamilisha ukarabati wa Jengo kuu la upasuaji lenye vyumba 8 vya upasuaji vikiwamo vyumba viwili (2) vya kupandikiza figo. Aidha, Kazi zingine zilizokamilishwa na Hospitali ya Taifa Muhimbili kwa kipindi hicho ni pamoja na kukamilisha ukarabati wa jengo la kusafisha figo ambalo kwa sasa lina jumla ya vitanda 42 vya kuchujia damu ukilinganisha na vitanda 24 mwaka 2015; kukamilisha ukarabati wa Jengo la Upasuaji wa kina mama wajawazito na kuongeza vyumba vya upasuaji kutoka vyumba viwili (2) hapo awali na kufikia vyumba 4 kwa hivi sasa; usimikaji wa *lift* mbili (2) katika majengo ya Kibasila na Mwaisela; Ukarabati na usimikaji wa mfumo wa hewa katika jengo la upasuaji wa kinywa.

60. Mheshimiwa Spika, Hospitali pia, imepokea vifaa mbalimbali vyenye thamani ya **shilingi billion 1.52** kutoka Taasisi ya "Archie Wood Foundation ya Scotland" vitakavyotumika katika jengo la huduma za Kinywa na Meno. Serikali imepeleka nchini India jumla ya Madaktari 4, wauguzi 2 wa kitengo cha Tiba ya Matumbo kwa ajili ya upandikizaji wa Ini, pamoja na mhandisi wa Vifaa Tiba. Serikali kwa kushirikiana na ubalozi wa India nchini, ilipeleka madaktari 10 na wauguzi 6 (kutoka hospitali ya Taifa Muhimbili) nchini India kwa ajili ya kozi mbalimbali za muda mfupi.

61. Mheshimiwa Spika, Hali ya upatikanaji wa dawa katika Hospitali ya Taifa Muhimbili imeendelea kuwa katika kiwango cha asilimia **95**. Jumla ya **Shilingi bilioni 1** huwekwa

katika mfuko wa fedha za kununulia dawa (**Drug Revolving Fund**) kila mwezi ili kukabiliana na changamoto za upatikanaji wa dawa. Aidha, Hospitali imeendelea na shughuli za ukusanyaji wa damu katika jamii (Blood Donation Outreach Services). Zoezi hili limepunguza kwa kiasi kikubwa sana ukosefu wa damu Hospitalini na kufanya upatikanaji wa damu salama kufikia **asilimia 79** katika kipindi cha mwezi Julai 2017 hadi Machi, 2018. Vilevile, Hospitali imeendelea kutoa huduma ya uchunguzi na tiba kwa ugonjwa sugu wa homa ya Ini (Chronic Hepatitis B), kwa kushirikiana na “Centre for Diseases Control” (CDC) ya Marekani.

62. Mheshimiwa Spika, ukusanyaji wa mapato ya Hospitali kwa kipindi cha Julai 2017 hadi Machi, 2018 umeongezeka na kufikia kiasi cha **Shilingi bilioni 46.51** ikilinganishwa na **Shilingi bilioni 31.91** zilizokusanywa katika kipindi kama hicho 2016/17. Hii ni sawa na ongezeko la **asilimia 45.7**. Pia katika kipindi cha Julai hadi Machi 2018, Hospitali ilitoa huduma kwa wagonjwa wa msamaha zenye thamani ya **Shilingi bilioni 3.4** ikilinganishwa na huduma zenye gharama ya **Shilingi bilioni 2.21** zilizotolewa katika kipindi cha Julai hadi Machi, 2017.

Taasisi ya Mifupa Muhimbili (MOI)

63. Mheshimiwa Spika, Taasisi ya MOI imeendelea kutekeleza majukumu yake ya kutoa huduma ya matibabu ya mifupa, upasuaji mishipa ya fahamu na ubongo. Huduma hizi zimekuwa zikitolewa kwa weledi kwa kutumia wataalamu wazalendo. Kati ya Julai 2017 hadi Machi 2018, MOI imeshatoa matibabu ya upasuaji kwa **wagonjwa 4,001** kati yao; upasuaji mifupa wagonjwa 3,121 kubadilisha nyonga wagonjwa 120, goti wagonjwa 88, upasuaji wa uti wa mgongo wagonjwa 227, ubongo wagonjwa 94, na watoto wenye vichwa vikubwa na mgongo wazi wagonjwa 351. Aidha, mwezi Februari 2018, **Taasisi kwa mara ya kwanza imeweza kufanya upasuaji wa mgongo kwa njia ya matundu (Laparascopy) kwa kushirikiana na madaktari wa Hospitali ya BLK ya India**. Upasuaji huo ulifanyika kwa mafanikio makubwa, lengo mahsusi ikiwa ni kuwapatia weledi madaktari wa MOI ili waweze kufanya upasuaji huo.

64. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2017/18, Taasisi ilikamilisha jengo la MOI awamu ya III pamoja na ununuzi wa Vifaa tiba mbalimbali kutokana na fedha **Shilingi Bilioni 16.5** zilizopokelewa mwishoni mwa mwaka wa fedha 2016/2017. Kazi zilizofanyika ni pamoja na; kumalizia ujenzi wa jengo, Ununuzi wa vifaa tiba kwa ajili ya kutolea huduma katika Wodi za wagonjwa, Ununuzi wa mitambo na mashine zinazotumiwa kwenye vyumba vya upasuaji, Ununuzi wa vifaa tiba vya kufanyia wagonjwa mazoezi (Physiotherapy equipment), Ununuzi wa vifaa tiba vya chumba cha wagonjwa mahututi, na kitengo cha dharura, Ununuzi wa mashine za maabara, mashine za radiologia ikiwemo CT - Scan na MRI, Ununuzi wa mitambo ya hewa, kufulia umeme, na uchomaji wa taka zitokanazo na huduma za afya. Makusanyo katika Hospitali hii hadi mwezi Februari, 2018 yamefikia kiasi cha **Shilingi 10,807,695,141.93** ukilinganisha na kiasi cha **Shilingi 6,707,172,559.43** zilizokusanywa kuanzia mwezi Julai 2016 hadi mwezi Februari, 2017.

Taasisi ya Moyo - Jakaya Kikwete (JKCI)

65. Mheshimiwa Spika, Taasisi ya Moyo Jakaya Kikwete, ilihudumia jumla ya wagonjwa wenye matatizo ya moyo **42,029** kati ya hao, wagonjwa **1,440** walilazwa na wagonjwa wa nje walikuwa **40,589**. Aidha, kati ya hao wagonjwa 111, walifanyiwa upasuaji ambapo watu wazima walikuwa 52 na watoto walikuwa 59. Vilevile, Wagonjwa 157 walipatiwa matibabu kwa njia ya upasuaji wa moyo kupitia mshipa wa damu (cardiac catheterization interventions). Hivi sasa, **Taasisi ya Moyo Jakaya Kikwete inaweza kutoa huduma za upasuaji za ubingwa wa hali ya juu kwa asilimia 85** kwa huduma ambazo awali zilikuwa zikipatikana nje ya nchi. Hali hii imesaidia kupunguza rufaa za wagonjwa wa moyo nje ya nchi na kuipunguzia Serikali gharama ambapo hadi kufikia Machi 2018, wagonjwa wa moyo waliopolekwa India ni **12** kutoka wagonjwa **43** kwa mwaka 2016/17.

66. Mheshimiwa Spika, Taasisi kwa kushirikiana na Madaktari rafiki wa nchini Marekani walifanya kambi maalum ya matibabu ya umeme wa moyo kwa wagonjwa wenye mapigo ya moyo ambayo yako nje ya kiwango cha kawaida

kwa **kuwawekea betri maalum (pace maker)**. Jumla ya wagonjwa 11 walipatiwa matibabu kipindi cha kambi hiyo iliyofanyika mwezi Julai, 2017. Aidha, Taasisi ilipokea msaada wa vifaa vya chumba cha upasuaji ambavyo ni mashine ya usingizi na kitanda cha chumba cha upasuaji kutoka “Kuwait Fund” vyenye thamani ya **shilingi milioni 320**.

67. Mheshimiwa Spika, Taasisi kwa mara ya kwanza imefanya **upasuaji wa mishipa ya damu kwa kuunguza Laser therapy** ambapo wagonjwa wawili (2) walipatiwa huduma hii mwezi Septemba, 2017. Upasuaji huu umefanywa na Madaktari wa Taasisi kwa **asilimia 100**. Aidha, Madaktari wa Taasisi wamefanya **upasuaji wa moyo kwa kupandikiza mishipa ya moyo bila ya kusimamisha moyo (CABG off pump)** ambapo mgonjwa mmoja alinufaika na huduma hii kwa kipindi cha Julai-Desemba, 2017. Pia, Taasisi kwa kushirikiana na wataalam wa hospitali ya BLK ya nchini India ilitoa huduma za upasuaji maalum wa moyo (complex heart condition) ambapo jumla ya wagonjwa watatu walifanyiwa upasuaji mwezi Septemba, 2017.

Mheshimiwa Spika, Madaktari wa Taasisi kwa kushirikiana na Madaktari bingwa kutoka USA/Italy – “Mending Kids International” walitoa huduma za kibingwa kupitia Kambi ya matibabu iliyoendeshwa mwezi Oktoba, 2017 ambapo watoto 30 pamoja na watu wazima 26 walipatiwa huduma ya upasuaji maalum wa moyo kwa kupitia tundu dogo/ mishipa ya damu kutumia mtambo maalum (Cath lab). Pia, mwezi Novemba 2017, Taasisi ilifanya kambi maalumu ya upasuaji kwa watu wazima. Kambi hii ilihudumiwa na Madaktari bingwa kutoka “Saifee Hospital” ya nchini India kwa kushirikiana na Madaktari wa Taasisi ambapo jumla ya wagonjwa 14 walipatiwa matibabu haya.

68. Mheshimiwa Spika, katika kuimarisha ushirikiano na Taasisi za Kimataifa katika kutoa huduma za kibingwa, mnamo mwezi Novemba 2017, Taasisi ilifanya kambi ya upasuaji wa moyo bila kufungua kifua (Catheterization) kwa kutumia mishipa wa damu wa mkono ambapo jumla ya wagonjwa 33 walifanyiwa upasuaji huo. Aidha, katika kipindi

hicho Taasisi kwa kushirikiana na Madaktari kutoka SACH nchini Israel iliendesha kambi ya upasuaji wa moyo bila kufungua kifua (catheterization) kwa watoto wadogo ambapo jumla ya watoto 18 walipatiwa matibabu hayo. Vilevile, Mwezi Februari 2018, Taasisi kwa kushirikiana na madaktari kutoka Taasisi ya "Open Heart International" ya nchini Australia iliendesha kambi ya upasuaji wa kufungua kifua kwa watoto na watu wazima ambapo jumla ya wagonjwa 16 wenye matatizo ya moyo walipata matibabu hayo na kati ya hao, watoto walikuwa tisa na watu wazima saba.

69. Mheshimiwa Spika, katika kushiriki maadhimisho ya Siku ya Moyo mwezi Septemba, 2017, Taasisi ilitoa huduma ya vipimo vya afya kwa jamii ambavyo vilihusisha upimaji wa shinikizo la damu, upimaji wa uzito, urefu, na uwiano wa uzito na urefu (BMI) na upimaji wa kiwango cha sukari mwilini ambapo jumla ya watu 800 walipatiwa huduma hizo. Kati ya hao, Watu 400 waligundulika kuwa na matatizo mbalimbali ya kiafya ikiwa ni pamoja na shinikizo la juu la damu. Aidha, Taasisi imeweza kukusanya mapato ya jumla ya **Shilingi 8,462,092,000** Katika kipindi cha hadi Machi 2018 ikilinganishwa na kiasi cha **Shilingi 4,105,000,000.00** kilichokusanywa katika kipindi hicho mwaka 2016.

Taasisi ya Saratani Ocean Road (ORCI)

70. Mheshimiwa Spika, Wizara yangu imeendelea kutoa huduma kwa wagonjwa wa Saratani ambapo hadi kufikia mwezi Machi 2018, jumla ya wagonjwa **46,470** walipatiwa huduma. Kati ya hao, **43,599** ni wagonjwa wa nje na **2,871** ni wagonjwa ambao walilazwa. Aidha, Taasisi imeboresha tiba za mionzi ya nje kwa kufunga kifaa kiitwacho '*multi-leaf collimator*' katika mashine ya EQ80 ambacho kimenunuliwa kwa kushirikiana na Shirika la Nguvu za Atomiki Duniani (IAEA). Vilevile, Taasisi imenunua vyanzo vipya vya mionzi kupitia Bohari ya Dawa kwa gharama ya **shilingi 473,363,437.50**. Hatua hii imeboresha utoaji wa tiba ya mionzi ya ndani kwa kutibu **wagonjwa 70** kutoka **wagonjwa 30** kwa siku.

71. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2017/18, Taasisi imeanzisha huduma za wodi za binafsi ambayo ina vitanda **4 vya VIP na vitanda 20 vya binafsi**. Hatua hii imesaidia kuboresha huduma kwa wagonjwa wenye uhitaji huo na pia kuongeza mapato. Lengo la huduma hizi ni kuhakikisha kuwa wananchi wenye uwezo wa kuchangia gharama wanakaa katika wodi binafsi. Kukamilika kwa wodi binafsi kumechangia kuongezeka kwa makusanyo ya Taasisi, ambapo katika kipindi Julai 2017 hadi Machi 2018, jumla ya **shilingi 86,622,300** zilikusanywa ikilinganishwa na kiasi cha **shilingi 40,320,000** kilichokusanywa kwa kipindi cha mwaka 2016/17. Hii ni sawa na ongezeko la **asilimia 53**. Aidha, Taasisi imeendelea kuboresha utoaji huduma kwa kutumia mfumo wa kieletroniki uitwao INAYA na kwa sasa unatumika kwa **asilimia 80** katika sehemu za huduma. Hatua hii imewezesha upatikanaji wa huduma kuwa wa haraka zaidi na kuimarisha takwimu pamoja na kudhibiti upotevu wa mapato ya Taasisi.

72. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2017/18, Taasisi imetengeneza sehemu 3 za kusubiria, ambapo wagonjwa hukaa wakati wanasubiri huduma za uchunguzi na tiba. Maeneo hayo ni katika sehemu ya **mapokezi**, sehemu ya **tiba ya mionzi** na sehemu ya Kliniki ya Bima ya Afya. Hatua hii imefanya wagonjwa kuwa na sehemu nzuri na yenye utulivu wakati wakisubiri huduma katika Taasisi. Aidha, Taasisi inaendelea **kufunga mashine za tiba mpya na za kisasa za mionzi aina ya "Linear Accelerator"**, (LINAC) 2 na 'CT Simulator' (1) ambazo zimenunuliwa kwa gharama ya **shilingi 9,500,000,000**. Mashine hizo zitaiwezesha Taasisi kutoa huduma ya matibabu ya mionzi na kupunguza muda wa wagonjwa kusubiria tiba kutoka **wiki 6** sasa kufikia **wiki 2** na kuongeza ufanisi katika tiba inayotolewa. Vilevile, Taasisi tayari imewapeleka mafunzoni nje ya nchi watumishi 7 kwa ajili ya kuongeza ujuzi wa kutumia mashine hizo ambao ni Madaktari bingwa 2, Wataalamu wa tiba ya mionzi 2, *Medical physicist* 2 na *Bio-engineer* 1.

73. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2017/18, Hali ya upatikanaji wa dawa kwa wagonjwa wa saratani imeendelea kuimarika ambapo hadi kufikia Machi 2018

ilikuwa imefikia wastani wa **asilimia 85** na kwa wagonjwa wenye saratani ya mlango wa kizazi, matiti, tezi dume, njia ya chakula (oesophagus) na ngozi upatikanaji wa dawa imeendelea kuwa **asilimia 100**. Mafanikio haya yametokana na Serikali kuendelea kuchukua juhudi za makusudi katika kuboresha upatikanaji wa dawa za saratani katika Taasisi hii. Aidha, Taasisi imeendelea kuimarisha upatikanaji wa dawa katika duka la dawa la jamii la Taasisi ambapo dawa za saratani zinapatikana kwa kiwango cha **asilimia 100** kwa muda wote. Duka la Dawa la Jamii limeimarisha upatikanaji wa dawa muda wote hata kwa wagonjwa wa saratani wa kipato cha chini. Hatua hii inamaanisha kuwa endapo aina ya dawa haipatikani katika Duka la Dawa la bila malipo mgonjwa ataweza kuinunua katika Duka hili kwa gharama nafuu badala ya kuinunua kutoka maduka ya nje.

Hospitali ya Benjamin Mkapa –Dodoma

74. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2017/18, Hospitali imeendelea kutoa huduma kwa wagonjwa ambapo jumla ya Wagonjwa **39,527** walihudhuria na kupata matibabu. Kati ya hao, wagonjwa 38,511 walikuwa wa Nje na **1,016** walilazwa. Aidha, Hospitali imefunga na kuanza kutumia mashine na vifaa vya uchunguzi wa magonjwa mbalimbali ya binadamu, mashine hizo ni *MRI, CT-Scan, Mammography, General Purpose X-ray, Ultra sound* na vifaa mbalimbali vya maabara. Vilevile, jumla ya wagonjwa waliofanyiwa vipimo mbalimbali walikuwa 28,736, ikiwemo *Ultra-Sound* wagonjwa 3,745, *Plain X-Ray* wagonjwa 2,081, *Mammography* wagonjwa 46, *CT- Scan* wagonjwa 832, *MRI* wagonjwa 739, *Fluoroscopy* wagonjwa 139, *OGD* wagonjwa 342 na *Laboratory* wagonjwa 20,812.

75. Mheshimiwa Spika, Hospitali ilipokea msaada wa vifaa vya macho vyenye thamani ya shilingi milioni 300 kutoka shirikisho la kidini nchini Marekani liitwalo LDS pamoja na Taasisi ya matibabu ya macho iitwayo “Moran Eye Center”. Aidha, Hospitali kwa kushirikiana na Chuo Kikuu cha Dodoma (UDOM) na wafadhili hao toka nchini Marekani iliendesha Kambi ya uchunguzi na matibabu ya macho kwa siku 4 mwezi Machi, 2018 ambapo wananchi walipatiwa huduma za

vipimo mbalimbali. Vilevile, wataalam watatu wapo mafunzoni katika Hospitali ya Taifa Muhimbili kwa ajili ya kupata mafunzo ya matibabu ya saratani kwa watoto wadogo. Pia, Ujenzi wa Jengo la awamu ya II unaendelea kukamilishwa ikiwa ni pamoja na kupaka rangi, ufungaji wa mifumo ya maji safi na taka, ufungaji mifumo ya umeme na mfumo wa mashine za kupoza hewa.

76. Mheshimiwa Spika, Katika kuimarisha huduma za kibingwa, mnamo tarehe 22/3/2018, Hospitali kwa kushirikiana na TOKUSHIKAI Medical group kutoka nchini Japan, ilifanikiwa **kufanya upandikizaji figo kwa mara ya kwanza kwa mgonjwa mmoja mwenye umri wa miaka 51**. Hali ya mgonjwa inaendele vizuri na amepewa ruhusa kwenda nyumabani. Aidha, Matayarisho ya **kuanzisha huduma za upasuaji wa moyo** yapo katika hatua za mwisho za ukamilishwaji. Vile vile Hospitali iko katika hatua za mwisho za **kuanzisha huduma ya kusafisha damu** kwa wagonjwa wa figo kwa kutumia mashine maalum (Hemodialysis). Pia, hospitali imefanikiwa kuanzisha huduma za chumba cha wagonjwa mahututi (ICU). Upatikanaji wa dawa katika hospitali ilikuwa kwa **asilimia 95.2** kwa kipindi cha Julai 2017 hadi Machi 2018. Uwezo wa hospitali kukusanya mapato umeendelea kuimarika ambapo jumla ya **Shilingi 1,892,978,585** kimekusanywa hadi Machi 2018 ukilinganisha na **Shilingi 794,162,415** zilizokusanywa katika kipindi cha Julai 2016 hadi Februari 2017 kwa mwaka 2016/17.

Hospitali ya Taifa ya Afya ya Akili Mirembe

77. Mheshimiwa Spika, Hospitali ya Mirembe na Tasisi ya Isanga imeendelea kutoa huduma kwa wagonjwa wa afya ya akili. Kwa kipindi cha mwezi Julai 2017 hadi Machi 2018, jumla ya wagonjwa **153,951** walipatiwa tiba pamoja na huduma nyingine za utengemao wa akili katika Hospitali ya Mirembe. Kati ya hao **124,542** walikua ni wagonjwa wa ndani (yaani wagonjwa waliolazwa na **29,409** walikua ni wagonjwa wa nje.

Aidha, wagonjwa 42 wa Taasisi ya Isanga waliruhusiwa kurudi majumbani baada ya kupitia taratibu na idhini ya Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria kutolewa. Vilevile, kati ya wagonjwa 60 walioonwa na Bodi za Isanga, 55 wameombewa Ruhusa kwa Waziri wa Katiba na Sheria kutolewa baada ya kutimiza muda wao kisheria; mara baada ya kibali kutoka watasindikizwa makwao. Pia, katika kipindi cha mwezi Julai 2017 hadi Machi 2018 Taasisi ilipokea wagonjwa 61 kwa uchunguzi na kuandikiwa taarifa za kisheria ili kuweza kusaidia mahakama mbalimbali nchini.

78. Mheshimiwa Spika, hali ya upatikanaji wa dawa imeendelea kuimarika na kufikia zaidi ya **asilimia 90** kwa dawa muhimu za magonjwa ya akili. Hali ya upatikanaji wa dawa muhimu za magonjwa mengine ilikuwa zaidi ya **asilimia 80**. Aidha, hospitali imeendelea kutoa huduma za kibingwa kwa wagonjwa wa akili wa kawaida na wagonjwa wa akili walio na tuhuma za uvunjaji wa sheria kwa kuwafanyia uchunguzi, kutoa ushauri kwa mahakama, Tiba kwa umeme, Tiba kwa vikundi, Tiba kwa familia, Tiba kwa maongezi na Tiba kwa kazi (Occupational Therapy) kwa wataalamu wa kada mbalimbali ikiwemo madaktari bingwa wa afya ya Akili (Psychiatrist), Saikolojia (Clinical Psychologist), Mishipa ya fahamu (Clinical Neurologist) na wengine.

79. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2017/18, hospitali imeendelea na ujenzi wa Jengo la kuhudumia waathirika wa Dawa za kulevya lililopo chini ya Hospitali ya Mirembe katika eneo la Itega ambapo mkandarasi yupo katika eneo husika anaendelea na kukamilisha ujenzi ili huduma zianze kutolewa mapema. Aidha, hospitali imeendelea kujenga uwezo wa Watumishi kwa kuwapeleka mafunzoni kusomea fani mbalimbali kulingana na mahitaji ya Hospitali ambapo jumla ya watumishi 12 wapo masomoni katika kada za Udaktari, Uuguzi, Fiziotherapia, Maabara na kilimo. Kati ya hao daktari bingwa mmoja ameenda Nchini Nigeria kujiendeleza na fani ya ubingwa wa hali ya juu katika kuwahudumia wagonjwa wa akili watoto na vijana. Mara baada ya kurejea Hospitali inategemea kuwa na utaalumu

wa kibingwa wa hali ya juu katika kuhudumia watoto wenye shida ya akili. Vilevile, Hospitali imepokea watumishi wapya 10 wa kada mbalimbali ili kukabiliana na upungufu wa watumishi wa hospitali ya Mirembe, kati ya watumishi waliopokelewa ni wauguzi 5 na wahudumu wa afya 5.

Hospitali ya Rufaa ya Magonjwa ya Kifua Kikuu- Kibong'oto 80. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka 2017/18, Hospitali iliendelea kutoa huduma za utambuzi na matibabu ya Kifua kikuu, Kifua kikuu sugu, VVU na magonjwa mengine ya kuambukiza. Katika kipindi hiki, Hospitali imetoa huduma kwa Wagonjwa **16,300**. Aidha kati ya Wagonjwa hao wagonjwa wa Kifua Kikuu walikuwa **235**, Kifua Kikuu Sugu (MDR-TB) wagonjwa **290**, wagonjwa wa Kifua Kikuu na Ukimwi (TB/HIV) **2,034** na Magonjwa ya kawaida wagonjwa **13,741**. Vilevile, Hospitali imeweza Kutoa elimu kwa wataalamu 239 (Madaktari, wauguzi, wataalam wa maabara pamoja na wafamasia) kutoka mikoa mbalimbali nchini kwa ajili ya kuwajengea uwezo wa kuanzisha matibabu ya kifua kikuu sugu (Multi-Drug Resistant TB, MDR TB). Pia Hospitali imeweza kuzindua jengo la kutolea huduma kwa waathirika mahala pa kazi (occupational Health Services). Pia, Wizara kwa kushirikiana na Southern African Development Community (SADC) imeanzisha huduma za afya kwa wachimbaji Madini na familia za Wachimbaji Madini.

81. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka 2017/18, Hospitali imeanzisha huduma za Fiziotherapia kwa wagonjwa wenye mapafu yenye uwezo hafifu kutokana na TB, madhara ya vumbi kwa wachimbaji madini na matibabu mengine yanayohitaji mazoezi ya viungo. Hospitali imeweza kuhudumia wagonjwa wote wa Kifua Kikuu Sugu (DR-TB) ambao walilazwa kwa kuwapima uwezo wao wa mapafu mwanzoni mwa matibabu na kuanzisha programu ya kutibu mapafu kwa wale wenye uwezo hafifu wa Mapafu. Aidha, **hali ya upatikanaji wa dawa muhimu katika hospitali ni asilimia 90**. Vilevile hospitali imeweza kusambaza dawa za mstari wa pili za kupambana na Kifua Kikuu (second line anti TB medicine) katika mikoa yote 26 nchini ambayo ina wagonjwa wenye kifua Kikuu Sugu (MDR-TB).

Hospitali ya Rufaa Kanda ya Nyanda za Juu Kusini Mbeya

82. Mheshimiwa Spika, hospitali ya Rufaa Kanda ya Nyanda za Juu Kusini Mbeya ilihudumia jumla ya wagonjwa **131,982** kutoka mikoa 7 ambayo ni Katavi, Rukwa, Songwe, Mbeya, Ruvuma, Njombe na Iringa. Kati ya hao, wagonjwa **14,982** walilazwa na wagonjwa **117,000** walikuwa ni wagonjwa wa nje. Katika kipindi cha 2017/18, Hospitali imeendelea kuboresha huduma za kibingwa kwa kuongeza miundombinu ya kutolea huduma. Ukarabati wa kupanua jengo la kutolea huduma za dharura unaendelea ambapo baada ya kukamilika kutakuwa na ongezeko la vyumba vya ushauri (consultation rooms) 3 na chumba chenye vitanda 3 kwa ajili ya kuhudumia wagonjwa mahututi. Chumba cha awali kimefanyiwa maboresho na kuweza kuwa na vitanda 2 vya kuhudumia wagonjwa mahututi. Kwa ujumla hospitali itakuwa na uwezo wa kuhudumia wagonjwa mahututi 5 kwa wakati mmoja. Aidha, eneo la mapokezi ya wagonjwa limepanuliwa kwa lengo la kupunguza msongamano wa wagonjwa na kuwapunguzia muda wa kupatiwa huduma. Vilevile, jengo la huduma za Uzazi na Mtoto (RCH) katika kitengo cha wazazi Meta limepanuliwa kwa kuongezwa vyumba vinne pamoja na sehemu ya kusubiria. Ujenzi wa wodi za watoto uliotekelezwa kwa kutumia fedha za ndani umekamilika na kuongeza vitanda vya hospitali kufikia **553** kutoka vitanda **477** vya mwaka 2016/17.

83. Mheshimiwa Spika, Katika kuboresha huduma katika hospitali ya Kanda ya Rufaa ya Mbeya, Wizara inatarajia kupokea madaktari wanne (4) kutoka nchini China ambao ni wa fani za usingizi, mifupa, upasuaji wa watoto na ICU. Aidha, Upatikanaji wa dawa katika hospitali ya kanda ya rufaa Mbeya umekuwa katika kiwango cha **asilimia 95** hivyo wananchi wameondolewa usumbufu wa kufuata dawa nje ya hospitali. Aidha , Ukusanyaji wa mapato katika kipindi cha Julai 2017 hadi Machi 2018 yalikuwa **Shilingi 9,931,439,974.57** ukilinganisha na **Shilingi 5,607,223,511.78** kwa mwaka 2016/17.

Hospitali ya Rufaa ya Kanda ya Ziwa Bugando

84. Mheshimiwa Spika, Hospitali ya Rufaa ya Kanda ya Ziwa, Bugando imeendelea kutoa huduma za kibingwa kwa wagonjwa kutoka mikoa 8 ya Kanda ya Magharibi na Kanda ya Ziwa ambayo ni Mwanza, Geita, Mara, Kagera, Simiyu, Kigoma, Shinyanga na Tabora. Katika mwaka 2017/18, Hospitali ilihudumia jumla ya wagonjwa **128,101** ambapo wagonjwa wa nje walikuwa **108,738** na wagonjwa wa kulazwa ni **19,363**. Kwa kipindi cha Julai hadi Machi 2018, hospitali ilifanya upasuaji kwa wagonjwa **72** wenye matatizo ya Saratani ya Utumbo mpana, saratani za tumbo, magonjwa ya pua na koo pia uti wa mgongo. Upasuaji huu ulifanywa na Madaktari wazalendo kwa kushirikiana na madaktari kutoka Marekani (Mending Kids). Pia, Hospitali imenunua Mashine ya kutibu mionzi ya ndani (Brachytherapy) kwa kushirikiana na Shirika la nguvu la Atomiki Duniani (IAEA). Kuhusu Huduma ya tiba ya saratani, jumla ya wagonjwa **131** wa saratani ya mlango wa kizazi walipatiwa huduma ya tiba ya saratani kwa njia ya mionzi (Radiotherapy).

85. Mheshimiwa Spika, kuanzia mwezi Novemba 2017, Hospitali imeanzisha Kliniki za kibingwa ambazo zinafunguliwa baada ya masaa ya kawaida ya kazi ambapo hadi sasa, zaidi ya wagonjwa **1,000** wamehudumiwa kupitia utaratibu huo. Huduma nyingine ya Kibingwa zilizotolewa ni pamoja na usafishaji damu kwa wagonjwa wenye figo zisizo na uwezo wa kufanya kazi (Haemodialysis), ambapo jumla ya wagonjwa **48** wamepata huduma hii kwa mizunguko **1,436**. Aidha, hospitali imeendelea kuimarisha huduma ya uchunguzi wa magonjwa kwa kununua na kufunga mashine 6 mpya kwa ajili ya vipimo mbalimbali vya damu. Pia Hospitali imenunua mashine 2 za vipimo vya moyo na 1 ya ultrasound, pamoja na mashine ya **CT Scan (128 slice)** kwa gharama ya **Shilingi bilioni 1.7** kutokana na mapato ya ndani.

Hospitali ya Rufaa ya Kanda Kaskazini (KCMC)

86. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2017/18, Hospitali imeendelea kuboresha na kutoa huduma kwa wananchi wa

mikoa ya Kilimanjaro, Arusha, Manyara na Tanga ambapo kati ya Julai 2017 na Machi 2018, jumla ya wagonjwa **143,665** walihudumiwa. Kati ya hao, wagonjwa **16,551** walilazwa na wagonjwa **127,114** ni wa nje.

87. Mheshimiwa Spika, Hospitali imeweza kuhudumia wagonjwa **1,123** wa saratani ambapo wagonjwa 47 walipatiwa huduma shufaa (Palliative care). Aidha, kwa kuzingatia umuhimu wa elimu kwa jamii juu ya maradhi ya saratani, Hospitali kwa kushirikiana na Taasisi ya "Mission Eine Welt" ya nchini Ujerumani, imeanzisha kampeni maalum ijulikanayo kama PrevACamp yaani *Prevention and Awareness Campaign* yenye lengo la kutoa elimu juu ya saratani, kuainisha mila na imani potofu na kufanya uchunguzi wa viashiria vya awali vya saratani. Kampeni hii ilianza Mwezi Oktoba 2017 kwa kambi ya wiki moja ya uchunguzi iliyofanyika katika hospitali ya KCMC ambapo jumla ya wananchi **1,006** (wanawake **915** na wanaume **91**) walijitokeza kufanyiwa uchunguzi wa awali na mwezi Februari 2018 ilifanyika Kambi nyingine huko Machame ambapo jumla ya wananchi **300** (wanawake **232** na wanaume **68**) waliweza kufanyiwa uchunguzi wa awali wa viashiria.

88. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2017/18, Hospitali imeboresha huduma ya Afya ya Kinywa na Meno kwa kununua viti maalum vya wagonjwa na mashine maalum za X-ray za kinywa. Aidha, hospitali imeongeza vyumba vya kutolea huduma kutoka vitatu (3) vya awali hadi vitano (5). Vilevile, hospitali imendelea kutoa huduma ya kusafisha damu kwa kutumia mashine (Hemodialysis), ambapo jumla ya wagonjwa **107** (wanaume 74 na wanawake 33) wamehudumiwa ambapo jumla ya mizunguko **1,865** ya usafishaji wa damu kwa kutumia figo bandia ilifanyika kwa wagonjwa hawa. Pia, hospitali kwa kushirikiana na Shirika la Msamaria Mwema (GSF), Hospitali imefungua duka jipya la dawa na hivyo kuwezesha upatikanaji wa dawa muhimu kwa wagonjwa.

Hospitali za Rufaa za Mikoa

89. Mheshimiwa Spika, Uendeshaji wa Hospitali za Rufaa za Mikoa ulikuwa unasimamiwa na kuratibiwa na OR-TAMISEMI. Hata hivyo, baada ya maelekezo ya Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania aliyoyatoa tarehe 25 Novemba 2017, usimamizi na uendeshaji wa Hospitali hizi sasa upo chini ya Wizara ya Afya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto. Hospitali za Rufaa za Mikoa zilizopo ni 28.

90. Mheshimiwa Spika, Pamoja na huduma za matibabu za kawaida, Hospitali za Rufaa za Mikoa hutoa huduma za kibingwa ambazo hazitolewi katika hospitali ngazi ya Halmashauri/Wilaya. Huduma muhimu za kibingwa zinazopaswa kutolewa katika Hospitali za Rufaa za Mikoa ni pamoja na: Upasuaji (General Surgery), Magonjwa ya Wanawake na Uzazi (Obstetrics & Gynaecology), Magonjwa ya Watoto (Paediatrics & Child Health), Magonjwa ya ndani (Internal Medicine), Magonjwa ya Kinywa na Meno (Dentistry) na Radiolojia (Radiology). Wizara imeweka mikakati ya muda mfupi, muda wa kati na mrefu ili kuhakikisha kwamba huduma zinazotolewa katika Hospitali hizo zinaboreshwa. Mikakati hiyo ni pamoja na **kuboresha miundombinu ya kutoa huduma, kuongeza idadi ya madaktari bingwa, kuboresha upatikanaji wa dawa**, kupanga kwa uwiano watumishi wa Hospitali za Rufaa za Mikoa kwa kuzingatia huduma na uzito wa kazi zinazotolewa na hospitali hizo, kuanzisha na kuboresha huduma za afya kwa njia ya masafa (**telemedicine**) kwa kila Hospitali ya Rufaa ya Mkoa na kufanya huduma hiyo kutumika kama kiunganishi kati ya Hospitali hizo na Hospitali za Rufaa za Kanda na Taifa, kuboresha utoaji wa huduma za uchunguzi wa maabara na radiolojia kwa kupanua na kuimarisha miundombinu ya huduma za uchunguzi ikiwa ni pamoja na kununua na kuweka vifaa vya kisasa vya maabara na radiolojia.

91. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha Julai 2017 hadi Machi 2018, Hospitali za Rufaa za Mikoa (28) zilihudumia jumla ya wagonjwa **1,637,835** ambapo wagonjwa wa nje

walikuwa **1,329,364** na wagonjwa wa ndani walikuwa **308,471** kama inavyooneshwa kwenye **kiambatisho namba 3**

Udhibiti wa Magonjwa Yasiyo ya Kuambukiza (NCDs)

92. Mheshimiwa Spika, Napenda kulitaarifu Bunge lako Tukufu kwamba kumekuwa na ongezeko la Magonjwa Yasiyo ya Kuambukiza hapa nchini. Utafiti wa viashiria vya magonjwa yasiyo ya kuambukiza uliofanywa na Wataalam wa Wizara kwa kushirikiana na Taasisi ya utafiti wa magonjwa ya binadamu (NIMR) mwaka 2012, ulionesha kuwa kuna ongezeko kubwa la viashiria vinavyosababisha magonjwa yasiyo ya kuambukiza. Utafiti huo ulionesha kuwa asilimia 15.9 ya wananchi wanavuta sigara, asilimia 29.3 wanakunywa pombe, asilimia 97.2 wanakula mboga mboga na matunda chini ya mara tano kwa wiki. Aidha utafiti ulionesha kuwa, asilimia 26 ya wananchi ni wanene kupita kiasi, asilimia 26 wana lehemu nyingi mwilini, asilimia 33.8 wana mafuta mengi mwilini, asilimia 9.1 wana kisukari na asilimia 25.9 wana shinikizo kubwa la damu. Utafiti pia ulionesha kwamba, asilimia 25 ya wananchi waliohojiwa hawajishughulishi na kazi zinazotumia nguvu na hawafanyi mazoezi yeyote.

93. Mheshimiwa Spika, mapambano dhidi ya magonjwa yasiyo ya kuambukiza yamekuwa yakiendelea ndani ya Wizara yangu na yamejikita zaidi katika masuala ya Kinga, kama tunavyofahamu kuwa **Kinga ni bora kuliko Tiba**. Tangu kuanzishwa kwa kampeni ya **"Afya Yangu Mtaji Wangu"** ilizinduliwa na **Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan**, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Wizara imeendelea kuhimiza jamii kuhusu umuhimu wa kufanya mazoezi mara kwa mara sambamba na kujepusha na visababishi vingine vya magonjwa yasiyo ya kuambukiza ikiwemo ulevi kupita kiasi na uvutaji wa sigara na tumbaku. Aidha, Wizara imeendelea kushirikiana na Wadau kufanya Kampeni za uchunguzi wa magonjwa yasiyo ya kuambukiza katika Mikoa yote. Nitumie fursa hii kulipongeza Bunge lako tukufu kwa kuanzisha Jukwaa la Waheshimiwa Wabunge la Kupambana na Magonjwa Yasiyo ya Kuambukiza ili waweze kupata elimu namna ya kujikinga na Magonjwa Yasiyo ya

Kuambukiza na kuwaelimisha wananchi juu ya magonjwa hayo.

94. Mheshimiwa Spika, Kuhusiana na suala la kupambana na athari za matumizi ya madawa ya kulevya, tunavyo jumla ya vituo 5 nchini kwa sasa vinavyotoa matibabu kwa waathirika wa dawa za kulevya kwa kutumia dawa ya *Methadone*. Vituo hivi vipo Hospitali ya Taifa ya Muhimbili, Hospitali ya Mwananyamala na Temeke (Mkoa wa Dar es Salaam), Itega (Dodoma), Hospitali ya Sekou Toure (Mwanza) na Hospitali ya Rufaa Mbeya. Hadi kufikia Machi 2018, vituo hivi vilikuwa vimesajili waathirika wa dawa za kulevya wapatao **5,560**. Pamoja na kutibu uraibu, vile vile vituo hivi vinatoa matibabu ya magonjwa yanayoambatana na matumizi ya dawa za kulevya kama vile VVU/UKIMWI, Kifua kikuu, Homa ya ini (Hepatitis B na C) pamoja na magonjwa mengine yanayowapata watumiaji wa dawa za kulevya. Kwa sasa, dawa ya *Methadone* inapatikana katika mfumo rasmi wa ununuzi, Utunzaji na Usambazaji kwa kutumia Bohari ya Dawa (MSD). Hatua hii, inasaidia kuhakikisha kuwa vituo vyote vilivyofunguliwa na vitakavyo funguliwa vitapata dawa ya kutosha na kwa wakati.

Upatikanaji wa Damu Salama

95. Mheshimiwa Spika, Katika kuhakikisha upatikanaji wa uhakika wa damu salama, Mpango wa Taifa wa Damu Salama umeendelea kukusanya, kuhifadhi na kusambaza damu salama katika vituo vya kutolea huduma za afya. Katika kipindi cha kuanzia Julai 2017 hadi Machi 2018 Mpango ulifanikiwa kukusanya idadi ya chupa za damu **233,953** ambazo ni sawa na **asilimia 101** ya lengo la makusanyo kwa mwaka ambalo lilikuwa ni kukusanya chupa za damu **230,000**. Aidha, chupa zote za damu (**233,953**) zilizokusanywa zilipimwa makundi ya damu pamoja na magonjwa makuu manne ambayo ni UKIMWI (HIV), Homa ya ini (HBV & HCV) na kaswende (syphilis) kabla ya kugawa kwenye vituo vya kutolea huduma kabla ya kuzitoa kwa wahitaji. **Nitumie Bunge lako Tukufu kuwashukuru wananchi wote wanaojitolea kuchanga damu. Aidha nitoe rai kwa wataanzania kuchangia**

damu mara kwa mara ili kuokoa maisha ya wagonjwa hasa wanawake wajawazito na watoto wa umri chini ya miaka 5.

Huduma za uchunguzi wa Magonjwa

96. Mheshimiwa Spika, Wizara imeendelea kuboresha huduma za maabara ambapo hadi kufikia mwezi Agosti 2017, jumla ya maabara 76 kutoka maabara 66 katika mwaka 2016 ambazo zipo katika ngazi za Mikoa, Wilaya na Vituo vya Afya, zilishiriki kwenye utaratibu wa Shirika la Afya Duniani wa kutoa Ithibati hatua kwa hatua, na kupewa nyota za viwango vya ubora wa huduma za maabara. Maabara **33** ziliweza kupata kuanzia nyota moja **(1)** mpaka nne **(4)** za viwango vya ubora. Aidha, Maabara za Taifa, Kanda, Maalum na zile za Binafsi kumi **(10)** zimepata ithibati ya SADCAS ya kiwango cha kimataifa yaani **ISO 15189:2012**. Maabara hizo ni Maabara ya Taifa ya Afya ya Jamii (NHLQATC), Hospitali ya Kanda Bugando (BMC), Hospitali ya Kanda Mbeya (MRH), Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH), Kilimanjaro Christian Medical Centre (KCMC), Hospitali ya Mnazi Mmoja (Zanzibar), Hospitali ya Aga Khan, Maabara ya Lancet, Hospitali ya Mission Ndanda na Hospitali maalum ya Kibong'oto. Pia, Wizara inaendelea na ujenzi wa maabara ya Taifa ya Afya ya Jamii katika eneo la Mabibo, Dar es salaam. Mradi huu hadi kukamilika unatarajiwa kutumia kiasi cha **Shilingi 7,493,193,434.97.00**, zinazotolewa na Benki ya Dunia.

97. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2017/18, Wizara imeendelea kuboresha huduma na ubora wa vipimo katika maabara za tiba na afya ya jamii. Kupitia Maabara kuu ya Taifa ya Afya ya Jamii, serikali imeendelea kuimarisha ubora wa vipimo vya VVU katika vituo vinavyotoa huduma hii nchini kwa kuhakikisha vinapelekewa vipimo vya uhakiki wa ubora, kutoka 4,500 hadi 5,400 kutoka mwaka 2017 hadi 2018 na tunatarajia kuongeza vituo vingine 600 kabla ya mwisho wa mwaka 2018. Pia katika mpango huu wa kuhakiki ubora zaidi ya matoleo 80 ya vitendanishi vya kupima VVU na Malaria

yamefanyiwa uhakiki kabla ya kusambazwa kwa watumiaji nchini kwa kipindi cha mwaka 2017/18.

98. Mheshimiwa Spika, ili kupambana magonjwa ya mlipuko serikali inaendelea na juhudi za kuimarisha upimaji wa magonjwa ya mlipuko, ikiwemo kuimarisha mfumo wa kusafirisha sampuli nchini, kutoa mafunzo kwenye maabara za Rufaa za Mikoa zilizoko mikoa ya mipakani katika utambuzi wa magonjwa ya Mlipuko, ambapo maabara 11 zimewezeshwa kupima na kutambua magonjwa ya mlipuko na usugu wa vimelea vya magonjwa. Utaratibu huu utaendelea kwa awamu kwa maabara nyingine zilizobakia ili kuhakikisha kuwa maabara zote zinapata uwezo huu. Aidha, maabara ya Taifa ya Afya ya Jamii (Public Health Laboratory) inayojengwa na serikali katika eneo la Mabibo (Dar es Salaam) itasaidia kuboresha huduma za uchunguzi wa Magonjwa ya mlipuko. Maabara hii itafanya kazi kwa kushirikiana na Maabara kuu ya Taifa pamoja na ile iliyopo katika Hospitali ya Rufaa ya Mbeya katika kudhibiti magonjwa haya. Vilevile, Serikali kupitia Jumuiya ya Afrika Mashariki kwa ushirikiano na serikali ya Ujerumani inatarajia kuanzisha maabara 3 zinazohamishika, hali itakayosaidia ugunduzi wa magonjwa katika maeneo husika kwani tutaweza kutumia gari maalum iliyobeba vifaa vya maabara hadi eneo la tukio la mlipuko na hivyo kuharakisha uchunguzi, tiba na njia nyingine za kinga.

99. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2017/18, Wizara imeendelea kuboresha na kutoa huduma za **uchunguzi wa magonjwa kwa njia ya Radiolojia** katika hospitali zenye mashine hizo za uchunguzi (Ultrasound, X-ray, CT, MRI). Vilevile, Serikali imeandaa Mwongozo wa vifaa vya radiolojia nchini 'Standard Medical Radiology and Imaging Equipment Guidelines). Aidha, Wizara inakamilisha taratibu za kupokea mashine za kidijitali 34 kutoka kampuni ya Philips ambapo Awamu ya Kwanza itahusisha Hospitali kumi (10) za Umma za Rufaa za Mikoa ya **Manyara, Kagera, Ruvuma, Singida** na ya Halmashauri za **Nzega, Magu, Mpanda, Songwe, Njombe na Bariadi**.

100. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2017/18, Wizara imeendelea kuboresha **huduma za ufundi wa vifaa na vifaa tiba** kwa kuwa zina umuhimu mkubwa katika utoaji wa huduma za Afya katika ngazi zote. Wizara kwa kushirikiana na Serikali ya Korea kupitia taasisi ya KOFIH ilitoa mafunzo ya ujuzi wa kufanya matengenezo ya vifaa vyenye teknolojia za kisasa ikiwa ni pamoja na vifaa vya chumba cha upasuaji, Maabara, Utakasishaji, Radiolojia, Wodi ya Wazazi, dharura na wodi ya wagonjwa mahututi kwa mafundi 30 wa vifaa tiba kutoka katika Hospitali ya Taifa Muhimbili, Hospitali Tatu (3) za kanda, Hospitali 2 za tiba maalum, Hospitali Nne(4) za mikoa, Hospitali Saba (7) za Wilaya, Hospitali mbili (2) za Jeshi(JWTZ 1 na Polisi 1), Bohari ya Dawa (MSD) na vyuo viwili (2).

Huduma za Tiba Asili na Tiba Mbadala

101. Mheshimiwa Spika, Wizara inatambua mchango wa huduma za Tiba Asili na Tiba Mbadala katika utoaji wa huduma za afya nchini. Katika kipindi cha kuanzia Julai 2017 hadi Machi 2018, Serikali imeendelea kutoa elimu kuhusu Sera, Sheria, Kanuni na Miongozo mbalimbali kupitia njia za mitandao ya kijamii, magazeti, radio na runinga. Aidha, Wataalam na watafiti **24** wa Tiba Asili kutoka Taasisi za ITM-MUHAS, NIMR na GCLA wamekuwa wakipata mafunzo kutoka kwa wataalam **watatu (3)** kutoka Jamhuri ya Watu wa China kuhusu namna bora ya kutafiti na kutengeneza dawa za asili. Vilevile, Waganga wa tiba asili **107** walipata elimu kuhusu **usajili wa dawa** za asili, na kwa kushirikiana na ITM-MUHAS, waganga **25** wa tiba asili walipata mafunzo ya muda mfupi (siku 7) kuhusu namna bora ya kuandaa dawa za asili.

Upatikanaji wa Dawa, Vifaa, Vifaa Tiba na Vitendanishi

102. Mheshimiwa Spika, Katika kipindi cha Julai 2017 hadi Machi 2018, Wizara yangu imeendelea kuhakikisha kwamba hali ya upatikanaji wa dawa, vifaa, vifaa tiba na vitendanishi katika vituo vya kutolea huduma za afya vya umma inaendelea kuimarika. Hali ya upatikanaji wa dawa, vifaa,

vifaa tiba na vitendanishi katika Bohari ya Dawa (MSD) imeendelea kuimarika hadi kufikia wastani wa **asilimia 81** kwa Dawa muhimu 135. Aidha, katika kipindi hicho, hali ya upatikanaji wa dawa, vifaa, vifaa tiba, vitendanishi na chanjo ilifikia **asilimia 92 kwenye vituo vya kutolea huduma za afya nchini**. Vilevile, kutokana na kuendelea kuwasili kwa dawa, vifaa, vifaa tiba, vitendanishi na chanjo nchini, na kwa mujibu wa mikataba iliyopo kati ya wazalishaji na Bohari ya Dawa, hali ya upatikanaji wa dawa kwenye hospitali inatarajiwa kuimarika na kufikia asilimia 89 ifikapo mwishoni mwa mwezi Aprili 2018.

103. Mheshimiwa Spika, katika kupunguza gharama za ununuzi wa Dawa, vifaa, vifaa tiba na vitendanishi na kuongeza upatikanaji wake, Wizara kupitia Bohari ya Dawa imeingia Makubaliano ya muda mrefu (Framework Agreement) na wazalishaji wa dawa 110 na kati ya hao 10 ni wazalishaji wa ndani. Aidha, hatua hii imesaidia kupunguza bei ya dawa kwa wastani wa **asilimia 40**, ukilinganisha na bei ya zamani ya mawakala au washitiri wa kawaida kabla ya utaratibu wa kununua dawa moja kwa moja kutoka kwa wazalishaji. Vilevile, hadi kufikia Machi 2018, Wizara ilikuwa imepokea Jumla ya **Shilingi 70,940,858,412** kwa ajili ya ununuzi wa dawa Vifaa, Vifaa Tiba na chanjo. Kati ya fedha hizo **Shilingi 59,917,232,844.00** ni kwa ajili ya ununuzi wa dawa, vifaa, vifaa tiba na vitendanishi na **Shilingi 10,838,846,362.00** kwa ajili ya ununuzi wa chanjo.

104. Mheshimiwa Spika, mbali na kuongezeka kwa hali ya upatikanaji wa dawa, vifaa, vifaa tiba na vitendanishi, matumizi yasiyo sahihi ya dawa yamezidi kuongezeka hasa matumizi yasiyo ya lazima ya dawa aina ya antibiotiki na uchomaji wa sindano usiokuwa wa lazima. Aidha, tabia ya baadhi ya wagonjwa kwenda moja kwa moja kwenye maduka ya dawa na kununua dawa bila ushauri wa daktari wala kuwa na cheti cha dawa imeendelea kuongezeka na hivyo kuathiri matumizi sahihi ya dawa nchini. Vilevile, baadhi ya wagonjwa kusitisha matumizi ya dawa kabla ya muda sahihi wa matumizi pale tu wanapojisikia wamepata unafuu.

105. Mheshimiwa Spika, Katika kukabiliana na changamoto hiyo Wizara yangu ilifanya yafuatayo:

- i. Kuandaa Mkakati wa uhamasishaji Jamii juu ya matumizi sahihi ya dawa nchini (Communication Strategy To Promote Rational Use of Medicines to the Community)
- ii. uzinduzi Mpango wa Taifa wa kupambana na usugu wa dawa aina ya *antimicrobials* (National Action Plan on antimicrobial resistance) na unaendelea kutekelezwa.
- iii. Kupitia Kitengo cha Huduma za Dawa (PSU) Wizara ilishiriki katika vipindi mbalimbali vya Radio na Runinga katika kuelimisha Jamii juu ya matumizi sahihi ya dawa.
- iv. Kamati za Dawa na Tiba zimeundwa katika Hospitali zote nchini ili kusimamia matumizi sahihi ya dawa. Vilevile, kamati za Uendeshaji za vituo vya Afya na Zahanati zimeendelea kuhimizwa kusimamia matumizi sahihi ya dawa katika maeneo yao.

106. Mheshimiwa Spika, Katika kutekeleza maagizo ya Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya kuanzisha viwanda vya dawa Nchini ili kuongeza upatikanaji wa dawa na vifaa tiba, Wizara yangu kwa kushirikiana na Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji iliweza kuandaa mkutano mkubwa kwa lengo la kuwaleta pamoja wawekezaji wenye nia ya kuwekeza katika viwanda vya dawa na vifaa tiba. Jumla ya wadau mia nne thelathini **(430)** walihudhuria mkutano huo na wawekezaji thelathini na nane **(38)** walijitokeza kuwekeza katika uzalishaji wa dripu (*infusion*), uzalishaji wa bomba za sindano, uzalishaji wa vifungashio vya dawa, uzalishaji wa bidhaa za pamba zinazotumika hospitalini, uzalishaji wa dawa za kuhifadhi maiti. Aidha, Serikali imeweka utaratibu maalumu wa kuwafuatilia wawekezaji hawa walionyesha nia ili kuhakikisha wanafanikiwa katika azma yao ya kuwekeza. Serikali itaendelea kuhakikisha inatoa fursa ya soko la kutosha kwa dawa na vifaa tiba vitakavyozalishwa hapa nchini kwa kutenga bajeti ya kukidhi mahitaji ya dawa na vifaa tiba

nchini. Uwepo wa Viwanda hivyo utawezesha Serikali kuokoa fedha nyingi za kigeni zinazotumika kuagiza dawa toka nje ya nchi. Jitihada hizi zitasaidia kuongeza uzalishaji wa ndani ambao kwa sasa hivi ni asilimia 6 hivyo na kupunguza kiwango cha uagizaji wa dawa nje ya nchi ambao kwa sasa ni asilimia 94.

UHAKIKI UBORA WA HUDUMA ZA AFYA

107. Mheshimiwa Spika, Wizara imeendelea kufanya Uhakiki na Ukaguzi kwa vituo vya kutolea huduma za Afya. Katika kipindi cha Julai 2017 hadi Machi 2018, Wizara ilifanya zoezi la tathmini ya mara ya pili (re-assessment) ya kutoa nyota kulingana na ubora kwa Vituo vya Kutolea Huduma za Afya ya Msingi (Zahanati, Vituo vya Afya na Hospitali katika Halmashauri/Wilaya) katika mikoa 14 ya Dar es Salaam, Iringa, Geita, Kagera, Katavi, Kigoma, Mara, Mwanza, Pwani, Tanga, Tabora, Singida, Simiyu na Shinyanga. Jumla ya Vituo **3,856** vilipewa hadhi ya nyota kulingana na ubora wa huduma zinazotolewa. Vigezo vinavyotumika kupima ubora wa huduma ni pamoja na uongozi wa kituo, upatikanaji wa dawa, utendaji kazi wa watumishi, ubora wa huduma za maabara, ushirikishwaji wa wananchi, huduma za tiba ya dharura na rufaa, vifaa, vifaa tiba na vitendanishi na matumizi ya takwimu. Katika matokeo ya tathmini ya awali ya mwaka 2016, jumla ya vituo **1,244** sawa na **asilimia 33** ya vituo vyote **3,713** vilivyofanyiwa tathmini ya ubora katika mikoa **vilipata nyota sifuri** na vituo **62** sawa na **asilimia 2 vilipata nyota 3 au zaidi**, ukilinganisha na tathmini ya mara ya pili iliyofanyika mwaka 2017/18 katika mikoa 14, ambapo vituo 180 sawa na **asilimia 4.7 tu ndivyo vimepata nyota sifuri na Vituo 749 sawa na asilimia 19.4 vilipata nyota 3 na zaidi**. Matokeo haya ya tathmini ya pili yameonesha kuimarika kwa ubora wa huduma katika vituo hivyo, ambako ndio wananchi wengi wanapata huduma kama ilivyochambuliwa katika **Kiambatisho Na 4** limefafanua zaidi.

108. Mheshimiwa Spika, Mipango ya Uimarishaji Ubora wa huduma za afya kwa kila Kituo iliandaliwa na utekelezaji unaendelea kwa kushirikiana na Timu za Uendeshaji Afya za

Halmashauri. Aidha, Wizara imekamilisha Mwongozo wa viwango vya kutolea huduma katika hospitali za rufaa ngazi ya Mkoa, Kanda na Taifa. Kwa kutumia viwango hivi, tayari tathmini imefanyika katika Hospitali za Rufaa za mikoa ya Mbeya, Tanga, Lindi, Mtwara, Kigoma, Kagera, Geita, Mara, Mwanza na Shinyanga ili kupima Ubora wa Huduma za Afya katika hospitali hizo. Matokeo ya tathmini hiyo yanaonesha kuwa Hospitali nne (Geita, Kigoma, Mara na Shinyanga) zimepata nyota moja na hospitali sita (Kagera, Lindi, Mbeya, Mtwara, Mwanza na Tanga) zimepata nyota mbili. Mikoa iliyobaki inaendelea kufanyiwa tathmini. Maeneo yaliyoonekana kuwa na changamoto ni ukosefu wa wataalam bingwa, huduma za tiba za dharura, huduma za wagonjwa mahututi na huduma za upasuaji. Mipango ya Uimarishaji Ubora wa huduma za afya kwa kila Hospitali iliandaliwa na utekelezaji unaendelea kwa kushirikiana na Timu za Menejimenti za Hospitali husika.

109. Mheshimiwa Spika, aidha, Wizara imeendelea na maandalizi ya kuanzisha huduma za dharura katika barabara kuu. Huduma hizi zitatekelezwa chini ya udhamini wa Benki ya Dunia kupitia mradi wa Southern Africa Trade and Transport Facilitation (SATTF) unaosimamiwa na TANROADS. Maandalizi hayo yamehusisha ununuzi wa magari ya kubebea wagonjwa (ambulances) **12**, mabasi madogo mawili ya wagonjwa (rider vans) na magari ya uokoaji **5** yenye uwezo wa kuinua magari yaliyopata ajali na kukata vyuma (rescue vans). Vilevile imewezesha kununua vifaa vya mawasiliano pamoja na vifaa tiba na vifaa vya kufundishia wataalam wa dharura. Aidha, Wizara imeandaa michoro ya vituo vya kutolea huduma katika barabara kuu vitakavyojengwa na kutumika katika awamu ya kwanza inayohusisha barabara kutoka Dar es salaam hadi Ruaha Mbuyuni. Vilevile, kupitia ufadhili wa *Bloomberg Initiative on Global Road Safety*, Wizara imetoa mafunzo kwa Waandishi na Wanasheria kuhusu masuala ya Usalama Barabarani ambapo viashiria vitano vinavyoongoza kwa kusababisha ajali za barabarani na madhara yake ambavyo ni kutokuvaa mikanda, kutokuvaa kofia ngumu, kutomkalisha mtoto kwenye kiti maalum,

kunywa pombe na kuendesha gari na mwendokasi vinafanyiwa kazi.

Ushirikiano wa Ndani na Nje ya Nchi

110. Mheshimiwa Spika, Wizara yangu imeendelea kuimarisha ushirikiano na nchi rafiki pamoja na Jumuiya mbalimbali katika masuala ya Afya. Wizara iliratibu ushiriki katika mikutano ya Jumuiya mbalimbali za Kikanda na Kimataifa, kwa nia ya kuimarisha utoaji wa huduma katika Sekta ya Afya ambapo Wizara iliandaa na kuwa mwenyeji wa Mkutano wa Mawaziri wa Afya Jumuiya ya Nchi za Mashariki, Kati na Kusini mwa Africa (ECSA-Health Community) uliofanyika nchini, Mwezi Machi 2018. Aidha, Wizara imeendelea kuimarisha ushirikiano kupitia jumuiya za kikanda ikiwemo SADC, EAC, African Union, Great Lakes Initiative Africa (GLIA) na ECSA-HC pamoja na ushirikiano na nchi marafiki (bilateral cooperations) kupitia *Joint Permanent Commissions* (JPCs).

RASILIMALI WATU KATIKA SEKTA YA AFYA

111. Mheshimiwa Spika, Katika kuongeza idadi ya wataalamu wa Afya nchini, Wizara imeendelea kushirikiana na Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi NACTE katika kusimamia ubora wa mafunzo ya kada za Afya zisizo katika kiwango cha shahada. Katika kipindi cha kuanzia Julai 2017 hadi Machi 2018, jumla ya wanafunzi **16,214** walichaguliwa kujiunga na vyuo vya Afya. Kati ya hao wanafunzi **6,564** walichaguliwa kwenye vyuo vya Serikali na **9,650** kwenye vyuo binafsi katika programu za Uuguzi na Ukunga, Sayansi Shirikishi za Afya na wahudumu Afya ya Jamii. Aidha, Jumla ya wanafunzi **23,098** walifanya mitihani ya kuhitimu katika kipindi hiki, kati yao **10,669** ni wa Sayansi Shirikishi za Afya, **7,300** wa Uuguzi na Ukunga na wa Wahudumu Afya ya Jamii **5,129**.

112. Mheshimiwa Spika, Katika usimamizi wa mafunzo ya kada za afya zisizo katika kiwango cha shahada nchini, Wizara inao utaratibu wa kutathmini watahiniwa wote kwa usawa kwa kusahihisha mitihani ya kitaifa kwa pamoja

(central marking). Katika mwaka 2018, jumla ya watahiniwa **14,477** kutoka kwenye vyuo 177 vya Serikali na vyuo binafsi wamesahihishiwa mitihani yao na kupewa matokeo. Miongoni mwa watahiniwa, watahiniwa **10,669** ni wa kada ya Sayansi shirikishi za Afya na **3,808** fani za Uuguzi na Ukunga. Pia, jumla ya wakufunzi **139** kutoka vyuo **93** vya Uuguzi na Ukunga walifundishwa mbinu ya kutumia mitaala iliyohuishwa kwa mwaka wa masomo 2017/18.

113. Mheshimiwa Spika, Wizara imeendelea kushirikiana na wadau mbalimbali wa Maendeleo katika kutoa ufadhili wa mafunzo ya kibingwa ya muda mfupi na muda mrefu yanayolenga kuwajengea uwezo wa kiutendaji watumishi wa sekta ya Afya. Katika kipindi cha Julai 2017 hadi Machi 2018 jumla ya **Watumishi 376** wameendelea kulipiwa gharama za masomo yao ndani na nje ya nchi katika ngazi ya shahada ya Uzamili hususan Madaktari Bingwa katika fani za kipaumbele za upasuaji, magonjwa ya wanawake na uzazi, magonjwa ya watoto, magonjwa ya ndani na radiolojiawe.

114. Mheshimiwa Spika, Katika kipindi cha mwaka 2017/18, Wizara yangu, ilipokea kibali cha ajira ya watumishi **3,152** wa kada za afya kutoka Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora. Kibali hicho kilikuwa na nafasi za Madaktari Daraja la II **45**, Madaktari Bingwa (Medical Specialist) **24**, Madaktari Washauri (Medical Consultant) – **2**, Wauguzi Daraja la II **137** na kada nyingine za Afya **3,081** ambapo mchakato mzima wa kujaza nafasi za ajira ambazo Wizara ilipewa ulikamilika na Watumishi wote walipatikana isipokuwa Madaktari Washauri. Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais, TAMISEMI ilishawapangia Vituo vya kazi Watumishi hao. Aidha Katika kipindi hiki jumla ya Wataalam wa kigeni **35** walipata ajira katika taasisi mbalimbali za Serikali.

115. Mheshimiwa Spika, Wizara yangu, imeendelea kuboresha mazingira ya kufanyia kazi kwa watumishi ambao wanafanya kazi katika maeneo yenye mazingira magumu ili kuwapatia motisha ili kuendelea kutoa huduma za afya katika maeneo hayo. Katika kipindi cha Julai hadi Machi 2018 jumla ya nyumba 30 zimejengwa na kukamilika katika

Halmashauri tatu (3) za mkoa wa Manyara, ambazo ni ; Halmashauri za Kiteto 10, Simanjiro 10 na Hanang nyumba 10. Kukamilika kwa nyumba hizo kumeongeza idadi ya nyumba za watumishi zilizojengwa kupitia mradi huu wa 'Global Fund' na kufika nyumba **480** katika maeneo yenye mazingira magumu.

UGHARAMIAJI WA HUDUMA ZA AFYA

116. *Mheshimiwa Spika*, Wizara kwa kushirikiana na OR-TAMISEMI pamoja na Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya inaendelea na utekelezaji wa mpango wa Mfuko wa Afya ya Jamii (CHF). Hadi kufikia Machi 2018 Mfuko wa Afya ya Jamii (CHF) ulikuwa na jumla ya kaya **2,096,692** zilizojiunga ukilinganisha na kaya **2,030,666** zilizokuwa zimejiunga mwaka 2016/17. Aidha, wanufaika wameongezeka kutoka **12,183,996** mwaka 2016/17 hadi kufikia wanufaika **12,580,149** Machi 2018 sawa na **asilimia 25** ya Watanzania wote. Vilevile, katika kuchangia juhudi za wananchi wanaochangia CHF na kuboresha huduma zitolewazo, Serikali hutoa malipo ya tele kwa tele kwenye Halmashauri kulingana na kiwango cha makusanyo ya CHF. Malipo yaliyofanyika kwa Halmashauri kwa kipindi cha kuanzia Julai 2017 hadi Machi 2018 ni **Shilingi bilioni 1.4**. na hivyo kuwezesha Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya kulipa malipo ya Tele kwa Tele yenye jumla ya **Shilingi bilioni 15.8** kwa Halmashauri mbalimbali nchini tangu Mfuko ulipokabidhiwa jukumu hili mwezi Julai 2009.

117. *Mheshimiwa Spika*, ili kuongeza idadi ya wananchi watakapo kuwa wanahudumiwa na Mfuko huo, Wizara yangu kwa kushirikiana na OR - TAMISEMI imejipanga kuanza kutekeleza CHF iliyoboreshwa (iCHF) kabla ya mwisho wa mwezi Aprili, 2018. Katika maboresho hayo kila mwanachama ataweza kupata huduma kutoka ngazi ya zahanati hadi ngazi ya Hospitali ya Rufaa ya Mkoa bila kujali Kituo/Halmashauri alipojisajili tofauti na ilivyo sasa ambapo mwanachama wa CHF hupata huduma kwenye zahanati hadi ngazi ya Hospitali ya Wilaya/Halmashauri aliyojisajili tu.

118. *Mheshimiwa Spika*, Serikali ipo katika hatua za kuhakikisha inafikia malengo ya afya kwa wote (Universal

Health Coverage) ambapo kila mwananchi atakuwa na uhakika wa upatikanaji wa huduma bora za afya bila kuwa na kikwazo cha kifedha. Lengo ni kuwa ifikapo mwaka 2020 **asilimia 70** ya wananchi wawe wamejiunga na mifuko ya Bima ya Afya. Hali iliyopo sasa inaonesha kuwa idadi kubwa ya wananchi takribani **asilimia 68** nchini wapo nje ya Mfumo wa Bima ya Afya. Hii ina maana kuwa ni takribani ya **asilimia 32** ya watu wote ndiyo waliopo katika mfumo wa Bima za Afya nchini. Kwa hali hiyo, watu wengi nchini bado hawana uhakika wa kupata huduma za afya pindi wanapozihitaji kutokana na kuwa nje ya mfumo wa bima ya afya. Ili kuhakikisha kuwa wananchi hawa wanalindwa (Social protection) na athari hizo, Serikali iko katika hatua za kuboresha Mfumo wa Bima ya Afya kwa kuweka mazingira yatakayohakikisha kila mwananchi anapata huduma bora za afya pindi anapozihitaji. Katika kipindi cha Julai 2017 hadi Machi 2018, Wizara iliandaa na kuwasilisha Rasimu ya Waraka wa Baraza la Mawaziri wenye maelekezo ya kuboresha mfumo wa Bima za Afya nchini ikiwa ni pamoja na kutunga Sheria itakayomtaka kila Mtanzania kujiunga katika Mfumo wa Bima ya Afya. Baada ya kuwasilishwa kwa Rasimu hiyo, ulitolewa ushauri na maelekezo ambayo Wizara tayari imeshayafanyia kazi na tayari imeshaandaa rasimu nyingine ya Waraka wa Baraza la Mawaziri wenye kuzingatia ushauri ambao Wizara ilipatiwa. Rasimu ya Waraka huu unatarajiwa kuwasilishwa katika ngazi za maamuzi ndani ya Serikali kabla ya kuandaliwa kwa muswada wa sheria utakaowasilishwa bungeni kwa dhamira ya kutunga sheria itakayomtaka kila mwananchi kuwa mwanachama wa mfuko wa Bima ya Afya.

Mfuko wa Afya wa pamoja (Health Basket Fund)

119. Mheshimiwa Spika, Wizara imeendelea na jukumu la kuratibu Mfuko wa Pamoja wa Afya (Health Basket Fund) ulioanzishwa mwaka 1996. Kupitia Sekretarieti ya Uratibu wa Mfuko, vikao mbalimbali vya majadiliano kati ya Serikali na Wadau vimekuwa vikifanywa ikiwa ni pamoja na kutoa taarifa ya Serikali jinsi inavyotekeleza kazi zinazogharamiwa na fedha za Wadau. Kwa hivi sasa mfuko huo unachangiwa

na Wadau (7) ambao ni Denmark, Uswisi (SDC), Ireland, Canada, Benki ya Dunia, UNICEF na Korea Kusini.

Katika kipindi cha Julai 2017 hadi Machi 2018, kiasi cha **shilingi 26,674,357,344.00** kimepokelewa kupitia Mfuko wa Pamoja wa Afya. Kati ya fedha hizo, kiasi cha **shilingi 22,278,604,900.00**, sawa na asilimia 90 ya fedha zote zilipokelewa zilipelekwa na kutumika katika Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa lengo la kuboresha huduma za afya ngazi ya msingi. Fedha hizi hutumika kwa mujibu wa Mkataba wa Makubaliano kati ya Serikali na Wadau wa Maendeleo, ambapo **asilimia 33** ya fedha zinazopelekwa katika Halmashauri zinatakiwa kutumika kama nyongeza ya fedha kwa ajili ya ununuzi wa dawa, vifaa, vifaa tiba na vitendanishi na **asilimia 67** ni kwa ajili ya utekelezaji wa afua mbalimbali ambazo zinalenga katika kuboresha huduma za afya nchini ikiwa ni pamoja na kugharamia usambazaji na ufuatiliaji wa chanjo kwa kuimarisha mnyororo baridi (cold chain), uimarishaji wa huduma za dharura za mama na mtoto (CEmOC), udhibiti wa magonjwa yanayoambukiza na yasiyoambukiza pamoja na yale yasiyopewa kipaumbele na kuwajengea uwezo watoa huduma za afya.

120. Mheshimiwa Spika, Wizara kwa kushirikiana na OR-TAMISEMI imeanza utekelezaji wa azimio la kupeleka fedha moja kwa moja katika Vituo vya kutolea huduma za Afya nchini (Direct Health Facility Financing (DHFF) badala ya kuzipeleka kwenye Halmashauri zao. Hatua hii imelenga kuongeza ufanisi wa matumizi ya fedha za afya na kusogeza huduma karibu zaidi na wananchi. Utekelezaji wa azimio hili umeanza katika kipindi cha 2017/2018 ambapo fedha za Mfuko wa Pamoja wa Afya zilizotengwa kwa ajili ya matumizi ya vituo vya kutolea huduma za Afya zilipelekwa moja kwa moja kutoka Hazina kwenda katika Hospitali za Wilaya, Vituo vya Afya na Zahanati. Jumla ya **shilingi 45,751,004,800** zimetolewa na kupelekwa katika vituo **5,170**. Hatua hii imechangia kuboresha upatikanaji wa fedha katika vituo kwa wakati na kusaidia vituo kupanga mikakati ya kuboresha huduma na kuleta ufanisi.

Malipo kwa Ufanisi (Results Based Financing- RBF)

121. Mheshimiwa Spika, Wizara inatekeleza Mpango wa Malipo kwa ufanisi ambao ni ubunifu unaolenga kuongeza uwajibikaji wa Watoa huduma za afya pamoja na kuboresha upatikanaji wa rasilimali fedha ili kuboresha upatikanaji na utumiaji wa huduma za afya nchini. Utekelezaji wa Mpango wa malipo kwa ufanisi hupimwa kwa viashiria muhimu hasa vya afya ya mama na mtoto, ambavyo hulipwa kwa kazi inayofanyika baada ya uhakiki wa takwimu za viashiria hivyo. Msingi Mkuu wa mpango huu ni kwamba: "*fedha hulipwa kutokana na idadi ya wagonjwa/wateja na huduma bora iliyotolewa.*" Kadri kituo cha kutolea huduma za afya kinavyovutia zaidi wagonjwa na kutoa huduma bora ndivyo kitakavyopokea zaidi motisha kwa kituo na kwa watumishi. Pia, vituo vinapewa madaraka ya namna ya kupanga na kutumia mapato yatokanayo na fedha wanazopata.

122. Mheshimiwa Spika, Mpango huu kwa hivi sasa unatekelezwa katika Mikoa minane (8) ambayo ina kiwango kikubwa cha vifo vya akinamama na watoto ambayo ni Kigoma, Geita, Kagera, Shinyanga, Mwanza, Tabora, Simiyu & Pwani. Katika kipindi cha Julai 2017 hadi Machi 2018, jumla ya **Shilingi 35,917,673,288.88** zimepelekwa katika Mikoa (RHMT), Mamlaka za Serikali za Mitaa (CHMT) na vituo vya kutolea huduma za Afya (Hospitali, Vituo vya Afya na Zahanati) kwa ajili ya uboreshaji wa Miundombinu ya kutolea huduma za afya na malipo ya motisha kwa watumishi wa ngazi ya Mkoa (RHMT), ngazi ya Wilaya (CHMT), watoa huduma za Afya katika Hospitali, Vituo vya Afya na Zahanati.

Uimarishaji wa Mifumo ya Afya nchini

123. Mheshimiwa Spika, Wizara kupitia Kitengo cha Kuimarisha Mifumo ya Afya nchini (HSS) unaofadhiliwa na Mfuko wa Dunia 'Global Fund' imeendelea, kutekeleza shughuli mbalimbali za Uimarishaji wa Mifumo ya Afya. Wizara imefanya mafunzo kwa Wahasibu wanaohusika kwenye usimamizi wa miradi inayofadhiliwa na Mfuko huo katika ngazi ya Programu, Watekelezaji (Sub recipients) na Timu za

Uendeshaji wa Mipango Kabambe ya Afya kutoka Halmashauri. Jumla ya halmashauri 98 zilipatiwa mafunzo. Aidha Wizara kupitia Mpango huo, imeweza kulipa ada za wanafunzi 1,562 wanaosoma kozi za kada za kati za afya kutoka katika vyuo vya afya hapa nchini. Sambamba na hilo Wizara imeweza kukamilisha ujenzi wa majengo mbalimbali katika vyuo vya afya vya Mvumi, Tanga na Mirembe. Vilevile, Wizara imeweza kununua magari 181 kwa ajili ya kuiwezesha MSD kuimarisha utoaji wa huduma za usambazaji wa dawa hapa nchini. Pia Wizara imeweza kununua vifaa mbalimbali kwa ajili ya maabara za TFDA ili kuwawezesha kufanya kazi za uhakiki wa ubora wa dawa na chakula hapa nchini.

124. Mheshimiwa Spika, Wizara kwa kupitia Kitengo cha Uimarishaji wa Mifumo ya Afya kwa kushirikiana na vitengo mbalimbali kimeweza kutekeleza shughuli mbalimbali kupitia ufadhili wa UNICEF kwa ajili ya shughuli mbalimbali za uimarishaji wa mifumo ya afya ikiwemo uboreshaji huduma za mama na mtoto kwa Mikoa ya Mbeya, Iringa, Njombe na Songwe. Kitengo kimefanya Mafunzo ya kuzijengea uwezo wa kutimiza majukumu yake bodi za Afya za Halmashauri na kamati zake, Ufuatiliaji wa shughuli za huduma za Mama na Mtoto na kuzijengea uwezo na uelewa timu za usimamizi za Mikoa na Halmashauri juu ya zoezi la kupeleka fedha moja kwa moja katika vituo vya kutolea huduma za afya (DHFF).

TEKNOLOJIA YA HABARI NA MAWASILIANO

125. Mheshimiwa Spika, Wizara iliendelea kutekeleza Mpango Mkakati wa *eHealth strategy 2013-2018*. Katika mwaka 2017/18, Wizara kwa kushirikiana na OR-TAMISEMI na Taasisi ya Bill and Melinda Gates Foundation kupitia mdau wa maendeleo PATH ilizindua Mpango wa Uwekezaji (*Digital Health Investment Recommendation Roadmap*). Mpango huu umeainisha vipaumbele vinavyohitajika vya matumizi ya mifumo ya kielektroniki ili kuboresha huduma za afya katika ngazi zote, pamoja na umuhimu wa **kukusanya taarifa na matumizi sahihi ya takwimu za sekta ya Afya kwa ujumla**. Aidha, Wizara imefunga mfumo wa kielektroniki wa ukusanyaji wa taarifa za chanjo katika vituo vya Afya. Hadi

kufikia Machi 2018, jumla ya vituo **1,303** vya mikoa ya Arusha, Kilimanjaro Tanga, Manyara na Dodoma vilifungiwa mfumo na kupewa vifaa vya komputa. Vilevile jumla ya watumishi **3,258** walipewa mafunzo ya jinsi ya kutumia mfumo huu.

126. Mheshimiwa Spika, Wizara imeendelea kukamilisha ufungaji wa mfumo wa kielekitroniki katika hospitali za Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete, Taasisi ya Mifupa, Taasisi ya magonjwa ya saratani, Benjamin Mkapa, Mirembe, Hospitali ya Rufaa ya Mbeya na Bugando. Nia ni kuhakikisha kuwa tunapunguza matumizi ya karatasi (Paperless) na kuboresha utoaji wa huduma za afya. Aidha, Wizara kwa kushirikiana na mdau wa maendeleo CDC/MDH inaboresha miundombinu ya ndani ya TEHAMA ijulikanayo kama Local Area Network na kuweka vifaa vya TEHAMA kama vile kompyuta katika vituo vya kutolea huduma za Afya vifuatavyo; Buguruni, Kigamboni, Tandale, Chuo Kikuu Dar es Salaam na *Infectious Disease Centre* mkoani Dar es Salaam, Vituo vya Afya Kaigara, Rwamishenye, Kayanga na Kishanje mkoani Kagera. Kazi hii itakuwa imekamilika kabla ya Juni 2018. Vilevile Wizara imekamilisha mfumo wa kupokea maoni ya wananchi juu ya ubora wa huduma zinazotolewa katika vituo vya Afya nchini, ambapo mgonjwa au ndugu wa mgonjwa ataweza kutoa taarifa kupitia code namba *152*05*3#.

UTEKELEZAJI WA MIRADI YA MAENDELEO INAYOPATA RUZUKU TOKA SERIKALI KUU KWA MWAKA 2017/2018

127. Mheshimiwa Spika, Katika mwaka 2017/18, Wizara ilitenga kiasi cha **Shilingi 785,805,952,000** kwa ajili ya kutekeleza Miradi ya Maendeleo. Kati ya fedha hizi, **Shilingi, 336,300,000,000** ni fedha kutoka vyanzo vya ndani na **Shilingi 449,505,952,000** ni fedha kutoka vyanzo vya nje.

Miradi iliyotekelezwa kwa fedha za Ndani.

128. Mheshimiwa Spika, Katika kipindi cha Julai 2017 hadi Machi 2018, Wizara ilipokea **shilingi 74,756,079,206.00**(Fedha za Ndani) ambazo zilitumika kutekeleza miradi ifuatayo:

- i. Ununuzi wa dawa, vifa tiba na vitendanishi
- ii. Ununuzi na usambazaji wa Chanjo za watoto chini ya miaka 5 nchini
- iii. Kuanza hatua za awali za ujenzi wa Wodi ya wagonjwa wa *Private* katika Hospitali ya Taifa Muhimbili

Miradi iliyotekelezwa kwa fedha za Nje.

129. Mheshimiwa Spika, Katika kipindi cha Julai 2017 hadi Machi 2018, Wizara ilipokea fedha, dawa, vifaa na vitendanishi vyenye thamani ya **shilingi 321,015,218,137.12 kutoka katika Vyanzo vya Nje** kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli mbalimbali za kuboresha huduma za afya nchini kwa mchanganuo ufuatao:

Mfuko wa Afya wa Pamoja (Health Basket Fund)

Kazi zilizotekelezwa kupitia fedha za Mfuko wa Afya wa Pamoja zilizopokelewa na kutumiwa katika Fungu 52 ni pamoja na;

- i. kugharamia utekelezaji wa utaratibu wa malipo ya tele kwa tele kwa ajili ya Mfuko wa Afya wa Jamii (CHF),
- ii. Ukusanyaji wa Damu Salama na mapitio ya Rasimu ya Sera ya Afya,
- iii. Kutoa mafunzo juu ya CCHP na PlanRep3 kwa mikoa na halmashauri,
- iv. Kufanya uhakiki wa dawa, vifaa na vifa tiba vilivyopo nchini pamoja na kufanya uhakiki wa viashiria (Indicators) vinavyotumiwa na wadau katika kutoa fedha za Mfuko wa Pamoja (Basket Fund)
- v. Ada kwa ajili ya mafunzo ya uzamili

130. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha Julai hadi Machi 2018, Wizara ilipokea fedha nje ya ukomo wa bajeti **Shilingi**

82,515,009,463.82 ambazo zilipelekwa moja kwa moja OR-TAMISEMI kwa ajili ya kufanya ukarabati wa Vituo vya Afya ili viweze kutoa huduma za uzazi za dharura ikiwemo upasuaji kwa wanawake wajawazito wanaokabiliwa na uzazi pingamizi. Kati ya fedha hizo, **shilingi 63,015,009,462.82** kutoka Benki ya Dunia na **shilingi 19,500,000,000** kutoka Mfuko wa Afya wa Pamoja (Health Basket Fund). Fedha hizo zilitumika kugharamia utekelezaji wa miradi ifuatayo:

a) Mpango wa malipo kwa ufanisi (RBF)

Kukarabati miundombinu ya kutolea huduma za afya katika **Vituo 1,325** vya Serikali vya kutolea huduma za afya katika mikoa ya Shinyanga, Mwanza, Pwani, Tabora, Simiyu, Kigoma, Kagera na Geita. Aidha, jumla ya **shilingi 3,425,162,919** zilipelekwa katika Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa na kulipwa kama motisha kwa Timu za Uendeshaji wa shughuli za Afya za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa.

b) Uimarishaji wa huduma za dharura za mama na mtoto (CEmONC)

131. Mheshimiwa Spika, moja ya vipaumbele vya Serikali katika mwaka wa fedha 2017/18 ni kupunguza vifo vya akina mama na watoto vitokanavyo na uzazi. Katika kutekeleza azma hiyo serikali kwa kushirikiana na wadau wa maendeleo imeanza kufanya ukarabati/ ujenzi wa miundombinu ya kutolea huduma ikiwemo chumba cha upasuaji, maabara, wodi ya wazazi na wodi ya watoto utakaowezesha upatikanaji wa huduma kamili za uzazi ikiwa ni pamoja na upasuaji wa kumtoa mtoto tumboni, ili kupunguza vifo vya mama na watoto. Kupitia mpango huo, jumla ya vituo vya Afya 173 vinaboreshwa. Katika kutekeleza mradi huu, jumla ya **Shilingi 40,000,000,000** kutoka Banki ya Dunia kwa ajili ya kuboresha Vituo vya Afya 100 na **shilingi 19,500,000,000.00** kutoka Denmark kwa ajili ya vituo vya Afya zimepelekwa katika Halmashauri mbalimbali nchini kukamilisha kazi ya ukarabati na ujenzi ambao upo katika hatua mbalimbali chini ya uangalizi wa OR-TAMISEMI na Wizara ya Afya. Aidha Wizara kwa kushirikiana na TAMISEMI inakamilisha mchanganuo wa vituo vya afya 21 vitakavyoboreshwa kwa kutumia fedha za Mfuko wa Afya wa Pamoja.

Mfuko wa Dunia (Global Fund):

132. *Mheshimiwa Spika*, Katika kipindi cha Julai 2017 hadi Machi 2018, Wizara ilipokea fedha, dawa, vifaa tiba na vitendanishi vyenye thamani ya **shilingi 303,238,541,795.37** kwa ajili ya kupambana na Kifua Kikuu, UKIMWI na Malaria.

UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA TAASISI CHINI YA IDARA KUU YA AFYA

Bohari Kuu ya Dawa (MSD)

133. *Mheshimiwa Spika*, Katika kipindi cha mwaka wa Fedha 2017/2018, Bohari ya Dawa (MSD) imeendelea kutekeleza maelekezo ya Serikali kuhusu kununua dawa moja kwa moja kutoka kwa wazalishaji kwa kuingia makubaliano ya muda mrefu (Framework Agreement) na viwanda vya uzalishaji dawa. Jumla ya wazalishaji 110 tayari wana mikataba na MSD na kati ya hao wazalishaji 10 ni viwanda vya ndani. Mpango huu umewezesha MSD kufanikiwa kupunguza bei ya dawa 109 kwa wastani wa **asilimia 40**. Hali hiyo imesaidia vituo vya afya kuweza kununua dawa kwa bei nafuu na hivyo kuongeza kiasi cha dawa. Aidha, Bohari Kuu ya Dawa inaendelea kuimarisha mfumo wake wa usambazaji wa dawa ili kuhahikisha upatikanaji wa dawa na vifaa tiba katika vituo vya kutolea huduma za afya vya umma unafikia asilimia 100. Katika kufanikisha hili jumla ya magari 181 yamenunuliwa na Serikali kwa kushirikiana na Wadau wa Maendeleo, Magari hayo yalizinduliwa na Mhe. Rais tarehe **26 Machi, 2018**. Hali hiyo imewezesha vituo vya kutolea huduma za afya kuwa na dawa muhimu kwa asilimia **89.6**. Vilevile, upatikanaji wa dawa za **ARVs** umeimarika na kuwa kati ya **asilimia 92 hadi 100**

MFUKO WA TAIFA WA BIMA YA AFYA (NHIF)

134. *Mheshimiwa Spika*, Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya umeendelea kubuni na kutekeleza mikakati mbalimbali ili kuongeza wigo wa wanufaika wa bima ya afya. kufuatia utekelezaji wa mikakati hiyo, katika kipindi cha Julai 2017 hadi kufikia Machi 2018, Mfuko umeweza **kusajili idadi ya wanachama wapya wapatao 167,791** kutoka katika Sekta

ya Umma na Binafsi sawa na asilimia 97 ya lengo. Hivyo idadi ya wanachama wachangiaji wa Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya imeongezeka kutoka wanachama 753,992 waliokuwa wameandikishwa mwaka 2016/17 hadi kufikia wanachama 763,068 mwezi Machi 2018. Aidha, idadi ya wanufaika nayo iliongezeka kutoka 3,491,400 mwaka 2016/17 hadi kufikia wanufaika 3,619,697 mwezi Machi 2018 sawa na asilimia 7 ya Watanzania wote. Hii inaonyesha kuwa wanachama wa Mfuko wameongezeka kwa wastani wa asilimia 10 na wanufaika asilimia 7 katika kipindi cha miaka mitano.

135. Mheshimiwa Spika, Wizara kwa kushirikiana na OR-TAMISEMI pamoja na Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya inaendelea na utekelezaji wa mpango wa Mfuko wa Afya ya Jamii (CHF). Katika kipindi cha Julai 2017 hadi Machi 2018 kaya mpya zilizoandikishwa kwenye Mfuko wa Afya ya Jamii (CHF) zilikuwa 66,026 na kufanya jumla ya kaya 2,096,692 zilizojiunga ukilinganisha na kaya 2,030,666 zilizokuwa zimejiunga mwaka 2016/17. Aidha, wanufaika wameongezeka kutoka 12,183,996 mwaka 2016/17 hadi kufikia wanufaika 12,580,149 Machi 2018 sawa na asilimia 25 ya Watanzania wote. Aidha, mafanikio hayo yametokana na juhudi zinazofanywa na Mfuko za kuelimisha wananchi pamoja na kubuni mbinu mbalimbali za kuongeza wigo wa wanachama, kama kuanzishwa kwa mpango wa KIKOA (unaojumuisha kundi la wajasiriamali, vikundi vya vikoba, saccos na wavuvi), TOTO AFYA KADI (unaojumuisha watoto chini ya miaka 18), Wanafunzi wa vyuo vya Elimu ya Juu, Wastaafu na wanachama binafsi.

136. Mheshimiwa Spika, ili kuongeza idadi ya wananchi watakao kuwa wanahudumiwa na Mfuko huu wa Serikali, Mfuko kwa kushirikiana na Tume ya Maendeleo ya Ushirika (TCDC), unatarajia kuanzisha fao la bima linalolenga wakulima walio katika vyama vya ushirika nchini. Kupitia fao hilo lijulikanalo kama Ushirika Afya, wakulima walio katika vyama vya ushirika vya mazao ya Korosho, Pamba, Chai, Tumbaku na Kahawa watafikiwa kwa kuelimishwa na kuandikishwa kuwa wanufaika wa huduma za bima.

Kufanikiwa kwa mpango kutawawezesha wakulima kupata huduma za matibabu hata kipindi ambacho si cha msimu kupitia kadi zao.

137. Mheshimiwa Spika, Serikali imejipanga kuanza kutekeleza CHF iliyoboreshwa kuanzia mwezi Aprili, 2018. Katika maboresho hayo kila mwananchi ataweza kupata huduma kutoka ngazi ya zahanati hadi ngazi ya mkoa bila kujali Kituo/Halmashauri alipojisajili tofauti na ilivyo sasa ambapo mwanachama wa CHF hupata huduma kutoka ngazi ya zahanati hadi ngazi ya Halmashauri aliyojisajili tu. Kupitia Mpango huu wa CHF iliyoboreshwa, Halmashauri zitabaki na jukumu la kutoa huduma (service provider) na Ofisi ya Katibu Tawala wa Mkoa (RAS) kwa kushirikiana na mfuko wa NHIF itakuwa na jukumu la kuandikisha wanufaika, kukusanya fedha za wanachama na kulipa watoa huduma (purchaser). Kiwango cha chini cha kuchangia kwenye mfuko kitakuwa sawa kwa wananchi wote na kiinatarajiwa kuwa **Shilingi 30,0000** kwa mwaka kwa familia ya watu sita. Aidha, katika kuimarisha ushirikishwaji wa wananchi, vikao vya kijiji vitapewa fursa ya kuteua maafisa watakaokuwa na jukumu la kusajili wananchama na kuwahamasisha pamoja na kukusanya michango. Nitoe rai kwa Waheshimiwa Wabunge, kwa nafasi zao na ushawishi mkubwa walionao katika jamii tunayoishi, kuendelea kuwaelimisha wananchi wote umuhimu wa kujiunga na kuchangia katika mfuko huo wa bima ya afya ili waweze kupata huduma za tiba bila kikwazo cha fedha.

138. Mheshimiwa Spika, Utekelezaji wa CHF iliyoboreshwa ni Mkakati wa Serikali wa muda mfupi wakati tukijiandaa kuleta mswada katika bunge lako tukufu wa kuwa na Mfuko mmoja wa bima ya afya ambao kila mwananchi atalazimika kujiunga na kuchangia ili kuhakikisha kila mwananchi anakuwa na uhakika wa kupata huduma za afya bila kikwazo cha fedha pale anapohitaji. Katika Mkakati huo NHIF itapewa jukumu la kusimamia huduma za bima ya afya nchini na Mfuko wa CHF ulioboreshwa utakuwa ni sehemu ya fao moja wapo ya bima ya afya yatayokuwa yanatolewa na NHIF. Kwa msingi huo wananchi wote waliopo kwenye sekta rasmi

na wale waliopo kwenye Sekta isiyo rasmi wataweza kuhudumiwa ndani ya Mfuko wa NHIF.

Mpango wa Bima kwa Wanawake Wajawazito na Watoto

139. Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia NHIF na kwa kushirikiana na Benki ya Ujerumani (KfW) inatekeleza Mpango wa NHIF/CHF kwa Wanawake Wajawazito na Watoto ujulikanao kama **Tumaini la Mama**. Mpango huu ulianza kutekelezwa mwaka 2012 ambapo kina mama wajawazito hulipiwa kadi za NHIF/CHF na kuwa na uhakika wa kupata matibabu katika kipindi chote cha ujauzito na miezi sita baada ya kujifungua kwa mama na mtoto.

140. Mheshimiwa Spika, Mpango huu una lengo la kupunguza vifo vya kina mama na watoto ili kwenda sambamba na utekelezaji wa malengo ya kimataifa ya maendeleo endelevu (SDGs). Katika kipindi cha kuanzia Julai 2017 mpaka Machi 2018, **akina mama 199,954 na watoto 20,998** walikuwa wamesajiliwa na kunufaika na mpango huu. Tangu kuanzishwa kwa mpango, tayari wanawake wapatao 875,375 wamenufaika katika mikoa ya Mbeya, Tanga, Lindi, Mtwara na Songwe.

Uboreshaji wa Huduma za Afya

141. Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia NHIF ya Afya ina utaratibu wa kuvikopesha vituo vya kutolea huduma mikopo yenye lengo la kuboresha upatikanaji wa huduma za afya nchini. Mikopo hii ni pamoja na vifaa tiba, ukarabati wa vituo, dawa na vitendanishi.

Katika kipindi cha Julai 2017 hadi Machi 2018 Mfuko umetoa kiasi cha Shilingi bilioni 24 kwa ajili ya mikopo ya vifaa tiba, dawa na vitendanishi na ukarabati wa majengo kati ya Shilingi bilioni 43 zilizoidhinishwa. Kati ya hizo, Shilingi milioni 518.17 kwa ajili ya vifaa tiba na kiasi cha Shilingi milioni 450.37 kimetolewa kwa ajili ya ukarabati wa majengo na Shilingi bilioni 23.1 kimetolewa kwa ajili ya kukamilisha ujenzi na ununuzi wa vifaa tiba katika Hospitali ya Benjamin Mkapa

na ile ya Mkoa wa Dodoma. Tangu kuanzishwa kwa utaratibu huu mwaka 2009 hadi kufika Machi 2018 jumla ya Shilingi Bilioni 32 zimekwisha idhinishwa kwa vituo 375. Jumla ya mikopo yenye thamani ya Shilingi Bilioni 20 kwa vituo 228 imeshatolewa. Mchanganuo zaidi umeoneshwa katika Jedwali namba 1

Jedwali 1 kuhusu Mchanganuo wa mikopo iliyotolewa kipindi cha Jan-Machi 2018

Na.	AINA YA MKOPO	KIASI	
		KILICHOIDHINISHWA	KILICHOTOLEWA
1	Ujenzi wa Hospitali ya Benjamin Mkapa	30,000,000,000	22,764,789,759
2	Ujenzi wa Hospitali ya Mkoa wa Dodoma	3,000,000,000	363,779,600.00
3	Ununuzi wa Vifaa Tiba – vituo vya Umma	5,000,000,000	217,044,361
4	Ununuzi wa Vifaa Tiba – Sekta binafsi	3,000,000,000	301,125,500
5	Ukarabati wa Vituo vya Serikali katika Halmashauri/Mikoa mbalimbali nchini	2,000,000,000	450,373,225
	Jumla	43,000,000,000	24,097,112,445

Malipo kwa Watoa huduma

142. Mheshimiwa Spika, Katika kipindi cha Julai hadi Machi 2018, Mfuko uliendelea kuwalipa watoa huduma waliosajiliwa na Mfuko ikiwa ni jukumu lake la msingi kwa huduma zitolewazo kwa wanachama wake. Katika kipindi cha kuanzia mwezi Julai 2017 hadi Machi 2018, Mfuko ulilipa Watoa huduma jumla ya **Shilingi bilioni 134.92** kwa huduma mbalimbali zilizotolewa kwa wanachama sawa na asilimia 92% ya malipo ukilinganisha na kiasi cha **Shilingi 147,421.63 milioni** zilizotolewa na watoa huduma wote waliosajiliwa na kuwasilisha madai. Malipo ya madai kwa Watoa huduma hayakufanyika kwa asilimia 100 kutokana na sababu mbalimbali zikiwemo kutozingatiwa kwa miongozo ya tiba,

kutozingatiwa kwa masharti ya mkataba wa huduma baina ya Mfuko na Watoa Huduma na uwasilishwaji wa madai ya udanganyifu kunakofanywa na baadhi ya watoa huduma wasio waaminifu.

143. Mheshimiwa Spika, katika kuchangia juhudi za wananchi wanaochangia CHF na kuboresha huduma zitolewazo, Serikali hutoa malipo ya tele kwa tele kwenye Halmashauri kulingana na kiwango cha makusanyo ya CHF, fedha ambazo hurejeshwa katika vituo vya kutolea huduma. Malipo yaliyofanyika kwa Halmashauri kwa kipindi cha kuanzia Julai 2017 hadi Machi 2018 ni **Shilingi bilioni 1.4** na hivyo kuwezesha jumla ya **Shilingi bilioni 15.8** kulipwa kwa Halmashauri mbalimbali nchini tangu Mfuko ulipokabidhiwa jukumu hili mwezi Julai 2009.

Mpango wa kuwapeleka Madaktari bingwa maeneo ya pembezoni

144. Mheshimiwa Spika, Mfuko umekuwa ukitekeleza mpango wa kupeleka Madaktari bingwa katika Mikoa ya pembezoni kila mwaka kwa huduma za kibingwa. Katika kipindi cha Julai-2017 hadi Machi 2018, mikoa 2 ya Lindi na Mtwara imeshafikiwa kwa ajili ya zoezi hili. Mikoa mingine ambayo imewahi fikiwa tangu tangu kuanzishwa kwa zoezi hili ni pamoja na; Kigoma, Rukwa, Katavi, Pwani, Shinyanga, Manyara, Mara, Simiyu, Tabora, Singida, Kagera, Ruvuma, Iringa na Njombe. Mpango huu unafanywa kwa kushirikiana na Hospitali ya Taifa ya Muhimbili, Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete, Taasisi ya Saratani Ocean Road, Taasisi ya Mifupa MOI na Hospitali za Rufaa. Mpango huu umesaidia sana kufikisha huduma za matibabu za kibingwa sehemu mbalimbali hasa za pembezoni ili kuwapatia fursa wanachama na wananchi kupata huduma ambazo wangelazimika kuzifuata katika miji mikubwa zilipo hospitali hizo. Aidha, utaratibu huu umewezesha Madaktari wa mikoa husika kupata uzoefu na mafunzo kwa vitendo kutoka kwa madaktari bingwa. Mfuko utaendelea kutekeleza utaratibu huu kwani umekuwa wa manufaa kwa wananchi na wanufaika wa Mfuko kwa ujumla.

MAMLAKA YA CHAKULA NA DAWA (TFDA)

145. Mheshimiwa Spika, Wizara yangu kupitia Mamlaka ya Chakula na Dawa, inatekeleza Mpango Mkakati mpya wa miaka mitano (5) wa Mamlaka ya Chakula na Dawa (2017/18 - 2021/22). Utekelezaji wa kazi katika kipindi cha Julai 2017 hadi Machi 2018, umezingatia malengo mkakati ya taasisi ambayo ni: Kuhakikisha usalama, ubora na ufanisi wa dawa, vipodozi, vifaa tiba na vitendanishi, kuhakikisha usalama na ubora wa chakula, kuboresha huduma za maabara, kuimarisha utoaji elimu kwa umma na kuboresha huduma kwa wateja, kuimarisha uwezo wa Mamlaka katika kutoa huduma za kiudhibiti, kutoa huduma kwa waathirika wa Virusi vya UKIMWI na wenye magonjwa yasiyoambukiza, kuimarisha na kutekeleza kwa ufanisi Mkakati wa Taifa wa kupambana na kuzuia rushwa na kuboresha masuala ya jinsia na mazingira.

146. Mheshimiwa Spika, Mamlaka ilifanya tathmini ya maombi 1,223 (sawa na 85.1%) ya usajili wa vyakula kati ya maombi 1,437 yalipokelewa kwa ajili ya usajili wa bidhaa za chakula, ambapo maombi 1,243 yaliidhinishwa, 56 yalikataliwa kwa kutokidhi vigezo. Aidha, jumla ya sampuli 3,491 (80.7%) kati ya sampuli 4,324 za bidhaa za chakula, dawa, vipodozi na vifaa tiba zilichunguzwa, ambapo sampuli 3,163 (90.6%) zilikidhi vigezo na sampuli 328 hazikukidhi vigezo na hivyo bidhaa husika kutosajiliwa na nyingine kuondolewa kwenye soko.

147. Mheshimiwa Spika, Mamlaka ilifanya kaguzi za viwanda 42 vya dawa katika nchi za Bangladesh, India, China, Pakistan na Misri ambapo viwanda 15 vilikidhi vigezo, 15 vilipewa maelekezo ya kufanya marekebisho na 12 kutokidhi vigezo. Viwanda 5 vya chakula vilikaguliwa nje ya nchi katika nchi za India (2), Zambia (1), Vietnam (1) na China (1) ambapo vyote vilikidhi vigezo. Aidha, Mamlaka imeendelea na utoaji wa elimu kwa umma kwa makundi mbalimbali ya wananchi kuhusu madhara ya dawa, vipodozi hatarishi na usalama wa chakula pamoja na jumbe fupi zilirushwa kupitia redio, runinga, magazeti na mitandao

mbalimbali ya kijamii. Vilevile, Mamlaka imeimarisha mfumo wa kieletroniki wa kupokea taarifa za madhara yatokanayo na matumizi ya dawa, vifaa tiba na vipodozi kwa kuwezesha Watanzania kutuma taarifa kwa njia ya ujumbe mfupi wa simu za mikononi kwa kupiga namba *152*00#.

148. Mheshimiwa Spika, mfumo wa kupokea taarifa za usajili wa vitendanishi kwa njia ya mtandao umetengenezwa na kuanza kutumika na hivyo kupunguwa kwa muda wa kushughulikia maombi yanayowasilishwa na wateja. Mamlaka imeweza kuweka taarifa za bidhaa zote zilizosajiliwa nchini kwenye mtandao ambao umeunganishwa na mfumo wa kielektroniki wa ndani (www.tfda.go.tz/portal/registered-products). Taarifa hizi zinasaidia wananchi na wateja kwa ujumla kuona bidhaa zilizosajiliwa na tarehe za kuisha muda wa usajili.

MAMLAKA YA MAABARA YA MKEMIA MKUU WA SERIKALI

149. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha wa 2017/18, Taasisi iliyokuwa Wakala wa Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali ilibadilishwa rasmi na kuwa Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali kwa sheria Na. 8 ya mwaka 2016. Katika kuhakikisha kwamba Mamlaka inafanya kazi kwa ufanisi, mamlaka imesaini mikataba mitatu (3) ya ununuzi wa mitambo na vifaa vya maabara vyenye thamani ya **shilingi bilioni 1.4**, vifaa hivyo vinatarajiwa kupokelewa kabla ya mwezi Juni, 2018. Aidha, ukarabati wa Maabara ya DNA Makao Makuu Dar es Salaam umeanza na unategemewa kumalizika mwezi Juni 2018. Vilevile, jumla ya sampuli **57,046** zinazojumuisha makosa ya jinai, vinasaba, maji safi, maji taka, kemikali, vyakula, dawa na bidhaa nyingine za viwandani zilipokelewa kwa ajili ya uchunguzi. Kati ya hizo ni sampuli **51,387** sawa na asilimia **88.6** ndizo zilizochunguzwa. Pia, Wizara yangu kupitia Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali ilifanya matengenezo kinga ya vifaa na mitambo na kununua vitendanishi ambavyo vimesaidia kutoa matokeo sahihi na kwa wakati hivyo kulinda afya na mazingira na kusaidia utoaji haki katika vyombo vya maamuzi.

150. Mheshimiwa Spika, Mamlaka ilitoa jumla ya **vibali 13,465** vya kemikali kwa wadau mbalimbali kwa ajili ya kuingiza na kusafirisha kemikali ndani na nje ya nchi. Aidha, **wadau 541** wa kemikali walisajiliwa baada ya kukidhi vigezo vinavyotakiwa katika kutoa huduma mbalimbali za kemikali hapa nchini.

TAASISI YA CHAKULA NA LISHE (TFNC)

151. Mheshimiwa Spika, Wizara yangu kupitia Taasisi ya Chakula na Lishe imeendelea kutekeleza majukumu mbalimbali katika kuimarisha utoaji wa huduma za Lishe nchini. Aidha, katika kutekeleza azma ya Serikali ya kupunguza vifo vya watoto wadogo na wachanga nchini, Taasisi imeendelea kuratibu zoezi la kitaifa la utoaji wa vitamini A ya nyongeza kwa watoto wenye umri kati ya miezi 6 – 59 na dawa za **kutibu minyoo** kwa watoto wenye umri wa miezi 12 – 59. Msisitizo katika kipindi hiki ulikuwa ni kufuatilia na kutoa usaidizi katika Mikoa na halmashauri ambazo zilibainika **kutofikia asilimia 90 inayopendekezwa na shirika la Afya Duniani**. Mikoa na Halmashauri hizo ni Simiyu (Bariadi), Mwanza (Magu), Shinyanga (Kishapu), Singida (Itigi), Kigoma (Buhigwe na Uvinza), Katavi (Mpanda), Rukwa (Nkasi) na Tabora (Uyui). Vilevile, katika kipindi hiki, Taasisi ilikamilisha maandalizi ya mpango kazi wa kuzuia upungufu wa madini joto mwilini; mpango unaoainisha kazi mbalimbali zinazolenga kuimarisha upatikanaji na matumizi ya chumvi yenye madini joto katika jamii.

152. Mheshimiwa Spika, Taasisi ya Chakula na Lishe kwa kushirikiana na Taasisi ya *Food and Nutrition Institute iliyopo Zurich – Switzerland* ilifanya utafiti wa kubaini Athari za Mabadiliko ya Hali ya Hewa kwa Kiashiria cha Madini-joto kwa Wanawake Walio Kwenye Umri wa Kuzaa. Utafiti huu ulifanyika katika Kata ya Kilema (Kati na Juu) katika Wilaya ya Moshi Vijijini ambapo ulihusisha Sampuli 211 zilizochukuliwa kwa awamu mbili za hali ya hewa tofauti; awamu ya kwanza mwezi Julai (kipindi cha baridi) na awamu ya pili mwezi Oktoba (kipindi cha joto). Vilevile, Taasisi inatarajia kufanya tafiti zenye lengo la kupata majibu ya

kisayansi kuhusu njia bora, inayokubalika na endelevu ya kuwasaidia wasichana walioko shuleni na nyumbani kupata virutubishi vya nyongeza (micronutrient supplements) ili kuwakinga na tatizo la upungufu wa damu mwilini.

153. Mheshimiwa Spika, Katika kufuatilia kiwango cha ufanisi katika utekelezaji wa afua za lishe nchini na kuhimiza uwajibikaji kwa watoa huduma, Wizara imeanza kutumia Kadi Alama ya Lishe (Nutrition Score Card). Kadi Alama hii ina jumla ya viashiria **18** ambavyo vinatumika kufuatilia utekelezaji wa afua za lishe na matumizi ya kadi hii yamezingatia uzoefu uliopatikana katika matumizi ya kadi alama nyingine zilizopo nchini kama ile ya Malaria na ile ya Afya ya Uzazi, Mama na Mtoto. Kutokana na ufanisi mkubwa katika matumizi ya kadi alama hii, Serikali ya Ethiopia ilituma wataalam wake sita kutoka Wizara ya Afya kuja Tanzania kujifunza jinsi ya kuandaa na kutumia mfumo huu kuwezesha kadi alama ya lishe ili ianze kutumika katika nchi hiyo.

154. Mheshimiwa Spika Taasisi kwa kushirikiana na OR-TAMISEMI iliandaa mikutano mahsusi ya kuwahamasisha viongozi na watendaji wa Mikoa na Halmashauri kuhusu kubaini na kujumuisha afua za lishe katika mipango na bajeti za Mikoa na Halmashauri husika. Mikutano hiyo iliwashirikisha washiriki wapatao 700 ambao ni Makatibu Tawala Wasaidizi wa Mikoa, Wakuu wa Idara (Afya, Mipango, Kilimo na Mifungo) na Makatibu wa Afya ngazi ya Halmashauri, Maafisa Lishe na Wadau wa Llishe kutoka baadhi ya Asasi zisizo za Kiserikali (NGOs). Zoezi hili lilihusisha pia uhamasishaji kuhusu Mpango Mkakati wa Taifa wa Utekelezaji wa Masuala ya Lishe (NMNAP), pamoja na kuhamasisha Halmashauri kutenga kiasi cha **Shilingi 1,000** kwa kila mtoto chini ya miaka mitano kwa ajili ya utekelezaji wa afua za kupambana na udumavu.

155. Mheshimiwa Spika, Taasisi inaendelea kutoa msaada wa kitaaluma kwa kuendesha mafunzo kuhusu matibabu ya utapiamlo mkali kwa watoto waliolazwa hospitalini (in-patient management of acute malnutrition) katika maeneo mbalimbali nchini. Katika kipindi hiki, watoa huduma **274** wamenufaika na mafunzo hayo katika Mikoa ya Lindi,

Shinyanga, Mbeya, Songwe, Iringa, Njombe, Dodoma, Simiyu na Ruvuma. Aidha, Taasisi imeendelea kutoa mafunzo kwa watoa huduma za afya katika vituo vya tiba vinavyotoa huduma kuhusu lishe na matunzo kwa watu wanaoishi na virusi vya UKIMWI. Mafunzo haya yalifanyika katika mikoa ya Dodoma, Singida, Tanga, Mtwara, Lindi na Arusha, ambapo Watoa huduma wapatao **622** na watu **15,832** wanaoishi na virusi vya UKIMWI na wenye utapiamlo walinufaika kupitia mafunzo haya ambapo wagonjwa walipatiwa pia matibabu kwa kutumia chakula dawa (Ready to Use Therapeutic Foods) na kupatiwa ushauri nasaha wa lishe bora.

TAASISI YA UTAFITI WA MAGONJWA YA BINADAMU (NIMR)

156. Mheshimiwa Spika, Wizara yangu kupitia Taasisi ya Uchunguzi wa Magonjwa ya Binadamu imeendelea kutekeleza majukumu yake ya Utafiti. Taasisi imefanya tafiti mbalimbali ikiwemo tafiti za Majaribio ya Chanjo ya UKIMWI, Tiba Mbadala, Afya ya mama na mtoto, Malaria na TB. Matokeo ya tafiti hizi yamesaidia kuandaa afua mbalimbali za kuboresha huduma kwa waathirika wa magonjwa hayo. Aidha, tafiti kwenye afya ya mama na mtoto zinalenga kuboresha mfumo wa afya hasa upatikanaji wa huduma ikiwemo chanjo, elimu ya lishe na hatua za kupunguza vifo vya mama na watoto chini ya miaka 5. Taasisi kwa kushirikiana na Wizara na wadau wa Afya imefanya tathmini ya uwepo wa maji salama na usafi wa mazingira (WASH) katika vituo vya afya mbalimbali vinavyotoa huduma za kujifungua. Taarifa zilizopatikana kutokana na utafiti huo ni kwamba, pamoja na Serikali kupitia Sekta ya Afya kulisitiza wananchi kwenda kujifungulia katika vituo vya kutolea huduma za Afya, bado yapo mapungufu makubwa ikiwa ni pamoja na yafuatayo; Asilimia 19 ya vituo hutumia maji toka vyanzo visivyoboreshwa vikiwemo vyanzo wazi kama mito na mabwawa na visima visivyoboreshwa; Asilimia 46.5 ya sampuli za maji zilizopimwa zilionekana kuwa na vimelea vya maambukizi ya magonjwa mbalimbali; Asilimia 42 ya vyumba vya kuzalia havikuwa na sehemu za kunawia mikono; Asilimia 10 ya vituo hasa zahanati vilikuwa na vyoo duni visivyoboreshwa na kuleta hatari ya maambukizi.

157. Mheshimiwa Spika, Wizara imejipanga kufanyia kazi matokeo yaliyobainishwa na utafiti huo kwa kuelekeza msukumo mkubwa katika eneo la afya Kinga ikiwa ni pamoja na kushirikiana na OR-TAMISEMI kuhakikisha kuwa Mamlaka za Serikali za Mitaa zinatenga fedha katika bajeti zao kwa ajili ya kuondoa changamoto zilizobainishwa na utafiti huo.

158. Mheshimiwa Spika, Wizara kupitia NIMR imeendelea kufanya tafiti za dawa asili zinazoonesha matumaini ya awali katika kupunguza makali au kutibu magonjwa ya malaria, UKIMWI na magonjwa nyemelezi, ugonjwa wa Ini, shinikizo la damu, kisukari na kupunguza lehemu mwilini, uvimbe wa **tezi dume kwa wanaume na dawa inayoongeza nguvu za kiume** kwa wanaume. Baadhi ya dawa hizo zinatayarishwa kwa ajili ya usajili na Mamlaka ya Chakula na Dawa Tanzania.

BARAZA LA FAMASIA

159. Mheshimiwa Spika, katika kuhakikisha upatikanaji wa dawa karibu na wananchi waishio vijijini, Wizara kupitia Baraza la Famasia imesajili jumla ya maduka ya Dawa Muhimu **1,255** yaliyopo katika Mikoa ya Tanga, Mara, Morogoro, Mbeya, Geita, Pwani, Mwanza, Mtwara, Lindi, Arusha, Simiyu, Kagera, Ruvuma, Dodoma, Njombe na Singida. Hadi sasa kuna maduka ya Dawa Muhimu kufikia **11,763** yaliyosajiliwa ambalo ni ongezeko la asilimia **10.6** ikilinganishwa na maduka **10,508** ya mwaka 2016.

UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU CHINI YA IDARA KUU MAENDELEO YA JAMII

Uwezeshaji Wanawake

160. Mheshimiwa Spika, Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR-TAMISEMI) imeendelea kuratibu utendaji wa Mfuko wa Maendeleo ya Wanawake. Katika mwaka 2017/18, Wizara imeendelea kuzihimiza Halmashauri kuchangia asilimia 5 ya mapato yao ya ndani katika Mfuko. Katika kipindi cha Julai hadi Disemba 2017, **Halmashauri 130** kati ya **185** zilichangia **Shilingi bilioni**

7.3 katika Mfuko ikilinganishwa na **Shilingi bilioni 8.9** zilizochangiwa na Halmashauri kwa mwaka 2016/17. Fedha zilizochangiwa ni sawa na **asilimia 26** ya **Shilingi bilioni 28.3** zilizopaswa kuchangiwa kwa mwaka 2017/18. Fedha hizo zilitolewa kama mikopo kwa **vikundi 4,365** vyenye **wanawake wajasiriamali 39,449** . Natarajia kuwa, hadi kufikia mwezi Juni, 2018, uchangiaji wa mapato ya ndani kwa kila Halmashauri utaongezeka. Hivyo, natoa wito kwa Wakurugenzi wa Halmashauri zote nchini kuhakikisha wanachangia fedha katika Mfuko wa Maendeleo ya Wanawake kama wanavyopaswa.

161. Mheshimiwa Spika, Wizara kwa kushirikiana na Halmashauri ya Mtwara imeviwezesha **vikundi vinne vyenye wanawake wajasiriamali 20** kupata stadi za ujasiriamali na uendeshaji biashara, utunzaji wa kumbukumbu, uwekaji akiba na marejesho baada ya kupatiwa mikopo yenye thamani ya **Shilingi milioni 69** kutoka fedha za Mfuko wa Maendeleo wa Wanawake zilizotolewa moja kwa moja na Wizara. Aidha, kutokana na stadi na mikopo hiyo wanawake hao wamewezeshwa kuchimba mabwawa mawili na kuyajengea uzio kwa ajili ya ufugaji wa samaki, kupanua eneo la kilimo cha mbogamboga kutoka ekari nne hadi kufikia ekari nane na kupanua ujenzi wa mabanda kwa ajili ya ufugaji wa kuku.

162. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2017/18, Wizara kwa kushirikiana na OR - TAMISEMI iliratibu uhamasishaji wa wanawake kuanzisha na kujiunga na vikundi vya kiuchumi (SACCOS na VICOBA) kwa kufanya majaribio ya utekelezaji wa Mwongozo wa Uhamasishaji wa Wanawake Kuanzisha na Kujiunga na Vikundi vya Kiuchumi katika Halmashauri za Rombo mkoani Kilimanjaro na Mvomero mkoani Morogoro. Kutokana na uhamasishaji huo, **jumla ya vikundi 88** vyenye **wanachama 1,807 (Ke 1,517 na Me 290)** vilianzishwa vikiwemo VICOBA na Vikundi vya Hisa. Vikundi hivyo vimewawezesha wanachama kuchangia na kukuza mitaji yenye thamani ya Shilingi milioni 50 ambayo imewawezesha kuanzisha na kuwekeza katika biashara na miradi mbalimbali ya uzalishaji ikiwemo kilimo na ufugaji.

163. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2017/18, Wizara imezindua na kuratibu utekelezaji wa **Programu ya Kikundi Mlezi**. Programu hii inalenga kuwalea wajasiriamali wanawake wanaoanza kwa kuwaunganisha na wanufaika wa Mfuko wa Maendeleo ya Wanawake na vikundi vya kiuchumi vinavyofanya vizuri ili waweze kujifunza mbinu na stadi za ujasiriamali. Programu inatekelezwa katika mikoa 6 ya Pwani, Kigoma, Songwe, Katavi, Rukwa na Mbeya. Katika kipindi cha Julai hadi Machi, 2018, jumla ya **wanawake wajasiriamali 30** waliunganishwa na **vikundi 25** vinavyofanya vizuri vilivyopo katika mikoa hiyo. Aidha, katika Programu ya Kikundi Mlezi, **wanawake 1,131** waliwezesha kupata mafunzo ya urasimishaji na uboreshaji wa bidhaa wanazozalisha kwa kuwaunganisha na mamlaka za uhibitaji na usimamizi ikiwemo Mamlaka ya Chakula na Dawa Tanzania (TFDA), Shirika la Viwango Tanzania (TBS) na Shirika la Viwanda Vidogo (SIDO) kwa ajili ya kutatua changamoto mbalimbali za uendeshaji wa biashara na miradi yao.

164. Mheshimiwa Spika, Wizara kwa kushirikiana na wadau mbalimbali wakiwemo SIDO, Mfuko wa Fursa Sawa kwa Wote(EOTF) na Baraza la Taifa la Uwezesaji Wananchi Kiuchumi iliendelea kuwezesha ushiriki wa wanawake katika Maonesho ya Biashara ya Kitaifa na Kimataifa. Katika mwaka 2017/18, **wanawake wajasiriamali 1,183** kutoka mikoa **26** ya Tanzania Bara waliwezesha kushiriki katika Maonesho ya Sabasaba, Juakali, Nanenane na VICOBA. Kutokana na ushiriki huo, wanawake wajasiriamali waliweza kujifunza mbinu mbalimbali za kuboresha bidhaa na kupata uzoefu kuhusu upatikanaji wa masoko kutoka kwa washiriki wa mikoa mingine na nchi nyingine.

165. Mheshimiwa Spika, Wizara kupitia Benki ya Wanawake Tanzania (TWB) imeendelea kutoa huduma za fedha ikiwa ni pamoja na mikopo yenye riba nafuu na mafunzo ya ujasiriamali kwa wajasiriamali hususan wanawake katika mikoa **saba ya Dar es Salaam, Mwanza, Dodoma, Iringa, Ruvuma, Njombe na Mbeya**. Katika mwaka 2017/18, **wajasiriamali 6,237 (Ke 5,097 na Me 1,140)** walipatiwa mikopo ikilinganishwa na **wajasiriamali 6,267 (Ke 4,596 na**

Me 1,671) mwaka 2016/17. Juhudi hizi zimewesha **wajasiriamali 87,063 (Ke 71,744 na Me 15,319)** kupata mikopo tangu mwaka 2010. Kwa upande wa thamani ya mikopo iliyotolewa mwaka 2017/18, benki ilitoa mikopo ya **Shilingi bilioni 10.1** ikilinganishwa na **Shilingi bilioni 13.3** mwaka 2016. Tthamani ya mikopo iliyotolewa tangu mwaka 2010 mpaka Machi, 2018 ni **Shilingi bilioni 131.9**.

166. Mheshimiwa Spika, Aidha, Benki ya Wanawake Tanzania imefungua **vituo 244** vya kutolea mikopo na mafunzo kwa wanawake wajasiriamali katika mikoa ya Dar es Salaam (115), Mwanza (46), Dodoma (27), Mbeya (5), Iringa (9), Ruvuma (24) na Njombe (18) katika mwaka 2017/18 ikilinganishwa **na vituo 88** mwaka 2016/17 sawa na ongezeko **la asilimia 177**. Benki ya Wanawake Tanzania pia iliwapatia wananchi uelewa kuhusu kujiwekea akiba akiba kwa kile wanachokipata kwa kufungua akaunti. Katika mwaka 2017/18, jumla ya **akaunti 10,415 (Ke 7,811 na Me 2,604)** zilifunguliwa hadi kufikia **akaunti 88,397** Machi, 2018 katika matawi mawili ya Benki ya Wanawake Tanzania (**tawi la Mkwepu na Mjasiriamali**) kutoka mwaka 2009. Kati ya akaunti hizo, **akaunti 65,419 ni za wateja wanawake sawa na asilimia 74, akaunti 20,961 za wanaume na akaunti 2,017 za makampuni**

167. Mheshimiwa Spika, ukatili wa kijinsia bado ni tatizo hapa nchini. Takwimu za Jeshi la Polisi kwa mwaka 2017, zinaonyesha kuwa, matukio ya ukatili wa kijinsia yalikuwa 41,416 mwaka 2017 ikilinganishwa na matukio 31,996 mwaka 2016. Katika kukabiliana na tatizo hilo, Wizara yangu imekuwa ikiratibu utekelezaji wa Mpango Kazi wa Taifa wa Kutokomezwa Ukatili Dhidi ya Wanawake na Watoto (2017/18 – 2021/22). Lengo la mpango huu ni kupunguza vitendo vya ukatili dhidi ya wanawake na watoto. Katika mwaka 2017/18, Wizara kwa kushirikiana na wadau mbalimbali imezijengea uwezo Kamati za Ulinzi na Usalama wa Wanawake na Watoto za ngazi ya mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa kuhusu uratibu na namna ya kukabiliana na ukatili wa kijinsia hususan dhidi ya wanawake na watoto. Jumla ya waratibu 52 toka katika ngazi ya Mkoa wamejengewe uwezo wa kuratibu afua za kukabiliana na

ukatili. Vile vile Mamlaka za Serikali za Mitaa 19 za: Kasulu (W), Kasulu (TC), Kibondo, Kakonko, Kibaha, Ludewa, Kaliua, Wanging'ombe, Rungwe, Kyela, Mbeya (DC), Kiteto, Mkuranga, Busega, Busenga, Dodoma (M), Uyui, Tabora (M) na Rufiji

Maendeleo ya Jamii

168. Mheshimiwa Spika, Wizara, inaendelea kuamsha ari ya Wananchi kushiriki katika kujitelea maendeleo yao sambamba na kushiriki shughuli za ujenzi wa Miradi ya Maendeleo kwa kutumia nguvu kazi pamoja na rasilimali zinazowazunguka katika maeneo yao. Katika kipindi cha Julai hadi Machi 2018, Wizara imefanya uhamasishaji katika Mikoa 11 ya Iringa, Dodoma, Mwanza, Pwani, Kigoma, Katavi, Rukwa, Songwe, Mbeya, Kagera na Shinyanga. Uhamasishaji huu umewezesha ujenzi wa majengo ya Kituo cha Afya Mondo, Wilaya ya Misungwi (Mwanza); ujenzi wa bwawa la maji Maghangu Mpwapwa (Dodoma); ujenzi wa Zahanati Ufyambe (Iringa); ujenzi wa shule ya sekondari na kituo cha afya – Uvinza (Kigoma); ujenzi wa shule ya sekondari na kituo cha afya – Mpanda (Katavi); ujenzi wa kituo cha afya – Sumbawanga (Rukwa); ujenzi wa kituo cha afya – Mbozi (Songwe); ujenzi wa shule ya sekondari – Manispaa ya Mbeya (Mbeya); kuchangia fedha na vifaa kwa ajili ya ujenzi wa nyumba ya mtumishi wa Makazi ya wazee (Kagera); kuzindua Kituo cha Mkono kwa Mkono (One Stop Centre) cha wahanga wa ukatili wa kijinsia na ukatili wa watoto Wilaya ya Kahama (Shinyanga) na ujenzi wa madarasa mawili katika Kijiji cha Chambasi, Kisarawe (Pwani). Miradi hii iligharimu kiasi cha Shilingi 229,127,100, kati ya hizo mchango wa wananchi ni Shilingi 112,341,250 sawa na asilimia 49.03. Fedha hii imesaidia Serikali kuokoa gharama na kujengea jamii umiliki endelevu wa miradi mbalimbali wanayoanzisha katika maeneo yao.

169. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2017/18 wataalamu wa maendeleo ya jamii 175 kutoka Sekretarieti za Mikoa 26 na Mamlaka za Serikali za Mitaa 184 walijengewa uwezo wa kuamsha ari ya wananchi kushiriki kwenye uchumi wa

viwanda, utekelezaji wa Mpango wa Taifa wa Kutokomeza Ukatili dhidi ya Wanawake na Watoto (2017/18 - 2021/22) na uwezeshaji wa wanawake kiuchumi hususani katika kuzalisha mazao ya kilimo, mifugo na uvuvi ambayo ni malighafi ya viwanda vidogo vidogo na vya kati katika maeneo yao.

170. Mheshimiwa Spika, Wizara imeendelea kusimamia na kuratibu **uzalishaji wa wataalam wa Maendeleo ya Jamii** kutoka katika vyuo 8 vya maendeleo ya jamii vya Buhare, Mlale, Misungwi, Rungemba, Mabughai, Ruaha, Uyole na Monduli. Vyuo hivyo hutoa mafunzo ya Maendeleo ya jamii katika ngazi ya Cheti na Stashahada. Katika mwaka 2017/18, jumla ya **wanafunzi 1,588** (Ke 984 na Me 604) **walidahiliwa** ikilinganishwa na 3,248 (Ke 1,987 na Me 1,261) mwaka 2016/17. Aidha, katika mwaka 2017/18, jumla ya **wanafunzi 3,320** (Ke 1,947 na Me 1,373) **walihitimu** katika Vyuo 8 vya Maendeleo ya Jamii ikilinganishwa na **wahitimu 3,694** (Ke 2,228 na Me 1,466) mwaka, 2016/17.

171. Mheshimiwa Spika, Wizara imefanya mapitio ya mtaala wa mafunzo ya Vyuo vya Maendeleo ya jamii ili kupata wahitimu mahiri wenye kuendana na mahitaji ya soko la ajira kwa sasa pamoja na mabadiliko ya sayansi na teknolojia. Mtaala huo utatumika katika Vyuo 6 vya Maendeleo ya Jamii vya Buhare, Ruaha, Uyole, Mlale, Monduli na Rungemba. Kwa upande wa vyuo vya maendeleo ya jamii-Ufundi mitaala yao ilifanyiwa mapitio mwaka 2016/17.

Mashirika Yasiyo ya Kiserikali

172. Mheshimiwa Spika, Wizara imeendelea kuratibu Mashirika Yasiyo ya Kiserikali kwa kuweka mazingira wezeshi ya kuchangia katika kuleta maendeleo ya Taifa. Kwa kipindi cha Julai hadi Machi, 2018, jumla ya **Mashirika Yasiyo ya Kiserikali 192 yalisajiliwa**. Kati ya mashirika yaliyosajiliwa, **mashirika 21** yalisajiliwa katika ngazi ya Kimataifa, **162** katika ngazi ya Kitaifa na **Mashirika 9** ngazi ya Wilaya. Usajili huu umewezesha jumla ya **mashirika 8,211** kusajiliwa nchini kuanzia mwaka 2005 hadi Machi, 2018 (**Kiambatanisho Na.5**). Mashirika haya yamechangia uboreshaji wa huduma za

kijamii katika nyanja za afya, elimu, maji, mazingira, kilimo, haki za binadamu, utawala bora, jinsia, ufugaji na uvuvi, wanyama pori na nishati.

173. Mheshimiwa Spika, katika kuhakikisha kuwa mashirika haya yanaendesha shughuli zao kwa matakwa ya sheria na taratibu za nchi, **Wizara ilihakiki mashirika** na hadi kufikia Machi, 2018, Mashirika Yasiyo ya Kiserikali **4,868** yalikuwa yamehakikiwa. Aidha, katika uhakiki huo, wizara imebaini jumla ya **mashirika 513** yenye sifa za mashirika ambayo yaliyokuwa yamesajiliwa chini ya Sheria nyingine na kuyajumuisha chini ya Sheria ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali Na.24 ya mwaka 2002. Hatua hii imesaidia kuimarisha uratibu na usimamizi mzuri wa mashirika haya katika misingi ya uwazi, utoaji taarifa na uwajibikaji kwa jamii.

Haki na Maendeleo ya Mtoto

174. Mheshimiwa Spika, ukatili dhidi ya watoto bado ni tatizo kubwa hapa nchini. Kwa mujibu wa Takwimu za Jeshi la Polisi Kuhusu Hali ya Uhalifu kwa mwaka 2017, **matukio ya ukatili dhidi ya watoto yalikuwa 13,457** ikilinganishwa na **matukio 10,551** mwaka 2016 sawa na ongezeko la **asilimia 28**. Ongezeko hili tunaamini ni kutokana na elimu inayoendelea kutolewa na Serikali pamoja na wadau wa maendeleo ya mtoto kuhusu malezi katika familia na jamii kuelewa umuhimu wa kutoa taarifa za matukio katika Mamlaka husika. Katika kukabiliana na tatizo hilo, Wizara kwa kushirikiana na wadau imeendelea kutekeleza Mpango Kazi wa Taifa wa Kutokomeza Ukatili Dhidi ya Wanawake na Watoto (2017/18 – 2021/22). Katika mwaka 2017/18, Kazi zilizofanyika chini ya mpango huu ni **kutoa elimu kuhusu athari za mila na desturi zenye madhara kwa jamii ikiwemo ukeketaji, mimba na ndoa za utotoni** kwa makundi mbalimbali katika jamii. Jumla ya **wananchi 13,020** walipatiwa elimu wakiwemo wanafunzi 8,546, walimu 476, wazee wa mila 56, viongozi wa dini 64, ngariba 38, waendesha bodaboda 168, wazazi/walezi 3,600 na watendaji 72 kutoka mikoa ya Shinyanga, Mara, Tabora, Lindi, Dodoma, Tanga, Dar es Salaam na Katavi.

175. Mheshimiwa Spika, Wizara kwa kushirikiana na wadau imeendelea kuwapatia huduma watoto waliofanyiwa ukatili kupitia **Huduma ya Simu kwa Watoto (Child Help Line)**. Katika mwaka 2017/18, simu 18,464 zilipokelewa kuhusu ukatili dhidi ya watoto. Kati ya simu hizo, simu za watoto 1,072 (Ke 621 na Me 451) ziliwezesha kupata huduma (chakula, vifaa vya shule na huduma za sheria na afya) ikilinganishwa na simu za watoto **441 (Ke 325 na Me 96)** waliopata huduma mwaka 2016/17 sawa na ongezeko la asilimia **143**.

176. Mheshimiwa Spika, Wizara imeendelea kuchukua hatua ili **kuzuia ukatili dhidi ya watoto** kwa kuwajengea uwezo **watoa huduma kwa wahanga wa ukatili 1,192** kuhusu namna ya kushughulikia mashauri ya watoto ili kuboresha huduma hizo. Watoa huduma hao ni pamoja na: Maafisa Upelelezi wa mikoa ya Kipolisi, Maafisa Polisi Makao Makuu ya Jeshi la Polisi, Maafisa Maendeleo ya Jamii, Maafisa Ustawi wa Jamii na wajumbe wa Timu za Ulinzi na Usalama wa Mtoto kutoka Halmashauri **15 katika mikoa 7**.

177. Mheshimiwa Spika, maendeleo ya watoto wa kike yamekuwa yakikutana na vikwazo mbalimbali ikiwemo **mimba na ndoa za utotoni**. Kwa mujibu wa Tafiti ya Afya ya Uzazi na Mtoto na Viashiria vya Malaria Tanzania ya mwaka 2015-16, mimba za utotoni ni asilimia 27. Mikoa inayoongoza ni Katavi (45%), Tabora (43%), Dodoma (39%), Morogoro (39%) na Mara (37%). Katika kukabiliana na ndoa na mimba za utotoni, Wizara imezindua **Kampeni ya Kuzuia Mimba za Utotoni ya "Mimi Msichana Najitambua: Elimu ndiyo Mpango Mzima"** Uzinduzi huo ulifanyika katika Kilele cha Maadhimisho ya Siku ya Mtoto wa Kike Duniani, Tarime - Mara tarehe 11/10/2017. Kampeni hii imelenga kutoa hamasa kwa watoto wa kike kutumia klabu katika shule za msingi na sekondari ili kuelekeza muda wao mwingi katika elimu, kujitambua na kutoa taarifa za ukiukaji wa haki zao. Aidha, wananchi 13,284 wakiwemo, wanafunzi (8,546), walimu (476), Viongozi wa dini (110), wazee wa mila na watu mashuhuri (90), ngariba (38), waendesha bodaboda (261), wazazi/walezi (3,600) na watendaji wa vijiji (113) kutoka mikoa ya Shinyanga, Tabora,

Lindi, Dodoma, Dar es Salaam, Tanga, Mara na Katavi walipewa elimu kuhusu madhara ya mimba na ndoa za utotoni.

178. Mheshimiwa Spika, katika kuhakikisha **watoto wanashiriki katika maendeleo yao** na kujitambua, kwa mwaka 2017/18 Wizara imeendelea kuwezesha ushiriki wa watoto katika mabaraza na klabu za wasichana za Kujikinga na mimba za utotoni. Jumla ya **mabaraza ya watoto 13 na klabu 600** katika shule za msingi na sekondari zimeanzishwa kwa kipindi cha Julai, 2017 hadi Machi, 2018 na kufikia idadi ya **mabaraza 1,669 na Klabu 2,000**.

Huduma ya Malezi, Makuzi na Maendeleo ya Awali ya Watoto

179. Mheshimiwa Spika, Wizara imeendelea kusimamia utoaji wa huduma ya malezi, makuzi na maendeleo ya awali ya watoto walio chini ya miaka mitano walio katika vituo vya kulelea watoto wadogo mchana (Day Care Centres) vya Serikali na Binafsi. Kwa kipindi cha Julai, 2017 hadi Machi, 2018, **vituo 139** vilipatiwa **usajili** ikilinganishwa na vituo **270** vilivyopatiwa usajili mwaka 2016/17 na hivyo kufikia **vituo 1,046** vilivyosajiliwa nchi nzima. Aidha, watoto 6,075 (Ke 4,018 na Me 2,057) waliandikishwa katika vituo vya kulelea watoto wadogo mchana 2016/17 ikilinganishwa na watoto 4,450 (Ke 3,097, Me 1,353) mwaka 2015/16.

180. Mheshimiwa Spika, Wizara imeendelea kuhakikisha kuwa Walezi wa Watoto wanakuwa na uwezo wa kutoa **malezi stahiki katika vituo vya kulelea watoto wadogo** mchana (Day Care Centres). Katika kufanikisha azma hii, Walezi 600 kutoka Manispaa ya Temeke, Ubungo, Kigamboni na Ilala walijengewa uwezo kwa kupatiwa mafunzo kuhusu programu ya malezi, makuzi na maendeleo ya awali ya mtoto ikiwemo uanzishaji na uendeshaji wa vituo vya kulelea watoto wadogo mchana. Aidha, Wizara imeendelea kuhimiza vituo kuajiri walezi wenye sifa. Hadi kufikia Machi, 2018 jumla ya Walezi wa Watoto 1,882 walikuwepo katika

vituo ikilinganishwa na **Walezi 1,652** mwaka 2016/17 sawa na ongezeko la **asilimia 14**.

181. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2017/18, Wizara imeendelea **kuzalisha wataalamu wa malezi, makuzi na maendeleo ya awali ya mtoto** katika Chuo cha Ustawi wa Jamii Kisangara. Jumla ya wanafunzi 83 (Ke 58 na Me 25) walidahiliwa kwa mwaka 2017/18 ikilinganishwa na wanafunzi 56 (Ke 39 na Me 17) waliodahiliwa mwaka 2016/17. Aidha, wanafunzi 52 (Ke 35 na Me 17) wahitimu katika mwaka 2017/18 ikilinganishwa na wahitimu 8 wote wanawake mwaka 2016/17.

Huduma za Ustawi kwa Watoto

182. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2017/18, Wizara kwa kushirikiana na Asasi Zisizo za Kiserikali imeendelea kuhakikisha upatikanaji wa huduma za msingi za malezi, matunzo na ulinzi kwa **watoto walio katika mazingira hatarishi nchini**. Jumla ya **watoto 6,132 (Ke 2,972 na Me 3,160)** walio katika mazingira hatarishi walipatiwa huduma za msingi katika **makao ya watoto 157** yanayoendeshwa na Taasisi za dini, Mashirika ya watu binafsi na Serikali (**Kiambatanisho Na. 6**) ikilinganishwa na **watoto 4,515 (Ke 2519 na Me 1,996)** mwaka 2016/17. Kati ya watoto hao, **watoto 78 (Ke 43 na Me 35)** wanaishi katika Makao ya Taifa ya Watoto Kurasini ambayo yanamilikiwa na Serikali. Aidha, Kwa kipindi cha Julai, 2017 hadi Machi, 2018, jumla **ya leseni 14 za usajili wa Makao ya watoto** zimetolewa ikilinganishwa na leseni 50 kwa mwaka 2016/17 na kufikia idadi ya makao 157 nchi nzima. Kati ya makao hayo, **moja ni la Serikali na 156** yanamilikiwa na kuendeshwa na watu binafsi, Mashirika yasiyo ya Kiserikali ya kijamii au Taasisi za kidini. **Nitumie fursa hii kuwataka watu/Taasisi zote zinazotoa huduma za malezi kwa watoto wanaoishi katika mazingira magumu kujisajili katika Halmashauri zao mara moja.**

183. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2017/18, Wizara kwa kushirikiana na Shirika la Railway Children Afrika (RCA) imefanya zoezi la utambuzi wa watoto wanaoishi na kufanya

kazi mtaani katika Halmashauri za Ilala, Kinondoni, Temeke, Kigamboni, Ubungo, Arusha, Iringa, Mbeya Jiji, Wilaya ya Mbeya, Dodoma, Nyamagana na Ilemela. Jumla ya **watoto 6,393 (Ke 1,528 na Me 4,865)** walitambuliwa wakiishi na kufanya kazi mtaani katika kipindi cha Disemba, 2017 hadi Januari, 2018. Kati yao, **watoto 1,385 (Ke 410 na Me 975)** walitambuliwa wakiishi na kufanya kazi mtaani kwa muda wa usiku. Wizara inatekeleza mkakati wa kushughulikia tatizo la watoto wanaoishi na kufanya kazi mitaani kwa kuwaunganisha watoto na familia zao. Kati ya watoto waliotambuliwa, **watoto 952 (Ke 83 na Me 869)** wameunganishwa na familia zao.

184. Mheshimiwa Spika, Wizara imeendelea kuhakikisha kuwa **watoto walio katika mkinzano na Sheria** wanapata haki za msingi ikiwa ni pamoja na huduma za sheria na elimu katika mahabusu tano za watoto za Mbeya, Moshi, Tanga, Arusha na Dar es Salaam. Katika mwaka 2017/18, jumla ya **watoto 291 (Ke 13 na Me 278)** walio katika mkinzano na sheria waliwezesha kupata huduma za msingi (chakula, malazi, mavazi, huduma za matibabu na elimu) ikiwa ni pamoja na huduma za msaada wa kisheria ikilinganishwa na watoto **255 (Ke 18 na Me 237)** mwaka 2016/17 sawa na ongezeko la **asilimia 14**. Aidha, Wizara kwa kushirikiana na Kanisa Katoliki Jimbo Kuu la Dar es Salaam imeboresha miundombinu katika mahabusu ya watoto Dar es Salaam kwa kuchimba kisima cha maji sambamba na usimikaji wa tenki la maji lenye ujazo wa lita 10,000.

185. Mheshimiwa Spika, Wizara kwa kushirikiana na Wizara ya Katiba na Sheria imewachepusha **watoto 126 (Ke 24 na Me 102)** kutoka katika mfumo rasmi wa haki jinai kwa kuwarekebisha tabia na kuwaunganisha na familia zao ikilinganishwa na **watoto 72 (Ke 8 na Me 64)** waliochepushwa mwaka 2016/17 sawa na ongezeko la **asilimia 67**. Aidha, katika mwaka 2017/18, Wizara imeendelea kuwezesha huduma za msingi (chakula, malazi, mavazi na huduma za matibabu) ikiwa ni pamoja na marekebisho ya tabia, elimu na mafunzo kwa **watoto wa kiume 35** waliobainika na makosa ya jinai waliopo katika **Shule ya Maadilisho Irambo Mbeya**

ikilinganishwa na **watoto 72** mwaka 2016/17. Katika kipindi hiki Shule ya Maadilisho ilishika nafasi ya kwanza katika Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya kwenye mtihani wa Moko wa Taifa wa Darasa la Saba na watoto wote walifaulu mtihani wa Darasa la Saba.

186. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2017/18, Wizara kwa kushirikiana na OR - TAMISEMI imeendelea na juhudi ya kuhakikisha kuwa watoto wanalelewa katika ngazi ya familia kulingana na Sheria ya Mtoto Na.21 ya mwaka 2009 kwa kutoa **huduma za malezi ya kambo na uasilili**. Wizara imewezesha **watoto 44 (Ke 24 na Me 20)** kuwekwa chini ya malezi ya kambo ikilinganishwa na **watoto 54 (Ke 21 na Me 33)** mwaka 2016/17. Aidha, **watoto 17 (Me 8 na Ke 9) waliasiliwa** mwaka 2017/18 ikilinganishwa na **watoto 21 (Ke 11 na Me 10)** mwaka 2016/17.

187. Mheshimiwa Spika, Wizara imeendelea kuwatambua Watu wa Kuaminika (Fit Persons) ili kulea watoto walio katika mazingira hatarishi. Juhudi hii imewezesha **Watu wa Kuaminika 187** kutambuliwa katika Halmashauri 19 mwaka 2017/18. Hadi kufikia Machi, 2018, jumla ya **watoto 243** wamepitia kwenye familia za watu wa kuaminika katika Halmashauri 19 za Magu DC, Kasulu DC, Kasulu TC, Musoma Dc, Iringa MC, Iringa DC, Mufindi DC, Njombe DC, Makete DC, Mbeya Jiji, Mbeya DC, Mbarali DC, Hai DC, Temeke DC, Arusha DC, Kakonko DC, Kibondo DC, Misenyi DC na Chunya DC. Watu wa kuaminika huchaguliwa na wanajamii ili kulea watoto walio katika mazingira hatarishi.

Huduma za Ustawi kwa Wazee

188. Mheshimiwa Spika, Wizara imeendelea kuratibu upatikanaji wa **huduma za msingi kwa wazee wasiojiweza**. Katika mwaka 2017/18, jumla ya wazee wasiojiweza 517 (Ke 250 na Me 267) wanaoishi katika **makazi 17 ya Serikali** walipatiwa huduma za msingi - chakula, malazi, mavazi na matibabu (**Kimbatanisho Na.7**) ikilinganishwa na wazee 465 (Ke 221 na Me 244) mwaka 2016/17 sawa na ongezeko la asilimia 11. Aidha, Wizara imeendelea kuimarisha mazingira

ya kutolea huduma za ustawi wa jamii katika makazi 17 ya wazee ya Serikali kwa kujenga bwani la kukaa **wazee 20 (Ke 10 na Me 10)** katika Makazi ya Wazee Kolandoto na uwezesaji wa vifaa ikiwa ni pamoja na bajaji 10, vifaa vya jikoni na vifaa vya huduma ya kwanza katika Makazi 17 ya Wazee ya Serikali.

189. Mheshimiwa Spika, Wizara kwa kushirikiana OR - TAMISEMI iliwezesha **wazee 506,943 (Ke 220,312 na Me 286,631) kupata vitambulisho vya matibabu bure** katika kipindi cha Julai hadi Machi, 2018 ikilinganishwa na wazee 74,590 waliopata vitambulisho vya matibabu bure mwaka 2016/17. Juhudi hizi zimewezesha kufikia idadi ya **wazee 581,533 (Ke 254,793 na Me 326,740)** waliopata vitambulisho ikiwa ni **asilimia 35** ya **wazee 1,657,206** waliotambuliwa katika Halmashauri zote (**Kiambatanisho Na. 8**). Kupatiwa vitambulisho hivi ni hatua ya mpito kuelekea kuwapatia wazee walengwa Bima za afya ili waweze kupata matibabu bora bila vikwazo. Aidha, katika Maadhimisho ya **Siku ya Wazee Duniani** yaliyofanyika tarehe 01/10/2017 mjini Dodoma, Wizara iliwezesha **wazee 320** kupima afya zao na kupatiwa ushauri wa kitabibu.

Huduma za Usuluhisho wa Migogoro ya Ndoa na mashauri ya matunzo kwa watoto

190. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2017/18, Wizara kupitia Baraza la Usuluhishi wa Ndoa lililopo chini ya usimamizi wa Kamishna wa Ustawi wa Jamii na Ofisi za Ustawi wa Jamii za Halmashauri zimeendelea kutoa huduma za usuluhishi wa migogoro ya ndoa kwa familia. Kwa kipindi cha Julai, 2017 hadi Machi, 2018, jumla ya **mashauri ya migogoro ya ndoa 13,382** yalipokelewa na kufanyiwa usuluhishi katika Halmashauri mbalimbali nchini na Baraza la Kamishna wa Ustawi wa Jamii (**Kiambatanisho Na.9**) ikilinganishwa na **mashauri ya migogoro ya ndoa 8,454** mwaka 2016/17. Kati ya mashauri hayo, mashauri **11,326 sawa na asilimia 85 yamesuluhishwa** na yamekamilika, mashauri 1,397 sawa na asilimia 10 yamepelekwa mahakamani na mashauri 659 sawa na asilimia 5 yanaendelea na usuluhishi.

191. *Mheshimiwa Spika*, katika kuhakikisha kuwa, watoto wanapata matunzo kutoka kwa wazazi, Wizara imeendelea kufanyia kazi mashauri ya matunzo ya watoto nchini. Kwa kipindi cha mwezi Julai, 2017 hadi Machi, 2018 jumla ya **mashauri ya matunzo ya watoto 11,815** yalipokelewa. Kati ya mashauri hayo, 4,965 yalihusu matunzo ya watoto walio ndani ya migogoro ya ndoa na 5,708 watoto waliozaliwa nje ya ndoa. Kati ya **mashauri yaliyopokelewa, 10,673** yalikamilika kuwezesha huduma kwa watoto na mashauri 1,142 yaliyopewa rufaa kwenda mahakamani ikilinganishwa mashauri ya matunzo ya watoto 12,406 yaliyokamilika mwaka 2016/17 (matunzo ya watoto walio kwenye migogoro ya ndoa 6,557, matunzo ya watoto waliozaliwa nje ya ndoa 4,133 na mashauri 1,716 yaliyopewa rufaa kwenda mahakamani).

USHIRIKIANO WA NDANI NA NJE YA NCHI

192. *Mheshimiwa Spika*, Wizara kwa kushirikiana na Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa na wadau wa sekta itaendelea kuadhimisha siku mbalimbali za maendeleo na ustawi wa jamii kitaifa na kimataifa kwa lengo la kuhamasisha na kufikisha ujumbe kwa umma. Baadhi ya siku hizo ni Siku ya Wanawake, Watoto, Familia, Wazee na Mtoto wa Kike.

UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA TAASISI ZILIZO CHINI YA IDARA KUU YA MAENDELEO YA JAMII

Taasisi ya Maendeleo ya Jamii Tengeru

193. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka 2017/18, Taasisi ya Maendeleo ya Jamii Tengeru **ilidahili jumla ya wanafunzi 1,169** katika fani ya Maendeleo ya Jamii ikiwa ni ongezeko la **asilimia 86** ya udahili wa **wanafunzi 628** mwaka 2016/17. Kati ya wanafunzi waliodahiliwa, **wanafunzi 486** walidahiliwa katika ngazi ya cheti, **wanafunzi 83** Stashahada na **wanafunzi 600** ngazi ya Shahada. Aidha, **wanafunzi 684** waliohitimu mwaka 2017/18 ikilinganishwa na **wahitimu 609** mwaka 2016/17 ikiwa ni ongezeko la **asilimia 12**.

194. Mheshimiwa Spika, Taasisi pia imefanya tafiti tatu ambazo ni Tathmini ya mahitaji ya Ushiriki wa Jamii katika kijiji cha Kikwe wilaya ya Arumeru, tafiti kuhusu watoto walio katika mazingira hatarishi katika sekta isiyo rasmi katika Wilaya ya Arumeru (utafiti kuhusu watoto katika masoko ya jamii) na Tathmini ya changamoto inayowakabili Maafisa Maendeleo ya Jamii Tanzania katika Halmashauri. Matokeo ya tafiti hizi yatawezesha Taasisi ya Maendeleo ya Jamii Tengeru na Wizara kuboresha utoaji wa mafunzo na utekelezaji wa shughuli za maendeleo ya jamii.

Taasisi ya Ustawi wa Jamii – Kijitonyama

195. Mheshimiwa Spika, Taasisi ya Ustawi wa Jamii - Kijitonyama imeendelea kutoa mafunzo katika ngazi ya Cheti, Diploma, Shahada, Stashahada ya Uzamili na Shahada ya Uzamili. Katika mwaka 2017/18, Taasisi ilidahili wanafunzi **1,185 (Ke 811 na Me 374)** katika fani zitolewazo katika ngazi mbalimbali ikiwa upungufu wa **asilimia 6.91 ya wanafunzi 1,273** waliodahiliwa mwaka 2016/17. Upungufu huu umetokana na kuzuiliwa kudahili wanafunzi katika kozi za jioni kwa ngazi ya Shahada. Kati ya wanafunzi waliodahiliwa, wanafunzi 421 walidahiliwa katika ngazi za Cheti, 409 Diploma, 315 Shahada, 28 Stashahada ya Uzamili na 12 Shahada ya Uzamili. Aidha, **wanafunzi 1,122 (Ke 722 na Me 400) walihitimu** mwaka 2016/17 katika fani na ngazi mbalimbali ikilinganishwa na wanafunzi 1,172 (Ke 789, Me 383) waliohitimu mwaka 2015/16 sawa na **ongezeko la asilimia 4.2**.

196. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2017/18, Taasisi ya Ustawi wa Jamii – Kijitonyama imeendelea kuboresha majengo na miundombinu ya kufundishia na kujifunzia kwa kufanya ukarabati wa jengo lenye **madarasa 8 na ujenzi wa maktaba awamu ya 6 umekamilika na awamu ya 7** imeanza. Aidha, Taasisi imewezesha **watumishi wanne** kuhudhuria mafunzo katika fani na ngazi mbalimbali za masomo. Kati yao, wawili waliwezesha kuhudhuria masomo katika ngazi ya **Uzamili na wawili ngazi ya Uzamivu**.

C: VIPAUMBELE VYA WIZARA KWA MWAKA 2018/19

197. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2018/19, Wizara kupitia fungu 52 (Idara kuu ya Afya) imejiwekea vipaumbele vifuatavyo ili kuboresha utoaji wa huduma za afya nchini;

i) Kuimarisha huduma za chanjo kwa watoto ili kuendelea kubaki katika viwango vya juu vya utoaji wa huduma za chanjo ili kuwaepusha watoto na magonjwa yanayoweze kuepukika kwa chanjo

ii) Kuimarisha huduma za kinga dhidi ya magonjwa yanayotokana na kutozingatia kanuni za usafi na usafi wa mazingira kama magonjwa ya kuhara, kuhara damu na kipindupindu kwa kuongeza uhamasishaji na usimamizi wa usafi na usafi wa mazingira.

iii) Kuimarisha huduma za kinga dhidi ya magonjwa yasiyoambukiza kama magonjwa ya moyo, kisukari na saratani kwa kuhamasisha jamii kuepukana na tabia hatarishi na kujijengea tabia ya kufanya mazoezi mara kwa mara na kuzingatia ulaji wa vyakula unaofaa ili kujiepusha na hatari ya kupata magonjwa hayo.

iv) Kuimarisha huduma za afya ya uzazi na mtoto nchini ili kupunguza idadi ya vifo vya wanawake na watoto vinavyotokana na Uzazi kwa kukarabati na kujenga Wodi Maalum kwa ajili ya Watoto wachanga (Neonatal Care Units) katika Hospitali za Rufaa za Mikoa 7 na Wodi za Wazazi na kujenga vyumba vya wagonjwa mahututi (ICU) wanaotokana na uzazi katika Hospitali za Rufaa za Mikoa (5) mitano yenye viwango vikubwa vya vifo vitokanavyo na uzazi.

v) Kupunguza maambukizi ya Malaria, TB na VVU/UKIMWI;

vi) Kuimarisha upatikanaji wa damu salama nchini ikiwa ni pamoja na ujenzi wa Vituo 12) kukusanyia Damu Salama (*Satellite Blood Banks*) katika mikoa 12 yenye uhitaji.

vii) Kuimarisha upatikanaji wa dawa, vifaa, vifaa tiba na vitendanishi katika vituo vyote vya umma vya kutolea huduma za za afya nckiahini

viii) Kuimarisha huduma za matibabu ya kibingwa nchini katika Hospitali za Rufaa za Mikoa, Hospitali za Rufaa za Kanda, Hospitali Maaluma na za Kitaifa ili kusogeza huduma hizi karibu zaidi na wananchi na kupunguza rufaa za nje ya nchi zisizo na ulazima

ix) Kuimarisha ubora wa huduma zinazotolewa katika vituo vya afya vinavyomilikiwa na Serikali

x) Kuboresha vyuo vya mafunzo ya afya ili kuendelea kuzalisha wataalam wenye ubora kwa kufanya upanuzi na ujenzi wa majengo na ukarabati kwenye Vyuo vya Mafunzo ya Afya vya Uuguzi vya Nachingwea, Kibondo, Kagemu, Kondo, Same na Kiomboi; Vyuo vya Mafunzo ya Maafisa Afya vya Bombo Tanga, Mpwapwa na Ngudu Mwanza; vyuo vya Maafisa Tabibu vya Kibaha, Tanga na katika Chuo cha Maabara cha Singida

xi) Kuimarisha Mifumo ya Habari, Takwimu na Teknolojia ili kurahisisha upatikanaji wa Takwimu katika sekta ya Afya.

xii) Kuimarisha mfumo wa ugharimiaji wa huduma za afya nchini kwa kuongeza wigo wa huduma za bima ya afya kwa wananchi ili kufikia malengo ya kuwa na bima kwa wananchi wote na kufikia lengo la afya kwa wote (Universal Health Coverage – UHC).

198. Mheshimiwa Spika, ili kutekeleza vipaumbele vilivyoainishwa katika mwaka 2018/19, kazi zitakazotekelezwa ni pamoja na;

HUDUMA ZA KINGA

199. Mheshimiwa Spika, Katika kipindi cha 2018/19, Wizara itaendelea kutekeleza afua mbalimbali za huduma za kinga ikiwa ni pamoja na;

- i. Kununua na kusambaza **chanjo za watoto** kulingana na mahitaji ya nchi ambapo jumla ya **shilingi bilioni 30** zimetengwa.
- ii. Kuendelea kutoa chanjo ya kwa wasichana wenye miaka kati ya 9 – 14 ili kukabiliana na saratani ya mlango wa kizazi nchi nzima
- iii. Kuongeza wigo na kasi ya uibuaji na tiba kwa wagonjwa wa kifua kikuu katika mikoa yote nchini, ambapo kiasi cha **Shilingi bilioni 5** kimetengwa kwa ajili ya kugharamia ununuzi wa vifaa (catridges) na dawa kwa ajili ya **uchunguzi na matibabu ya kifua kikuu**.

Huduma za Afya ya Uzazi na Mtoto

- i. Kukarabati na kujenga Wodi Maalum kwa ajili ya Watoto wachanga (Neonatal Care Units) katika Hospitali za Rufaa za Mikoa 7 ya Dar es Salaam, Katavi, Geita, Rukwa, Kilimanjaro, Iringa na Kigoma ambapo **shilingi milioni 900** zimetengwa.
- ii. Kupanua Wodi za Wazazi na kutenga vyumba vya wagonjwa mahututi wanaotokana na uzazi katika Hospitali za Rufaa za Mikoa (5) ya Mbeya, Shinyanga, Morogoro, Pwani na Kigoma mitano ya ambapo, **shilingi bilioni 1** zimetengwa.
- iii. Kuimarisha upatikanaji wa huduma ya damu salama kwa kujenga Vituo 12 vya kukusanyia Damu Salama (Satellite Blood Banks) katika mikoa 12 ambapo kiasi cha **shilingi bilioni 4.3** kimetengwa
- iv. Kununua na kusambaza dawa na vifaa vya uzazi wa mpango katika vituo vya kutolea huduma nchini ambapo Serikali imetenga jumla ya **shilingi bilioni 22.5**
- v. Kununua dawa za malaria kwa ajili ya kinamama wajawazito (Sulphadoxine +pyrimethamine), dawa za kuokoa maisha ya mama wajawazito ikiwa ni pamoja na

oxytocin (dawa ya kuzuia kutokwa) na damu baada ya kujifungua, magnesium sulphate (kwa ajili ya kifafa cha mimba), Fefol (kwa ajili ya kuongeza damu) pamoja na Viuadudu (Biolarvicides) ambapo **shilingi bilioni 8.5** zimetengwa.

vi. Kununua na kusambaza vitanda, magodoro, mashuka na vitanda vya kuzalia mama wajawazito ambapo kiasi cha **shilingi bilioni 4.9** kimetengwa

vii. Kuendelea kuboresha upatikanaji wa huduma za uzazi za dharura ikiwemo upasuaji wa kumtoa mtoto tumboni kwa kusimamia ukamilishaji wa ukarabati vituo vya afya 208 ili viweze kutoa huduma ya upasuaji kwa akina mama wanaokabiliwa na uzazi pingamizi

viii. Kutoa chanjo ya kwa wasichana wenye miaka kati ya 9 - 14 ili kukabiliana na saratani ya mlango wa kizazi nchini

HUDUMA ZA TIBA

Dawa, Vifaa, Vifaa Tiba na Vitendanishi.

200. Mheshimiwa Spika, Katika kipindi cha 2018/19 Wizara itaendelea kuimarisha hali ya upatikanaji wa Dawa, Vifaa, Vifaa Tiba na Vitendanishi nchini kwa kununua na kuvisambaza katika vituo vya kutolea huduma za afya. **Jumla ya shilingi bilioni 270 zimetengwa.** Aidha, ili Kuboresha miundombinu ya kutolea huduma kwa kununua vitanda, magodoro, mashuka na kuvigawa katika vituo vya kutolea huduma za afya nchi nzima ambapo **shilingi bilioni 4.9** zimetengwa

Uimarishaji wa Huduma za Matibabu ya Kibingwa

201. Mheshimiwa Spika katika mwaka 2018/19, **Wizara itaendelea** kuimarisha upatikanaji na utoaji wa huduma za matibabu ya kibingwa nchini ambapo kazi zitakazotekelezwa ni pamoja na:

- i. Kuendelea na huduma za kupandikiza figo (renal transplant) katika Hospitali ya Taifa Muhimbili na Hospitali ya Benjami Mkapa
- ii. Kuendelea kutoa huduma za upandikizaji wa vifaa vya kusaidia kusikia kwa kuweka *cochlear implants* katika Hospitali ya Taifa Muhimbili
- iii. Kuendelea na ujenzi wa jengo maalum kwa wagonjwa wanaolipia (private wing) katika Hospitali ya Taifa Muhimbili ambapo jumla ya **shilingi bilioni 16** zimetengwa.
- iv. Kuanzisha Mfuko wa kugharamia Vipandikizi (*Establish revolving fund for procurement of implants*) katika Taasisi ya Mifupa (MOI) ambapo kiasi cha **shilingi bilioni 4.2** kimetengwa
- v. Kununua na kusimika vifaa vya kisasa vya uchunguzi na matibabu ya Saratani katika Taasisi ya Saratani Ocean Road ikiwa ni pamoja na PET Scan **ambapo kiasi cha shilingi bilioni 14.5** zimetengwa.
- vi. Kuendelea na ujenzi wa jengo na kusimikia vifaa vya uchunguzi (X-Ray Building), pamoja na kununua vifaa vya tiba ya mionzi, katika Hospitali ya Rufaa ya Kanda ya Mbeya ambapo kiasi cha **shilingi bilioni 5** zimetengwa.
- vii. Wizara itaendelea na ujenzi wa Hospitali ya Kanda ya Kusini Mtwara ili kusogeza huduma za afya za kibingwa kwa wananchi wa kanda hiyo, ambapo, kiasi cha **shilingi bilioni 1** kimetengwa.
- viii. Wizara imepanga kununua *Ambulances* 27 kwa ajili ya kuimarisha mfumo wa rufaa Nchini

Ukarabati na ujenzi wa Hospitali za Rufaa za Mikoa

202. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka wa fedha 2018/19 Wizara imetenga kiasi cha **shilingi bilioni 30** kwa ajili ya

kuimarisha utoaji wa huduma za afya katika Hospitali za Rufaa za Mikoa kwa kutekeleza kazi zifuatazo;

i) Ukarabati wa Miundombinu ya kutolea huduma za afya katika Hospitali za Rufaa za Mikoa

ii) Kuanzisha na kuboresha vitengo vya dharura (Emergency Units) katika Hospitali za Rufaa za Mikoa

iii) Ujenzi wa Hospitali za Rufaa za Mikoa katika Mikoa ya Katavi, Njombe, Geita, Simiyu, Songwe na Mara

Uhakiki wa Ubora wa Huduma za Afya

203. Mheshimiwa Spika, katika kuimarisha ubora wa huduma za afya nchini, Wizara imekamilisha Mwongozo wa Viwango vya Msingi kwa Vituo vya kutolea huduma za afya nchini (Basic Health Facilities Standards) ambao utanza kutumika mwaka 2018/19. Aidha, Wizara itafanya tathmini ya Ubora wa Huduma zinazotolewa katika vituo vya kutolea huduma za Afya nchini vya umma na kuvipatia hadhi stahiki pamoja na kuvisajili na kuvipatia leseni kulingana na mwongozo huo.

204. Mheshimiwa Spika, Wizara iko katika hatua za mwisho za majadiliano na Global Fund ili kupata fedha za kufanya maboresho ya huduma katika hospitali za rufaa za mkoa 9, hospitali ngazi ya halmashauri 25, vituo vya afya 21 na zahanati 156 baada ya kufanyiwa tathmini na kupewa nyota. Vituo hivi viko katika mikoa ya Kilimanjaro, Mara, Rukwa, Tanga, Iringa, Ruvuma, Mbeya, Njombe na Songwe. Kiasi cha fedha zitakazotumiwa ni **milioni 20** kwa kila zahanati, **milioni 50** kwa kila kituo cha afya, **milioni 100** kwa kila hospitali ya halmashauri, na **milioni 200** kwa kila hospitali ya mkoa.

Rasilimali Watu katika Sekta ya Afya

205. Mheshimiwa Spika, Wizara itaendelea kusimamia eneo la rasilimali watu katika ya afya kwa kufanya ukarabati

na upanuzi wa vyuo afya ambapo jumla ya **shilingi bilioni 8** zimetengwa

VIPAUMBELE VYA WIZARA KWA MWAKA 2018/19 - FUNGU 53
206. *Mheshimiwa Spika*, Katika mwaka wa fedha 2018/19, Wizara kupitia Fungu 53 itatekeleza vipaumbele vifuatavyo:

(i) Kukuza usawa wa jinsia na uwezeshaji wa wanawake kiuchumi;

(ii) Kuimarisha upatikanaji wa haki na huduma za ustawi wa jamii kwa wazee na watoto;

(iii) Kuwezesha utekelezaji wa Mpango wa Taifa wa Kutokomeza Ukatili Dhidi ya Wanawake na Watoto wa mwaka 2017/18 – 2021/22 ili kupunguza ukatili dhidi yao kwa asilimia 50;

(iv) Kuboresha mazingira ya kufundishia na kujifunzia katika Taasisi ya Maendeleo ya Jamii Tengeru na Taasisi ya Ustawi wa Jamii – Kijitonyama;

(v) Kuboresha majengo na miundombinu katika makazi ya wazee, Makao ya Taifa ya Watoto Kurasini, mahabusu za watoto na Shule ya Maadilisho

(vi) Kuweka mazingira wezeshi ili Mashirika Yasiyo ya Kiserikali kuchangia katika kuleta maendeleo ya Taifa; na

(vii) Kuamsha ari ya wananchi kushiriki katika shughuli za maendeleo.

207. *Mheshimiwa Spika*, ili kutekeleza vipaumbele vilivyoainishwa katika mwaka 2018/19, kazi zitakazotekelezwa ni pamoja na:

Kukuza Usawa wa Jinsia na Uwezeshaji Wanawake

208. *Mheshimiwa Spika*, Wizara itaendelea kutekeleza afua mbalimbali za kukuza usawa wa kijinsia na uwezeshaji wanawake kwa:

(i) Kuratibu uhamasishaji wanawake wa kuanzisha na kujiunga na vikundi vya kiuchumi ikiwemo SACCOS na VICOBA na kuwaunganisha wanawake na fursa za mikopo;

(ii) Kuwezesha uingizaji wa masuala ya jinsia katika Sera, Mipango na Mikakati ya Sekta; na

(iii) Kuendelea kutokomeza ukatili wa kijinsia hususan dhidi ya wanawake kwa kutekeleza Mpango wa Taifa wa Kutokomeza Ukatili Dhidi ya Wanawake na Watoto wa mwaka 2017/18 – 2021/22.

Maendeleo Jamii

209. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2018/19, Wizara itaendelea kutekeleza yafuatayo:

(i) Kuendelea kuamsha ari ya wananchi kushiriki katika miradi ya maendeleo katika maeneo yao;

(ii) Kufanya tathmini ya Sera ya Maendeleo ya Jamii ya mwaka 1996; na

(iii) Kuboresha mazingira ya kujifunzia na kufundishia katika vyuo vya Maendeleo ya Jamii.

Mashirika Yasiyo ya Kiserikali

210. Mheshimiwa Spika, Wizara itaendelea kuweka mazingira wezeshi kwa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali kushiriki kikamilifu katika kuchangia maendeleo na ustawi wa jamii kwa kutekeleza yafuatayo:

(i) Kuendelea kusajili Mashirika Yasiyo ya Kiserikali;

(ii) Kuendelea kufuatilia utendaji wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali na kuhakikisha yanatoa mchango unaotarajiwa kwa maendeleo na kufuata Sheria ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali Na.24 ya mwaka 2002; na

(iii) Kutathmini utendaji wa Sera ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali ya mwaka 2001.

Haki na Maendeleo ya Mtoto

211. Mheshimiwa Spika, Katika kipindi cha 2018/19, Wizara itaendelea kutekeleza afua mbalimbali ili kuhakikisha watoto wanapata haki zao kwa kutekeleza yafuatayo:

(i) Kutathmini utekelezaji wa Sera ya Maendeleo ya Mtoto ya mwaka 2008;

(ii) Kuimarisha hali ya upatikanaji wa haki za msingi za mtoto;

(iii) Kukuza ari na mwamko wa jamii katika kulinda haki na ustawi wa maendeleo ya mtoto; na

(iv) Kuendelea kutekeleza Mpango wa Taifa wa Kutokomeza Ukatili Dhidi ya Wanawake na Watoto wa mwaka 2017/18 – 2021/22.

Huduma za Ustawi wa Jamii

212. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2018/19, Wizara kwa kushirikiana na wadau itaendelea kutekeleza na kuboresha yafuatayo;

(i) Kuwezesha upatikanaji wa huduma ya malezi, makuzi na maendeleo ya awali ya watoto;

(ii) Kutoa huduma kwa watoto walio katika mazingira hatarishi na watoto walio katika mkinzano na sheria;

(iii) Kusajili makao ya watoto walio katika mazingira hatarishi;

(iv) Kuimarisha hali ya upatikanaji wa haki na huduma za msingi kwa wazee wasiojiweza; na

(v) Kutoa huduma za usuluhishi wa migogoro ya ndoa katika familia.

Rasilimali Watu katika Sekta ya Maendeleo na Ustawi wa Jamii

213. Mheshimiwa Spika, Wizara itaendelea kusimamia utoaji wa mafunzo ya maendeleo na ustawi wa jamii katika Vyuo nane vya Maendeleo ya Jamii, Chuo cha Ustawi wa Jamii Kisangara, Taasisi ya Maendeleo ya Jamii Tengeru na Taasisi ya Ustawi wa Jamii – Kijitonyama. Katika mwaka 2018/19 shughuli zifuatazo zitatekelezwa:

(i) Kudahili **wanafunzi watarajiwa 6,848**. Kati yao, **wanafunzi 3,653** katika Vyuo nane vya Maendeleo ya Jamii, **wanafunzi 50** Chuo cha Ustawi wa Jamii Kisangara, **wanafunzi 1,200** Taasisi ya Maendeleo ya Jamii Tengeru na **wanafunzi 1,945** Taasisi ya Ustawi wa Jamii – Kijitonyama;

(ii) Kuendelea kugharamia mafunzo ya uzamili na uzamivu kwa Wakufunzi na Wahadhiri wa kada mbalimbali;

(iii) Kuendelea kuboresha miundombinu katika Vyuo vya Maendeleo ya Jamii (Mlale na Misungwi); na

(iv) Kuendelea kuajiri Wakufunzi na Wahadhiri katika Vyuo vya Maendeleo ya Jamii, Taasisi ya Maendeleo ya Jamii Tengeru, Taasisi ya Ustawi wa Jamii – Kijitonyama na Chuo cha Ustawi wa Jamii Kisangara.

D: SHUKRANI

214. Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua nafasi hii ya kipekee kuzishukuru nchi za Denmark (DANIDA), Uswisi (SDC), Korea Kusini (KOICA), Ireland (Irish Aid), Canada (DFATD) na Mashirika ya Maendeleo ya Kimataifa yakiwemo Benki ya Dunia na UNICEF kwa kutoa misaada katika Mfuko wa Pamoja wa Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee

na Watoto ambao umesaidia kwa kiasi kikubwa kuboresha huduma za afya nchini. Pia, napenda kuzishukuru nchi za Canada, China, Cuba, Hispania, India, Italia, Japan, Marekani, Misri, Sweden, Uingereza, Ujerumani na Ufaransa na ambazo zimeendelea kuisaidia Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto kwa njia mbalimbali.

215. Mheshimiwa Spika, vilevile nayashukuru mashirika mengine ya Kimataifa kwa ushirikiano wao waliotoa kwa Wizara. Mashirika haya yanajumuisha Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB), Mfuko wa Dunia wa Kupambana na UKIMWI, Kifua Kikuu na Malaria (Global Fund), Jumuiya ya Nchi za Ulaya (EU), GAVI, Shirika la Kimataifa la Nguvu za Atomiki (IAEA), Shirika la Afya Duniani (WHO), Shirika la Umoja wa Mataifa la Kudhibiti UKIMWI (UNAIDS), Shirika la Umoja wa Kimataifa la Maendeleo (UNDP), UNFPA, UN-Women, Shirika la Afya Duniani (WHO) na Benki ya Dunia (WB). Wengine ni Abbott Fund, BASIC NEED (UK), ACF – Canada, Baylor College of Medicine ya Marekani, Canadian Bar Association, CDC, CORDAID (Netherlands), CUAMM, DANIDA, DFID, Engender Health (USA), EED, Elizabeth Glaser Paediatric Aids Foundation (EGPAF), Family Health International (FHI360), FINIDA, GIZ, Good Samaritan Foundation (GSF), German TB and Leprosy Relief Association (GLRA), HelpAge International, ILO, Jane Adams School of Social Work ya Chuo Kikuu cha Illinois Marekani, John Snow Incorporation (JSI), KfW, Global Partnership for Education (GPE), Madaktari Afrika na Madaktari Wasio na Mipaka (Medicins Sans Frontieres – MSF), MSERIOR, ORIO, P4H, SAREC, SDC, SIDA (Sweden), Shirika la Upasuaji la Spain, SIGN la Marekani, na Shirika la Human Resource Capacity Project, Touch Foundation, USAID na, Children Investment Foundation Fund (CIFF), World Lung Foundation.

216. Mheshimiwa Spika, tunawashukuru pia Wadau wa Maendeleo ambao ni African Programme for Orchorcerciasis Control, Africare, Axios International, Aids Relief Consortium, AIHA, ASCP, ASM, APHL, Balm and Gillead Foundation, Bill and Melinda Gates Foundation, Clinton Health Access Initiative, CLSI, CMB, Christoffel Blinden Mission (CBM), Christian Relief

Services (CRS), Department of Defence ya Marekani, Community of Saint Egidio (DREAM), Duke University, ECSA, Futures Group, Glaxo Smith Kline (GSK), General Electric (GE – USA), Havard University na University of Maryland, Helen Keller International, Henry Jackson Foundation, IMA, ICAP, International Trachoma Initiative, Intrahealth, International Eye Foundation, I-TECH, Jhpiego, Johns Hopkins University, Labiofarm Industry, London School of Hygiene and Tropical Medicine, Management Science for Health (MSH), MEDA, Merck & Company, Malaria No More, Military Advancement for Medical Research, NOVARTIS, Pathfinder, PATH, President’s Emergency Plan for AIDS Relief (PEPFAR), Pharm Access International, PactWorld, Plan International, Pfizer, Qiagen, Research Triangle Institute (RTI), Regional Psychosocial Support Initiatives (REPSSI), Saint Thomas Hospital- London, Save the Children, SightSavers International, Global Health Supply Chain (GHSC) na University of Columbia, URC, USA-Presidential Malaria Initiative (PMI), World Vision, FXB, Walter REED Army Institute of Research (WRAIR) na World Education Inc.

217. Mheshimiwa Spika, katika kipindi hiki cha utendaji wangu wa kazi nikiwa Waziri, nimepata ushirikiano mkubwa kutoka kwa viongozi na wafanyakazi wa Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto. Napenda kumshukuru **Mheshimiwa Dkt. Faustine Ndugulile (Mb.)**, Naibu Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto kwa ushirikiano anaonipa katika kutekeleza majukumu yangu. Aidha, naomba kuwashukuru **Dkt. Mpoki M. Ulisubisya** Katibu Mkuu (Afya) na **Bibi Sihaba Nkinga** Katibu Mkuu (Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto) kwa mchango wao katika kuwezesha utekelezaji wa majukumu yangu. Vilevile, nawashukuru **Prof. Muhammad Bakari Kambi**, Mganga Mkuu wa Serikali, Makamishna, Wakurugenzi na Wakuu wa Vitengo vya Wizara. Nawashukuru pia, Mkurugenzi wa Hospitali ya Taifa Muhimbili Prof. Lawrence Museru, Mkurugenzi wa Taasisi ya Mifupa Muhimbili (MOI) Dr. Respicious Boniface Rwezimula; Mkurugenzi wa Taasisi ya Moyo Jakaya Kikwete (JKCI), Prof. Mohamed Janabi; Mkurugenzi wa Taasisi ya Saratani ya Ocean Road (ORCI); Dr. Julius Mwaiselage; na Mkurugenzi wa Hospitali ya Benjamin Mkapa (BMH) Dkt.

Alphonse Chandika; Mkurugenzi wa Hospitali Maalum ya Kibong'oto Dkt. Riziki Kisonga, Mkurugenzi wa Hospitali ya Afya ya Akili Mirembe Dkt. Erasmus Mndeme, Mkurugenzi wa Hospitali ya Rufaa ya Kanda Mbeya Dkt. Godlove Mbwangi; Mkurugenzi wa Hospitali ya Rufaa ya Kanda Bugando Dkt Abel Makubi; Mkurugenzi wa Hospitali ya Rufaa ya Kanda ya KCMC Dkt Gilead Masenga. Aidha, nichukue fursa hii pia kuzishukuru Taasisi zilizo chini ya Wizara pamoja na Waganga Wakuu wa Mikoa na Wilaya, Waganga Wafawidhi wa Hospitali, Vituo vya Afya na Zahanati, Wakuu wa Vyuo vya Mafunzo vilivyo chini ya Wizara na wafanyakazi wote wa Wizara na Mashirika ya Dini (FBOs), ya kujitolea na Binafsi. Natoa shukrani kwa sekta zote ambazo tunashirikiana nazo katika kutoa huduma za afya, maendeleo ya jamii na ustawi wa jamii pamoja na wananchi wote kwa ushirikiano wao. Nawaasa waendeleo kuzingatia misingi ya huduma bora na kufanya kazi kwa bidii kwa manufaa ya taifa letu.

218. Mheshimiwa Spika, natumia fursa hii kuishukuru familia yangu, kwa upendo na uvumilivu na kunitia moyo katika kutekeleza majukumu yangu ya Kitaifa. Aidha Napenda kuwashukuru wananchi wote wa Mkoa wa Tanga kwa ushirikiano wanaoendelea kunipatia katika kuendeleza Mkoa wetu. Naahidi kuwa nitaendelea kuwatumikia kwa akili na nguvu zangu zote ili kuleta Maendeleo katika Mkoa wetu.

E: MAOMBI YA FEDHA KWA KAZI ZILIZOPANGWA KUTEKELEZWA KATIKA MWAKA WA FEDHA 2018/19

Fungu 52 - Afya

Mapato

219. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2018/19 Wizara imekadiria kukusanya mapato ya **Shilingi 240,042,508,157.00** Kati ya fedha hizo **Shilingi 220,267,010,057.00** zitakusanywa katika mashirika na taasisi zilizo chini ya Wizara na **Shilingi 19,775,498,100.00** ni kutoka makao makuu.

Matumizi ya Kawaida

220. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka 2018/19, Wizara inakadiria kutumia kiasi cha **Shilingi 304,473,476,000.00** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 88,465,756,000.00** zitatumika kwa ajili ya Matumizi Mengineyo na **Shilingi 216,007,720,000.00** zitatumika kwa ajili ya Mishahara ya Watumishi.

Miradi ya Maendeleo

221. *Mheshimiwa Spika*, kwa upande wa shughuli za maendeleo, Wizara inakadiria kutumia **Shilingi 561,759,999,000** kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo. Kati ya hizo, fedha za ndani ni **Shilingi 184,959,999,000** na fedha za nje ni **Shilingi 376,800,000,000.00**

Jumla ya Makadirio ya Bajeti kwa 2018/19 kwa Fungu 52 ni Shilingi 866,233,475,000.00

Fungu 53 – Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto Mapato

222. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka 2018/19, Wizara imekadiria kukusanya **Shilingi 3,090,796,000** kutokana na ada za wanafunzi kutoka Vyuo 8 vya Maendeleo ya Jamii na Chuo cha Ustawi wa Jamii Kisangara, ada ya usajili wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali na mauzo ya vitabu vya zabuni.

Matumizi Kwa mwaka 2018/19

223. *Mheshimiwa Spika*, Bajeti ya Wizara kwa mwaka 2018/19 inakadiriwa kuwa **Shilingi 32,140,649,000**. Kati ya makadirio hayo, Matumizi ya Kawaida ni **Shilingi 27,226,804,000** na Miradi ya Maendeleo ni **Shilingi 4,913,845,000**.

Matumizi ya Kawaida

224. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka 2018/19, Wizara inakadiria kutumia kiasi cha **Shilingi 27,226,804,000** kwa ajili

ya Matumizi ya Kawaida. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 15,116,962,000** ni Mishahara ya watumishi na **Shilingi 12,109,842,000** ni Matumizi Mengineyo.

Miradi ya Maendeleo

225. Mheshimiwa Spika, kwa upande wa shughuli za maendeleo, Wizara inakadiria kutumia **Shilingi 4,913,845,000** kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 1,500,000,000** ni fedha za ndani na **Shilingi 3,413,845,000** ni fedha za nje.

226. Mheshimiwa Spika, Jumla kuu ya fedha inayoombwa kwa mwaka 2018/19, kwa Fungu 53 ni **Shilingi 32,140,649,000**.

227. Mheshimiwa Spika, Jumla kuu ya fedha inayoombwa kwa mwaka 2018/19, **Shilingi 898,374,124,000**

228. Mheshimiwa Spika, Hotuba hii inapatikana pia katika tovuti za Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto www.moh.go.tz. na www.mcdgc.go.tz.

229. Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.

WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

(Hoja Ilitolewa lamuliwe)

MWENYEKITI: Sasa namwita Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu, Mheshimiwa Serukamba. *(Makofi)*

MHE. PETER J. SERUKAMBA - MWENYEKITI KAMATI YAKUDUMA YA BUNGE YA HUDUMA NA MAENDELEO YA JAMII: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Kanuni ya 99(9) ya Kanuni za Bunge, Toleo la Januari, 2016 naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto kwa mwaka wa fedha 2017/2018, pamoja na maoni ya

Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2018/2019.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Kanuni ya 6(5)(a) na 7(1) ya Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016, Kamati hii ina majukumu la kusimamia utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto na Bajeti ya Wizara hii. Aidha, kwa mujibu wa Kanuni ya 7(1) ya Nyongeza ya Nane ya Kanuni hizo, Kamati hii ina wajibu pia wa kushughulikia Bajeti ya Mwaka ya Wizara hii ya Fungu 52 - Idara Kuu Afya, Fungu 53 - Idara Kuu ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu ya muda, mambo mengi sitayasoma lakini yako kwenye hotuba yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kufanya uchambuzi wa taarifa ya utekelezaji wa bajeti ya mwaka wa fedha 2017/2018 Kamati ilifanya mapitio ya maoni na mapendekezo yaliyotolewa wakati wa kupitisha Bajeti ya mwaka 2017/2018. Jumla ya mapendekezo 20 yalitolewa kwa ajili ya Wizara kufanya utekelezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilifanya uchambuzi wa utekelezaji wa mpango wa bajeti ikiwemo ukusanyaji wa maduhuli na upatikanaji wa fedha kama inavyoonesha katika kitabu chetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi kufikia Februari, 2018 Wizara kupitia Fungu 52 imepokea kiasi cha shilingi bilioni 576.52 sawa na asilimia 53 tu ya bajeti ya mwaka mzima iliyopitishwa na Bunge lako Tukufu cha shilingi trilioni 1.07. Kati ya fedha hizo, shilingi bilioni 190.75 zilipokelewa kwa ajili ya matumizi ya kawaida ya Wizara.

Kuhusu fedha za miradi ya maendeleo kupitia Fungu 52 Wizara ilitengewa shilingi bilioni 785. Hadi kufikia mwezi Februari, 2018 kiasi cha shilingi bilioni 385.7 ambacho ni sawa na asilimia 49 kilipokelewa na Wizara katika miradi hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni maoni ya Kamati kuona kuwa miradi ambayo ilianza kazi na Wakandarasi wote inaendelea. Upo uhaba wa rasilimali watu na changamoto zinazokumba taasisi nyingi zikiwemo Chuo cha Maendeleo ya Jamii Rungemba, Hospitali ya Rufaa ya Kanda -Mbeya inayohudumia takribani mikoa saba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu upungufu wa watumishi, ni maoni ya Kamati kuwa kulingana na umuhimu wa taasisi hizi ni vema Serikali ikatoa kibali cha ajira kwa ajili ya kutatua changamoto za rasilimali watu katika taasisi hizi na taasisi nyingine nchini ili kuhakikisha wananchi wanapata huduma ya afya kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara inatarajia kutekeleza malengo mbalimbali katika mwaka 2018/2019 Fungu 52 na Fungu 53 yakioanisha malengo hayo na mikakati mbalimbali kwa ajili ya kuboresha afya ya Watanzania kama ilivyoelezwa kwa kina kwenye taarifa iliyowasilishwa na Wizara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2018/2019 kupitia Fungu 52 - Idara Kuu Afya, Wizara inatarajia kukusanya kiasi cha shilingi bilioni 240 ikiwa ni ongezeko la 5% la kiasi cha shilingi bilioni 227 iliyokadiriwa kwa mwaka wa fedha 2017/2018. Aidha, kwa kupitia Fungu 53 - Idara Kuu Maendeleo ya Jamii inakadiri kukusanya shilingi bilioni tatu sawa na ongezeko la asilimia 32 la makadirio ya makusanyo ya mwaka uliopita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2018/2019 Wizara kupitia Fungu 52 inakadiri kutumia shilingi bilioni 886.23 kwa ajili ya kutekeleza majukumu yake. Kati ya fedha hizo, kiasi cha shilingi bilioni 304.47 ni sawa na asilimia 34 kwa ajili ya matumizi ya kawaida na kiasi cha shilingi bilioni 561.75 sawa na asilimia 65.6 ni kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tathmini ya uchambuzi wa Kamati imeonesha kuwa makadirio ya matumizi kwa Fungu 52 yameshuka kwa asilimia 19.6 ikilinganishwa na makadirio

ya matumizi ya shilingi trilioni moja yaliyoidhinishwa mwaka uliopita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara kupitia Fungu 52 - Idara Kuu Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto kwa mwaka wa fedha wa 2018/2019 imepanga kutumia shilingi bilioni 32.14. Kati ya fedha hizo, shilingi bilioni 27.2 sawa na asilimia 84.7 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi bilioni 4.91 ni sawa na asilimia 15.3 ni kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, makadirio haya ya fedha yamepungua kwa asilimia 8.1 ikilinganishwa na makadirio ya hili katika mwaka wa fedha 2017/2018.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kielelezo Na. 4 kinaonyesha picha nzuri ya ulinganisho wa makadirio ya upatikanaji wa fedha kwa Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa maoni na ushauri wa mapendekezo ya Kamati kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kupungua kwa Bajeti ya mwaka wa fedha wa 2018/2019 kama ilivyoelezwa kwenye uchamuzi, Bajeti ya Wizara ya Afya Fungu 52 na Fungu 53 imepungua katika mwaka huu 2018/2019.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa makubaliano ya Azimio la Abuja la mwaka 2001 ambapo Tanzania ni kati ya nchi zilizosaini makubaliano hayo ambapo Serikali ilipaswa kutenga trilioni 4.6 sawa na asilimia 15 ya Bajeti nzima ya Serikali kwa mwaka wa fedha wa 2018/2019. Kamati inaishauri Serikali kuongeza Bajeti ya Wizara ya Afya kila mwaka ili iweze kufikia lengo la asilimia 15 kama ambavyo ilikubaliwa katika Azimio la Abuja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu bajeti ya mwaka 2017/2018, katika uchambuzi wa kamati ilibainika kuwa kufika Februari, mwaka 2018 Wizara ilikuwa imepokea asilimia 57 ya bajeti yote. Kamati inaishauri Serikali kuwa licha

ya mwaka fedha kuelekea mwishoni, ni matarajio ya Kamati kwamba Serikali itapeleka fedha hizo zilizotengwa kwa mwaka 2017/2018 kama ambavyo Bunge lako Tukufu liliidhinisha ili huduma zilizopangwa ziweze kutekelezwa ikiwemo ujenzi wa miradi ya maendeleo ya Wizara kupitia Fungu 52 kama vile Hospitali ya Rufaa ya Mbeya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lishe bora ndiyo msingi wa ukuaji wa mwanadamu yeyote kuanzia mtoto akiwa tumboni mwa mama mpaka anapozaliwa na hata ukuaji wake baada ya kuzaliwa. Lishe duni hupelekea kupata madhara makubwa ikiwemo udumavu, vifo vya watoto chini ya miaka mitano, uwezo mdogo wa kufuatilia masomo darasani, hata upeo wa kufanya ubunifu katika kujiletea maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania ni nchi ya tatu Barani Afrika inayoongoza kwa udumavu na ya kumi duniani inayoongoza kwa udumavu uliokithiri. Aidha, kwa Tanzania mikoa inayoongoza kwa lishe duni na kupelekea kuwa na utapiamlo uliokithiri ni pamoja na Singida, Arusha na Manyara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa asilimia kubwa ya vifo vya watoto chini ya miaka mitano vinasababishwa na lishe duni kwa maana ya utapiamlo ambapo mtoto huyo akiugua homa ya kuharisha ni rahisi sana kupoteza maisha kwa muda mfupi kwa kuwa mwili wake hauna uwezo wa kuhimili magonjwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilifanya uchambuzi kwa kutumia takwimu za Twaweza ambazo zinaonesha kwamba kila baada ya dakika 12 mtoto mmoja wa Kitanzania hupoteza maisha kutokana na utapiamlo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hesabu za kawaida kipindi cha Bunge cha masaa manne ya asubuhi kuanzia saa tatu mpaka saa saba mchana takribani watoto 20 wa Kitanzania wasio na hatia hupoteza maisha ambapo ikijumuishwa na masaa ya jioni ni watoto 35 wanakufa kutokana na lishe duni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa uchambuzi huo, Kamati inaona kwamba kwa muda ambao Waheshimiw Wabunge watakaa Dodoma kwa ajili ya kujadili Bajeti ya Serikali ya mwaka wa fedha wa 2018/2019 ambao ni kwa muda wa siku 87 ambapo takribani watoto 10,440 wa Kitanzania watakuwa wamepoteza maisha ambao ni sawa na wapiga kura 27 kwa kila Mbunge wamepoteza watoto wao kwa kipindi hicho kutokana na lishe duni. Hii ni idadi kubwa sana na inatisha sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni maoni ya Kamati kuwa suala la lishe siyo suala la Wizara ya Afya pekee, bali ni suala la kimaendeleo kwa nchi yetu ambalo linahitaji mkakati mahsusi unaotekelezeka kwa kushirikiana na sekta mbalimbali zenye kuimarisha lishe bora kwa Watanzania ili waweze kushiriki vyema katika utekelezaji wa kauli mbiu ya Awamu ya Tano ya Tanzania ya viwanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lishe bora ni suluhu ya matatizo mengi katika jamii ikiwemo ukuaji bora kwa akili ya kuweza kuwa wabunifu na kuleta maendeleo. Lishe bora itasaidia kupunguza mafarakano katika nchi na kuifanya nchi kuwa ya amani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inashauri ni wakati sasa Serikali kuchukua hatua za makusudi kupunguza janga hili ambalo ni janga kubwa zaidi ya janga la UKIMWI kwa vitendo kwa kufuata Mpango wa *National Multisectoral Nutrition Action Plan – NMNAP 2016 - 2021* utekelezwe kwa kuwa katika andiko hilo imeainisha sababu za kwa nini nchi iwekeze katika lishe (ukurasa wa 13 -14) ili kuinua uchumi na kuweza kupunguza matatizo mengi yatokanayo na lishe duni. Hii ni ili kuondoa katika uongozaji wa nchi zenye lishe duni Afrika na duniani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utoaji wa huduma za afya katika vituo vya kutolea huduma unategemea kati ya uwepo wa vifaa, vifaatiba, vitendanishi na rasilimali watu. Uchambuzi wa Kamati ulibaini kuwa kumekuwa na changamoto kubwa ya upungufu wa rasilimali watu kwa

takribani asilimia 48 katika vituo vya kutolea huduma ya afya kuanzia ngazi ya zahanati mpaka hospitali kubwa kutokana na changamoto mbalimbali ikiwemo uondolewaji wa watumishi wa afya katika ajira kutokana na zoezi la uhakiki wa vyeti na Serikali bado haijapeleka watumishi mbadala katika maeneo hayo.

Aidha, kwa mujibu wa utafiti uliofanywa na Taasisi ya *Engender Health* mwaka 2007, Mkoa wa Kigoma una upungufu zaidi wa watumishi wa afya kwa wastani wa asilimia 65.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kielelezo namba 5 kinaonesha ulinganisho wa upungufu wa wataalam wa afya wa ujuzi kwa kila watu 10,000 katika mwaka 2012 mpaka 2016.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati imebaini kuwa upungufu huu umepelekea hata baadhi ya hospitali kama vile Hospitali ya Kanda ya Rufaa ya Mbeya kuajiri watumishi kwa mfumo wa mkataba ili waweze kusaidia kutoa huduma hizo katika maeneo hayo na kulazimika kutumia mapato yake ya ndani kulipia watumishi hao maslahi yao ikiwemo mishahara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaupongeza sana uongozi wa hospitali hiyo kwa kufanya jitihada za kuchukua jukumu la Serikali la kuajiri watumishi wa mkataba ili kuhakikisha kwamba wananchi wa kanda hiyo wanapata huduma kwa wakati kwani ni haki yao ya kimsingi. Aidha, Kamati imesikitishwa sana na Serikali kutofanya jukumu lake la kuhakikisha watumishi wa sekta ya afya wanakuwa wa kutosha ili waweze kuokoa maisha ya Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni maoni ya Kamati kutokana na changamoto hii, baadhi ya wananchi wamegeuza maduka ya dawa kuwa ndiyo sehemu zao za kupata tiba kwa wakati na baadhi ya wananchi kujitibu wenyewe (*self medication*) na kupelekea kupata matibabu ambayo siyo sahihi na hatimaye ugonjwa kutengeneza sugu

(*disease resistance*) mwillini ambayo ni hatari kwakuwa athari yake inazidi kuwa kubwa na kuendelea kuliletea Taifa hasara katika kupambana na magonjwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaishauri Serikali kwa ujumla wake (Wizara ya Afya, Utumishi na TAMISEMI) kuweka mpango mkakati wa kuweza kuitatua changamoto hii ya uhaba wa watumishi wa sekta ya afya nchini kwa kutenga fedha, utoaji wa vibali vya ajira mpya ya watumishi hao ili kuweza kutekeleza wajibu wa Serikali wa kuokoa maisha ya Watanzania ili waweze kupata fursa ya kushiriki katika maendeleo yao binafsi, lakini na nchi nzima kwa ujumla wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jukumu la ununuzi na usambazaji wa dawa kwa wananchi ni la Serikali, Wizara ya Afya inalitekeleza na Bohari Kuu ya Dawa. Kwa mujibu wa taarifa ya Wizara inaonesha kuwa usambazaji wa dawa kwa wananchi umeongezeka kufikia asilimia 89.6 kwa upande wa dawa muhimu (*essential medicines*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa licha ya taarifa ya Wizara kuonesha kuwa usambazaji na uwepo wa dawa muhimu katika vituo vya kutolea huduma ya afya kuongezeka, lakini bado kumekuwa na changamoto ya dawa hizo kumfika mlaji kwa maana ya mgonjwa anapokwenda katika kituo cha kupata huduma ya afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni maoni ya Kamati kuwa Serikali ifanye utafiti mdogo wa kuona dawa hizi zinaishia wapi licha ya usambazaji kuongezeka kwa asilimia kubwa ili kuweza kuitatua changamoto hiyo, kwani hitaji la mgonjwa mmoja mmoja ni kupata dawa pale anapohitaji katika ugonjwa unaomsumbua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inapongeza Serikali kwa kuiwezesha Hospitali ya Taifa Muhimbili kuanzisha huduma ya upandikizaji wa figo. Kamati iliarifiwa kuwa mgonjwa mmoja alikuwa amepandikizwa figo na wengine

wanne walitarajiwa kupandikizwa kabla ya kuisha kwa mwezi huu wa Aprili. Upandikizaji huu wa figo hapa nchini utasaidia kupunguza gharama za kupeleka wagonjwa nje ya nchi kwani wastani mgonjwa mmoja hutumia kiasi cha shilingi milioni 100 wakati huduma hiyo hapa nchini inatolewa kwa shilingi milioni 20 tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaishauri Serikali kuendelea kusomesha Wataalam wetu na kuhakikisha kunakuwepo na vifaa vya kisasa ili huduma kubwa za matibabu ziweze kuwa zinapatikana nchini na hivyo kupunguza gharama ambazo Taifa limekuwa likiingia la kupeleka wagonjwa wa figo nje ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama tunavyofahamu, Taasisi ya *MOI* imekuwa ikiboresha huduma zake siku hadi siku na hivyo kuongeza idadi ya wagonjwa wanaofanyiwa upasuaji wa mifupa, ubadilishaji wa nyonga, upasuaji wa uti wa mgongo, ubongo pamoja na upasuaji kwa watoto wanaozaliwa na vichwa vikubwa au mgongo wazi. Kamati inatambua kuwa mwezi Februari, 2018 Taasisi kwa mara ya kwanza imeweza kufanya upasuaji wa mgongo kwa njia ya matundu kwa kushirikiana na Daktari kutoka Hospitali ya BLK ya India.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati imebaini kuwa licha ya taasisi hii kufanya vizuri katika huduma zake, bado changamoto ya fedha kupelekwa ili waweze kutekeleza jukumu lake kwa mwaka wa fedha 2017/2018 iliidhinishiwa shilingi bilioni 3.8 kwa ajili ya kununua vifaa tiba lakini fedha hizi hazijatolewa. Kamati inaitaka Serikali kutoa fedha hizi kabla ya mwaka huu wa fedha kwisha. Aidha, Kamati inashauri utaratibu huo wa kushirikisha wataalam kutoka nje katika kufanya upasuaji, uendelezwe ili kuweza kuwasaidia Madaktari wetu kupata utalaam zaidi na hivyo kupunguza gharama za kupeleka wagonjwa nje ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete imekuwa na mafanikio makubwa kutokana na kazi nzuri wanayofanya. Hata hivyo, taasisi hii bado imekuwa

haipewi bajeti yake kama inavyoidhinishwa na Bunge lako tukufu. Mwaka wa fedha 2017/2018 ilitengewa kiasi cha shilingi bilioni mbili kwa ajili ya ununuzi wa vifaatiba. Hata hivyo mpaka Kamati inakutana na Wizara kwa ajili ya uchambuzi wa bajeti fedha hizo zilikuwa bado hazijatolewa. Kamati inaona bado Serikali haijawa na nia ya kuiwezesha Taasisi hii licha ya kwamba imesaidia kupunguza gharama za kupeleka wagonjwa nje kupata matibabu ya moyo. Kamati inaitaka Serikali ihakikishe fedha hizo zilizoidhinishwa na Bunge lako Tukufu zinatolewa kabla ya mwaka huu kwisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inatambua kazi kubwa zinazofanywa na Hospitali ya Rufaa ya Kanda Mbeya. Kamati ilishuhudia namna Menejimenti ya Hospitali ya Rufaa ya Kanda Mbeya wanavyofanya kazi nzuri licha ya bajeti finyu na upungufu wa Watumishi. Kamati inaishauri Serikali izigeuze hospitali hizi kuwa Hospitali Maalum kama ilivyo Hospitali ya Muhimbili, Bugando na KCMC kwa kuwa na bodi yake ili kurahisisha maamuzi kwa faida ya utoaji wa huduma za afya kwa wananchi kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inatambua kazi kubwa inayofanywa na Taasisi ya Utafiti wa Magonjwa ya Binadamu *NIMR*, hata hivyo imekuwa haiwezeshe kikamilifu kutimiza majukumu yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kipindi cha miaka miwili mfululizo, Bunge lako tukufu limekuwa likitenga Bajeti ya Taasisi hii, shilingi milioni 800 ili kuwezesha ujenzi wa kiwanda cha kutengeneza dawa asili lakini fedha hizi zimekuwa hazitolewi. Mwaka 2018/2019 *NIMR* imepangiwa shilingi milioni 200 kukamilisha kiwanda hiki ikiwa ni pamoja na kukata vyumba (*partitioning of laboratory and office*). Kamati inaitaka Serikali kuhakikisha fedha hizi zinatolewa zote na kwa wakati ili kazi ya kuzalisha dawa zitokanazo na mitishamba ianze.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huduma ya mama na mtoto imekuwa ikikumbana na changamoto mbalimbali.

Pamoja na taarifa za Wizara kuonesha kuwa huduma hii imeendelea kuboreshwa kwa kusambaza dawa na vifaa pamoja ujenzi wa vituo vya afya na chanjo, Kamati inaona bado msukumo zaidi unahitajika hasa katika upatikanaji wa chanjo mbalimbali. Kamati inashauri fedha zilizotengwa katika mwaka huu wa fedha 2018/2019 kwa ajili ya huduma ya mama na mtoto kiasi cha shilingi blioni 12.2 zitolewe zote kwa wakati zikiwemo za ukarabati wa wodi maalum ya watoto wachanga na upanuzi wa wodi ya wazazi ili kuendelea kupunguza vifo vya akina mama na watoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu ujenzi na uboreshaji wa vituo vya afya na upatikanaji wa gari za wagonjwa; Kamati inampongeza sana Waziri wa Afya kwa kuhakikisha vituo vya afya vinajengwa kwa wingi hapa nchini, pia kunakuwepo na magari ya kubeba wagonjwa (*ambulance*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inafahamu umuhimu wa ukarabati na ujenzi wa miundombinu ya kutolea huduma ikiwemo chumba cha upasuaji, maabara, wodi ya wazazi na wodi ya watoto utakaowezesha upatikanaji wa huduma kamili za uzazi. Pia Kamati inafahamu jumla ya shilingi bilioni 40 kutoka Benki ya Dunia zimetolewa kwa ajili ya kuboresha vituo vya afya 100, shilingi bilioni 19 kutoka Denmark zimepokelewa kwa Halmashauri mbalimbali nchini kukamilisha kazi ya ukarabati na ujenzi ambao upo katika hatua mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uboreshaji wa vituo vya afya tafsiri yake ni kupunguza vifo vya wananchi hususani vifo vya mama na mtoto vitokanavyo na uzazi lakini pia kupunguza msongamano katika Hospitali za Wilaya, Mkoa na Rufaa kutokana na uwepo wa huduma muhimu katika vituo hivyo. Kamati inashauri Serikali kuhakikisha fedha hizi zinatumiwa vizuri na vituo vya afya vikamilike kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, magonjwa yasiyoambukiza (*non-communicable disease*) ambayo yanajumuisha Saratani, Sukari, Presha na Figo yamekuwa yakiongezeka na kuua Watanzania wengi. Kamati inafahamu jitihada

zinazofanywa na Serikali katika kutoa chanjo ya saratani ya shingo ya uzazi kwa watoto wa kike chini ya miaka 14. Hata hivyo, bado wananchi wengi hawana ufahamu wa namna ya kujikinga na magonjwa haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Bima ya Taifa kutengeneza vifurushi vya Bima; Serikali iunde mfumo bora wa ugharamiaji wa afya ili uweze kuwa ni sehemu ya kinga na ulinzi ambao wananchi wanapatwa majanga kama vile ugonjwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi karibuni Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alielekeza Hospitali zote za Mikoa kupelekwa chini ya usimamizi wa Wizara ya Afya, jambo ambalo Kamati imekuwa ikishauri kwa muda mrefu sana. Kamati imefarijika sana kuona Serikali inatekeleza jambo hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ugonjwa wa UKIMWI hapa nchini umekuwa ukipigwa vita kwa namna mbalimbali ikiwemo kuwakinga watu wasipate maambukizi mapya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na mfumo wa ugatuaji wa madaraka unaotumika katika utoaji huduma ya afya kwa wananchi, kuna umuhimu mkubwa wa Wizara mama na TAMISEMI kufanya ushirikiano zaidi katika lengo kuu ambalo ni kuhakikisha wananchi wanapata huduma bora ya afya, kwa wakati na mahali walipo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maendeleo ya nchi yoyote huletwa kwa ushirikiano wa Serikali na wananchi ambao wanaelewa tatizo na namna gani ya kulitatuwa. Wananchi hao wanahitaji ushauri kutoka kwa wataalamu mbalimbali wanaoweza kuwapa mwanga wa namna ya kuyafikia maendeleo ambao ni Maafisa wa Maendeleo ya Jamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchukua fursa hii kukushukuru wewe binafsi kwa kunipa muda kuwasilisha taarifa hii mbele ya Bunge lako tukufu. Napenda kumshukuru sana Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia Wazee na

Watoto, Mheshimiwa Ummu Ally Mwalimu pamoja na Naibu Waziri Mheshimiwa Dkt. Faustine Ndugulile kwa ushirikiano wao mkubwa wanaoendelea kuutoa kwa Kamati wakati wote wa shughuli za Kamati. Aidha, napenda kuwashukuru Makatibu Wakuu wa Wizara Kuu ya Afya, Idara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto pamoja na Maafisa Waandamizi wa wizara na taasisi zake zote kwa ushirikiano waliutoa kwa Kamati yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuchukua nafasi hii kuwashukuru wadau wote wa Sekta ya Afya, Maendeleo ya jamii, Jinsia, Wazee na Watoto kwa kazi nzuri wanayoendelea kuifanya kwa wananchi wetu na kwa ushirikiano wao mkubwa wanautoa kwa Serikali kama kutoa huduma za afya. Wadau hawa ni pamoja na *PEPFAR*, *UNDP*, pamoja na *SIKIKI*, *Engender Health* kupitia Mradi wa Thamini Uhai, *Policy Forum* na *TWAVEZA*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaishauri Serikali kushirikiana zaidi na wadau wa afya katika juhudi zote kwa ajili ya manufaa ya kiafya ya wananchi wa Kitanzania na wakati mwingine hulazimika kufika pale ambapo Serikali kwa namna moja au nyingine imeshindwa kufika kutoa huduma kwa wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee kabisa naomba sana niwashukuru Wajumbe wa Kamati yangu kwanza kwa kuendelea kuniamini na kunichagua kuwa Mwenyekiti wao. Pili, naomba nimshukuru sana Makamu Mwenyekiti wangu, niwashukuru Wajumbe wote wa Kamati wa Huduma ya Bunge na Maendeleo ya Jamii, kwa kazi nzuri ambayo wamekuwa wakiifanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuwashukuru kwa dhati Watumishi wa Ofisi ya Bunge, wakiongozwa na Ndugu Stephen Kagaigai, Katibu wa Bunge, Ndugu Athman Hussein Mkurugenzi Idara ya Kamati ya Bunge, Ndugu Dickson Bisile Mkurugenzi Msaidizi kwa kuisaidia na kuiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake kwa weledi mkubwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee kabisa naomba niwashukuru sana Bi. Pamela Pallangyo na Bi. Agnes Nkwera Makatibu wa Kamati; Bi. Modesta Kipiko - Msaidizi wetu wa kufanya kazi kwa weledi mkubwa kwa kuishauri Kamati ili kutekeleza vyema majukumu yetu na kuhakikisha kuwa taarifa hii inakamilika kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, sasa naliomba Bunge lako tukufu likubali kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Afya na Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto pamoja na taasisi zake kwa mwaka wa fedha 2018/2019 kama yalivyowasilishwa na mtoa hoja Fungu 52 jumla ya shilingi 866,236,475,000/= na Fungu 53 jumla ya shilingi 32,140,649,000/=.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**TAARIFA KUHUSU UTEKELEZAJI WA WIZARA YA AFYA,
MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO WA
BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2017/2018 PAMOJA NA
MAONI YA KAMATI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA
MATUMIZI YA WIZARA HIYO KWA MWAKA WA FEDHA
2018/2019 – KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

SEHEMU YA KWANZA

MAJUKUMU YA KAMATI NA MUUNDO WA TAARIFA

1.0 UTANGULIZI

Mheshimiwa Spika, Kwa mujibu wa Kanuni ya 99 (9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016 naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018, pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019.

Mheshimiwa Spika, Kwa mujibu wa Kanuni ya 6(5)(a) na 7(1) ya Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016, Kamati hii ina jukumu la kusimamia utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto na Bajeti ya Wizara hii. Aidha, kwa mujibu wa Kanuni ya 7(1) ya Nyongeza ya Nane ya Kanuni hizo, Kamati hii inao wajibu pia wa kushughulikia Bajeti ya kila Mwaka ya Wizara hii kwa maana ya **Fungu 52** Idara Kuu Afya na **Fungu 53** Idara Kuu Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto.

Vile vile, Kanuni ya 98 (1) ya Kanuni za Bunge, imeweka sharti la Kamati za Kisekta, ikiwemo Kamati hii, kufanya Ukaguzi wa Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo iliyopo chini ya usimamizi wa Kamati hii ikiwemo Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto.

Naomba kutoa Taarifa kuwa Kamati ilifanya Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo iliyotengewa Fedha chini ya Wizara hii kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018 na kufanya Uchambuzi wa Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019 ambayo ni Fungu 52 na 53.

Mheshimiwa Spika, Baada ya maelezo hayo, naomba kutoa taarifa hii ambayo inafafanua mambo manne (4) yafuatayo:-

- i. Hali halisi katika Utekelezaji wa Mapendekezo ya Kamati kwa Mwaka unaoisha;
- ii. Mapitio ya Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018 na Utekelezaji wa miradi ya Maendeleo;
- iii. Uchambuzi wa Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hii kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019; na
- iv. Maoni na Ushauri wa Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019;

SEHEMU YA PILI

2.0 UCHAMBUZI WA KAMATI KATIKA MASUALA MBALIMBALI

2.1 Utekelezaji wa Ushauri wa Kamati

Mheshimiwa Spika, Katika kufanya Uchambuzi wa Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti ya Mwaka wa Fedha 2017/2018, Kamati ilifanya Mapitio ya Maoni na Mapendekezo yaliyotolewa wakati wa kupitisha Bajeti ya Mwaka 2017/2018. Jumla ya Mapendekezo ishirini (20) yalitolewa kwa ajili ya Wizara kufanya utekelezaji.

Mheshimiwa Spika, Katika Maoni, Ushauri na Mapendekezo yaliyotolewa na Kamati iliyopita, yapo maoni yaliyoweza kutekelezwa kikamilifu, yanayoendelea kutekelezwa na ambayo hayajatekelezwa kabisa na Wizara. Katika ushauri uliotekelzwa.

Kamati inaipongeza Serikali na Wizara kwa jitihada hizo na yale ambayo yanaendelea kutekelezwa Kamati inaiomba Wizara kuendelea kusimamia ili yatekelezwe kama ilivyoshauriwa. Na yale ambayo hayajatekelezwa kwa sababu ya kutopata Fedha toka Serikalini Kamati inaiagiza Wizara kufuatilia Fedha hizo na kuyatekeleza mara moja kabla ya Mwaka wa Fedha 2017/2018 haujamalizika, **Rejea Kiambatisho Namba 1.**

3.0 UCHAMBUZI WA TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA MPANGO WA BAJETI NA UZINGATIAJI WA MAONI YA KAMATI KWA MWAKA WA FEDHA 2017/2018.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilifanya uchambuzi wa utekelezaji wa Mpango wa Bajeti ikiwemo ukusanyaji wa maduhuli na upatikanaji wa fedha kama inavyooneshwa ifuatavyo:-

3.1 Uchambuzi wa Ukusanyaji wa Maduhuli kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018

Mheshimiwa Spika, katika vikao vyake vilivyofanyika kwa muda wa siku mbili kuanzia tarehe 22 hadi 2 Machi, 2018,

Kamati ilifanya uchambuzi wa Makusanyo ya Maduhuli kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018.

Mheshimiwa Spika, Katika Mwaka wa Fedha wa 2017/2018, Wizara ilikadiria kukusanya kiasi cha shilingi **Bilioni 227.041** katika **Fungu 52 (Idara Kuu Afya)** ambapo katika Ukusanyaji wa maduhuli hayo hadi kufikia mwezi Machi 2018 Wizara imefanikiwa kukusanya kiasi cha shilingi **Bilioni 144.143** sawa na **asilimia 63.48** tu ya lengo.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Fungu 53 (Idara Kuu ya Maendeleo ya Jamii) Wizara ilikadiria kukusanya kiasi cha shilingi **Bilioni 2.101**. Hadi kufikia mwezi Februari, 2017 Idara hii imekusanya kiasi cha shilingi **Bilioni 1.510** sawa na **asilimia 72.0** ya lengo.

Mheshimiwa Spika, kama inavyoonesha, Makadirio ya makusanyo ya fedha Katika Fungu 52 na Fungu 53 kwa mwaka wa Fedha 2017/2018 bado hayajafikia **asilimia 75** ambayo ni robo tatu ya mwaka wa fedha husika. Kamati inaamini kwamba kwa muda uliobaki Idara Kuu Afya (Fungu 52) itaweza kukamilisha Makadirio ya Makusanyo yao kadiri ilivyojiwekea malengo yake. (**Rejea Kielelezo Na. 1**)

Mheshimiwa Spika, kama inavyoonekana, katika **Fungu 53** (Idara Kuu Maendeleo ya Jamii) Wizara imefanikiwa kukusanya kwa **asilimia 72** ya makadirio yaliyowekwa. Kamati inaipongeza Wizara kwa kufanya ukusanyaji mzuri wa maduhuli ikilinganishwa na makusanyo ya Mwaka wa Fedha 2016/2017 na haya yote ni kutokana na ushauri wa Kamati uliotolewa mwaka jana kwamba wabuni vyanzo vingine vya makusanyo na kuweza kupiga hatua ya kulifikia lengo.

Mheshimiwa Spika, Idara Kuu Afya kwa kipindi kilichopita ilikuwa inafanya vizuri sana katika ukusanyaji wa maduhuli kupitia Taasisi zake lakini kwa Mwaka wa Fedha wa 2017/2018 uchambuzi wa Kamati unaonesha kwamba makusanyo yameshuka ikilinganishwa na miaka iliyopita. ***Kamati inaanza kuwa na mashaka kwamba mifumo bora iliyokuwa imewekwa ya makasanyo imeanza kuteteleka na***

kusababisha Idara Kuu hii kushindwa kufikia malengo yake ya makusanyo.

Kielelezo Na. 1: Ukusanyaji wa Maduhuli kwa Mwaka 2017/2018

Chanzo: Randama za Wizara na usanifu wa Kamati

3.2 Upatikanaji wa Fedha kutoka Hazina

Mheshimiwa Spika, Ugharamiaji wa huduma za afya kwa wananchi wa Tanzania unategemea fedha za ndani na fedha za nje kwa maana ya wafadhili wa Afya. Kwa Mwaka wa Fedha wa 2017/2018 Wizara kupitia Mafungu yake (52 & 53) ilipanga kutekeleza shughuli zake za utoaji wa huduma ya afya kwa wananchi kwa kutumia fedha za ndani.

Mheshimiwa Spika, hadi kufikia mwezi Februari 2018 Wizara kupitia **Fungu 52** ilikuwa imepokea kiasi cha shilingi **Bilioni 576.52** sawa na **asilimia 53** ya bajeti ya mwaka mzima iliyopitishwa na Bunge ya kiasi cha shilingi **Trilioni 1.07**. Kati ya fedha hizo shilingi **Bilioni 190.75** zilipokelewa kwa ajili ya matumizi ya kawaida ya Wizara

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa katika matumizi mengineyo, Wizara imepokea kiasi cha shilingi **Bilioni 59.3** sawa na **asilimia 92.6** ya shilingi **Bilioni 64** zilizoidhinishwa na Bunge.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Fedha za Miradi ya Maendeleo kupitia **Fungu 52** Wizara ilitengewa shilingi **Bilioni 785**. Kati ya Fedha hizo, shilingi **Bilioni 336.3** zilikuwa ni kutoka vyanzo vya ndani na shilingi Bilioni 449.5 ni kutoka vyanzo vya nje. Hadi kufikia mwezi Februari, 2018 kiasi cha shilingi **Bilioni 385.77** ambacho ni sawa na **asilimia 49** kilipokelewa na Wizara ili kuweza kutekeleza miradi hiyo.

Kamati imebaini kuwa katika fedha hizo zilizopokelewa, fedha kutoka vyanzo vya ndani zilizotolewa ni shilingi **Bilioni 64.7** sawa na **asilimia 19** tu ya Fedha iliyoidhinishwa na kwa upande wa fedha za nje shilingi **Bilioni 321** sawa na **asilimia 71.4** zilipokelewa.

Kamati inawashukuru wadau wote wa Maendeleo waliowezesha upatikanaji huu wa fedha na ina amini kabla ya Mwaka wa Fedha kuisha watakamilisha kutoa asilimia 29 iliyobaki.

Mheshimiwa Spika, Kwa upande wa **Fungu 53 (Idara Kuu Maendeleo ya Jamii)**, hadi kufikia mwezi Februari, 2018 Wizara ilikuwa imepokea jumla ya shilingi **Bilioni 15.46** sawa na **asilimia 44** ya kiasi cha fedha kilichoidhinishwa cha shilingi **Bilioni 35.30** kwa ajili ya matumizi ya kawaida. Aidha, fedha kwa ajili ya utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo kati ya kiasi cha shilingi **Bilioni 2.60** zilizoidhinishwa na Bunge, hadi kufikia mwezi Februari, 2018 kiasi cha shilingi **Milioni 921** sawa na **asilimia 35** tu ndicho kilikuwa kimepokelewa.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa fedha zilizotengwa kwa ajili ya utekelezaji wa shuguli za Wizara (**Fungu 52 & 53**) kwa Mwaka wa Fedha wa 2017/2018 zimetolewa kwa kiasi ambacho hakiridhishi na kinyume na matarajio ya Mpango wa Bajeti ambao kwa pamoja kwa

maana ya Serikali na Bunge tulikubaliana. **(Rejea Kielelezo Na. 2)**

Kielelezo Na. 2: Upatikanaji wa Fedha kwa Mwaka 2017/2018

Chanzo: Taarifa ya Wizara na Usanifu wa Kamati

3.3 Maelezo kuhusu Miradi ya Maendeleo iliyokaguliwa

Mheshimiwa Spika, Kwa mujibu wa Kanuni ya 98 (1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Januari, 2016, Kamati ilifanya ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo iliyotengewa fedha katika Mwaka wa Fedha 2017/2018. Idara Kuu Afya Fungu 52, ilitengewa kiasi cha **shilingi 785,805,952,000.00**. Kati ya fedha hizo kiasi cha **shilingi 336,300,000,000.00** ambayo sawa na **asilimia 42.7** ni kutoka vyanzo vya ndani na kiasi cha shilingi **449,505,952,000** ni fedha kutoka vyanzo vya nje kwa maana ya wafadhili.

Aidha, kupitia **Fungu 53** Wizara ilitengewa kiasi cha shilingi **2,606,278,000.00** kwa ajili ya kutekeleza Miradi ya Maendeleo. Kati ya fedha hizo, kiasi cha shilingi **606,278,000.00** sawa na **asilimia 30.3** tu ya ni kutokana na vyanzo vya ndani na **asilimia 69.7** ni kutokana na fedha za wafadhili.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilifanikiwa kufanya ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo mitatu (3) iliyo chini ya Wizara hii kama ifuatavyo;

3.3.1 Mradi wa Upanuzi na Ukatabati wa Chuo cha Maendeleo ya Jamii – Rungemba, Mufindi -Iringa (Namba ya Mradi 6330)

Mheshimiwa Spika, Mradi wa Ukarabati wa Chuo cha Maendeleo ya Jamii – Rungemba ni moja kati ya Vyuo 7 vya Maendeleo ya Jamii vinavyotekelezwa kupitia Mradi Namba 6330 ambavyo kwa ujumla wake katika Mwaka wa Fedha 2017/2018 kupitia **Fungu 53** vilitengewa jumla ya **shilingi 832, 000,000/=**. Kati ya Fedha hizo shilingi **Milioni 258,000,000/=** zilitengwa kwaajili ya Chuo cha Maendeleo ya Jamii cha Rungemba. Mnamo tarehe 16 Machi, 2018, Kamati ilifanya ukaguzi katika chuo hicho kilichopo Mkoa wa Iringa, Wilaya ya Mufindi. Katika ukaguzi wake Kamati ilijulishwa kuwa kiasi cha fedha **shilingi 258,000,000/=** kilichoidhinishwa na Bunge ili kitumike katika Mwaka wa Fedha wa 2017/2018 kwa ajili ya ujenzi wa jengo la mihadhara na kumalizia kuweka uzio hakikutolewa na Serikali mpaka wakati Kamati inafanya ziara ya Ukaguzi.

Mheshimiwa Spika, Kwakuwa Kamati ilifika katika chuo hicho ililazimika kukagua madarasa mawili yenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 180 kwa mara moja yaliyofanyiwa ukarabati na Chuo kupitia fedha zilizotengwa na Wizara katika Mwaka wa Fedha 2016/2017 kiasi cha **shilingi 43,196,537.48**

Mheshimiwa Spika, Kamati ina amini Vyuo hivi vinasaidia kuzalisha wataalam ambao ni nyenzo na chachu muhimu katika maendeleo ya nchi kwa kuwa Wataalam hawa ndiyo wenye jukumu la kuamsha ARI ya wananchi kushiriki katika mambo mbalimbali ya kujiletea Maendeleo katika jamii zetu. ***Serikali haina budi kuhakikisha fedha zinazotengwa kwaajili ya Vyuo vya Maendeleo ya Jamii zinatolewa zote na kwa wakati ili wataalam hawa waweze kusoma katika mazingira yanayoridhisha ili kuleta matokeo yenye tija katika jamii.***

3.3.2 Mradi wa Ukarabati wa Chuo cha Maendeleo ya Jamii – Uyole (Namba ya Mradi 6330)

Mheshimiwa Spika, Mnamo tarehe 18 Machi, 2018, Kamati ilifanya Ziara ya Ukaguzi wa **Mradi Namba 6330** wa Chuo cha Maendeleo ya Jamii Uyole kilichopo katika Mkoa wa Mbeya. Kama ilivyokuwa kwenye Chuo cha Maendeleo ya Jamii cha Rungemba, kati ya shilingi **832,000,000/=** zilizotengwa katika Mwaka wa Fedha 2017/2018 kwa ajili ya Vyuu 7 vya Maendeleo ya Jamii, Chuo hiki cha Uyole kilitengewa kiasi cha shilingi **216,271,050/=** Kati ya Fedha hizo shilingi **117, 271,050/=** zilitengwa kwa ajili ya ununuzi wa Samani za jengo la Utawala na Shilingi **99,000,000/=** kwa ajili ya kukamilisha kazi za Ujenzi wa Maktaba ikiwemo kuweka vigae (*Tiles*), kupiga rangi, ujenzi wa vyoo na Mashimo ya Maji taka, kuweka umeme na kufunga dari.

Mheshimiwa Spika, Mpaka Kamati inafanya Ziara ya Ukaguzi hakuna fedha yoyote iliyokuwa imetolewa. Aidha, Kamati ilibaini uwepo wa nyufa katika baadhi ya kuta za Jengo la Maktaba na hivyo kuelekeza maeneo hayo yafanyiwe marekebisho ili kuepusha kuharibika kwa jengo hilo.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilifanya ukaguzi wa Jengo la Utawala ambalo ujenzi wake ulianza Mwaka 2015/2016 na limegharimu kiasi cha shilingi **277,000,000** (Kati ya fedha hizo, fedha za ndani ni **245,600,000/=** na fedha kutoka Serikalini **31,400,000/=**). ***Kamati ilipongeza Wizara kwa Ujenzi wa Jengo la Utawala ambalo limetumia fedha kidogo na kuwa na ubora unaoridhisha***

Mheshimiwa Spika, Kamati inasikitishwa na hali hii ya Miradi mingi kutopelekewa fedha ambazo Bunge lako Tukufu liliidhinisha kutokana na mapendekezo ya Serikali yenyewe baada ya kujipima katika mikakati yao. Ni rai ya Kamati kuwa, Serikali ihakikishe fedha zilizoombwa kwaajili ya ukarabati wa Chuo hiki zinatolewa mapema kabla ya Mwaka huu wa

fedha wa 2017/2018 kuisha ili Chuo kiweze kudahili wanafunzi wengi zaidi kwani Kamati ilijulishwa kuwa uwezo wa chuo ni kuchukua wanafunzi 600, lakini mpaka sasa wanaodahiliwa ni wanafunzi 300 tu sawa na **asilimia 50** tu ya uwezo wake. Udahili huu hafifu unachangiwa na miundombinu isiyoridhisha.

3.3.3 Mradi wa Hospitali ya Kanda Mbeya (Namba ya Mradi 5422)

Mheshimiwa Spika, mnamo tarehe 19 Machi, 2018 Kamati ilifanya ziara ya ukaguzi wa mradi wa upanuzi wa Hospitali ya Rufaa ya Kanda Mbeya. Mradi huo ni wa ujenzi wa jengo la Radiolojia kwa ajili ya kutatua changamoto ya msongamano wa wagonjwa kutokana na ufinyu wa jengo katika Hospitali hiyo. Ujenzi huo ulianza mnamo mwaka 2011 na makadirio ya mradi yalikuwa ni shilingi **Bilioni 4** ambapo katika mwaka wa Fedha wa 2017/2018 kiasi cha shilingi **Billion 2** kiliidhinishwa na Bunge lako Tukufu kwa ajili ya ukamilishaji wa mradi ambazo hazikutolewa kabisa. Fedha hizo zilikuwa ni kwaajili ya kufanya manunuzi ya vifaa na vifaa tiba kwa ajili ya Hospitali ili iweze kutoa huduma ya Radiolojia. Aidha, ilitarajiwa kwamba jengo hili mara litakapokamilika litafungwa mashine mbalimbali kwa ajili ya kutoa huduma iliyo bora kwa wagonjwa kama vile vipimo vya CT Scan na MRI.

Mheshimiwa Spika, mpaka Kamati inafanya ziara katika hospitali hiyo Kamati ilielezwa kuwa mradi ulikuwa umekamilika kwa **asilimia 62**, hata hivyo Kamati ilipotembelea mradi huo, wajumbe hawakuafiki kiwango cha ukamilikaji wa ujenzi kwa asilimia ambayo ilitajwa kwa mujibu wa taarifa ya Wizara. Ni maoni ya Kamati kuwa, kwa kiwango cha utekelezaji wa mradi huo ni chini ya asilimia 62 iliyoielezwa kwa kuwa mradi unaonekana ni sehemu ya chini ya jengo (*Basement structure*) ndiyo iliyokamilika na kazi kubwa inahitaji kuendelea kufanyika. Aidha, Kamati inaona kuwa, kwa hatua ambayo mradi umefikia hautaweza kukamilika kwa asilimia 100 kwa kiasi cha fedha ambacho kinadaiwa kubaki ambacho ni shilingi **Milion 800** tu.

3.4 Matokeo na Maoni ya Jumla kuhusu Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018

Mheshimiwa Spika, Baada ya Kamati kufanya Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo iliyotengewa Fedha kwa Mwaka wa Fedha wa 2017/2018 kama ambavyo taarifa yake imeeleza, Kamati inatoa Ushauri ufuatao;

a) Hali ya Upatikanaji wa Fedha za Miradi ya Maendeleo

Mheshimiwa Spika, Kama ilivyoelezwa hapo awali, hakuna kiasi chochote cha fedha kilichotolewa kwa ajili ya utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo mitatu (3) katika Wizara hii ambayo Kamati imeweza kutembelea, hivyo kusababisha miradi hiyo kusimama. Serikali kutopeleka fedha kwa wakati katika Miradi ya Maendeleo husika linaonekana kuwa ni jambo la kawaida kwa Serikali kwani miradi mingi ilianza zaidi ya miaka minne iliyopita na mpaka sasa bado miradi hiyo haijakamilika.

Mheshimiwa Spika, Hali hii inapelekea kuibuka kwa changamoto mbalimbali ikiwemo kuvunjika kwa mikataba na kuongezeka kwa gharama za miradi wakati inapomalizika ikilinganishwa na makadirio ya awali ya gharama za ujenzi wa mradi husika kwa kuwa thamani ya fedha hubadilika mwaka hadi mwaka. ***Ni maoni ya Kamati kuwa fedha zinazoidhinishwa na Bunge lako Tukufu baada ya Serikali yenyewe kujitathmini zipelekwe zote na kwa wakati ili miradi iweze kutekelezwa na kutatua changamoto iliyokusudiwa.***

b) Uingiaji na Uvunjwaji wa Mikataba ya ujenzi na wakandarasi

Mheshimiwa Spika, Miradi mingi ya ujenzi imekuwa ikitumia wakandarasi mbalimbali ambao waliaminika kuwa na uwezo wa kufanya kazi hizo. Kamati imebaini kuwa kuna baadhi ya wakandarasi walipewa jukumu kubwa kuliko uwezo wao wa kufanya kazi husika ambapo mwisho wa siku taasisi lililazimika kuvunja mkataba na kutafuta mkandarasi mwingine ili aweze kukamilisha kazi husika.

Aidha, kutokana na mabadiliko ya maamuzi ya Serikali kwamba kuanzia mwaka 2015 ujenzi wa majengo ya taasisi za kiserikali ufanywe na Wakala wa Majengo Tanzania (Tanzania Building Agency -TBA) kumepelekea Hospitali ya Rufaa ya Kanda Mbeya na Chuo cha Maendeleo ya Jamii Uyole kuvunja mikataba na wakandarasi wa awali. Kuvunja huko kwa Mikataba kumepelekea kuongezeka kwa gharama za ujenzi wa miradi husika. ***Ni maoni ya Kamati kuwa, Miradi ambayo iliyoanza kazi na wakandarasi wengine nje ya Wakala wa Majengo basi Serikali iingie mkataba wa ujenzi wa mradi na Mkandarasi ambaye amekwisha fanyiwa upekuzi hasa wa uwezo wake wa kutekeleza mradi huo. Kwa kufanya hivyo, Serikali itaweza kupunguza hasara zisizokuwa na sababu katika fedha za Miradi ya maendeleo. Aidha, Wakala wa Majengo ajitathmini kama anatosha katika utekelezaji wa Miradi ya Serikali katika kiwango kinachohitajika kwani kuwa wakala wa majengo hakumpi uhalali wakala huyo wa kutekeleza miradi ya Serikali chini ya kiwango au makubaliano ya mradi husika.***

c) Serikali iweke Utaratibu wa kupata Hati Miliki za Maeneo yake

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia taasisi zake imekuwa ikimiliki maeneo ambayo ni makubwa na yanapakana na wananchi wa maeneo hayo. Miradi iliyotembelewa na Kamati ni ile inayotekelezwa katika maeneo makubwa na ambayo hayana hati miliki kabisa au baadhi ya eneo kuwa nayo hivyo kusababisha malumbano na wananchi ambao wanaishi karibu na maeneo hayo. Hali hii inaipelekea hasara kwa Serikali kwa kulipa fidia kwa wananchi hao na wakati mwingine kupeleka shauri mahakamani kwa ajili ya kupata haki stahiki. Na wakati mwingine zinashindwa kufanya shughuli za maendeleo katika maeneo yao kama ilivyoelezwa katika Chuo cha Maendeleo ya jamii Rungemba.

Mheshimiwa Spika, ***Ni maoni ya Kamati kuwa Serikali ihakikishe maeneo yote ya taasisi zake yanakuwa na hati miliki ili kupunguza migogoro isiyokuwa ya lazima.***

d) Taarifa za uwepo wa vyuo katika jamii

Mheshimiwa Spika, Udahili wa wanafunzi katika vyuo unategemea taarifa na uelewa wa umahiri wa vyuo husika katika jamii. Kamati imebaini kwamba baadhi ya vyuo kama vile vyuo vya maendeleo ya jamii (Uyole na Rungemba) havifahamiki kwa wananchi hivyo kupelekea kukosa idadi ya wanafunzi kulingana na uwezo (*Capacity*) ya chuo husika. Hali hii inasababisha hata kupunguza ukusanyaji wa mapato ya ndani ya vyuo husika na hivyo kushindwa kujitendesha na kutegemea fedha kutoka Serikali Kuu.

Mheshimiwa Spika, Ni maoni ya Kamati kuwa, vyuo hivyo vitengeneze mpango mkakati wa kuhakikisha vinajitangaza kwa wananchi ili waweze kupata uelewa wa uwepo wa vyuo hivyo na kuwafanya wajunge na masomo katika vyuo husika.

e) Uhaba wa rasilimali watu

Mheshimiwa Spika, Utekelezaji wa majukumu kwa ufanisi wa utoaji wa huduma katika taasisi mbalimbali unategemea na uwepo wa rasilimali watu wenye weledi na ambao wanapata stahiki zao kama watumishi wa Serikali. Kamati imebaini kwamba, katika taasisi ambazo Kamati imetembelea kama vile Chuo cha Maendeleo ya jamii Rungemba ina upungufu wa rasilimali watu kwa **asilimia 43.7** ya mahitaji yao. Aidha, katika Hospitali ya Rufaa ya Kanda Mbeya ambayo inahudumia takribani mkoa 7 ina upungufu wa watumishi kwa **asilimia 47** ya uhitaji. Hali hii imeilazimu Hospitali kutumia mapato yake ya ndani kuajiri baadhi ya watumishi kwa mkataba ili waweze kutoa huduma bora kwa wananchi.

Mheshimiwa Spika, Ni maoni ya Kamati kuwa, kulingana na umuhimu wa taasisi hizi ni vyema Serikali ikatoa kibali cha ajira kwa ajili ya kutatua changamoto ya rasilimali watu katika taasisi hizi na taasisi nyingine nchini ili kuhakikisha wananchi wanapata huduma bora ya afya na kwa wakati.

4.0 UCHAMBUZI WA MPANGO WA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2018/2019

Mheshimiwa Spika, Katika kikao chake na Wizara, Kamati ilipokea, kujadili na kuchambua Mpango wa Makadirio wa Mapato na Matumizi wa Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019.

Mheshimiwa Spika, Wizara inatarajia kutekeleza malengo mbalimbali katika Mwaka wa Fedha 2018/2019 katika **Fungu 52 & 53** yakioanisha malengo hayo na Mikakati mbalimbali kwa ajili ya kuboresha afya za watazania kama ilivyoelezwa kwa kina kwenye Taarifa iliyowasilishwa na Wizara.

Mheshimiwa Spika, Pamoja na malengo mengi ambayo Wizara kupitia Fungu 52 na 53 imeyaeleza, Malengo hayo yameonekana kuwa yana tija katika suala zima la uboreshaji wa Sekta ya Afya kwa kuzingatia Mipango Mikakati mbalimbali pamoja na makubaliano ya Kitaifa na Kimataifa yenye lengo la kuimarisha utoaji wa Huduma ya Afya nchini. Malengo ambayo Wizara inatarajia kutekeleza ni yale ambayo yameainishwa katika miongozo mbalimbali ikiwemo Dira ya Taifa ya Maendeleo (2025), Mpango wa Maendeleo wa Muda Kati 2017/2018-2020/2021, Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Miaka Mitano (2017/2018-2020/21), Malengo ya Maendeleo Endelevu (*Sustainable Development Goals 2030*), Sera ya Afya (2007) Mpango Mkakati wa IV wa Sekta ya Afya (2015-2020). Aidha, Malengo haya yote yanalenga katika kuhakikisha kuwa huduma za afya zenye uwiano wa kijijografia, viwango vya ubora wa hali ya juu, gharama nafuu lakini pia huduma ambazo ni endelevu. Kwa kutekeleza Malengo haya ya Afya kutapelekea kuwa na jamii yenye afya bora na Ustawi wa Jamii ambao utachangia kupelekea Jamii iliyo bora katika Ustawi wa jamii kwa ujumla.

4.1 Uchambuzi wa Makadirio ya Mapato

Mheshimiwa Spika, Katika Mwaka wa Fedha 2018/2019 kupitia **Fungu 52** (Idara Kuu Afya), Wizara inatarajia kukusanya

kiasi cha **Shilingi Bilioni 240** ikiwa ni ongezeko la **asilimia 5** la kiasi cha **shilingi Bilioni 227** kilichokadiriwa kukusanywa katika Mwaka wa Fedha 2017/2018.

Aidha, Wizara kupitia Fungu 53 (Idara Kuu Maendeleo ya Jamii) inakadiria kukusanya kiasi cha **shilingi Bilioni 3** sawa na ongezeko la **asilimia 32** la makadirio ya Makusanyo ya Mapato ya shilingi **Bilioni 2.1** ya Mwaka wa Fedha 2017/2018. Makusanyo haya yanatarajiwa kufanywa kutokana na ada za wanafunzi katika vyuo vya Maendeleo ya Jamii Nane (8).


Mheshimiwa Spika, Mchanganuo wa ulinganisho huo wa Makusanyo ya Maduhuli ni kama inavyooneshwa kwenye Kielelezo Namba 3.

Kielelezo Na. 3: Ulinganisho wa Mapato kwa Mwaka 2017/2018 na 2018/2019

ULINGANISHO WA MAKUSANYO YA MADUHULI 2017/2018 NA 2018/2019

IDARA	2017/2018	2018/2019	ONGZEKO	ONGZEKO %
IDARA KUU AFYA (52)	227,041,160,573	240,042,508,157	13,001,347,584	5.42
IDARA KUU MAENDELEO YA JAMII (53)	2,101,874,000	3,090,796,000	988,922,000.00	32.00
JUMA	229,143,034,573	243,133,304,157	13,990,269,584.00	5.75

Chanzo: Taarifa ya Wizara



Chanzo. Taarifa ya Wizara na Usanifu wa Kamati

Mheshimiwa Spika, Kamati inaipongeza Wizara kwa kuongeza Makadirio haya ya Mapato na ina amini itaweka utaratibu madhubuti wa kuhakikisha fedha hizi zote zinakusanywa kabla ya Mwaka wa Fedha ujao wa 2018/2019 kuisha.

4.2 Uchambuzi wa Makadirio ya Matumizi

Mheshimiwa Spika, Katika Mwaka wa Fedha 2018/2019 Wizara kupitia Fungu 52 (Idara Kuu Afya) inakadiria kutumia kiasi cha **shilingi Bilioni 886.23** kwa ajili ya kutekeleza majukumu yake. Kati ya fedha hizo, kiasi cha shilingi Bilioni **304.47** sawa na **asilimia 34** kwa ajili ya matumizi ya kawaida na kiasi cha shilingi **561,759,999,000.00** sawa na **asilimia 65.6** ni kwa ajili ya utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo.

Mheshimiwa Spika, Tathmini ya Uchambuzi wa Kamati imeonesha kuwa makadirio ya matumizi kwa **Fungu 52** yameshuka kwa **asilimia 19.6** ikilinganishwa na makadirio ya matumizi ya shilingi **Trilioni 1** yaliyoidhinishwa katika Mwaka wa Fedha wa 2017/2018


Mheshimiwa Spika, Wizara kupitia, **Fungu 53** (Idara Kuu Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto) kwa Mwaka

wa Fedha wa 2018/2019 imepanga kutumia kiasi cha shilingi **Bilioni 32.14** kati ya fedha hizo, kiasi cha shilingi **Bilioni 27.22** sawa na **asilimia 84.7** ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na shilingi **Bilioni 4.91** sawa na **asilimia 15.3** ni kwa ajili ya utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo.

Mheshimiwa Spika, Makadirio haya ya fedha yamepungua kwa **asilimia 8.1** ikilinganishwa na makadirio ya hili katika mwaka wa fedha 2017/2018. Aidha, licha ya bajeti nzima katika Fungu hili kuonekana limepungua kama ilivyoelezwa lakini katika makadirio hayo fedha za Miradi ya Maendeleo zinaonekana kuongezeka kwa **asilimia 46.9**. **Kamati inaona kuwa jambo la kuongeza fedha katika fungu hili ni jema lakini Kamati bado ina mashaka na mwenendo utolewaji wa fedha hizi.**

Mheshimiwa Spika, Kielelezo Na. 4 kinaonyesha picha nzuri ya ulinganisho wa Makadirio ya upatikanaji wa Fedha kwa Wizara hii.

Kielelezo Na. 4: Ulinganisho wa Bajeti kwa Mwaka 2017/2018 na 2018/2019



SEHEMU YA TATU

5.0 MAONI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI

Mheshimiwa Spika, Kamati ilikamilisha kufanya Uchambuzi wake kwa Bajeti ya Mwaka wa Fedha 2017/2018 na 2018/2019 katika mafungu yote yaliyo chini ya Wizara hii. Kufuatia uchambuzi huo wa kina Kamati inaomba kutoa Maoni, Ushauri na Mapendekezo yafuatayo;

5.1 Kupungua kwa Bajeti ya Mwaka wa Fedha wa 2018/2019

Mheshimiwa Spika, Bajeti ya Wizara ya Afya kupitia Fungu 52 (Idara Kuu Afya) kwa Mwaka wa Fedha wa 2018/2019 imepangiwa kiasi cha shilingi Bilioni 886.236 kwa ajili ya utekelezaji wa majukumu yake ikiwemo Miradi ya Maendeleo. Bajeti hii imepungua kwa asilimia 19.6 ikilinganishwa na Bajeti ya Mwaka wa Fedha wa 2017/2018 ambapo Wizara ilitengewa kiasi cha shilingi Trilioni 1.07. Aidha, kupitia Fungu 53 Bajeti imepungua kwa asilimia 8.9 ikilinganishwa na Bajeti ya Mwaka wa Fedha wa 2017/2018.

Mheshimiwa Spika, Ni maoni ya Kamati kwamba Serikali inapunguza juhudi zake za ugharamiaji wa utoaji wa huduma za afya nchini kwani kwa kupunguza bajeti hii kutaleta athari kubwa katika utoaji wa huduma kwa wananchi. Kamati inahoji ni nini nia ya Serikali katika uimarishaji wa huduma za afya kwa wananchi?

Mheshimiwa Spika, Kwa mujibu wa makubaliano ya Azimio la Abuja la Mwaka 2001 ambapo Tanzania ni kati ya nchi zilizosaini makubaliano hayo ambapo Serikali ilipaswa kutenga kiasi cha shilingi Trilioni 4.86 sawa na asilimia 15 ya Bajeti nzima ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha wa 2018/2019. Kamati inaishauri Serikali kuongeza Bajeti ya Afya kila mwaka ili iweze kufikia asilimia 15 kama ambavyo ilikubaliwa katika Azimio la Abuja licha ya kwamba muda wake wa utekelezaji umepita na kwa kuwa ni jambo jema basi Serikali iendelee kulifanyia kazi.

5.2 Utekelezaji wa Bajeti ya Mwaka wa Fedha wa 2017/2018

Mheshimiwa Spika, Mwaka wa Fedha wa 2017/2018 Bunge lako Tukufu lilipitisha Bajeti ya Wizara ili iweze kuendelea kutoa huduma za afya kwa wananchi wake kwa wakati na katika ubora unaotarajiwa. Katika Mwaka huo wa Fedha 2017/2018 Fungu 52 Bunge lilipitisha kiasi cha shilingi **Trilioni 1.07** ikijumuisha Fedha za maendeleo. Katika uchambuzi wa Kamati ilibainika kuwa mpaka kufikia mwezi Februari, 2018 Wizara ilikuwa imepokea **asilimia 57** ambapo kiasi kikubwa cha fedha zilizotolewa kilikuwa kwa ajili ya matumizi ya kawaida na Mishahara ya watumishi ambayo lazima itolewe ili kusimamia maslahi ya watumishi. Katika fedha zilizopokelewa na Wizara, ni fedha za maendeleo ambazo ni **asilimia 49** tu ya fedha zote zilizotengwa kwa ajili ya utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo ambapo fedha za ndani zilizopokelewa ni asilimia 19 tu na fedha za nje ni asilimia 71 ya kiasi kilichotengwa.

Mheshimiwa Spika, Ni maoni ya Kamati kuwa huduma za afya kwa wananchi hazijatolewa kadiri ya matarajio a walio wengi kwa kuzingatia upatikanaji wa Fedha kuwa hafifu kutoka Serikali kwenda Wizara ya Afya. ***Kamati inashauri Serikali kuwa licha ya Mwaka wa Fedha kuwa unaelekea mwishoni ni matarajio ya Kamati kwamba Serikali itapeleka fedha zote zilizotengwa kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018 kama ambavyo Bunge lako Tukufu liliidhinisha ili huduma zilizopangwa ziweze kutolewa ikiwemo ujenzi wa Miradi ya Maendeleo ya Wizara kupitia Fungu 52 kama vile Hospitali ya Rufaa ya Kanda Mbeya.***

5.3 Uboreshaji wa Hali ya Lische Nchini

Mheshimiwa Spika, Lische bora ndiyo msingi wa ukuaji wa mwanadamu yeyote kuanzia mtoto akiwa tumboni mwa mama mpaka anapozaliwa na hata ukuaji wake baada ya kuzaliwa. Lische duni hupelekea kupata madhara makubwa ikiwemo udumavu (Stunting), vifo kwa watoto chini ya miaka mitano, uwezo mdogo wa kufuatilia masomo darasani na hata upeo wa kufanya ubunifu katika kujiletea maendeleo.

Mheshimiwa Spika, Tanzania ni nchi ya tatu (3) Barani Afrika inayoongoza kwa udumavu na ya kumi (10) duniani inayoongoza kwa udumavu uliokithiri. Aidha, kwa Tanzania mikoa inayoongoza kwa lishe duni na kupelekea kuwa na utapiamlo uliokithiri ni pamoja na Singida, Arusha na Manyara.

Mheshimiwa Spika, Uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa, asilimia kubwa ya vifo vya watoto chini ya miaka mitano vinasababishwa na lishe duni kwa maana ya utapiamlo ambapo mtoto huyo akiugua homa ya kuharisha ni rahisi sana kupoteza maisha kwa muda mfupi kwa kuwa mwili wake hauna uwezo wa kuhimili ugonjwa.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilifanya uchambuzi kwa kutumia takwimu za Twaweza ambazo zinaonesha kwamba kila baada ya dakika 12 mtoto mmoja wa kitanzania hupoteza maisha kutokana na utapiamlo. Kwa hesabu za kawaida kwa kipindi cha Bunge cha masaa manne (4) ya asubuhi kuanzia saa tatu kamili mpaka saa saba mchana takribani watoto 20 wa kitanzania wasio na hatia hupoteza maisha ambapo ikijumuishwa na masaa ya jioni ni watoto 35 wanakufa kutokana na lishe duni.

Mheshimiwa Spika, Kwa uchambuzi huo, Kamati inaona kwamba kwa muda ambao wabunge watakaa Dodoma kwa ajili ya kujadili Bajeti ya Serikali ya Mwaka wa Fedha wa 2018/2019 ambao ni kwa muda wa siku 87 ambapo takribani watoto 10,440 wakitanzania watakuwa wamepoteza maisha ambao ni sawa na wapiga kura wake 27 wa kila Mbunge wamepoteza watoto wao kwa kipindi hicho kutokana na lishe duni. Hii ni idadi kubwa sana na inatisha sana.

Mheshimiwa Spika, ni maoni ya Kamati kuwa suala la lishe si suala la Wizara ya Afya pekee bali ni suala la kimaendeleo kwa nchi yetu ambalo linahitaji Mkakati mahsusuni unaotekelezeka kwa kushirikiana na sekta mbalimbali ziweze ya kuimarisha lishe bora kwa watanzania ili waweze kushiriki vyema katika utekelezaji wa kauli mbiu ya Awamu ya Tano
Tanzania ya Viwanda.

Mheshimiwa Spika, Lishe bora ni suluhu ya matatizo mengi katika jamii ikiwemo ukuaji bora wa akili ya kuweza kuwa wabunifu na kuleta maendeleo, lishe bora itasaidia kupunguza mifarakano katika nchi na kuifanya nchi izidi kuwa ya amani. Kamati inashauri ni wakati sasa Serikali kuchukua hatua za maksudi za kupunguza janga hili ambalo ni janga kubwa zaidi ya janga la UKIMWI kwa kutumia kwa vitendo Mpango Mkakati wake wa Kitaifa (National Multisectrol Nutrition Action Plan – NMNAP 2016- 2021) utekelezwe kwa kuwa katika andiko hilo imeainisha sababu za kwanini nchi iwekeze katika LISHE (ukurasa wa 13-14) ili kuinua uchumia na kuweza kupunguza matatizo mengi yatokanayo na lishe duni ili pia kuondoka katika uongozaji wa nchi zenye lishe duni Afrika na duniani kwa ujumla.

5.4 Upungufu wa Watumishi wa Afya kwa asilimia 48

Mheshimiwa Spika, utoaji wa huduma za afya katika vituo vya kutolea huduma unategemeana kati ya uwepo wa vifaa, vifaa tiba, vitendanishi na rasilimali watu. Uchambuzi wa Kamati ulibaini kuwa kumekuwana changamoto kubwa ya upungufu wa rasilimali watu kwa takribani **asilimia 48** katika vituo vya kutolea huduma za afya kuanzia ngazi ya Zahanati mpaka Hospitali kubwa kutokana na changamoto mbalimbali ikiwemo uondolewaji wa watumishi wa afya katika ajira kutokana na zoezi la uhakiki wa vyeti na Serikali bado haijapeleka watumishi mbadala katika maeneo hayo. Aidha, kwa mujibu wa utafiti uliofanywa na Taasisi ya *Engender Health* Mwaka 2017, Mkoa wa Kigoma una upungufu zaidi wa Watumishi wa Afya kwa wastani wa **asilimia 65**.

Mheshimiwa Spika, Kielelezo Na. 5 kinaonesha ulinganisho wa upungufu wa wataalam wa afya wenye ujuzi kwa kila watu 10,000 katika Mwaka 2012 na 2016.

Kielelezo Na. 5

ULINGANISHO WA WATAALAM WA AFYA WENYE UJUZI KWA KILA WATU 10,000 KWA MWAKA 2012 NA 2016		
MKOA	2012	2016
DAR ES SALAAM	6.7	19.9
IRINGA	9.7	15.2
NJOMBE	11.4	14.3
KILIMANJARO	10.6	13.1
PWANI	10.1	12.3
RUVUMA	7.3	11.5
MOROGORO	7.6	11.4
MWANZA	5.7	11.1
ARUSHA	8.9	10.1
SINGIDA	6.3	8.8
LINDI	6.3	8.6
MTWARA	5.8	8.6
DODOMA	6	8.5
TANGA	6.3	8.1
MBEYA	7	7.6
MARA	5.8	7.5
RUKWA	4.8	7.2
MANYARA	7.3	6.7
KAGERA	6	6.5
SHINYANGA	5.1	6.4
TABORA	3.9	5.8
KATAVI	2.8	5.3
GEITA	3.5	5.2
SIMYU	2.6	4.8
KIGOMA	3.5	4.7
KITAIFA	6.5	9.6

Mheshimiwa Spika, Kamati imebaini kuwa, upungufu huu umepelekea hata baadhi ya Hospitali kama vile Hospitali ya Kanda ya Rufaa ya Mbeya kuajiri watumishi kwa mfumo wa mkataba ili waweze kuwasaidia katika kutoa huduma hizo katika maeneo yao na kulazimika kutumia mapato yake ya ndani kuwalipa watumishi hao maslahi yao ikiwemo mishahara. Kamati inaupongeza sana uongozi wa Hospitali hiyo kwa kufanya jitihada ya kuchukua jukumu la Serikali la kuajiri watumishi wa mkataba ili kuhakikisha kwamba wananchi wa kanda hiyo wanapata huduma kwa wakati kwani ni haki yao ya kimsingi. Aidha, Kamati pia imesikitishwa sana na Serikali kutofanya jukumu lake la kuhakikisha watumishi wa Sekta ya afya wanakuwa wa kutosha ili waweze kuokoa maisha ya watu.

Mheshimiwa Spika, Ni maoni ya Kamati kuwa kutokana na changamoto hii baadhi ya wananchi wamegeuza maduka ya dawa kuwa ndiyo sehemu zao za kupata tiba kwa wakati na baadhi ya wananchi kujitibu wenyewe (*Self Medication*) na kupelekea kupata matibabu ambayo siyo sahihi na hatimaye ugonjwa kutengeneza sugu (*Disease Resistance*) mwilini ambayo ni hatari kwakuwa athari yake inazidi kuwa kubwa na kuendelea kuliltea taifa hasara katika kupambana na magonjwa husika.

Mheshimiwa Spika, Kamati inashauri Serikali kwa ujumla wake (Wizara ya Afya, Utumishi na TAMISEMI) kuweka mpango mkakati wa kuweza kuitatua changamoto hii ya uhaba wa watumishi wa sekta ya afya nchi kwa kutenga fedha, utoaji wa vibali vya ajira mpya ya watumishi hao ili kuweza kutekeleza wajibu wa Serikali wa kuokoa maisha ya watazania na waweze kupata fursa ya kushiriki katika maendeleo yao binafsi lakini na nchi nzima kwa ujumla wake.

5.5 Upatikanaji wa Dawa kwa mgonjwa katika vituo vya kutolea huduma ya afya

Mheshimiwa Spika, jukumu la ununuzi na usambazaji wa dawa kwa wananchi ni la Serikali kupitia Wizara ya afya ikitekelezwa na Bohari Kuu ya Dawa. Kwa mujibu wa taarifa

ya Wizara inaonesha kuwa usambazaji wa dawa kwa wananchi umeongezeka hadi kufikia asilimia **89.6 kwa upande wa dawa muhimu (Essential Medicines).**

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa kamati umebaini kuwa licha ya taarifa ya Wizara kuonesha kuwa usambazaji na uwepo wa dawa muhimu katika vituo vya kutolea huduma ya afya kungezeka lakini bado kumekuwa na changamoto ya dawa hizo kumfika mlaji kwa maana ya mgonjwa anapokwenda katika kituo cha kupata huduma ya afya.

Mheshimiwa Spika, ni maoni ya Kamati kuwa, Serikali ifanye utafiti mdogo wa kuona dawa hizi zinaishia wapi licha ya usambazaji kungezeka kwa asilimia kubwa ili kuweza kuitatua changamoto hiyo, kwani hitaji la mgonjwa mmoja mmoja ni kupata dawa pale anapohitaji kutibu ugonjwa unaomsumbua.

5.6 Hospitali ya Taifa Muhimbili

Mheshimiwa Spika, Kamati inapongeza Serikali kwa kuiwezesha Hospitali ya Taifa Muhimbili kuanzisha huduma ya upandikizaji wa Figo. Kamati iliarifiwa kuwa mgonjwa mmoja alikuwa amepandikizwa figo na wengine wanne walitarajiwa kupandikizwa kabla ya kuisha kwa Mwezi huu wa Aprili. Upandikizaji huu wa figo hapa nchini utasaidia kupunguza gharama za kupeleka wagonjwa nje ya nchi kwani kwa wastani mgonjwa mmoja hutumia kiasi cha shilingi Milioni 100 wakati huduma hiyo hapa nchini inatolewa kwa shilingi milioni 20 tu.

Kamati inaishauri Serikali kuendelea kusomesha Wataalam wetu na kuhakikisha kunakuwepo na vifaa vya kisasa ili huduma kubwa za matibabu ziweze kuwa zinapatikana nchini na hivyo kupunguza gharama ambazo Taifa limekuwa likiingia la kupeleka wagonjwa wa figo nje ya nchi.

5.7 Taasisi ya Mifupa MOI

Mheshimiwa Spika, kama tunavyofahamu Taasisi ya MOI imekuwa ikiboresha huduma zake siku hadi siku na hivyo kuongeza idadi ya wagonjwa wanaofanyiwa upasuaji wa Mifupa, ubadilishaji wa nyonga, upasuaji wa uti wa mgongo, ubongo pamoja na upasuaji kwa watoto wanaozaliwa na vichwa vikubwa na mgongo wazi. Kamati inatambua kuwa Mwezi Februari Mwaka huu Taasisi kwa mara ya kwanza imeweza kufanya upasuaji wa mgongo kwa njia ya Matundu kwa kushirikiana na Daktari kutoka Hospitali ya BLK ya India.

Mheshimiwa Spika, Kamati imebaini kuwa licha ya taasisi hii kufanya vizuri katika huduma zake bado kuna changamoto ya fedha kupelekwa ili waweze kutekeleza majukumu yake. Katika Mwaka wa Fedha 2017/2018 MOI iliidhinishwa **shilingi Bilioni 3.8** kwa ajili ya kununua vifaa Tiba lakini fedha hizi hazikutolewa. ***Kamati inaitaka Serikali kutoa fedha hizi kabla ya Mwaka huu wa fedha kuisha. Aidha, Kamati inashauri Utaratibu huu wa kushirikisha wataalam kutoka nje katika kufanya upasuaji uendelezwe ili kuweza kuwasaidia Madaktari wetu kupata utalaam zaidi na hivyo kupunguza gharama za kupeleka wagonjwa nje ya nchi.***

5.8 Taasisi ya Moyo Jakaya Kikwete (JKCI)

Mheshimiwa Spika, Taasisi ya Moyo JKCI imekuwa na mafanikio makubwa kutokana na kazi nzuri wanayofanya. Hata hivyo, Taasisi hii bado imekuwa haipewi bajeti yake kama inavyoidhinishwa na Bunge lako Tukufu. Katika Mwaka wa Fedha 2017/2018 JKCI ilitengewa kiasi cha **shilingi Bilioni 2** kwa ajili ya ununuzi wa Vifaa Tiba, hata hivyo mpaka Kamati inakutana na Wizara kwaajili ya uchambuzi wa Bajeti fedha hizo zilikuwa bado hazijatolewa. Kamati inaona bado Serikali haijawa na nia ya dhati ya kuiwezesha Taasisi hii licha ya kwamba imesaidia kupunguza gharama za kupeleka wagonjwa nje kupata matibabu ya moyo. ***Kamati inaitaka Serikali ihakikishe fedha hizi zilizoidhinishwa na Bunge lako Tukufu zitolewe zote kabla ya Mwaka wa Fedha huu kuisha.***

5.9 Hospitali ya Rufaa ya Kanda Mbeya na Hospitali ya Mtwara

Mheshimiwa Spika, Kamati inatambua kazi kubwa zinazofanywa na Hospitali hizi. Kamati ilishuhudia namna Menejimenti ya Hospitali ya Rufaa ya Kanda Mbeya inavyofanya kazi nzuri licha ya bajeti finyu na upungufu wa Watumishi. Kamati inashauri Serikali izigeuze Hospitali hizi kuwa Hospitali Maalum kama ilivyo Hospitali ya Muhimbili, Bugando na KCMC kwa kuwa na Bodi yake ili kurahisisha maamuzi kwa faida ya utoaji wa huduma za afya kwa wananchi kwa wakati.

5.10 Taasisi ya Utafiti wa Magonjwa ya Binadamu NIMR

Mheshimiwa Spika, Kamati inatambua kazi kubwa inayofanywa na Taasisi hii. Hata hivyo imekuwa haiwezeszwi kikamilifu kutimiza majukumu yake, kwa kipindi cha miaka miwili mfululizo, Bunge lako limekuwa likitenga Bajeti ya Taasisi hii kiasi cha shilingi Milioni 800 ili kuwezesha ujenzi wa Kiwanda cha kutengeneza dawa asili lakini fedha hizi zimekuwa hazitolewi. Katika Mwaka huu wa Fedha 2018/2019, NIMR imepangiwa shilingi Milioni 200 ili kukamilisha kiwanda hiki ikiwa ni pamoja na kukata vyumba (*partitioning of Laboratory and Office*). ***Kamati inaitaka Serikali kuhakikisha fedha hizi zinatolewa zote na kwa wakati ili kazi ya kuzalisha dawa zitokanazo na mitishamba ianze.***

5.11 Huduma ya Mama na Mtoto

Mheshimiwa Spika, huduma ya mama na mtoto imekuwa ikikumbana na changamoto mbalimbali. Pamoja na Taarifa za Wizara kuonesha kuwa huduma hii imeendelea kuboreshwa kwa kusambaza dawa na vifaa pamoja ujenzi wa vituo vya afya na chanjo, Kamati inaona bado msukumo zaidi unahitajika hasa katika upatikanaji wa chanjo mbalimbali. ***Kamati inashauri fedha zilizotengwa katika mwaka huu wa fedha 2018/2019 kwa ajili ya Huduma ya Mama na Mtoto kiasi cha shilingi Bilioni 12.2 zitolewe zote kwa wakati zikiwemo za ukarabati wa Wodi maalum ya Watoto***

wachanga (Neonatal Care Units) na upanuzi wa wodi za wazazi ili kuendelea kupunguza vifo vya akina mama na watoto.

5.12 Ujenzi na uboreshaji wa Vituo vya Afya na Upatikanaji wa Gari za Wagonjwa

Mheshimiwa Spika, Kamati inapongeza juhudi zinazofanywa na Waziri wa Afya za kuhakikisha vituo vya afya vinajengwa kwa wingi lakini pia kunakuwepo na magari ya kubeba wagonjwa (Ambulance). Kamati inafahamu umuhimu wa ukarabati na ujenzi wa miundombinu ya kutolea huduma ikiwemo chumba cha upasuaji, maabara, wodi ya wazazi na wodi ya watoto utakaowezesha upatikanaji wa huduma kamili za uzazi. Kamati inafahamu jumla ya shilingi Bilioni 40 kutoka Benki ya Dunia zim etolewa kwaajili ya kuboresha vituo vya Afya 100 na Shilingi Bilioni 19.5 kutoka Denmark zimepelekwa katika Halmasahuri mbalimbali nchini ili kukamilisha kazi ya ukarabati na ujenzi ambao upo katika hatua mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, Uboreshaji wa Vituo vya afya tafsiri yake ni kupunguza vifo vya wananchi na hususan vifo vya mama na mtoto vitokanavyo na uzazi lakini pia kupunguza msongamano katika Hospitali za Wilaya, Mkoa na Rufaa kutokana na uwepo wa huduma muhimu katika vituo hivyo. Kamati inashauri Serikali kuhakikisha fedha hizi zitumike vizuri na vituo vya afya vikamilike kwa wakati.

5.13 Magonjwa yasiyoambukiza (Non- Communicable Disease)

Mheshimiwa Spika, Magonjwa yasiyoambukiza ambayo yanajumuisha Saratani, Sukari, Presha na Figo yamekuwa yakiongezeka na kuua watanzania wengi. Kamati inafahamu jitihada zinazofanywa na Serikali katika kutoa chanjo ya saratani ya shingo ya kizazi kwa watoto wa kike chini ya miaka 14. Hata hivyo, bado wananchi wengi hawana ufahamu wa namna ya kujikinga na magonjwa haya hasa Sukari, Presha na Figo. ***Kamati inashauri Serikali ihamasishe***

jamii katika kujikinga na magonjwa haya ikiwa ni pamoja na kufanya vipimo vya mara kwa mara ili kuepuka kugundulika na magonjwa haya yakiwa katika hatua za mwisho ambazo hazitibiki. Mtaalam wa Afya Mike Adams amewahi kusema " Today, more than 95% of all chronic disease is caused by food choice, toxic food ingredients, nutritional deficiencies and lack of physical exercise." .Serikali haina budi kuendelea kuelimisha jamii juu ya umuhimu wa kulinda afya zao.

5.14 Bima ya Taifa itengeneze vifurushi vya Bima (Insurance Product packages)

Mheshimiwa Spika, Serikali iliunda mfumo bora wa ugharamiaji wa afya kwa wananchi (Bima ya Afya ya Taifa) ili uweze kuwa ni sehemu ya kinga na ulinzi endapo mwananchi anapatwa na majanga kama vile ugonjwa. Bima hii inawahudumia takribani **asilimia 27** tu ya watanzania hasa walioko katika ajira rasmi kwa maana ya Serikali na sekta binafsi.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaona kwamba wananchi ambao hawako katika mfumo rasmi wa ajira wakiwemo wafanyabiashara ndogo ndogo hawajaweza kunufaika na mfumo huu kutokana na kukosekana na vifurushi wanavyoweza kuvimudu kulingana na uwezo wao wa kipato cha kila siku. Ikumbukwe kwamba afya bora ndiyo nguzo ya kila mwananchi ili aweze kutekeleza majukumu yake na endapo afya itatatetereka kila kitu kinasimama zikiwemo shughuli za uzalishaji ili kuweza kujipatia kipato cha kila siku.

Mheshimiwa Spika, kutokana na changamoto hiyo, Kamati inashauri kuwa Wizara ya Afya (Bima ya afya ya Taifa) kuangalia namna bora ya kutengeneza vifurushi mbalimbali ambavyo vitawalenga wananchi wa kawaida kwa kuzingatia hali ya vipato vyao kwa kuwa bima ya afya ya jamii imeonekana kusua sua na kutozaa matunda basi iweke kifurushi ambacho kitamuwezesha mwananchi mmoja mmoja hasa wale wa sekta isiyo rasmi nao waweze kunufaika na huduma za Bima ya afya ya Taifa.

5.15 Hospitali za Mikoa kuhamishiwa Wizara ya Afya

Mheshimiwa Spika, Hivi karibuni Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alielekeza Hospitali zote za Mikoa kupelekwa chini ya usimamizi wa Wizara ya Afya, jambo ambalo Kamati imekuwa ikishauri Wizara kwa muda mrefu sana. Kamati imefarijika sana kuona Serikali imesikiliza na kuufanyia kazi ushauri wa Kamati kwa vitendo. Pamoja na umuhimu wa kufanya hivyo, Kamati inaona bado kuna haja ya Serikali kuhakikisha Hospitali hizi zote zinakuwa na Wataalam (Specialists) wa magonjwa mbalimbali kama Moyo na figo. Uwepo wa Wataalam hawa kutasaidia kupunguza msongamano katika Hospitali za Rufaa.

Mheshimiwa Spika, pamoja na Serikali kutekeleza ushauri huo wa Kamati bado inaendelea kushauri tena Serikali kulitazama suala la hospitali za Wilaya nazo kuwekwa chini ya usimamizi wa Wizara ya Afya ili kuweza kuendelea kuleta tija ya utoaji wa huduma ya afya kwa wananchi wa Tanzania. ***Ni maoni ya Kamati kuwa, kuwa kufanya hivyo Wizara itakuwa na mamlaka ya kusimamia huduma za afya kuanzia ngazi ya Wilaya mpaka Rufaa kwa kuweza kupata taarifa kamili za changamoto ambazo hospitali hizo zinasimamia na kuweza kuhakikisha hospitali chini ya Wizara zinakuwa na vifaa muhimu vya tiba, dawa pamoja na vifaa tiba. Kamati inashauri TAMISEMI ibaki kusimamia Zahanati na Vituo vya afya nchini.***

5.16 Upatikanaji wa Fedha za Serikali kwa ajili ya Ununuzi wa Dawa za Kufubaza Makali ya UKIMWI

Mheshimiwa Spika, Ugonjwa wa UKIMWI hapa nchini umekuwa ukipigwa vita kwa namna mbalimbali ikiwemo kuwakinga watu wasipate maambukizi mapya ya UKIMWI, kuwapa tiba stahiki watu walioambukizwa na kuhakikisha wanapata dawa kwa ajili ya kufubaza makali ya UKIMWI. Kwa mujibu wa takwimu watu wapatao 1,400,000 wanahisiwa kuwa na virusi vya UKIMWI na wengi wao wapo katika matibabu kwa maana ya kutumia dawa za kufubaza Virusi vya UKIMWI.

Mheshimiwa Spika, Ni dhahiri Serikali imekuwa ikitenga fedha kwaajili ya manunuzi ya dawa za kufubaza makali ya VVU lakini fedha hizo hazitolewi na Serikali kama ilivyopangwa. Kwa mujibu wa tafiti za SIKIKA katika Mwaka wa Fedha wa 2016/2017 **shilingi Bilioni 10** zilitengwa ambalo ni jambo jema sana kwani Serikali haikuwahi kutenga kiasi kikubwa namna hii. Aidha, katika Mwaka wa Fedha 2017/2018 ilitengwa tena shilingi Bilioni 10 lakini mpaka sasa hakuna fedha yoyote iliyopelekwa kwa ajili ya ununuzi wa ARVs.

Mheshimiwa Spika, Licha ya kwamba watu wanaoishi na VVU wanaendelea kupata dawa lakini ifahamike kwamba dawa hizo zinatokana na ufadhili wa nje. Kamati inapata hofu kama siku wafadhili hawa wakiacha misaada ghafla je, watu 1,400,000 wanaotumia ARVs watabaki katika hali gani?

Mheshimiwa Spika, Kamati ina maoni kwamba Serikali ihakikishe inaweka mikakati madhubuti wa uimarishaji wa utoaji wa fedha za kununua dawa za kufubaza makali ya VVU kutoka vyanzo vya ndani ikiwa ni pamoja na kuimarisha Mfuko wa UKIMWI wa Taifa (Aids Trust Fund) ili baada ya muda Tanzania kama nchi iwe inaweza kuhudumia watu wake wanaoishi na VVU.

5.17 Ushirikiano wa Wizara ya Afya na TAMISEMI

Mheshimiwa Spika, pamoja na Mfumo wa ugatuuji wa madaraka unaotumika katika kutoa huduma ya afya kwa wananchi, kuna umuhimu mkubwa wa Wizara mama na TAMISEMI kufanya ushirikiano zaidi ili kufikia lengo Kuu moja ambalo ni kuhakikisha wananchi wanapata huduma bora ya afya na kwa wakati na mahali walipo. Mwananchi hahitaji kujua kama aliyemhudumia ni TAMISEMI au ni Wizara anachohitaji mwananchi ni kupata huduma kwa wakati muafanka. Pamoja na kwamba Wizara inasimamia Sera, basi kuwepo na mfumo wa kuhuisha mikakati yao ya utoaji wa huduma bora kwa wananchi badala ya kila Wizara kujitetea kwamba hili ni la TAMISEMI au hili ni la Wizara.

Mheshimiwa Spika, imekuwa ni kawaida sasa kwa mwananchi akikosa huduma bora ya afya anayeanza kulalamikiwa ni Wizara mama na siyo TAMISEMI, hii ni kutokana na kwamba mwananchi anafahamu kwamba Wizara ya Afya ndiye mwenye jukumu la msingi la kuhahakikisha mwananchi anapata huduma mahalia alipo.

Ni maoni ya kamati kuwa, ni muhimu Wizara ya Afya pamoja na TAMISEMI sehemu ya afya kufanya mikakati ya maksudi ya kuhahakikisha wanachokifanya wizara zote zinafahamu badala ya kukwepana kwa maelezo kuwa mmoja anasimamia Sera na mwingine anasimamia utendaji kwa maana ya miundombinu, vifaa na vifaa tiba pamoja na watumishi.

5.18 Serikali ilinde Haki ya mtoto

Mheshimiwa Spika, Mtoto yoyote duniani ana haki sawa kama mwanadamu ya kuishi, kulindwa dhidi ya unyanyasaji, udhalilishaji wa aina yoyote ile. Haki hizi zipo kwa mujibu wa sheria na makubaliano mbalimbali ya kitaifa na hata kimataifa. Kamati imebaini kwamba kumezuka mtindo wa watoto kudhalilishwa kwa namna moja ama nyingine kuanzia ngazi ya familia kwa maana ya mzazi, mlezi na hata kijamii. Udhalilishaji huu unafanyika kwa njia mbalimbali ikiwemo kubakwa, kulawitiwa na hata kupigwa picha za mnato au video na kuzisambaza mitandaoni.

Mheshimiwa Spika, ikumbukwe kwamba taarifa za mitandaoni zinaishi na watoto wa leo ni taifa la kesho na athari zake zitakuja kuonekana hapo baadae na kumsababishia mtoto huyu kushindwa kushiriki katika masuala mbalimbali yakiwemo ya kisiasa, kiuchumi na hata kijamii.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaishauri Serikali kuwa, ihakikishe inalinda haki za watoto wetu dhidi ya unyanyasaji na udhalilishaji wa aina yoyote ile kwa kuwachukulia hatua za kisheria wale wote wanaohusika na vitendo hivi ili kuweza kukomesha matendo hayo ya kinyanyasaji nay a kidhalilishaji.

5.19 Upungufu wa Maafisa Maendeleo ya Jamii

Mheshimiwa Spika, Maendeleo ya nchi yoyote huletwa kwa ushirikiano wa Serikali na wananchi ambao wanaelewa tatizo na namna gani ya kulitatua. Wananchi hao wanahitaji ushauri kutoka kwa taalamu ambao wanaweza kuwapa mwanga wa namna ya kuyafikia maendeleo wanayoyatamani ambao ni maafisa maendeleo ya jamii.

Mheshimiwa Spika, maafisa maendeleo ya jamii waliandaliwa ili waweze kuwa chachu ya maendeleo katika maeneo mbalimbali hapa nchini na maeneo ambayo yamepata maafisa hayo kumekuwa na matokeo makubwa katika kusukuma maendeleo katika jamii wanazofanyioa kazi. Aidha, pamoja na umuhimu wao kumewa na upungufu mkubwa wa maafisa maeneleo ya jamii na hivyo kuleta athari ya maendeleo katika maeneo husika kwenda kwa kasi isiyoridhisha.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa takwimu za Wizara - Idara Kuu Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto zinaonesha kwamba kuna upungufu wa takribani **asilimia 57.5** kwa kuwa maafisa maendeleo waliopo ni takriban 1700 na wanaohitajika ni takriban 4000 ambayo ni makadirio ya juu. Upungufu huu unasababisha mipango mikakati ya maendeleo katika jamii kutotekelezwa kwa wakati kwa manufaa ya wananchi.

Mheshimiwa Spika, ni maoni ya Kamati kuwa, ni muhimu Serikali kulipa kipaumbele suala hili ili waweze kuwasaidia kuamsha ari ya maendeleo kwa wananchi katika maeneo mbalimbali ya nchi ili kuweza kufanikisha nchi kufikia katika uchumi wa kati.

6.0 HITIMISHO

Mheshimiwa Spika, Napenda kuchukua nafasi hii, kukushukuru wewe binafsi kwa kunipa muda wa kuwasilisha taarifa hii mbele ya Bunge lako Tukufu. Pia napenda kumshukuru sana Waziri wa Afya na Maendeleo ya Jamii, Jinsia

Wazee na Watoto Mheshimiwa Ummu A. Mwalimu (Mb) pamoja na Naibu Waziri Mheshimiwa Faustine Ndugulile (Mb) kwa ushirikiano wao mkubwa wanaoendelea kuutoa kwa Kamati wakati wote wa shughuli za Kamati. Aidha, napenda kuwashukuru Makatibu Wakuu wa Wizara Idara kuu Afya na Idara Kuu ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto pamoja na Maafisa Waandamizi wa Wizara na Taasisi zake zote kwa ushirikiano waliutoa kwa Kamati hii.

Mheshimiwa Spika, naomba kuchukua nafasi hii kuwashukuru Wadau wote wa Sekta ya Afya na maendeleo ya jamii, Jinsia, Wazee na Watoto kwa kazi nzuri wanayoendelea kuifanya kwa wananchi wetu na kwa ushirikiano wao mkubwa wanautoa kwa Serikali katika kuendeleza kutoa huduma bora ya Afya kwa wananchi wetu. Wadau hao ni wale wa nje na ndani ya nchi kamavile PEPFAR, UNDP, Wadau hao ni pamoja na SIKIKA, Engender Health kupitia Mradi wa THAMINI UHAI, Policy Forum na TWaweza.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaishauri Serikali kushirikaiana zaidi na wadau hawa Aafya kwani juhudi zao zote ni kwa ajili ya manufaa ya kiafya ya wananchi wa kitanzania na wakati mwingine hulazimika kufika pale ambapo Serikali kwa namna moja au nyingine imeshindwa kufika kutoa huduma kwa wananchi wake.

Mheshimiwa Spika, Kwa nafasi ya pekee kabisa naomba nimshukuru Makamu Mwenyekiti wangu na niwashukuru Wajumbe wa Kamati ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii, kwa kazi nzuri ambayo wamekuwa wakiifanya ya kujadili na kuchambua Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hii kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019 pamoja na changamoto ya muda lakini walikuwa tayari kutekeleza majukumu yao. Kwa heshima kubwa, naomba kuwatambua kwa majina Waheshimiwa wafuatao:

1. Mhe. Peter Joseph Serukamba, Mb, Mwenyekiti
2. Mhe. Juma S. Nkamia, Mb M/ Mwenyekiti
3. Mhe. Salma Rashid Kikwete, Mb Mjumbe
4. Mhe. Mhe. Hussein M. Bashe, Mb Mjumbe
5. Mhe. Rose Cyprian Tweve, Mb Mjumbe

6. Mhe. Grace Victor Tendega, Mb	Mjumbe
7. Mhe. Peter Ambrose P. Lijualikali, Mb	Mjumbe
8. Mhe. Bernadetha K. Mushashu, Mb	Mjumbe
9. Mhe. Vicky Paschal Kamata, Mb	Mjumbe
10. Mhe. Deogratius Francis Ngalawa, Mb	Mjumbe
11. Mhe. Amina Nassoro Makilagi, Mb	Mjumbe
12. Mhe. Kabwe Zuberi Ruyagwa Zitto, Mb	Mjumbe
13. Mhe. Susan Anselm Lyimo, Mb	Mjumbe
14. Mhe. John Peter Kadutu, Mb	Mjumbe
15. Mhe. Machano Othman Said, Mb	Mjumbe
16. Mhe. Kasuku Samson Bilago, Mb	Mjumbe
17. Mhe. Mgeni Jadi Kadika, Mb	Mjumbe
18. Mhe. Joseph Osmund Mbilinyi, Mb	Mjumbe
19. Mhe. Khamis Yahya Machano, Mb	Mjumbe
20. Mhe. Mch. Dkt. G. P. Rwakatara, Mb	Mjumbe
21. Mhe. Seleman Said Bungara, Mb	Mjumbe
22. Mhe. Khalifa M. Issa, Mb	Mjumbe
23. Mhe. Jaku Hashim Ayoub, Mb	Mjumbe
24. Mhe. Joseph Leonard Haule, Mb	Mjumbe
25. Mhe. Oscar Rwegasira Mukasa, Mb	Mjumbe

Mheshimiwa Spika, Napenda kuwashukuru kwa dhati Watumishi wa Ofisi ya Bunge, wakiongozwa na Ndg. Stephene Kagaigai, Katibu wa Bunge, Ndugu Athman Hussein Mkurugenzi Idara ya Kamati za Bunge na Ndugu Dickson Bisile Mkurugenzi Msaidizi kwa kuisaidia na kuiwezesha Kamati hii kutekeleza majukumu yake kwa weledi mkubwa. Kipekee nawashukuru sana Bi. Pamela Pallangyo na Bi. Agnes Nkwera Makatibu wa Kamati na Bi. Modesta Kipiko msaidizi wetu kwa kufanya kazi kwa weledi mkubwa wa kuishauri Kamati ili kutekeleza vyema majukumu yetu na kuhakikisha kuwa Taarifa hii inakamilika kwa wakati uliopangwa.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema haya, sasa naliomba Bunge lako Tukufu likubali kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Afya na Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto pamoja na Taasisi zake kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019, kama yalivyowasilishwa na mtoa hoja **Fungu 52** jumla ya shilingi **866,236,475,000.00** na **Fungu 53** jumla ya shilingi **32,140,649,000.00**

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha na ninaunga mkono hoja.

Mh. Peter Joseph Serukamba (Mb),
MWENYEKITI
KAMATI YA HUDUMA NA MAENDELEO YA JAMII
19 Aprili 2018

MWENYEKITI: Ahsante kwa kusoma vizuri.

Waheshimiwa Wabunge, mmesikia ripoti ya Kamati, Serikali ya Awamu ya Tano inapeleka dawa asilimia 85 kwenye vituo. Ni jambo zuri sana, hongereni. *(Makofi)*

Pia mmeisikia Kamati inasema, hizo dawa nyingine hazifiki kwenye vituo. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri utupatie majibu, zinapotelea wapi? Ni hatua zipi mtachukua kuhakikisha Umma wanapata matibabu ambayo Serikali hii inawapatia?

Tunaanza michango Waheshimiwa; tunaanza na Mheshimiwa Lucy Owenya ajiandae Mheshimiwa Catherine Ruge atafuatiwa na Mheshimiwa Neema Mgaya. Dakika tano Mheshimiwa Lucy Owenya, Mheshimiwa Catherine dakika tano na Mheshimiwa Neema dakika 10.

MHE. LUCY F. OWENYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kupata nafasi ya kwanza kwa kuwa mchangiaji wa kwanza katika Wizara hii ya Afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda Serikali itueleze ni kwa kiasi gani wanajiandaa kuweza kutenga ile asilimia 15 ya bajeti ili waweze kutekeleza lile Azimio la Abuja? Wasipofanya hivi wanashindwa kutekeleza mambo yao ya maendeleo, wanashindwa kujenga vituo vya afya na kupata vifaa kwa ajili ya hizi hospitali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumzie KCMC. Napenda niwapongeze sana KCMC, Mheshimiwa Waziri ameeleza kwamba wametibu wagonjwa 1,100 wenye matatizo ya saratani na wanaweza wakafanya vizuri zaidi. Wamejaribu kutafuta wafadhili, wamewafadhili wamepata vifaa vyote vya mionzi na kila kitu wamepata kwa ajili ya ile *unity* ya saratani. Kinachopungua pale ni lile jengo *banker* kwa ajili ya mionzi. Wanahitaji karibu shilingi bilioni tano, lakini mnaweza mkawasaidia kwa kuwapa kwa awamu. Siyo lazima muwape yote kwa pamoja. Mkiweza kuwapa hizo fedha kwa ajili ya kujenga ile *banker* itawasaidia sana kupunguza msongamano katika Hospitali ya *Ocean Road*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hotuba yake nimeona Mheshimiwa Waziri anatoa sana fedha nyingi kwa ajili ya *Ocean Road*, lakini pia KCMC ikisaidiwa, mtasaidia sana hii Kanda ya Kaskazini kupunguza msongamano katika Hospitali ya *Ocean Road*. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niizungumzie hospitali yetu ya Mkoa wa Kilimanjaro ambayo ni Hospitali ya Mawenzi. Hospitali ile Mheshimiwa Waziri naomba itupiiwe jicho. Ni Hospitali ya Rufaa lakini haina *Emergency Unit*. Tunaomba mhakikishe kuna *Emergency Unit* na iwe *fully equipped*, kuwe na timu ambayo inaweza ikahudumia wakati wa *emergency*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile Hospitali ya Mawenzi haina *isolation room*. Unakuta mgonjwa ana *TB* analazwa na mgonjwa mwenye malaria. Sasa mgonjwa mwenye malaria anaenda hospitali kutibiwa malaria akirudi nyumbani anaweza akapata *TB*. Kwa hiyo, tunaomba sana mtuhakikishe kwamba kunakuwa na *isolation room* pale Mawenzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kile Kitengo cha Wagonjwa wenye Matatizo ya Akili kwa kweli kiko kwenye hali mbaya sana. Wale wauguzi wanafanya kazi pale lakini unakuta saa nyingine hawa watu wenye magonjwa ya akili wanaweza wakawapiga. Sasa kutoka kule kwenye wodi ya wagonjwa

wenye akili mpaka waweze kupata msaada, hamna hata kengele ya kuweza kupiga ili waweze kusaidiwa. Kwa hiyo, unakuta wale wauguzi wana shida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapo hapo kuna ile *rehab* ambayo ina-*serve* kanda nzima ya Kaskazini, lakini ile *rehab* imesahaulika kabisa, haina uzio, hawapewi hata sabuni, hawapewi vyakula, unakuta watu wanajitolea kusaidia. Sasa nataka kujua hii Serikali mnasema mnawasaidia wanyonge, hapa mnawasaidia wanyonge kweli? Kwa sababu wale wanaoenda kule unakuta wengine hawana hata familia, wamekaa tu pale wameachwa hamna dawa. Ukiangalia madaktari, hawapo wa kutosha. Sasa sijui mna mpango gani wa kuhakikisha kwamba tunapata madaktari wa kutosha katika kada hii ya wagonjwa wenye matatizo ya akili? Kwa sababu nasikia ni madaktari 26 tu nchi nzima tulionao. Sasa kwa mtindo huu, sijui ni kwa jinsi gani mtaweza kuwasaidia hao wanyonge ambao mnasema mnawasaidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kuna upungufu mkubwa wa Madaktari wa Nusu Kaputi. Sijasikia kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri ni kwa kiasi gani mnaenda ku-*train* hawa madaktari wa nusu kaputi. Napenda Mheshimiwa Waziri wakati anakuja ku-*wind up* atuelezee ni nini anachoenda kufanya ili tuweze kupata madaktari wa kutosha wa nusu kaputi.

Sasa hivi tumeona kuna mafuriko yametokea katika Mji wetu wa Dar es Salaam na Morogoro. Tunajua mafuriko yakitokea kutakuwa na magonjwa ya mlipuko. Dar es Salaam mafuriko yakitokea watu ndio wanafungua yale ma-*septic tank*, kwa hiyo, unakuta maji yanachanganyika na vinyesi na tunajua kipindupindu kwa lugha ya sisi ambao sio Madaktari ni kwamba mtu amekula kinyesi. Sasa sijui Serikali mna mpango gani au mmejitarishaje kuhakikisha kwamba magonjwa ya milipuko yakitokea mnaenda kui-*handle* namna gani? Kwa sababu...

(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Ruge halafu Mheshimiwa Neema na Mheshimiwa George Lubeleje wajiandae.

MHE. CATHERINE N. RUGE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa fursa ili nami niweze kuchangia Wizara hii nyeti ya Afya. Mwaka 2001 *African countries* kwa maana ya AU na Tanzania ikiwa mmojawapo walisaini *convention ya Abuja declaration* na wakuu wote wa nchi walikubaliana kutenga angalau asilimia 15 ya bajeti yote ya nchi kwa ajili ya afya, lakini tukiangalia miaka 17 sasa hivi hilo halijawahi kutokea. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia bajeti ya mwaka 2017 ukurasa wa nane inaonesha Bunge tuliidhinisha *1.1 trillion* lakini pesa zilizopelekwa ni asilimia 57 tu. Pia hii bajeti ya *1.1 trillion* ilikuwa ni asilimia 3.5 ya bajeti nzima ya Taifa. Pesa za Maendeleo kwa Wizara ya Afya, pesa zilizotengwa kwa ajili ya maendeleo, pesa za ndani zilikuwa asilimia 24 tu zilizokwenda ambayo ni *almost eight billion* na pesa za nje zilienda shilingi bilioni 321 ambayo ni sawa sawa na asilimia 71. Sasa kama tunaweza kutenga pesa kidogo hivyo, kutokana na mapato ya ndani, tunategemea zaidi pesa za nje, hivi kweli tuna nia ya dhati ya ku-*improve* sekta ya afya? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukija kwenye bajeti ya Afya ya mwaka huu, imepungua kutoka *1.1 trillion* mpaka *0.9 almost* shilingi bilioni 898 ambayo ni pungufu ya asilimia 22. Hivi kweli *are we serious?* Tunawezaje kupunguza zaidi ya asilimia 20 kwenye sekta muhimu kama ya afya? Hii ni sekta inayo-*deal* na afya za watu, tunapunguza pesa kiasi hicho! Napenda Mheshimiwa Waziri wakati anakuja ku-*wind up* atueleze ametumia *criteria* gani kupunguza zaidi ya asilimia 20 ya bajeti ya Wizara hii? Ni kwa sababu labda changamoto zimepungua au magonjwa yamepungua? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia ukurasa wa 128 pia pesa zilizotengwa kwa ajili ya Fungu 52 - Wizara ya Afya,

bado pia ni kidogo sana na asilimia 67 imetengwa kutoka pesa za nje. Tuna *guarantee* gani kwamba tutazipata hizi pesa kutoka nje, kama sisi wenyewe *we are not committed* kutoa pesa za ndani kwa ajili ya afya za watu? (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichangie kuhusu vifo vya akina mama wakati wa kujifungua (*maternal mortality rate*). Taarifa ya *Tanzania Demographic Health Survey* ya mwaka 2015/2016 inaonesha vifo vya akina mama wakati wa kujifungua vimeongezeka kutoka akina mama 432 mpaka 556 kwa kila uzazi kwa watu laki moja. Moja ya sababu ni zaidi ya nusu ya akina mama wanajifungulia nyumbani. Pia hiyo taarifa inaonesha ni asilimia 46 tu ya akina mama wakati wa kujifungua wanahudumiwa aidha na daktari au muuguzi au *clinical officer*. Sasa tuna zaidi ya miaka 50 ya uhuru, *I think* Serikali ya CCM mmekuwa *very comfortable* ndiyo maana mnacheza na afya za watu. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kweli zaidi ya asilimia 50 ya akina mama wanaojifungua kwenye Taifa hili hawapati huduma wakati wa kujifungua na tunasema tuna nia ya dhati ya kupunguza vifo vya akina mama wakati wa kujifungua, *I think we need to be serious*. Mheshimiwa Ummu wewe ni mwanamke, wewe ni mama unajua ni jinsi gani mtu anapata shida kubeba mimba miezi tisa halafu anakuja anapoteza maisha au anapoteza maisha ya mtoto wake. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakuomba Mheshimiwa uliangalie hili suala kwa makini kama wewe mwenyewe ulivyoonesha kwenye hotuba yako ukurasa wa saba kwamba mnataka kutekeleza Dira ya Taifa ya Maendeleo ya mwaka 2025, Mpango wa Maendeleo wa Kati 2020/2021, lani ya Chama cha Mapinduzi 2015/2016 na *Sustainable Development Goals (SDG)* 2030 ambayo tunataka iwe chini ya akina mama 200 wanafariki wakati wa kujifungua; lakini tunaona *trend* inaongezeka. Sasa kama *trend* inaongezeka ndani ya mwaka mmoja, akina mama zaidi ya 100 wamefariki, tunafikiaje hiyo *less than 200* mwaka 2020. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa, niwaombe Wabunge wote akina mama zile shilingi trilioni 1.5 zilizopotea, tumwombe na tumuunge mkono Mheshimiwa Rais zipatikane ili tuweze kuboresha na kujenga vituo vya afya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, naomba kuiongelea Hospitali ya Jimbo langu ya Wilaya ya Serengeti. Hatuna hospitali ya Wilaya tangu uhuru.

(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Neema, Mheshimiwa Lubeleje na Mheshimiwa Mwenyekiti Najma Giga kwa dakika tano, wengine dakika 10.

MHE. NEEMA W. MGAYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi na mimi kuweza kuchangia hotuba hii ya Wizara ya Afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Rais Dkt. John Pombe Magufuli kwa kazi nzuri anayoifanya ya kuimarisha huduma ya matibabu ya kibingwa nchini Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeona hivi sasa kumekuwa na uimarishwaji wa huduma ya matibabu ya kibingwa Tanzania ikiwemo kupandikiza figo na kupandikiza vifaa vya kuongeza usikivu. Katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri tumeona wagonjwa wa figo walikuwa wanatibiwa nje ya nchi kwa gharama ya zaidi ya shilingi milioni 100, lakini hivi sasa tunaishukuru Serikali yetu hii ya Chama cha Mapinduzi sikivu kuleta huduma ndani ya nchi yetu kwa gharama nafuu ya shilingi milioni 20. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika shilingi milioni 100 sasa tunakwenda kutibu wagonjwa watano, hili nalo dogo? Tumeona ongezeko la wagonjwa wa sukari, *pressure* na magonjwa yote haya yanapelekea matatizo ya figo.

Naipongeza Serikali imeweza kuleta huduma hii wakati muafaka ambao Tanzania tunahitaji huduma hiyo kwa kiasi kikubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile nikwambie dada yangu Mheshimiwa Ummy, kwa kazi hii nzuri mnayoifanya, historia itakukumbuka. Profesa Mseru - Mkurugenzi Mkuu wa Hospitali ya Taifa Muhimbili, endelea kufanya kazi baba yangu, kazi yako nzuri, historia itakukumbuka. Vilevile natambua kabisa jitihada hizi ni msukumo mkubwa na jitihada kubwa anazozifanya Rais wetu Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumzie suala la Saratani ya shingo ya uzazi. Kwanza niipongeze Serikali yangu kwa kuwa sikivu. Serikali hii ya Chama cha Mapinduzi ni sikivu. Ukifuatilia hotuba yangu ya bajeti iliyopita ya mwaka 2017/2018 niliishauri Serikali ijikite katika suala zima la kinga katika magonjwa ya saratani ya shingo ya kizazi. Naipongeza Serikali na ninaishukuru, hivi sasa imeanza kutoa chanjo ya saratani ya shingo ya kizazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, chanjo hii sasa hivi inatolewa kwa wasichana wenye umri wa miaka 14, lakini naendelea kuiomba Serikali yangu sasa, nawapa ushauri mwingine, mhakikishe kwamba chanjo hii ya saratani ya shingo ya kizazi, mtoe elimu kule vijijini ili wananchi waelewe umuhimu wa chanjo hii. Kwa sababu jambo lolote jipya linapoingia nchini kwetu, watu hujawa na hofu. Kwa hiyo, kwa kupeleka elimu kule vijijini wakajua umuhimu huu, sasa watajitokeza wasichana wengi na wazazi watapeleka wasichana wao kwenda kupata huduma hiyo ya chanjo ya saratani ya shingo ya uzazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile kwa wale wanawake ambao wameshazidi umri wa miaka 14, naishauri Serikali iongeze jitihada za kuwapima ili tuweze kujua wangapi wamepata matatizo hayo na wangapi hawajapata. Kwa wale ambao wameshapata, basi waanze kupata matibabu kwa haraka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende kwenye suala la Hospitali za Rufaa za Mkoa. Naishukuru Serikali ya Awamu ya Tano imeweza kutupatia fedha, hivi sasa tupo kwenye ujenzi wa Hospitali yetu ya Mkoa ya Njombe.

Mheshimiwa Umy nataka ukija kutoa majumuisho yako hapa wakati unajibu hoja, nataka kujua Hospitali ya Mkoa wa Njombe, Serikali mmetupangia pesa shilingi ngapi ili kuweza kuikamilisha kwa sababu mkoa wetu ni mpya. Kila siku nasema mkoa wetu mpya bado mambo mengi tunahitaji. Kwa hiyo, naomba mtupe kipaumbele sisi watu Njombe, mtupe pesa za kutosha ili tuweze kukamilisha ujenzi wa hospitali yetu ya Rufaa ya Mkoa wa Njombe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa napenda kuzungumzia suala la hali ya mapambano dhidi ya UKIMWI. Nimesoma taarifa ya hali ya maambukizi ya UKIMWI nchini (*Tanzania HIV Impact Survey 2016/2017*); napenda kuishukuru Serikali na wadau mbalimbali, hivi sasa Mkoa wetu wa Njombe maambukizi ya UKIMWI yanazidi kupungua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa ya mwaka 2011/2012 inaonesha kwamba maambukizi ya UKIMWI yalikuwa asilimia 14.8 Mkoa wa Njombe, lakini taarifa ya mwaka 2016/2017 maambukizi ya UKIMWI yameshuka mpaka asilimia 11.4. Ninatambua hizi ni juhudi za Serikali pamoja na wadau mbalimbali wanaopambana na vita dhidi ya UKIMWI. Vilevile ushauri wangu kwa Serikali na wadau, ni muda muafaka sasa, mshuke kule chini kwa wananchi mkawasikilize maoni na ushauri wao ili kwa pamoja muweze kujua jinsi gani mtaweza kumaliza tatizo hili la UKIMWI.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeze Wizara ya Afya kwa kazi nzuri iliyofanya katika kuhakikisha kwamba sasa hivi dawa za Kifua Kikuu (*TB*) kwa watoto wetu zinapatikana. Zamani watoto wadogo walikuwa hawana dozi kamili ya dawa za kifua kikuu. Utakuta kile kidonge kinakatwa robo tatu, robo mbili, mara mtu anakosea kukata, mtoto anaongezewa dozi, mara mwingine anapewa dozi hajjakamilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishukuru Serikali kwamba sasa wameleta dawa za kifua kikuu kwa ajili ya watoto, dozi ambayo iko rafiki kwa watoto. Kama alivyosema Mheshimiwa Waziri, dawa ile ina *flavorya* matunda, kwa hiyo, hata mtoto anakuwa anakunywa kwa urahisi na anaweza kupata matibabu vizuri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa napenda niungane na Mheshimiwa Rais wetu Dkt. John Pombe Magufuli kumpongeza Profesa Mohamed Janabi wa Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete kwa kazi nzuri anayoifanya kuhakikisha utoaji wa matibabu ya moyo nchini kwetu Tanzania. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuunga mkono hoja. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Lubeleje na Mheshimiwa Najma jiandae.

MHE. GEORGE M. LUBELEJE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ili na mimi nichangie hii Wizara ya Afya.

Kwanza nampongeza sana Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Naibu Katibu na watendaji wote wa Wizara ya Afya. Naipongeza Hospitali ya Wilaya ya Mpwapwa, madaktari na wauguzi wanafanya kazi nzuri sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Afya ina kurugenzi kubwa mbili; kwanza Kurugenzi ya Tiba na Kurugenzi ya Kinga. Mimi niongelee kwanza Kurugenzi ya Tiba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, zahanati, vituo vya afya na hospitali, ili litwe hospitali ni dawa pamoja na watumishi. Naipongeza sana Serikali kwa kujitahidi kutenga fedha za kutosha kwa ajili ya kununua dawa. Naipongeza *MSD* kwa kununua dawa za kutosha na kununua magari ya kusambaza dawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ombi langu kwa Mheshimiwa Waziri wa Afya, hii fedha ya kununua dawa bado haitoshi. Tuendeleo kuongeza hela ya kununua dawa. Hii ni kwa sababu kama alivyosema Mwenyekiti, hizi dawa kweli zinasambazwa lakini kuna baadhi ya zahanati dawa hazifiki, sasa hii inakuwa ni shida. Kwa hiyo, *MSD* mna Kanda, hakikisheni Mameneja wenu wanatembelea kwenye zahanati na vituo vya afya wanakagua kama kweli dawa hizi zinawafikia wananchi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu upungufu wa watumishi, kama nilivyosema Wizara ya Afya ilikuwa na mpango wa kuongeza Vyuvo vya *Clinical Officers* na *Clinical Assistants*. Sasa kwa nini upungufu wa watumishi unaendelea? Kwa mfano, pale Mpwapwa kuna Chuo cha Afya, lakini vyuo kama vile wanaweza kupanua wakaongeza *Clinical Officers* wakachanganya pale Maafisa Afya, wanasoma na tunaongeza idadi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, zahanati nyingi sana Wahudumu wa Afya ndio wanaofanya kazi (*Medical Auxiliaries*) ndio wanaofanya kazi nzuri sana, lakini bahati mbaya sana unakuta zahanati moja ina mtumishi mmoja tu, *Medical Auxiliary*; hakuna *Clinical Officer* wala *Clinical Assistant*. Huyu ndio achome sindano, a-*prescribe* dawa na agawe dawa.

Naomba sana Wizara ya Afya itengewe fedha za kutosha ili waweze kuajiri watumishi wengi, kila zahanati iwe na *Clinical Officer* na *Clinical Assistant*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine nizungumzie Idara ya Afya Kinga na nizungumzie Maafisa wa Afya kuhamishiwa Ofisi ya Makamu wa Rais. Afisa wa Afya *is a professional* na wamesomea. Mimi mwenyewe ni *Retired Health Officer*. Wamesomea miaka mitatu mambo ya afya. Sasa tatizo linakuja wanahamishiwa Ofisi ya Makamu wa Rais, kwa sababu ya lile neno tu la *environmental* basi; lakini hawa wamesoma mambo ya *Public Health and Preventive Medicine*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nilikuwa nashauri, ukitembelea nchi nyingine kwa mfano Kenya, Uganda, Malawi na Namibia, Idara ya Afya Kinga ni idara kamili na ina *vote* yake kabisa, yaani Maafisa Afya wana idara yao kamili na Wakurugenzi wao, lakini hapa sasa tunaanza kuwagawa Maafisa Afya, wengine waende Ofisi ya Makamu wa Rais. Kwa hiyo, nakushauri Mheshimiwa Waziri, Maafisa Afya wote warudi Wizara ya Afya ili waweze kuimarisha kitengo hiki cha Idara ya Afya Kinga. Hawa ndio wanaoshughulika na usafi, kukagua mambo ya nyama, mahoteli na hizi *food premises*, lakini sasa ukiwapeleka kule, anaitwa Afisa Mazingira, haitwi tena Afisa Afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi vyuo nadhani mngevibadilisha majina. Sisi wakati tunasoma kilikuwa kinaitwa Chuo cha Maafisa wa Afya, lakini sasa mkishasema Chuo cha Afya ya Mazingira, Afisa Afya amesoma mambo mengi sana. *Syllabus* ya sasa wanasoma kama madaktari. Wanasoma mambo ya minyoo na mambo mengi sana; mambo ya *preventing*. Ukimuuliza Afisa Afya, kwanza ndio wanaokagua nyama (*meat inspectors*) wanajua *ante-mortem inspection* wanajua *post-mortem*. Unaweza ukachinja hapa ukatundika *carcass* ukimwambia Bwana Afya akague anakagua na anakwambia kabisa hawa ni *taenia solium*, hawa ni *taenia saginata*, wanakwambia. Ni wataalam wa haya magonjwa. Sasa kuwahamishia Ofisi ya Makamu wa Rais, *it is wrong*. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nilikuwa namwomba sana Mheshimiwa Waziri wa Afya, Maafisa Afya wote warudi na muanzishe kada ya *Health Assistant* au *Assistant Health Officer* kama zamani, kwa sababu hawa Maafisa Afya, wale wenye *Diploma* wengi wapo katika Wilaya lakini *Health Assistant* wanatakiwa wakae kwenye Zahanati. Kila Zahanati iwe na *Health Assistant*. Kazi yao kubwa ni elimu ya afya (*Health Education*), kuelimisha wananchi kuzungukia vijiji kuhusu usafi. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pale Muhimbili zamani tulikuwa na kituo chetu cha *Health Education Unit*, wapo

Maafisa Afya kwa ajili ya elimu ya afya. Hata hospitali zetu zote hizi tulikuwa tunatoa elimu ya afya kwa wagonjwa (*out-patient* na *in-patient*) lakini siku hizi sijui kama linafanyika hili. Kwa sababu kinga ni bora kuliko tiba. Kinga *is less expensive* lakini tiba ni *very expensive*. Mtu akiugua kipindupindu, gharama ya kumtibu ni ngumu, lakini ukimwambia mtu achimbe choo, achemshe maji ya kunywa na atunze usafi, umezuia ule ugonjwa. Kwa hiyo, kidogo inakuwa ni gharama nafuu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa na hayo machache. Nakushukuru sana kwa kunipa nafasi, ninaunga mkono hoja hii ya Mheshimiwa Waziri wa Afya, lakini waongeze bidii ya kutenga fedha kwa ajili ya kununua madawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile Hospitali yangu ya Mpwapwa iongezewe madawa na watumishi wa kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Najma, dakika tano halafu tutaendelea na Mheshimiwa Munde Tambwe Abdallah.

MHE. NAJMA MURTAZA GIGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Naomba niende *direct to the point* na naingia kwenye ukurasa wa 101 wa hotuba ya Mheshimiwa Waziri kuhusu haki na maendeleo ya mtoto. Ninashukuru kwamba Mheshimiwa Waziri amekiri mwenyewe kwamba ukatili dhidi ya watoto bado ni tatizo kubwa hapa nchini na asilimia 28 ambayo imeoneshwa kuongezeka katika wanaoripoti kuanzia mwaka 2016/2017 mimi ninasema bado hiyo itakuwa ni kidogo ikiwa Watanzania wengi watalielewa hili suala. Kwa hiyo, tunaweza tukafika hata kwenye asilimia 70.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa narudi tena kwenye ombi langu, namwomba Mheshimiwa Waziri kigezo cha kusema kwamba hawa wabakaji sugu, nikisema wabakaji sugu wa watoto wa kike na wa kiume sikusudii mtu mwingine

yoyote, sikusudii mbakaji wa mume kwa mke, hilo ni lao. Nakusudia watoto wadogo wa kike na wa kiume. Naomba sana tuache hii ya kufikiria kwamba tunapowaamulia au kuwatungia sheria hawa wabakaji sugu kuhasiwa, ni kosa au ni haki za kibinadamu, naomba niye kwenye Katiba ya Jamhuri ya Muungano Ibara ya 30. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba ninukuu; "Haki na uhuru wa binadamu ambapo misingi yake imeorodheshwa katika Katiba hii havitatumwiwa na mtu mmoja kwa maana ambayo itasababisha kuingiliwa kati au kukatizwa kwa haki na uhuru wa watu wengine au maslahi ya umma."

Pili, inasema: "Ifahamike kwamba masharti yaliyomo katika sehemu hii ya Katiba yanayofafanua misingi ya haki, uhuru na wajibu wa binadamu, hayaharamishi sheria yoyote iliyotungwa wala kuzuia sheria yoyote kutungwa au jambo lolote halali kufanywa kwa mujibu wa sheria hiyo kwa ajili ya:- (a) kuhakikisha kwamba haki na uhuru wa watu wengine au maslahi ya umma haviathiriwi na matumizi mabaya ya uhuru na haki za watu binafsi." *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kutumia ibara hiyo, ninaomba nikushawishi na ninaomba nishawishi Bunge, mwisho wa siku tusipolivalia njuga jambo hili litakuwa ni janga la kitaifa. Ninasema hivi nawaambieni mfano, mwisho wa siku hatima yake, kiongozi ambaye yupo mbele yetu sasa hivi ni mwanaume, atakuja kiongozi ambaye ana ndoa ya jinsia moja, hilo ndiyo mwisho wa siku. Kwa hiyo, naomba tusifanye masihara wala tusione hili jambo ni la utani. Taifa letu la kesho linakwenda kuangamia. Taifa letu lenye utamaduni bora Tanzania linakwenda kutoweka ikiwa tutakuwa hatupo makini katika suala hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninasema, Mheshimiwa Waziri kaa na Wizara husika tuangalie namna bora ya kutengeneza sheria ya kuwahasi wabakaji sugu wa watoto wetu wa kike na wa kiume ili tuweze kuondokana na janga hili sugu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hayo ndiyo yangu ya leo. Ahsante sana. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante. Waheshimiwa somo zito hilo. Hongera sana Mwenyekiti kwa maneno mazuri. Mheshimiwa Munde, ajjandae Mheshimiwa Azza Hilary. *(Makofi)*

MHE. MUNDE A. TAMBWE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa fursa hii nami niweze kuchangia katika Wizara ya Afya. Kwanza nianze kuipongeza Serikali yote kwa ujumla wake, nimpongeze Rais kwa kuweka nguvu za makusudi kabisa kuboresha Wizara ya Afya. Nampongeza Mheshimiwa Waziri Umyy kwa kazi nzuri anayoifanya pamoja na Naibu wake, tunaona matunda yao wanayoyafanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze na mambo yangu ya Mkoa wa Tabora kwanza. Kule Tabora tulikuwa tumejengewa Chuo cha Madaktari. Chuo kile kilikuwa kimekamili kwa asilimia 90 kuanzia mwaka 2014 mpaka magodoro yamo ndani ya chuo hicho, lakini mpaka sasa chuo hicho kimebakiza asilimia 10 tu kumaliziwa toka mwaka 2014 mpaka sasa hakijamaliziwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba sana Mheshimiwa Waziri kwa sababu kitu hiki sasa kinaenda chini ya Wizara yake, jengo lile linaharibika, pesa haionekani thamani yake kwa sababu jengo limeanza kupasuka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulikuwa tumejengewa jengo la kisasa la upasuaji, jengo lile limekamili kila kitu ndani toka mwaka 2014, mkandarasi hajalipwa pesa yake, amelifunga na kufuli jengo lile halitumiki, ukizingatia Hospitali ya Kitete ni Hospitali ya Rufaa, jengo letu la upasuaji ni la kizamani, halina vifaa vya kisasa. Jengo la kisasa tunalo, mkandarasi amelifunga.

Nawaomba Wizara wakae na mkandarasi waongee naye wampe ahadi, lifunguliwe jengo lile lianze kutumika, lina kila kitu ndani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa kuhusu madaktari; Tabora hatuna Madaktari Bingwa. Ikama yetu ya Mkoa wa Tabora, tunatakiwa tuwe na Madaktari Bingwa 21, lakini sasa tuna Madaktari Bingwa watano tu. Namwomba sana Mheshimiwa Waziri atusaidie. Pia tuna madaktari watatu wa kujitolea, wanafanya kazi nzuri sana. Namwomba Mheshimiwa Waziri wakati wa kuajiri asisahau kutupa nafasi hawa madaktari wanaojitolea mpaka leo hii, wanatufanyia kazi kubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wauguzi tunatakiwa tuwe nao 185, tunao 120. Tunaomba sana wakati wa kuajiri wauguzi watukumbuke. Tunasomesha Madaktari Bingwa watano, tunaiomba Wizara, madaktari hawa wakitoka kusoma, msije tena mkawahamisha mkawapeleka sehemu nyingine. Tunaomba mtuachie na sisi waweze kutusaidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba pia kuongeza majengo kwenye Hospitali yetu ya Rufaa ya Mkoa, majengo yake ni machache, *population* ya mkoa imeshakuwa kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nirudi tena kuipongeza Wizara ya Afya kwa kazi kubwa wanayofanya. Nashangaa tu mtu anaposema kwamba sisi tunajifanya kusaidia wanyonge, Serikali inajifanya ya wanyonge, lakini siyo kweli ya wanyonge. Hii Serikali ni ya wanyonge. Niwakumbushe kidogo tu, tulikuwa tuna bajeti ya shilingi bilioni 30 mwaka 2015; leo tuna bajeti ya shilingi bilioni 270 kwa ajili ya madawa. Yote hii ni juhudi za Mheshimiwa Rais kuhakikisha watu wake wanapata tiba za uhakika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii tunatibu watu bure. Wagonjwa wa UKIMWI wanatibiwa bure, wagonjwa wa TB wanatibiwa bure, wazee wanatibiwa bure, akina mama wajawazito wanatibiwa bure, watoto chini ya miaka mitano wanatibiwa bure. Zote hizi ni gharama kubwa zinazobebwa na Serikali ya Awamu ya Tano, watu wanasahau hivi vitu. Kila siku wanakuwa wanapenda kulaumu tu, hawapendi kuona mambo mazuri yanayofanywa na Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii siyo kazi ndogo, tuna wagonjwa wa UKIMWI wangapi? Leo Serikali ikisema wagonjwa wote wa UKIMWI wanunue dawa, ndugu zetu wangapi wataangamia? Naomba sana kuipongeza Serikali na kuitia moyo iendelee kufanya kazi kama inavyoendelea kutufanya kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimjibu Mheshimiwa Ruge alivyokuwa anasema kwamba vifo vya wajawazito takwimu zake...

(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)

MHE. MUNDE T. ABDALLAH: Mheshimiwa Mwenyekiti, nimwambie Mheshimiwa Ruge, hizo takwimu zake ni za mwaka 2015/2016.

MBUNGE FULANI: Siyo Waziri!

MHE. MUNDE T. ABDALLAH: Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali hii imewekeza sana kwenye zahanati na vituo vya afya. Ninaamini taarifa itakayokuja haitakuja na vifo hivyo vya akina mama wajawazito na watoto, naamini taarifa itakuwa imeboreshwa. Tumesikia taarifa ya Mheshimiwa Waziri, tumesikia taarifa ya Mwenyekiti wa Kamati jinsi Serikali ilivyowekeza kwenye Wizara ya Afya.

MHE. LUCY F. OWENYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

MHE. MUNDE T. ABDALLAH: Kwa hiyo, nataka niwaambie kwamba...

MHE. LUCY F. OWENYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

MHE. MUNDE T. ABDALLAH: ...hiki kitu hakitaendelea kuwa hivi, kazi iliyofanyika ni kubwa.

MHE. LUCY F. OWENYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

MWENYEKITI: Taarifa; Mheshimiwa Munde, subiri kidogo.

T A A R I F A

MHE. LUCY F. OWENYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimpe taarifa mzungumzaji kwamba amesema huduma za watoto na akina mama wajawazito ni bure. Akumbuke Mheshimiwa Waziri kuna ujumbe alitutumia akasema *MSD* imetoa *full delivery kit* na ita-*cost* shilingi 25,000 kwa kila *kit*. Kwa hiyo, siyo bure. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Munde, endelea.

MHE. MUNDE T. ABDALLAH: Mheshimiwa Mwenyekiti, hiyo taarifa si kubali kwa sababu mimi kwenye Mkoa wangu wa Tabora akina mama wanatibiwa bure. Mheshimiwa Waziri alisema yeyote anayetaka kujiboresha zaidi ile *kit* ilikuwa ni kubwa, ina vitu vingi, anaweza akachukua kwa shilingi 21,000 lakini siyo kusema kwamba watu hawatibiwi bure. Wajawazito wakienda Kitete Hospitali wanazaa bure.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, sikubaliani na alilolisema Mheshimiwa Owenya. Kama yeye Kilimanjaro wanazaa kwa pesa na watoto wanatibiwa kwa pesa, basi ni kwake. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia Mheshimiwa Ruge aliongelea kuhusu Azimio la Abuja...

(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)

MHE. MUNDE T. ABDALLAH: ...ameongea kuhusu Azimio la Abuja akisema kwamba pesa tulizozitenga ni chache. Nasema hivi ameangalia kwenye Fungu 52, lakini pesa za matibabu ziko pia kwenye fungu la TAMISEMI.

Ukichukua TAMISEMI, ukichukua na Wizara ya Afya ukajumlisha utapata pesa nyingi zilizotengwa kwa ajili ya Wizara ya Afya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiona makelele, ujue jua limewapiga kichwani. Kwa hiyo, hata huwa hainisumbui kwanza.

MHE. ESTHER N. MATIKO: Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, hii taarifa ya mwisho mchana huu.

T A A R I F A

MHE. ESTHER N. MATIKO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Napenda kabisa dada yangu Mheshimiwa Munde, unapotoa takwimu uwe na uhalisia wake au umwachie Waziri husika aje alijibu hilo la takwimu. Ukijumlisha zote, TAMISEMI na kwingine kote ni asilimia tisa. *Abuja Declaration* inasema asilimia 15. Sasa ukiwa unaongea uwe na *facts* katika takwimu.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Munde.

MHE. MUNDE T. ABDALLAH: Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Esther nakusheshimu na unajua nakuheshimu, tafadhali. Nimesema kwamba takwimu alizozitoa Mheshimiwa Ruge asilimia tatu siyo sawa. Ukichukua TAMISEMI, Afya, ukichukua na Fungu 52 huwezi kupata asilimia tatu, utapata zaidi ya asilimia tatu, ndicho nilichokisema, siyo kwamba nilichokisema sikijui. Nakijua na ninakifahamu. Narudia kusema, nakusheshimu sana Mheshimiwa Esther. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niongelee tena jambo moja ambalo limekuwa sana kwenye mjadala. Binafsi kama Munde na ni Mbunge wa wanawake siliungi mkono, naomba niseme wazi. Kumekuwa na mjadala wa kuiomba

Serikali igawe taulo za kike bure, mimi siungi mkono na sababu ninazo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rais anafanya kazi kubwa, Mheshimiwa Rais anajenga barabara, anasomesha watoto bure, madawati bure, kila kitu bure, tunataka tupeleke na *pads* bure! Kwa sasa bado nchi yetu haijafikia, tuache Serikali ijikite kwenye kazi inazozifanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, binafsi nitaunga mkono kama mkisema tupunguze kodi kwenye hizi taulo ili watu wazinunue kwa bei rahisi. Bado hatujafikia kugawa taulo hizi bure, uwezo huo hatuna. Tusitake kujazia Serikali mambo mengi, kesho na kesho kutwa tukaanza kuja kuwahoji mbona hili hamjalitimizwa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana wale wote wenye kuwa na hiyo azma ya kupewa taulo bure, mimi nasema sitaunga mkono, naendelea kupinga na nitaendelea kupinga siku hadi siku.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rais ameshatusomeshea watoto wetu bure, nasi kama wazazi tuwajibike; tuna sababu ya kuwajibika. Hatuwezi kutegemea kila kitu kiwe bure kwa Serikali. Hata Uingereza hawatoi hizo taulo bure. Kwa nini sisi kila kitu tunataka bure? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naendelea kusema, naendelea kuipongeza Serikali...

(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante kwa mchango wako. Mheshimiwa Azza Hillal Hamad.

MHE. AZZA H. HAMAD: Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema aliyenijalia afya njema nikaweza kuchangia Wizara ya Afya kwa siku ya leo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kuipongeza Serikali ya Awamu ya Tano kwa kazi kubwa inayoifanya. Niseme, maendeleo ni hatua kwa hatua. Kama ambavyo kwenye familia zetu huwezi kufanya kila kitu kwa siku moja, leo hii hata ukipata mabilioni ya pesa ukinipa siwezi nikamaliza matatizo niliyonayo na ndivyo ambavyo Serikali ya Awamu ya Tano inavyokwenda kutekeleza miradi ya maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitaje hatua kwa hatua ambayo yamefanyika katika Wizara ya Afya. Hatua ya kwanza, upandikizaji wa kifaa cha usikivu kwa watoto; hatua ya pili, upandikizaji wa figo na hatua ya tatu, chanjo ya saratani. Hizi ni hatua ambazo Serikali ya Awamu ya Tano imezifanya katika Wizara ya Afya kuhakikisha kwamba afya zetu zinakwenda kuimarika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hatua hizo, kipekee kabisa naipongeza Wizara ya Afya, Mheshimiwa Ummu na Naibu wake na watendaji wake wote kwa kushirikiana na TAMISEMI kuhakikisha kwamba tunakwenda kuboresha na kujenga vituo vyetu vya afya katika kata zetu. Yeye kama mama ameweka historia katika Wizara ya Afya, kama mama ameweka historia katika Taifa hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nisiishie kupongeza watu walioko juu tu, nampongeza *RMO* wangu wa Mkoa wa Shinyanga kwa kazi kubwa anayoifanya kwa sababu mpaka sasa hivi chanjo ya saratani ya shingo ya kizazi kwa Mkoa wa Shinyanga semina imekwishaanza. Wananchi wa Shinyanga wanapewa semina na hivi tunavyoongea, leo kuna semina inaendelea kwa ajili ya chanjo ya saratani ya kizazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niingie moja kwa moja sasa katika hoja nilizonazo. Katika hatua ambazo wamepitia Wizara ya Afya, niwaombe *NHIF* ni kwa nini yale malipo ambayo mmeyaweka kwa vikundi hamtaki kuyaweka kwa mtu mmoja mmoja? Watu wengi hawapo kwenye vikundi,

lakini wana utayari wa kuchangia hiyo shilingi 76,000 kwa ajili ya Bima ya Afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawashauri *NHIF* ruhusuni Bima ya Afya shilingi 76,000 ichangiwe kwa mtu mmoja mmoja na isiwe kwa vikundi. Tunakwenda kuwanyima haki wananchi ambao wako tayari kuchangia Bima ya Afya, kwani vikundi na mtu mmoja mmoja vina tofauti gani? Kwa sababu kama kikundi kina watu 20, mwisho wa siku watu watabaki 20 wale wale. Kwa hiyo, nawashauri muibadilishe iende ikachangiwe na mtu mmoja mmoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwashauri *NHIF* siyo kwamba wananchi wetu ni wagumu kulipa Bima ya Afya, tatizo elimu haipo. Shukeni mpaka kule chini, katoeni elimu kwa wananchi wetu, nini maana ya Bima ya Afya? Mtu akishaugua, ukishaenda hospitali, kama una Bima ya Afya ndiyo utatambua nini maana ya Bima ya Afya na kama hauna, utajuta kwa nini hukuwa na Bima ya Afya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo nawashauri *NHIF*, shukeni kule chini kwa wananchi wetu na ninawakaribisha Mkoa wa Shinyanga, njooni mtoe mafunzo kwa wananchi wa Mkoa wa Shinyanga ili waweze kujiunga na Bima ya Afya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naomba nijielekeze katika kitabu cha Mheshimiwa Waziri ukurasa wa 118. Ni mwaka wa nane niko ndani ya ukumbi huu wa Bunge, hakuna mwaka ambao sijawahi kusemea Hospitali ya Mkoa wa Shinyanga. Nimeangalia katika kitabu cha Mheshimiwa Waziri; ujenzi wa Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Shinyanga haimo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa masikitiko makubwa, Mheshimiwa Ummy ni ndugu yangu na rafiki yangu, lakini kwa hili nitakamata shilingi. Ujenzi wa Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Shinyanga una miaka zaidi ya mitano toka umeanza. Jengo lililokamilika pale ni jengo la utawala na wagonjwa wa nje. Unawezaje kusema kwamba pale tumekamilisha

ujenzi? Nawashauri Wizara ya Afya, hakuna sababu ya kwenda kuanzisha majengo mapya wakati yale ambayo yameshaanza hamjanyakamilisha. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili iitwe Hospitali ya Rufaa kuna mambo mengi ambayo yanatakiwa kukamilishwa. Kuna jengo la mama na mtoto linatakiwa lijengwe ambalo hatujaanza hata msingi, jengo hili la mama na mtoto litakuwa na maabara na chumba cha upasuaji ndani yake. Kwa nini msitupe angalau shilingi bilioni tatu tukaenda kujenga jengo hilo la mama na mtoto ndani yake kuna chumba cha upasusaji, kuna maabara, ili huduma zikawa zinafanyika pale? (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jengo ambalo wanasema kwamba liko tayari la utawala, halina hata *furniture* moja. Sasa tunakwendaje kutoa huduma za Hospitali ya Rufaa wakati tuna jengo la utawala peke yake? Hapo utasema kuna huduma inafanyika? Hapana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hili naomba Wizara ya Afya litizameni, mkakamilishe ujenzi wa Hospitali ya Rufaa ya Shinyanga ili nisisimame tena hapa kila siku kusema Shinyanga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkoa wa Shinyanga una upungufu mkubwa wa watumishi. Nianze na Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga. Halmashauri hii watumishi wanaotakiwa ni 571; watumishi waliopo ni 196 tu; upungufu ni 375; Halmashauri ya Mji wa Kahama ina upungufu wa watumishi 214; Hospitali ya Mkoa wa Shinyanga ina upungufu wa watumishi 189.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninawaomba Wizara ya Afya, upungufu huu wa watumishi unasababisha kwenda kutukanwa watumishi wetu wa afya kwamba hawafanyi kazi inavyotakiwa. Hii ni kwa sababu wanafanya kazi kwa kiwango kikubwa. Unakuta mtu mmoja anaandika, anakwenda kutoa dawa, anakwenda kuzalisha mtu huyo huyo mmoja. Matokeo yake, wale ni binadamu, kuna muda

unafika mtu amechoka, anaweza akakujibu vibaya mgonjwa ukachukia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini hili lote lipo ndani ya Wizara ya Afya, liangalieni suala la upungufu wa watumishi katika sekta ya afya, limekuwa ni tatizo kubwa na hivi tunavyokwenda kujenga na kuboresha vituo vyetu vya afya ni lazima tuhakikishe kwamba tuna watumishi wa kutosha, kwa sababu huduma nyingi zaidi zitakuwa zimeongezeka katika vituo vyetu vya afya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho lakini siyo kwa umuhimu, naomba niseme *delivery pack*. Kwa uelewa wangu, huduma ya mama na mtoto siyo kwamba imeondolewa kwenda kutolewa bure kule kwenye zahanati zetu na vituo vyetu vya afya kwa sababu ile dawa wanayochomwa akina mama wakati wa kujifungua bado itatoka kama kawaida na *gloves* zitapatikana kama kawaida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilivyoielewa, sijui kama niko tofauti, Mheshimiwa Waziri atasema; nilivyoielewa *delivery pack*, ni ule mfuko uliobeba vitu vyote ambao unamfanya mama huyu mjamzito aende nao hospitali siku ya kujifungua ukiwa na vifaa vyote tofauti na kubeba kanga na vitenge na vitu vingine.

(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante.

MHE. AZZA H. HAMAD: Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Wilfred Lwakatare dakika tano.

MHE. WILFRED M. LWAKATARE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru.

Kwanza niseme kabisa natambua Jimbo langu la Bukoba Mjini pamoja na pale Kyerwa angalau kupewa fedha za kupanua hospitali yetu *1.5 billion shillings*, inabidi nitambue hilo na ninalipongeza. Najua hatua hii itapunguza idadi kubwa ya wagonjwa ambao wanatibiwa kwenye Hospitali ya Rufaa pale Bukoba Mjini, sasa angalau itapatikana *alternative*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, kwenye ukurasa wa 103 kifungu namba 179 cha hotuba ya Mheshimiwa Waziri, amezungumzia huduma na malezi kwa ajili ya watoto wachanga na zile *care centres*. Sasa niseme, lipo tatizo la vituo hivi na siyo kwa Jimbo langu, nafikiri ni kwa Tanzania nzima, kwa utaratibu uliopo hivi sasa na kwa *Bukoba Town*, ni kwamba wale Maafisa wa Ustawi wa Jamii walitoa barua ambayo ilivifunga vile vituo. Ile barua kwa sababu waliandika kwa shinikizo baada ya kutiwa ndani na vyombo vya dola, waliamua vituo vifungwe siku hiyo hiyo wakati waliposhinikizwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa wakati wakivifunga wanarejea sheria ambayo kimsingi ipo, kwamba ili kufungua hizi *centres* lazima uwe umepata usajili kutoka kwa Kamishna. Tunatambua hiyo sheria, ipo, je, ni kweli inaendana na mazingira halisi ya hivi sasa na watoto tulionao?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimemsikia Waziri katika hotuba yake ametoa takwimu za vituo vilivyopo kwamba mwaka 2017/2018 wamesajili vituo 139; mwaka 2016/2017 vilisajiliwa vituo 270 na hadi sasa viko vituo 1,046 kwa Tanzania nzima. Sasa hii hali haiendani na ukweli kutokana na nini kinachoendelea katika mazingira yetu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nieleze kwa ufupi. Ni kwamba vituo hivi kwa mujibu wa sheria ili visajiliwe inabidi viwe na walezi wasiopungua 20; mlezi mmoja kwa *ratio* ya watoto 20, kuwe na *first aid kit*, kuwe na *fire extinguisher*, kuwe na vyoo vya mashimo matatu, kuwe na jiko la kupikia uji, kuwe na uzio uliozungushwa kwenye kituo kizima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakubali kwamba sheria hii inaweza ika-*apply* Oysterbay au Mikocheni, lakini kwa mwananchi ambaye yuko Katatolowanzi *Bukoba Town*, aliyeko Kaororo, aliyeko Nshambia, mimi nasema hiki kitu hakiwezi ku-*apply* kwa sababu hakiendani na mazingira ya wananchi wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwamba pamoja na sheria hii, iko sheria inayotambua kabisa kwamba kwenye sehemu ya 12, kwenye masharti mengineyo, kifungu cha 155 kinatambua kwamba Mamlaka ya Serikali za Mitaa inaweza kushauriana na Waziri wa masuala ya Ustawi wa Jamii kutoa sheria ndogo ya miongozo kwa kuzingatia mazingira ya eneo lenyewe, lakini maafisa wetu wamekuwa hawajikiti katika masharti haya, wao wanafunga vituo kwa kutegemea kwamba vyote visajiliwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri, nataka kutamka tena kwamba jambo hili kwa *size* ya nchi yetu na kwa jinsi mwamko ulivyopatikana kwa watu kuanzisha vituo vyao kwa maeneo mbalimbali, hata kwenye Kijiji cha Nkasi vituo vinafunguliwa...

(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante Mheshimiwa Lwakatare kwa mchango wako. Mheshimiwa Bhagwanji.

MHE. BHAGWANJI MAGANLAL MEISURIA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana nimepata nafasi hii, Mungu akuweke.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru Mwenyezi Mungu kwa sisi Wabunge sita tullopata ajali Morogoro, lakini sote tuko salama na amani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile nawashukuru watu wa Hospitali ya Morogoro, wananchi wake na madaktari wametuhudumia mara moja. Vilevile nawashukuru Hospitali ya Muhimbili na hospitali tuliyohamishiwa *MOI Hospital*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nawashukuru watu wa *NHIF* (watu wa Bima ya Afya), wameleta ndege mbili, *ambulance* nne, tumepata nafasi nzuri ya kupelekwa hospitali na tumepata huduma nzuri. Tunamshukuru Mwenyezi Mungu na tunamshukuru Rais wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile tunamshukuru Waziri wetu, Mheshimiwa Ummy, pamoja na Naibu wake, wamekuja hospitali kutuona, ametupa pole.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawashukuru Waheshimiwa Wabunge wote wa Bunge letu hili, nawashukuru pamoja na watu wangu wa Jimbo, wamekuja kuniona katika hospitali. Kwa hiyo, nasema kwa wote, ahsante sana. *(Makofi)*

(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, orodha yetu ya jioni tutaanza na Mheshimiwa Oliver, atakuja Mheshimiwa Dkt. Kamala na atafuatia Mheshimiwa Vicky Kamata.

Sasa nasitisha shughuli za Bunge mpaka saa 11.00.

(Saa 7.00 Mchana Bunge lilisitishwa hadi saa 11.00 jioni)

(Saa 11.00 Jioni Bunge lilirudia)

Mwenyekiti (Mhe. Mussa A. Zungu) Alikalia Kiti

MWENYEKITI: Tukae.

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea. Mchana nilitaja jina la kwanza Mheshimiwa, Oliver Semuguruka, ajiandae Mheshimiwa Dkt. Diodorous Kamala na Mheshimiwa Vicky Kamata ajiande.

MHE. OLIVER D. SEMUGURUKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipatia nafasi hii ili niweze kuchangia katika Wizara ya Afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniweza kusimama katika Bunge lako Tukufu, siyo kwa uwezo wangu bali ni kwa uwezo wake. Nampongeza Rais wetu mpendwa wa Jamhuri ya Muungano Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli kwa kazi nzuri anazofanya za kujenga Taifa letu, binafsi namuombea kwa Mwenyezi Mungu azidi kumtia nguvu ili aendelee kulijenga Taifa letu na sisi tuko nyuma yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nampongeza Makamu wa Rais Mama Samia Hassan Suluhu na Waziri Mkuu Kasim Majaliwa na Mawaziri wote, Naibu Mawaziri kwa kazi nzuri wanazozifanya kwa moyo wa dhati wa kujenga Taifa. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa nimpongeze dada yangu mpenzi Mheshimiwa Umyy Mwalimu na Mheshimiwa Dkt. Ndungulile kwa kazi nzuri wanazozifanya katika kitengo cha afya. Sasa naomba nijielekeze moja kwa moja katika mchango wangu katika Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa, naishukuru Serikali kwa mwaka wa fedha 2017/2018 kwa kutenga bilioni 3.5 kwa ajili ya ukarabati wa vituo vya afya vya Mkoa wa

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

Kagera. Pamoja na kazi nzuri zinazofanywa kwa upande wa afya, napenda kusemea wafanyakazi wa Murugwanza Wilaya ya Ngara, wafanyakazi 17 ambao hawajaingizwa kwenye *payroll* licha ya kuombewa kibali Wizarani na hupelekea kupata mishahara yao kwa shida. Naomba sana Wizara ya Afya pamoja na Serikali iweze kuwaona hawa watu ambao wanafanya kazi kwa moyo wao wote lakini hawajaingiziwa majina yao kwenye *payroll* mpaka muda huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wanapata shida sana na ikumbuke kwamba wanazo familia, wana watoto wanaowasomesha na mambo yao binafsi kwa ajili ya kupata fedha ili waweze kujikimu, lakini mpaka muda huu hawajaweza kupata mishahara wanadai zaidi ya muda mrefu sana hata wakipata mishahara wanaweza kupata mishahara wa mwezi mmoja miezi miwili, ambayo haikidhi mahitaji yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kuna wafanyakazi 49 walitolewa kwenye *payroll* na baadaye wakarudishwa wako chini ya Dayosisi ambao wanalipwa na Wizara, walivyorudishwa kwenye *payroll* hadi leo kuna *arrears* zao wanadai, ambapo kuna mtumishi anadai miezi kumi miezi sita, miezi mitano, hiyo pia inaleta shida sana katika kufanya kazi. Watu hawa wako kwenye kitengo ambacho ni mahsus lakini mtu unakuta ameshindwa hajapata mishahara zaidi ya miezi kumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli naomba Wizara iweze kuwaangalia hasa dada yangu mpenzi Mheshimiwa Ummy Mwalimu, najua ana moyo sana wa upendo hebu naomba aangalie Wilaya yangu ya Ngara jamani, hawa watu waweze kusaidiwa. Mheshimiwa Dkt. Ndungulile nilishamlilia sana nilishamwona uso kwa uso nikamwelezea kuhusu hawa watu lakini bado hawajapata mishahara yao, naomba sana waangalie kwa jicho la huruma. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vituo vya afya katika Wilaya ya Ngara tuna upungufu wa watumishi kwa asilimia 67, jambo linalotatiza huduma za afya. Hebu *imagine* asilimia

67 vituo vya afya hamna watumishi. Unaweza ukaenda kituoni ukakuta kuna Mganga mmoja huyu ndiyo *receptionist*, huyo ndiyo aangalie wazazi, huyo ndiyo angalie watoto na kila kitu. Jamani Wizara ya afya naomba watuangelie sana Wilaya ya Ngara, tuko mpakani mwa Rwanda na Burundi lakini tuko Tanzania, tunaomba watuangelie inawezekana wameshatusahau lakini tunaomba watuangelie kwa jicho la huruma. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia naomba kuongelea Watumishi wa Afya kutolipwa stahiki zao kwa muda mrefu kama vile *on call allowance* na malimbikizo ya mishahara, likizo na matibabu. Unakuta wafanyakazi wanafanya kazi kwa muda mrefu bado hawajapata stahiki zao, dada yangu Mheshimiwa Ummy Mwalimu Waziri wa Afya, Ustawi wa Jamii, Wazee na Watoto yaani mimi nakufa na yeye kwa sababu najua ni dada wa upendo nina imani ataweza kunisaidia huko ili tuweze kuwasaidia hawa ndugu zetu waweze kupata mishahara yao kwa wakati. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hospitali ya Nyamiaga inayomilikiwa na Serikali kwa asilimia 100, hiyo hospitali wodi ya wajawazito kuna vitanda vichache, unakuta wajawazito wanalala watatu hadi watano katika kitanda kimoja. *Imagine*, dada yangu Ummy ni mzazi kama mimi, wakati mwingine uchungu unakushika, unaenda kushika tumbo kumbe unashika la mwenzako, unaenda kushika mgongo unashika wa mwenzako, mmelala kitanda watu mko watatu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mheshimiwa Waziri aangalie hili, tupate angalau vitanda vya kutosheleza katika hospitali yetu ya Nyamiaga ambayo iko chini ya Serikali asilimia 100. Tunaweza tukasemea Murugwanza lakini Murugwanza iko chini ya Dayosisi na tuna watumishi wetu wa Serikali lakini Nyamiaga ni ya Serikali asilimia 100, lakini wagonjwa wanapata shida sana hasa akinamama wajawazito.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ni mama

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

nawawakilisha akinamama inaniuma sana, ninapokwenda nakuta akinamama wamelala watatu, watano kitanda kimoja na ile habari dada Ummy unaifahamu jinsi inavyouma, yaani sijui nisemeje, Mheshimiwa Dkt. Faustine Ndungulile naweza nikamwacha pembeni kwa sababu hajui uchungu wa akinamama tunaoupata wakati wa kujifungua. Kwa hiyo, naomba kwa kweli watuangelie kwa jicho la huruma sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunayo zahanati ya Kijiji cha Ishozi, Wilaya ya Misenyi iliangukwa wakati wa tetemeko la ardhi mpaka leo ukarabati wa zahanati hiyo haujaweza kufanyika ipasavyo. Naomba Serikali iweze kufanya ukarabati wa kutosha ili wale wananchi wa Ishozi kule Misenyi waweze kupata matibabu ya kutosha *especially* wazee, kuna watoto kuna akinamama, lakini hawapati huduma ile kutokana na kutokukarabatiwa kwa yale majengo yaliyoanguka kwa tetemeko. Sisi wa Mkoa wa Kagera hatukuliita tetemeko, lilikuja tu kwa bahati mbaya. Kwa hiyo, naomba Mheshimiwa Waziri na Wizara husika iweze kutusaidia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Halmashauri ya Wilaya ya Kyerwa haina hospitali ya Wilaya. Ile hospitali ina watu wengi sana pale Kyerwa kuna zaidi ya wananchi laki tatu, wote tunatuma kituo cha Kyerwa, naomba Serikali ituangelie kwa jicho la huruma tuweze kupata hospitali ya Wilaya katika Wilaya ya Kyerwa ili wananchi waweze kupata matibabu pasipo shida. Mheshimiwa dada yangu Ummy Mwalimu naomba anisikilize kwa makini sana na Mheshimiwa Dkt. Ndungulile nisije nikashika shilingi. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hospitali zote za Wilaya za Mkoa wa Kagera zina upungufu wa watumishi, kwa kweli tuna shida sana, kila Wilaya, kila zahanati kuna shida ya upungufu wa watumishi. Kipindi wanafanya uhakiki wa vyeti watu waliondoka wengi. Mheshimiwa baba yangu Mzee Mkuchika alishasema uhakiki ulishapita, sasa kwa nini wasiajiri watu wa kutosha katika hospitali zetu ili wazee, mama zangu, watoto, baba zangu waweze kupata huduma. Naomba sana watuangelie sana kwa jicho la huruma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Halmashauri za Manispaa za ya Bukoba na Muleba tayari zimeanza kujenga vituo vya afya. Je, ni lini Serikali au ina mpango gani wa kutenga pesa ili kuweza kusaidia hizi Halmashauri zikamilishe ujenzi wa vituo vile vya afya? Kwa sababu wananchi walishajitolea kwa moyo wao, tumejitolea kama wananchi kujenga vituo vya afya lakini havijakamilika, wanatusaidiaje ili tuweze kukamilisha vituo vile?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkoa wetu wa Kagera tuna visiwa 25 ambavyo vinakaliwa na wananchi, lakini visiwa vyote hivyo vina zahanati tano tu, katika zile zahanati...

(Hapa kengele illia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante, kwa mchango mzuri.

MHE.OLIVER D. SEMUGURUKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Dkt. Kamala, wajiandae Mheshimiwa Vicky Kamata na Mheshimiwa Maftah.

MHE. DKT. DIODORUS B. KAMALA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ya kutoa mchango wangu. Naomba nianze kutoa pongezi kwa Serikali yetu kwa kazi nzuri sana inayofanyika katika kudumisha na kuboresha huduma za afya, hongera sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama unavyofahamu sote tumeshuhudia bajeti ya dawa imeongezeka kutoka bilioni 30, mpaka bilioni 270 hili siyo jambo dogo. Nachukua nafasi hii kumpongeza pia Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri kwa kazi nzuri wanayofanya kusimamia sekta ya afya, nawapongeza sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, achukua nafasi hii pia kuwapongeza Wataalam wetu wanaosimamia *MSD* kwa

kazi nzuri waliyoifanya na wanayoendelea kuifanya ya kusambaza madawa, wamefanya mambo mengi pale, mengi yanaonekana kwa mfano, wakinunua magari kila mtu anayaona, ni rahisi kupongeza magari yanaonekana. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo kubwa walilolifanya zaidi ya magari ni kuweka mfumo wa *Car Tracking System* ambao gari inapobeba dawa za *MSD* ikisimama popote pale dereva atapigiwa simu hapohapo na kuambiwa mbona umesisima na ulikosimama siyo sehemu tuliyokutuma. Hili ni jambo kubwa na naomba waendele kufanya hivyo. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijamaliza hatua ya pongezi nimpongeze rafiki yangu, lakini pia Mkurugenzi Mkuu wa Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete, Mheshimiwa Profesa Janabi. Mwaka 2000 nilikutana na Profesa Janabi kule Japan alikuwa anafanya *PhD* yake, nikamuuliza sasa hii *PhD* unayosoma unasomea nini, aliniambia mambo mawili, moja sitalisema kwa sababu za kitalaam.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, alilisema, aliniambia angependa siku moja Tanzania waweze kufanya *operation* ya moyo bila kupasua moyo. Nikamwambia Mzee hii inawezekana, akasema ndiyo maana niko huku na itawezekana. Sasa hiyo ilikuwa ni ndoto yake mwaka 2000 leo hii sote tunakubali hapa Profesa Janabi na wenzake wanafanya kazi nzuri. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, huu moyo wa Profesa Janabi aliouonesha kwamba unapopelekwa nje kusoma basi ukisoma uwe na jambo ambalo unasema ukirudi Watanzania watanufaika namna gani. Kwa hiyo, nampongeza sana. Nakumbuka wakati ule Profesa Janabi alijaribu kunishauri akasema sasa Mheshimiwa umekuja huku Japan kwa nini usirudi na gari Tanzania nikamwambia na mimi nina ndoto yangu, hizi posho nikizikusanya hapa nikirudi nyumbani ndogo yangu ni kwenda kuwa Mbunge na nikaitekeleza. Kwa hiyo, Profesa Janabi wakati na mimi nakupongeza ukipata fursa na wewe usisite kunipongeza kwamba ndoto zako zilitimia,

lakini na ndoto za kwangu zilitimia, ndiyo maana leo hii nipo hapa, nakupongeza. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa nizungumze kwa haraka nimeshashukuru *MSD*. Pia namshukuru sana Mheshimiwa Waziri, nilipeleka ombi langu kwake rasmi, kwamba kituo chetu Bunazi hatuna mashine ya *anesthesia breathing machine*, leo hii nimepata taarifa za uhakika mashine hiyo imefika kwenye kituo na sasa mambo yote yanaenda vizuri. Namshukuru sana Mheshimiwa Waziri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sote tunafahamu kuwa Tanzania tumejaliwa miti ya asili mingi tu yenye uwezo wa kutengeneza madawa, nyote mnafahamu kuna dawa moja maarufu sana inaitwa *Cotecxin*, lakini dawa ile inatengenezwa kwa miti inayopatikana hapa Tanzania hasa pale Iringa. Wenzetu wanachukua miti wanapeleka kule wanatengeneza dawa wanatuuzia. Tanzania tunasema tunataka kujenga nchi ya viwanda lakini kujenga nchi ya viwanda ni jambo kubwa na hasa viwanda vya madawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu ni kwamba Wizara ya Afya ishirikiane na Wataalam wengine kuondoa vikwazo vinavyochelewesha Tanzania kuweza kujenga viwanda vya madawa. Nina rafiki yangu Mchina amekuja kuwekeza Tanzania kwenye kiwanda cha madawa na amewekeza, lakini ilimchukua miaka miwili kupata cheti cha kusajili dawa yake wakati Kenya inachukua siyo zaidi ya miezi sita kupata cheti cha kusajili dawa. Tanzania ya viwanda ina mambo mengi, naomba tushirikiane ili kuweza kuelekea huko. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna mpango mzuri unatekelezwa unaitwa *RBF (Result Based Financing)*, huu mpango ni mzuri sana unasaidia katika ujenzi wa kutoa miundombinu pamoja na motisha katika vituo vyetu vya afya na hasa kuboresha huduma ya mama na mtoto. Mpango huu nimeupenda sana kwa sababu pamoja na kusaidia miundombinu unatoa motisha kwa wafanyakazi kwa 25%.

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mango huo umesababisha hata Wakunga, Manesi wao wenyewe wanazunguka kutafuta nani mama mjazito anakaribia kujifungua ili aende akajifungulie kwenye kituo chake cha afya. Mpango huu ni mzuri na nashauri usambazwe kwa Tanzania nzima. Najua hivi sasa unatekelezwa katika mikoa saba, lakini mpango huu kwa kuwa umeonesha mafanikio ukisambazwa Tanzania nzima itakuwa jambo jema. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni la Bima ya Afya, natambua nimesoma kwenye hotuba kwamba sasa mpango huu wa huduma ya *CHF* iliyoboresha utanza 2018, mwaka 2018 ni sasa, mpango huu utawezesha kutoa ile *CHF* na wananchi wataweza kutibiwa si tu kwenye kituo kile cha afya, ataweza kutiwa kwenye zahanati kwenye vituo vya afya hadi hospitali ya mkoa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpango huu ni mzuri naomba utekelezwe kwa haraka na kwa kweli mimi niko tayari hata kusitisha mambo yote lakini mpango huu ukatekelezwe. Ni kwa sababu mpango huu ndiyo utaleta ukombozi mkubwa kwa Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa nimalize kwa jambo moja na lenyewe ni kwamba *MSD* wanajenga pale Kairabwa ujenzi wa Kairabwa *Logistics Center*. *Center* hiyo ni muhimu naunga mkono kwa asilimia 100 na namshukuru na Mkuu wa Mkoa wa Kagera anaunga mkono mpango huu. Kwa kweli Wabunge wengi wa Mkoa wa Kagera tunaunga mkono mpango huu, naomba ifanyike haraka itakavyofanyika ili *center* hiyo iweze kujengwa, tuweze kuboresha huduma za afya, madawa yawafikie wananchi kwa uharaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie kwa kusisitiza ule mpango *CHF* iliyoboreshwa, ni mzuri na utasaidia sana katika kuboresha huduma za afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.
(Makofi)

MWENYEKITI: Ahsante Mheshimiwa Vicky Kamata ajiandae Mheshimiwa Maftaha.

MHE. VICKY P. KAMATA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia hotuba hii iliyoko mbele yetu. Kwanza kabisa napenda nimshukuru Mungu kwa kuniwezesha kuisima tena katika Bunge hili na kuweza kuchangia bajeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niungane na wenzangu kumpongeza sana Mheshimiwa Umyy, Waziri wa Afya, Naibu wake, Mheshimiwa Dkt. Ndugulile, Katibu Mkuu na Viongozi wote, Watalaam wetu mbalimbali wa sekta hii ya afya, kwa jitihada kubwa wanazozifanya kuhakikisha kwamba afya ya Mtanzania inazidi kuimarika ili tuweze kufanya kazi na kuleta maendeleo kwenye nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na pongezi hizo naomba pia niwakumbushe Waheshimiwa Wabunge wenzangu jambo moja. Waheshimiwa Wabunge kazi yetu ni kuisimamia Serikali na kuishauri Serikali, nadhani hiyo ndiyo kazi yetu kubwa. Pia naamini kabisa kwamba sisi kuwa ndani ya Bunge hili siyo kwa sababu tuna akili kuliko wale tuliogombea nao tukawashinda, wala siyo kwamba sisi ni bora zaidi ya wale tuliogombea nao tukawashinda isipokuwa ni kwa neema tu. Mungu amepanda sisi tuingie kwa kipindi hiki tufanye hiyo kazi ya kuishauri Serikali na kusimamia siyo kuisifia Serikali au kuibomoa, hapana! Kuisimamia na kuishauri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikitoka kwenye hilo kwa kuwa nimewakumbusha na nashukuru makofi haya ni kwamba kweli mnaungana na mimi kwamba kazi yetu ni hiyo kusimamia na kuishauri, basi tuifanye kwa uaminifu na Mungu wetu atusaidie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kusema kwamba ni Mjumbe wa Kamati ya Huduma na Maendeleo ya Jamii maarufu *Guantanamo* na nilipata bahati ya kufanya ziara katika Mkoa wa Mbeya na Iringa ambapo tulikuwa

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

tunakwenda kukagua miradi ambayo ilikuwa imeidhinishwa pesa kwa bajeti ya 2017/2018.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumetembelea Chuo cha Maendeleo ya Jamii cha Lungemba kilichopo Mufindi – Iringa. Chuo kile kilikuwa kimetengewa milioni 258 kama nakosea nitarekebishwa na Wajumbe wenzangu lakini nina uhakika ni milioni 258 zilitengwa na tukaidhinisha pesa zile ziende kwa ajili ya mradi ule ili hiki Chuo cha Maendeleo ya Jamii huo mradi uweze kukamilika, tuweze kudahili wanafunzi wa kutosha ili waje watusaidie huko maana tunaitaka Tanzania ya viwanda, tunataka Tanzania kufikia uchumi wa Kati kwa kutegemea viwanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunawategemea sana hawa Maafisa Maendeleo washuke kule chini kwenye Kata zetu, wafanye hiyo kazi ya kuhamasisha maendeleo, wawe chachu kwa sababu watakwenda kule wakiwa wameelimishwa vya kutosha, wakatusaidie kule chini, kuhamasisha maendeleo kule chini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeenda kule pesa zile ambazo tumeidhinisha Bunge la Bajeti mwaka jana mwaka wa 2017/2018 pesa hazijakwenda mpaka tulivyoenda kukagua huo mradi na mpaka juzi ambapo tunajadili tena, tunachambua bajeti ya hii 2018/2019, taarifa tulizokuwa nazo mpaka dakika ya mwisho juzi hapa ni kwamba zile milioni 258 hazijakwenda mpaka sasa hivi tunapojadili bajeti nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeenda Chuo cha Maendeleo ya Jamii Uyole, kiko Mbeya. Chuo hicho kilikuwa kimetengewa zaidi ya milioni 216, tumefika kule pesa hazijakwenda mpaka mwisho sasa tunaingia bajeti nyingine 2018/2019 pesa hazijakwenda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumekwenda hospitali ya Rufaa ya Mbeya, hii ni hospitali ya Kanda inahudumia mikoa saba, hospitali hii tuliidhinisha kwenye Bunge hili bilioni 200 kwa ajili ya kununua madawa na kazi zingine huko nafikiri

na ujenzi wa jiolojia, kitu kama hicho mtanirekebisha wataalam ambao mnajua, lakini bilioni 200 tumeidhinisha kwenye Bunge hili. Mpaka tunaenda kuukagua ule mradi bilioni 200 zilikuwa hazijakwenda na mpaka juzi tunachambua bajeti hii ya mwaka mwingine 2018/2019, pesa zile hazijakwenda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi yetu ni kuisimamia Serikali na kuishauri sasa tunashauri zile pesa ziende hata kama mimi namheshimu sana Mheshimiwa Ummu na naamini wana dhamira ya dhati pamoja na Naibu wake na Katibu Mkuu wanafanya kazi kwa dhati, sasa sisi kama kazi yetu ni kusimamia kweli Serikali, ni kuishauri kweli Serikali, pesa ambazo tunakuwa tumepitisha humu ziwe zinaenda kule kutekeleza miradi ili hata uhalali wetu wa kuwa humu ndani uweze kuwepo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, maana kama tunaisimamia Serikali, tunaishauri, halafu tunaidhinisha pesa haiendi mpaka dakika za mwisho, tunakuja kujadili bajeti tena kwa mwaka mwingine, tunaidhinisha tena pengine hazitaenda tena. Kama zile za mwaka jana hazijakwenda tuna uhakika gani hizi tunazoidhinisha leo zitakwenda? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba sana, tusionekane kama *rubber stamp*, maana huko nje jamani *credibility* ya Bunge letu inaondoka watu wanafuatilia Bunge, watu wanafuatilia Bunge hili tutake, tusitake na wakija wakaanza kutudhihaki kama akina Pascal Mayala tusiwalaumu kwa sababu wao wanaamini kazi yetu ni kuisimamia na kuishauri Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tunapoishauri tunatakiwa tuhakikishe kwamba tunaidhinisha pesa mwaka unaofuata au muda unaotakiwa pesa zikiwa zimeshaenda au hazijaenda tuwe na haki ya kuuliza na tujibiwe tu vizuri siyo kwa lengo la kubomoa bali kwa lengo la kujenga. Nimesema kazi yetu ni kuishauri na kuisimamia, siyo kuibomoa wala kusifia siyo kazi yetu hiyo. (*Makofi*)

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana mimi nitaunga hoja hii mkono bila wasiwasi, lakini naomba tunapoidhinisha pesa ziwe zinaenda na kama kunakuwa kumetokea mabadiliko yoyote ya matumizi basi Bunge hili si ndiyo linatakiwa pia liidhinishhe hayo mabadiliko? Kwa hiyo, kama kuna mabadiliko, tuidhinishhe sasa hayo mabadiliko kwamba hii pesa haitaenda tena kwenye kile Chuo cha Maendeleo lakini tutaitumia kwenye *one, two, three, four* iende hivyo, ndiyo hivyo ndugu zangu tutafika, vinginevyo hatutafika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina imani sana na Mheshimiwa Ummy, nina imani sana na Serikali hii kupitia Wizara ya Afya, naamini kabisa kwamba bajeti hii itapita lakini msisitizo sasa tukubaliane kabisa, tunapopitisha ziende kweli. Naomba pia kwa ajili ya Mkoa wangu wa Geita. Mkoa wa Geita tuna ujenzi wa hospitali ya Mkoa na mpaka sasa hivi jitihada kubwa zimeshafanyika Mheshimiwa Ummy, rafiki yangu anajua. Kwa hiyo, tunaomba hizi pesa ambazo tunazipitisha sasa hivi hapa, ziende ili ile hospitali ikamilike.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia hatuna ma-*specialist* kwenye hospitali yetu ya Mkoa, tunaye mmoja tu na uhitaji kwa Mkoa wa Geita ni *Specialist 24*. Wauguzi tunao watatu katika Mkoa mzima, tunahitaji Wauguzi 30. Kwa hiyo, naomba sana Serikali yetu hii sikivu, basi isikie yale ambayo tunayapitisha humu yaende ili tuweze kuufikia uchumi wa kati unaotegemea viwanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Maftaha, wajjandae Mheshimiwa Risala na Mheshimiwa Grace Tendega.

MHE. MAFTAHA A. NACHUMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, namshukuru Mwenyezi Mungu *Subhanahu-Wataala*, lakini nikushukuru wewe kwa kunipa nafasi jioni hii ya leo.

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wenzangu hapa wamezungumza mambo mengi sana na hasa hasa suala zima la uzalendo la Daktari Janabi, nami niungane nao kwa kazi kubwa anayoifanya ya kuhakikisha kwamba anajitoa na haya maendeleo tunayoyaona kwenye upasuaji wa moyo ni kwa sababu ya jitihada binafsi za Daktari Janabi ambaye ameamua kutumikia Taifa letu hili la Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana kuna suala limeleezwa na Waheshimiwa Wabunge hapa, suala la *delivery kits* wale akinamama wanavyokwenda kijifungua katika hospitali zetu wanakuwa na changamoto kubwa sana juu ya vifaa vya kujifungulia. Suala hili limekuwa ni tatizo kubwa sana, tumekuwa tunaongea kwa muda mrefu sana ndani ya Bunge hili kwamba vifaa hivi viweze kutolewa katika hospitali zetu za Serikali, lakini jambo la kusikitisha sana mpaka leo hivi vifaa havitolewi kwa ajili ya akinamama wanapokwenda kujifungua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pale kwangu Mtwara Mjini nilipochukua pesa zangu nilinunua vifaa hivi vya milioni 30 zaidi ya akinamama 5,000 nimeweza kuwagawia, kila mmoja ujauzito ukifika miezi nane au miezi tisa anafika Ofisi ya Mbunge, nimeweza kuwagawia bure kabisa hizi *delivery kits*. Naomba sana Serikali iweze kuendeleza zoezi hili katika Majimbo yetu yote ya Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie pia suala hili la hospitali za Kanda. Tumekuwa tunazungumza sana ndani ya Bunge hili kwamba Kanda zote Tanzania zina hospitali za Kanda isipokuwa Kanda ya Kusini pekee mpaka leo bado hatuna hospitali ya Kanda. Tumekuwa tunaongea sana kila Bunge, hii ni mara yangu ya tatu nazungumza ndani ya Bunge hili na Serikali inaahidi kwamba tunajenga lile jengo. Mpaka leo jengo la *OPD* limejengwa kwa muda wa zaidi ya miaka 10, utafikiri hili jengo unajengwa mnara wa Babeli ambao ndiyo haujakwisha mpaka leo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana kwamba hospitali ya Kanda ya Kusini tunamaanisha Mtwara,

tunamaanisha Lindi, tunamaanisha pia kule Ruvuma mpaka leo hatuna hospitali ya Kanda, bajeti inayotengwa kwa ajili ya hospitali ya Kanda ya Kusini kila mwaka ni bajeti ambayo haitoshi hata lile jengo mpaka leo halijakamilika na tunaambiwa kila mwaka tutatenga pesa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la kusikitisha sana, unaweza ukaangalia kuna hospitali zingine za Wilaya tu, hospitali za maeneo mengine zimetengewa zaidi ya bilioni nne, zingine bilioni tano, lakini hospitali ya Kanda ya Kusini, taarifa nikipitia kwenye randama hapa naambiwa bilioni mia moja lakini mpaka leo hizo bilioni 100 zenyewe inakuwa ni kizungumkuti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana Mheshimiwa dada yangu Umy Mwalimu tunamheshimu sana, hiyo hospitali ya Kanda ya Kusini, Mtwara, Lindi na Ruvuma tunaomba atenge pesa katika Bunge hili katika bajeti hii ili hospitali iweze kwisha, tumechoka kuzungumza neno moja kila siku.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine naomba sana hospitali ya Mkoa wa Mtwara, hospitali ya Ligula *X-Ray* hakuna. Nimezungumza sana ndani ya Bunge hili, nimepiga kelele sana, nimeandika sana, hii ni bajeti yangu ya tatu nazungumzia suala hili kwamba hospitali ya Mkoa wa Mtwara haina *X-Ray* iliyoko yenyewe ni mbovu na hawa watu wa Ligula hospitali walifanya jitihada kuiomba *NHIF* waweze kuwanunulia kwa mkopo lakini hawataki na hili ni kwa sababu Wizara haiko *serious*. Tunaomba sana vifaa tiba hivi, *x-ray* ya hospitali ya Mkoa wa Mtwara iweze kununuliwa na isiwe ahadi kila siku, tulikuwa tunaomba sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia *CT Scanner* hatuna kwenye hospitali ya Mkoa, *CT Scanner* haipo sasa ni jambo la ajabu sana. Tumekuwa tunaomba sana, tunazungumza sana, tunaandika sana, namwomba dada yangu Mheshimiwa Umy Mwalimu safari hii aweze kuiangalia kwa namna ya kipekee kabisa hospitali ya Mkoa wa Mtwara hospitali hii ya Ligula juu ya vifaa tiba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumze pia suala la watumishi. Ukija hospitali ya Mkoa wa Mtwara watumishi wanaohitajika ni watumishi 681, watumishi waliopo Madaktari, Wauguzi na wengine wote ni 255 pekee, upungufu ni zaidi ya watumishi 455. Tunaomba sana Wizara hii ilete watumishi katika hospitali ya Mkoa wa Mtwara, hospitali ya Ligula ili sasa tuweze kupata huduma hizi za afya kama maeneo mengine ya Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la ajabu sana kwenye hospitali hii, tunaye *Specialist* mmoja pekee, hospitali ya Mkoa inayohudumia Majimbo 10 ya Mkoa wa Mtwara lakini ina *Specialist* mmoja tu. Naomba Wizara watulettee *Specialist* hospitali ya Ligula, hospitali ya Mkoa ili na sisi tuweze kupata tiba hizi kama maeneo mengine ya Tanzania. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumze pia suala hili la dawa ambalo limesemwa hapa na hotuba ya Mheshimiwa Waziri amesema kwamba sasa hivi upatikanaji wa dawa ni asilimia 85. Pia katika upatikanaji huo amezungumza suala la watu ambao wamepewa misamaha ya dawa, kwa mfano, watoto chini ya miaka mitano, lakini pia watu wenye magonjwa maalum kama vile *pressure* na kisukari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali halisi iliyopo kule ukipitia, ukienda hospitali, ukienda katika zahanati zetu, dawa zikishafika ndani ya muda mfupi tu wagonjwa wanaambiwa dawa zimekwisha waende wakanunue kwenye *pharmacy*. Sasa unashangaa hii misamaha, mtoto kapewa msamaha, mzee kapewa msamaha, lakini mwisho wa siku wanaambiwa kwamba eti zile dawa hazipo waende wakanunue kwenye *pharmacy* wakati tumempa msamaha wakati hana uwezo wa kujiendesha, hana uwezo wa kujihudumia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sera inasema wazee kuanzia miaka 60 wapate zile *card* za matibabu bure, lakini kuna jambo ambalo linatendeka huko wilayani, huko mikoani ambalo naomba usimamizi sana wa Mheshimiwa Waziri kwamba hizi *card* zitolewe sawasawa na takwimu

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

zinazotolewa hapa, kwa mfano, pale kwangu takwimu zinasema wazee 1,500 ndiyo wamepewa zile *card* za matibabu bure, lakini ukienda huko mitaani hata hao wazee kiuhalisia 1000 hawafiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba sana kwamba suala la kupewa takwimu ambazo siyo sahihi na Watendaji wa Serikali huko Halmashauri na huko Mikoani Mheshimiwa Ummu Mwalimu uweze kuzipitia na uweze kuhakikisha kwamba takwimu unazopewa kweli ni takwimu za ukweli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni suala hili la dawa hizi ambazo ni dawa maalum, dawa za kisukari, dawa za UKIMWI na dawa zingine ambazo ni dawa maalum ambazo zinatolewa na *Specialist* tu. Hapa nimeeleza kwamba Mtwara hospitali ya Mkoa ina *Specialist* mmoja tu sasa wagonjwa wanatoka wilayani huko, wanatoka kwenye Kata za mbali huko wanakwenda kuchukua dawa hizi kwenye hospitali ya Mkoa. Naomba sana hawa wanaoitwa *Medical Assistance* hawa wapewe mafunzo na Serikali huko huko waliko hizi dawa ziweze kupatikana, wagonjwa wasiwe wanatembea umbali wa kilomita 80 kuja kufutilia dawa za UKIMWI.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana Mheshimiwa Ummu Mwalimu kwa sababu tunamfahamu, uwezo huo anao, ahakikishe kwamba analeta mafunzo maalum kwa hawa *Specialist* kwenye hospitali zetu za Kata, vituo vyetu vya afya ili dawa hizi maalum ziweze kupatikana huko ili wagonjwa wetu wasitembee kwa umbali mrefu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru sana kwa kunipa nafasi. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Risala, jandae GraceVictor Tendega.

MHE. RISALA S. KABONGO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi kuchangia Wizara

hii ya Afya. Kwanza kabisa natambua jitihada za Waziri wa Afya pamoja na Naibu wake kwa kazi kubwa ambayo wanaifanya ya kusimamia afya ya mama na mtoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitajikita kwa akinamama ambao wana matatizo ya kupata ujauzito. Tatizo hili ni kubwa sana hapa nchini na linasababisha unyanyapaa pamoja na ndoa nyingi kuvunjika. Waathirika wakubwa wa tatizo hili ni wanaume na wanawake lakini inakuja kutokea kwamba wanawake ndiyo wanakuwa wanabeba tatizo hili. Kwa hiyo, namwomba Waziri aendelee kusimamia jambo hili ili wanawake wapunguziwe suala hili la unyanyapaa unaotokana na matatizo unaotokana na matatizo ya kupata ujauzito.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie *Dar IVF clinic* ambayo ni *clinic* inayotoa matibabu kwa akinamama hawa wanaoshindwa kupata ujauzito; hospitali hii imekuwa ikisaidia sana wanawake wanaoshindwa kupata ujauzito na wanawake wawili mpaka watatu wanahudumiwa kwa siku. Tunaweza kusema kwamba wanawake zaidi ya 50 wanahudumiwa matatizo haya ya kupata ujauzito kwa maana ya kupandikizwa watoto au kusaidiwa njia mbalimbali za kupata uzazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, gharama za matibabu ni kubwa sana kwenye suala hili. Mwanamke au familia inaingia kwenye gharama ya dola 7,000 au 8,000 hadi dola 10,000 kwa mwanamke kupata matibabau haya. Familia nyingi zinauza rasilimali lakini pia zinaingia katika mikopo kuingia katika kusaidia wanawake hawa kupata ujauzito. Ushauri wangu kwa Serikali ili kupunguza gharama hizi kwa familia dawa zinazotoka nje ili kusaidia wanawake hawa kupata ujauzito zina gharama kubwa, lakini pia nataka kuishauri Serikali pamoja na Wizara hii kuondoa kodi kwenye dawa hizi ili ziweze kupatikana kwa urahisi, lakini pia kuondoa vizuizi vingi vinavyoambatana na uingizwaji wa dawa hizi ili tuweze kusaidia wanawake hawa na kuondoa urasimu pia ambao unapelekea dawa hizi kuchelewa kuingia nchini. (Makofi)

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile ningependa kushauri Wizara ya Afya kusaidia dawa hizi kama zinaweza zipatikana kwenye *MSD* ili tuweze kuzipata kwa urahisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ambalo ningependa kuishauri Wizara ni Madaktari Wataalam, kama ilivyofanywa kwenye Taasisi ya Moyo kupandikiza Figo tunaomba Wizara itafute hawa wataalam ambao wanaweza kusaidia zoezi hili kwenye hospitali zetu za rufaa ili tuweze kusaidia wanawake hawa kupata ujauzito kwa gharama nafuu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine la tatu, nataka pia Wizara ione namna gani tunaweza kutoa elimu kwa jamii ili kuona tatizo hili siyo la wanawake pake yao bali na wanaume pia wanahusika. Hii litasaidia sana kuondoa unyanyapaa kwa wanawake ambao wanashindwa kupata ujauzito.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie pia kwa kumpongeza Waziri wa Afya na Naibu wake tena kwa kazi kubwa ambayo wanaifanya, lakini niwaombe kwenye zile zahanati zetu kwenye maeneo ambayo tunatoka kwenye Majimbo yetu, kwenye Mikoa yetu ziboreshwe kuna tatizo kubwa sana la maji kwenye zahanati zetu. Tunaomba namna ambavyo tunakarabati zahanati zetu tuweke gata ili kuweza kuvuna maji ya mvua na itasaidia sana kuweza kupata maji katika zahanati zetu na watu waweze kujifungua kwa usalama zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Grace Tendega wajiandae Mheshimiwa Asha Mashimba Jecha na Maria Ndila Kangoye.

MHE. GRACE V. TENDEGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi na mimi kuchangia bajeti hii ya afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa nafasi hii ya uhai kuweza kuwa mahali hapa kufanya kazi hii ambayo ni kwa ajili ya wananchi. Nitajielekeza moja kwa moja katika kuchangia bajeti hii. Namheshimu sana Mheshimiwa Waziri wa Afya pamoja na Naibu wake lakini katika majibu ya mwezi Mei mwaka 2017 kuna hoja ambazo tulikuwa tukiuliza kuhusu afya ya mama na mtoto na jinsi ambavyo wanaweza wakakinga akinamama kutopata vifo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika majibu haya tuliambiwa kwamba, Wizara na Serikali kwa ujumla imejipanga kuhakikisha kwamba wanapunguza katika vizazi hai 100,000 watafikia wanawake 292 angalau watakaokuwa katika hilo. Hata hivyo, sasa hivi mmeona wanawake katika vizazi hai 100,000 wanaopatwa na vifo ni 556, imepanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hiyo naomba majibu Mheshimiwa Waziri atuambie ni mkakati gani ambao wanaenda kufanya akinamama hawa wasiweze kupoteza maisha yao wakati wa uzazi. Tunaomba mkakati madhubuti wa Serikali ambao utakwenda kupunguza ama kumaliza tatizo hili la akinamama pamoja na kazi kubwa ambayo inafanyika ya kupeleka vifaa na kadhalika nini kilichopo hapo kinachopelekea ongezeko hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kingine ni bajeti kutotoka kwa wakati. Mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Huduma na Maendeleo ya Jamii, kama alivyokwisha sema mwenzangu tunatenga bajeti, lakini utekelezaji wake unakuwa ni mdogo sana. Waziri atuambie nini kinafanya hivyo, tumekwenda katika ziara katika Mkoa wa Iringa, tumekwenda Mkoa wa Mbeya, tumeona wenyewe, inafika mahali mnaona aibu kama Wabunge, mnakwenda kukagua miradi ambayo pesa hatukupeleka. Tunawaweka katika mazingira gani hawa Watendaji ambao tunasema tunakuja kukagua pesa ambazo zilitumwa, tuliidhinisha mwaka wa fedha huu wa 2017/2018 halafu mnakwenda pale hakuna hata shilingi moja iliyokwenda. *(Makofi)*

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumekwenda Chuo cha Rungemba cha Maendeleo ya Jamii, hakuna fedha iliyokwenda. Tumekwenda Chuo cha Uyole Maendeleo ya Jamii, hakuna fedha iliyokwenda. Tumekwenda katika Hospitali ya Rufaa ya Mbeya ambayo inahudumia mikoa saba lakini hakuna fedha iliyotengwa iliyokwenda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli wale Wakurugenzi wanafanya kazi kubwa sana. Mkurugenzi wa Hospitali ya Rufaa ya Mbeya ameweza hata kuajiri wafanyakazi kwa kutumia *own source*, kazi ambayo ilikuwa ifanywe na Serikali hii lakini amekwenda kufanya hiyo kazi. Tunampongeza kwa sababu wananchi waliweza kupata huduma. Tunaitaka Serikali ipeleke pesa wananchi waweze kupata huduma kama tunavyopitisha bajeti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, bajeti ya mwaka 2017/2018 iliongezeka kwa asilimia 35 kutoka bajeti ya 2016/2017, lakini bajeti hii ambayo tunaijadili sasa imepungua kwa asilimia 20. Hii maana yake nini? Ni kwamba tunakwenda kuwahangaisha wananchi tena kule, hawatapata madawa, hawatapata huduma bora inayotakiwa, vifaa tiba na kadhalika, hii inakwenda hadi kwenye Mkoa wangu wa Iringa, ukiangalia Mkoa wa Iringa Wilaya ya Kilolo ambako... *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante muda wako umekwisha. Mheshimiwa Asha Mashimba, wajiandae Mheshimiwa Maria Ndila Kangoye na Mheshimiwa Anna Lupembe.

MHE. ASHA MSHIMBA JECHA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia leo kusimama hapa katika Ukumbi wako huu wa Bunge, pia nikushukuru wewe kwa kunipa nafasi ya kuchangia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kazi nzuri na kubwa anayoifanya, tunaiona na mwenye macho haambiwi tazama. Pia nimpongeze Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, tunamwona na yeye

anavyoshiriki katika kuleta maendeleo ya Tanzania yetu. Niwapongeze Mheshimiwa Waziri Mkuu, Waziri wa Afya, Naibu Waziri wa Afya pamoja na Watendaji wake wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mnafanya kazi nzuri, Tanzania ni kubwa changamoto haziwezi zikaisha kwa siku moja, Wizara ya Afya ilivyokuwa jana siyo ya leo na tunavyoendelea itazidi kubadlika hatua baada ya hatua, c chapeni kazi Mwenyezi Mungu atawalipa kwa wema wenu mnaoufanya. *(Makofi)*

MBUNGE FULANI: Amina.

MHE. ASHA MSHIMBA JECHA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kuchangia kuhusu Bima ya Afya. Tanzania bima ya afya kwa wote inawezekana, Mheshimiwa Waziri naomba tukae na taasisi mbalimbali na vikundi mbalimbali kuona jinsi gani wananchi wanaweza kujiunga na bima ya afya. Wananchi wengi wakiweza kujiunga na Bima ya Afya itaweza kupunguza matatizo mengi ya kiafya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama alivyozungumza Mheshimiwa Azza asubuhi hapa, akasema kwamba sasa hivi inaelekezwa kwenye vikundi mjiweke pamoja, lakini kuna watu hawana vikundi kweli ila pesa wanazo, naamini watu wengi wakijitokeza kujiunga mmoja mmoja Wizara wanaweza mkakaa au taasisi zinaweza zikakaa zikawakusanya ule wingi wa vikundi ambao wanautaka. Kwa hivyo, mwananchi asikose bima ya afya kwa sababu hana kikundi cha kujiunga pamoja na kupata ile fursa ambayo wanavikundi wanaweza wakaipata. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie kuhusiana na afya ya uzazi, kwa kweli mwanamke anastahili kuenziwa, kutunzwa, kukingwa na unyanyasaji wowote ambao anaweza akaupata, kwa sababu bila ya mwanamke dunia hii isingeweza kuendelea. Kuna matatizo mengi ambayo yanamkumba mwanamke tumeona katika kitabu chako

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Waziri umezungumzia tezi ya shingo ya kizazi lakini mwanamke wakati huo huo anakumbwa na *fistula* yote yanamkosesha raha mwanamke. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suluhisho la hili wamesema wanzangumkwamba huduma hii isogezwe karibu na wananchi. Huduma kuifuata Dar es Salaam na sehemu nyingine kwenye hospitali za Kanda wananchi Tanzania hii wanaishi mbali sana na huduma wasipoipata kwa kweli uhai wao uko matatani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ugonjwa huu wa saratani ya mlango wa kizazi siyo tatizo la muda mfupi linachukua muda mrefu linahitaji uwe na hela, kama huna hela huwezi kufuatilia huduma hii na unakuta watu wengine wanashindwa kupata huduma hii, kutokana na ukosefu wa hela. Tunaomba Mheshimiwa Waziri pamoja na juhudi Serikali yetu inayochukua lakini tuzidi kuangalia, kuokoa vifo ambavyo umezungumza humu kwamba asilimia kubwa akinamama wanakufa kutokana na saratani ya shingo ya kizazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie unyanyasaji wa watoto, Mheshimiwa Najma Giga amezungumza, kwa kweli watoto wananyanyasika sana. Mheshimiwa Waziri pamoja na juhudi tuliyochukua tumeridhia maazimio kanuni, matamko, sheria ya kumlinda mtoto bado tunawaona watoto wananyanyasika. Basi katika mikoa yetu tuanzishe sehemu maalum ya watoto hawa kuweza kuwasaidia, unawakuta watoto pamoja na kwamba tunasema wana wazee wao, wanahangaika mitaanim wanazurura mitaani, watoto wale wanasaidiwa saa ngapi, wakiugua wanatibiwa na nani na tunaona saa nyingine mtoto anafika mpaka kwenye vyombo vya habari anatangaza au anatangaziwa kusaidiwa ugonjwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli imefikia mahali katika mikoa yetu kuwe na sehemu ambazo wale watoto kama wameshindwa kutibiwa na wanahitaji kusaidiwa basi usaidizi wao uwe wa karibu, tusiende mpaka kwenye

vyombo vya habari kutangaza ugonjwa kwa kweli ile hatumtendei haki yule mtoto ambaye anahitaji tumsaidie. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo naomba nichangie katika Wizara hii ni uzazi salama kwa mama. Mheshimiwa Waziri pamoja na jitihada kubwa iliyochukuliwa na Serikali yetu lakini bado tuendeleo kuokoa maisha ya mama na mtoto. Akinamama wengi wanapoteza maisha wakati wa kujifungua au wakati wa ujauzito, pengine inawezekana ni lile tatizo la asili la ukosefu wa lishe bora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hivyo, ipo haja ya kuwatumia Maafisa wa Afya au Maafisa wa Maendeleo ya Jamii kuihamasisha jamii juu ya lishe bora ili wakati wa kujifungua basi akinamama waweze kujifungua salama na kupunguza gharama kubwa ambayo anaweza akaitumia wakati ule. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri mimi sina zaidi isipokuwa naendelea kuipongeza Serikali yetu ya Chama cha Mapinduzi. Kwa kweli tumeona maendeleo makubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kumalizia katika kudumisha Muungano wetu, basi siyo vibaya kuwa tuna mashirikiano ya karibu sana na upande wa Zanzibar kwa sababu Wizara ya Afya najua siyo Wizara ya Muungano, lakini magonjwa hayana mipaka na utaalum hauna mipaka, kwa hivyo siyo vibaya kuongeza ushirikiano wetu wa karibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. (Makofi)

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Maria Ndila, ajiandae Mheshimiwa Anna Richard Lupembe.

MHE. MARIA N. KANGOYE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipatia nafasi ya kuchangia mchana huu wa leo. Awali ya yote nianze kwa kumshukuru Mungu kwa kunipatia afya ya kuweza kusimama mbele ya jukwaa hili. Pia nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

timu yote ya Wizara ya Afya kwa kazi nzuri wanayofanya. Mungu awabariki ana azidi kuwatia moyo. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitakuwa sijatenda haki kama sitompongeza Mheshimiwa Rais, kwa kazi nzuri anayofanya na kwa usikivu alionao. Tumekuwa tukiona maendeleo mbalimbali hata katika sekta hii ya afya katika ugawaji wa madawa na kuyasambaza, pia hata katika usambazaji wa magari ya kubebea wagonjwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, labda katika hili niseme ahsante sana kwa Serikali kwa *ambulance* ambayo tumepoke katika Kata ya Kabila, Jumamosi iliyopita imewasilishwa na Mbunge tunashukuru sana, sisi kama wananchi wa Magu tuna imani sana na Serikali hii na kwamba mnatusikiliza na tutazidi kuwa pamoja. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na pongezi hizo bado kuna changamoto kubwa sana ya ukosefu wa watumishi katika sekta ya afya. Zahanati zetu, hospitali zetu zina changamoto kubwa sana, hivyo basi Serikali ilianganalie hili kwa ukaribu kama ilivyotoa ajira hapo nyuma ijitafakari tena itoe kulingana na matakwa halisi. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na changamoto ya ukosefu ya chanjo kupungua kwa kasi bado kumekuwa na tatizo la chanjo ya kichaa cha mbwa. Chanjo hii imekuwa ni adimu imekuwa kama bahati nasibu, naomba Serikali ianganalie kwa ukaribu, kwanza ni gharama kwa mwananchi wa kawaida, sindano moja siyo chini ya Sh.30,000, lakini hata kuiyata hiyo sindano inaweza ikawa shida, ikakulazimu kutoka nje ya mkoa. Hivyo basi, tunaomba Serikali ianganalie kuanzia bei na upatikanaji wake kwani sindano zinazohitajika ni tatu, kwa hiyo Sh.90,000 kwa mwananchi wa kawaida ni kubwa sana. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo nimevaa uhalisia wangu, mimi kama *champion* wa hedhi salama sitajisikia vizuri kama

sitaishauri Serikali siku ya leo juu ya hedhi. Suala la hedhi tumekuwa tukilichukulia poa kwa sababu siyo ugonjwa, ndiyo kweli siyo ugonjwa lakini tatizo la hedhi kutokuwa salama ni changamoto kubwa sana na imekuwa ikisababisha magonjwa mengi mno.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri atakubaliana na mimi kwamba dawa nyingi *antibiotics* wanazosambaza katika vituo vyetu vya afya, katika hospitali zetu zinakuwa *consumed* na wanawake, wanawake ambao wanatibiwa magonjwa ambayo yanatokana na ukosefu wa hedhi salama, ni lazima tukubaliane na hilo. Ndiyo maana tunasimama hapa na kusema kwamba Serikali iangalie namna ya kuweza kutoa nyenzo za wanawake na wasichana katumia katika siku zao, tunachomaanisha ni kwamba ni bora tu-*prevent* magonjwa kuliko kuacha yatokee ndiyo tutoe dawa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo suala hili ni muhimu sana Serikali kuliangalia, pamoja na kwamba tunafahamu mnayo mambo mengi ya kutekeleza...

MWENYEKITI: Taarifa.

T A A R I F A

MHE. SABREENA H. SUNGURA: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumpa taarifa mzungumzaji, kwamba suala la hedhi salama ni suala ambalo ni la msingi sana na yeye kama *champion* nampongeza kwa sababu wasichana wetu vijijini wamefikia hatua mpaka wanatumia mavi ya ng'ombe na wengine wameathirika mpaka kuumwa na ..

MWENYEKITI: Ahsante. Utatuchukulia muda endelea.

MHE. MARIA N. KANGOYE: Mheshimiwa Mwenyekiti, naipokea taarifa hiyo kwa niaba ya wanawake wote wa Kitanzania. Kwa hiyo, tunaposema wapewe nyenzo hizi ni kwamba tunataka ku- *prevent* magonjwa kuliko kutibu na kama tunavyojua *prevention is better than cure*. Kwa hiyo,

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

tunaamini kabisa Serikali hii sikivu leo hii itaenda kujitafakari upya. Pamoja na kwamba wana mambo mengi tunaamini wanao wadau wengi ambao wanaweza wakawa-*aproach* wakaweza kuwasaidia katika hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati tunafikiria huko, tuangalie pia namna ya kupunguza bei ya hizi taulo za kike tuangalie kuanzia *VAT* kama zinaweza kufutwa zifutwe, kama kuna *possibility* ya *regulate* bei ili wanawake wote na wasichana waweze ku-*afford* itakuwa ni vema zaidi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hapo nianze kuchangia masuala yanayohusu mkoa wangu.

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, naomba utulivu ndani ya Bunge *please!*

MHE. MARIA N. KANGOYE: Katika Wilaya ya Ukerewe Mkoani Mwanza kumekuwa na changamoto nyingi sana za kiafya, kwa wale ambao hawaifahamu Ukerewe Wilaya hii ni muunganiko wa visiwa 38. Kipo Kisiwa cha Irugwa kina changamoto nyingi kwa nini nimekichagua chenye wote tu katika visiwa vyote 38.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwananchi kutoka Irugwa kuifikia hospitali ya Wilaya anachukua takribani saa nne na kuendelea, siyo kwamba katika kisiwa hiki hakuna zahanati, kisiwa hiki ni Kata pia na ina zahanati, lakini cha ajabu ni kwamba ina mtumishi mmoja tu ambaye ni Mhudumu ambaye hana ruhusa hata ya ku-*prescribe* nusu ya kidonge cha panado kwa mgonjwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni wakati sasa wa Serikali hii kusikiliza kilio hiki, wananchi wa Irugwa wameteseka kwa muda mrefu, naomba sana uwepo wa haraka sana wa kuwapatia wafanyakazi wa afya kwa sababu wamekuwa wakihangaika kwenda katika hospitali ya Wilaya na ukizingatia kwamba usafiri waotumia si salama...

T A A R I F A

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, hizi taarifa mnachukua muda wa mtoa hoja zake pale.

MHE. CECIL D. MWAMBE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nimpe taarifa mzungumzaji kwamba nilikuwa naongea hapa na Mbunge wa eneo husika, Wizara ya afya imetnga shilingi milioni 200 kwa ajili ya kununua boti kuwasaidia wakazi wa visiwani kuwafikisha hospitali ya Wilaya.

MHE. MARIA N. KANGOYE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kufahamu japo sijaipokea kama ambavyo unataka wewe, kwa sababu nina maana yangu ya kuchangia hivi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niendeleee kusema kwamba usafiri ule siyo salama na kama Serikali imetenga tunashukuru kwa usikivu wa Serikali ya Chama cha Mapinduzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia zahanati hii kuna haja ya kuipanua kuwa kituo cha afya kutokana na wingi wa mahitaji ya wananchi wa pale kwa ajili ya matibabu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Wilaya ya Kwimba, Jimbo la Sumve tunashukuru sana kwa ahadi ambayo mmetimiza ya kukitengea kituo cha afya cha Malya milioni 400. Ni mara nyingi Mbunge wa Jimbo hilo amekuwa kipiga kelele na mwaka jana nilimpa *support* ya kusimama hapa, na kuomba kwamba Serikali iangalie ahadi hizo. Akinamama walikuwa wanajifungulia kwenye sakafu, lakini leo Mheshimiwa Waziri ametufuta machozi, wameweza kututengea milioni 400, tunachoomba sasa ni kutupatia milioni 350 ambayo ni ya kununua vitanda na vifaa vya tiba ili shughuli ziweze kwenda kama ambavyo tulikuwa tunatarajia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Lupembe, wajiandae Mheshimiwa Stanslaus Mabula na Mheshimiwa Mary Chatanda.

MHE. ANNA R. LUPEMBE: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa naomba nikushukuru kwa kunipa muda huu wa kuweza kuzungumzia Wizara hii muhimu sana kwa sisi akinamama. Naomba nimshukuru kwanza Mungu ambaye ametulinda siku hii ya leo, ametupa kibali tuko mahali hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, naomba nimpongeze sana Mheshimiwa Rais kwa kazi kubwa ambayo anaendelea kuifanya, tunaona kwa ajili ya afya na pesa nyingi ambazo amezitenga tunaona na kushuhudia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimpongeze sana Waziri Mheshimiwa Umy Mwalimu pamoja na Naibu wake kwa kazi kubwa nzuri. Kusema kweli Mheshimiwa dada Umy Wizara ameiveza, lazima tumpongeze, Wizara ameiveza na ameimudu, hongera sana, Mungu ataendelea kukutetea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nikipongeze Kitengo cha Jakaya, Profesa Janabi pamoja na Mkurugenzi wa *Ocean Road*, Kitengo cha Sukari, Meno, *MSD* kwa kazi nzuri ambayo walikuja Mkoa wa Katavi kupima afya za wananchi wa Mkoa wa Katavi. Naomba sana kazi hii Mungu ataendelea kuwalipa na waendeele kuwatumikia Watanzania kwa sababu Katavi ni mbali, lakini walikuja kuangalia afya za Watanzania wa Mkoa wa Katavi na wasichoke nitawaomba waje tena kuangalia kwa sababu walipunguza matatizo mengi ingawa hawakumaliza lakini matatizo waliweza kuyaona na kuweza kuyamudu kiasi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkoa wa Katavi ni mkoa mpya. Tunajua Serikali katika ile mikoa mipya imepanga kujenga hospitali za mikoa. Mkoa wa Katavi 2017/2018 tulipangiwa bilioni moja, lakini pesa hii hatuwezi kujua ilienda wapi, kwa sababu mpaka leo uwanja ule uko wazi

wala hakuna kitu chochote ambacho kilifanyika, wala kuonesha dalili ya kujengwa hospitali ya Mkoa wa Katavi. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka huu vilevile sijaona kama tumepangiwa pesa au kuna dalili kwamba tumeambiwa kuwa tutajengewa hospitali ya mkoa sijaona dalili ya aina yoyote. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndani ya Mkoa wetu wa Katavi, jiografia ni mbaya sana. Nashukuru sana Mheshimiwa Umy alifika alijionea uhalisia, maana angekuwa hajajionea uhalisia angesema sifahamu, lakini uhalisia wa Mkoa wetu wa Katavi anaufahamu vizuri sana. Nashukuru sana Mheshimiwa Umy alikuja Mkoa wa Katavi na vilevile aliniahidi Wadi moja katika hospitali ya Manispaa ya Mpanda. Naisubiri sana hiyo Wadi ambayo aliwaahidi wananchi wa Wilaya ya Mpanda Manispaa, alisema atawajengea Wadi. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nishauri kwa sababu hii hospitali ya Mkoa inapangiwa pesa na mpaka sasa hivi hakuna kitu kinachoendelea, naomba kwa vile hospitali ya Manispaa ya Mpanda ina eneo kubwa sana na ndani ya hospitali ya Manispaa ya Mpanda tuna matatizo mengi makubwa kwa sababu majengo ya Wadi ni machache, Madaktari hatuna, Manesi ni wachache mno, Wahudumu ni wachache mno kusema ukweli!

Mheshimiwa Mwenyekiti, ile hospitali ya Manispaa ya Mpanda ndiyo imekuwa kama hospitali ya Mkoa, sasa wananchi wote wa Mkoa wa Katavi wanakwenda kwenye ile hospitali, wodi chache, vitanda hakuna! Sasa namwomba sana dada yangu Mheshimiwa Umy, mpenzi wangu, atusaidie basi aongeze hata Wadi tatu ndani ya hospitali ya Manispaa ili tuweze kukidhi mahitaji ya wananchi wa Wilaya ya Mpanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba sana Mheshimiwa Waziri atusaidie kwa sababu wananchi wa

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

Mpanda wanapata shida sana kimatibabu, ukiangalia vifaa tiba hatuna, vifaa tiba vyote, *x-rays* na kila kitu ni vibovu. Namwomba sana dada Ummu, Mheshimiwa Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto atusaidie vifaa tiba hatuna, wananchi wa Mpanda wanapata shida sana, wanakwenda Mbeya, wanakwenda Ikonda, lakini tukiiboresha hospitali ya Mpanda sidhani kama wananchi wa Mpanda watahangaika. Namwomba sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru sana Mheshimiwa Ummu alikuja katika Mkoa wa Katavi akaenda katika Wilaya ya Mlele katika Tarafa ya Inyonga. Namshukuru alipandisha ile hospitali ikawa hospitali ya Wilaya, kile kituo cha afya cha Inyonga. Hata hivyo, mpaka leo hatujapata hati na kama hujapata hati ya kuwa hospitali ya Wilaya ina maana vitu vyote vinasimama, ina maana Madaktari wale bado wanaendelea kuwa Madaktari wa kituo cha afya na dawa zinaendelea kuwa zile za kituo cha afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Ummu, akitusaidia kutupa hati kamili sasa kwa sababu jengo la *mortuary* limekwisha, kila kitu ambacho vile vigezo vyote walivyoviweka, vimekwisha, tunaomba hospitali ya Mlele ipatiwe hati iwe hospitali kamili ya Wilaya ya Mlele ili iweze kupunguza kasi ndani ya Manispaa ya Mpanda. Namwomba sana Mheshimiwa Ummu ili tuweze kupunguza matatizo kwa wagonjwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndani ya Wilaya yetu ya Manispaa ya Mpanda tuna vituo viwili vya afya. Vituo hivyo ni kituo cha llembo pamoja na Mwangaza. Vituo hivi havijapangiwa pesa, Mheshimiwa Ummu naomba atuoneshe katika hivi vituo vya afya ambavyo vinapunguza kasi ya uzazi salama, kwa ajili ya msongamano pale Makao Makuu Manispaa na hajavipangia pesa. Naomba Mheshimiwa Waziri kesho wakati anafunga basi atanionesha vituo hivi viwili vya afya, Kituo cha Afya llembo pamoja na Mwangaza pesa yake iko wapi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile tunahitaji Kituo cha Afya kati ya Mwamkulu na Kakese kwa sababu ni *distance* ndefu kuja Mjini vilevile kuna watu wengi zaidi. Tulikuwa tunahitaji kituo cha afya katika maeneo hayo ya Mwamkulu na Kakese. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru masuala ya Bima ya Afya hususan Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya. Nashukuru Mfuko huu unafanya kazi vizuri sana na Mkurugenzi anafanya kazi vizuri sana, ndani ya mkoa yote vituo vipo na wafanyakazi wapo. Hata hivyo, kila Mtanzania anahitaji kutibiwa vizuri na vilevile katika mfumo wao waliouweka ndani ya makundi kuwapa kikundi cha SACCOS na kadhalika ndiyo uwalipie Bima ya Afya Sh.79,000 ni sawa, lakini kila Mtanzania anahitaji matibabu, naomba huu mfuko...

(Hapa kengele illia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante kwa mchango wako mzuri.

MHE. ANNA R. LUPEMBE: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante umechangia vizuri sana. Mheshimiwa Mabula, jiandae Mheshimiwa Chatanda.

MHE. STANLAUS S. MABULA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nami naomba nitumie fursa hii kukushukuru na kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kupata nafasi ya kuchangia Wizara hii muhimu kwa ajili ya maisha ya Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni ukweli kwamba kazi kubwa inayofanywa na sekta hii au Wizara hii ya Afya inasaidia sana katika kuhakikisha Watanzania wanaendelea kuwa na afya bora, lakini watoto ambao wanazaliwa na wenyewe pia wanazaliwa kwenye mazingira mazuri yanayowafanya na wao wawe watu ambao mwisho wa siku watakuwa sehemu ya watu wa kutegemewa kwenye Taifa hili. *(Makofi)*

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumze mambo manne peke yake. Kwanza nizungumze juu ya upatikanaji wa madawa. Sote tunafahamu Serikali imefanya jitihada kubwa sana hasa katika suala zima la upatikanaji wa dawa. Taarifa iliyosomwa hapa na Mheshimiwa Waziri pia na Kamati inaonesha tumekwenda karibu asilimia 89 kwa mwaka 2017/2018, hii ni hatua moja kubwa sana. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimwombe Mheshimiwa Waziri, bado liko tatizo kule kwenye jamii. Watu wengi sana hawaelewi hizi dawa muhimu tunazozitungumza ni zipi, lakini dawa ambayo inapatikana kwenye zahanati, dawa ambayo inapatikana hospitali ya Wilaya unaweza usiipate kwenye kituo cha afya au kwenye zahanati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa niombe Wizara ichukue jambo hili kama sehemu ya utatuzi na elimu kwa jamii, itengeneze utaratibu kuanzia ngazi ya zahanati, ieleweke mtu anayekwenda kwenye zahanati ziko dawa za aina gani atakazopata, akiwa kituo cha afya atapata dawa ya aina gani na hospitali ya Wilaya atapata dawa ya aina gani, kwa sababu hili linatukumba hata sisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwananchi anaweza kupiga simu yuko kwenye kituo cha afya anasema dawa hii hakuna, lakini ukweli ni kwamba dawa ile wakati ule pale alipo siyo sehemu yake. Sasa hii lazima tujitahidi sana kutoa elimu ya kutosha ili muweze kutusaidia tuepuke matatizo mengi. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunafahamu juhudi kubwa zinazofanya na Serikali bila kuangalia motisha au haki za watumishi kule waliko na wanazozitegemea na zingine siyo kubwa sana Mheshimiwa Waziri. Kwa mfano, nimwombe sana, zile *allowance* za *uniform* zinazopatikana kwa mwaka pia *allowance* za likizo zao, lakini pia *on call allowance*, haya ni mambo ambayo yatatusaidia kuboresha zaidi huduma zetu za kiafya hasa kwa watumishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hawa watumishi ni wengi sana lakini pamoja na kazi kubwa wanayoifanya Mheshimiwa Waziri tunaamini kabisa kwamba tukiwatazama na wao kwa jicho jingine kwamba ni sehemu yetu na kazi hii ni kazi ya wito. Kazi ya wito ukipata stahiki zako ambazo ziko kwa mujibu wa sheria na wewe utaifanya kwa malengo yale yale uliyojiwekea na utakuwa umepiga hatua sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru Mheshimiwa Waziri, kwenye hotuba yake ameonsha moja ya kipaumbele ni kuhakikisha anaboresha miundombinu ya hospitali. Mheshimiwa Waziri hili ni jambo kubwa sana, miundombinu ya hospitali zetu nyingi kwa muda mrefu imekuwa siyo rafiki lakini kwa sasa amejitahidi sana kwa kufanya jambo hili. Hapa nazungumzia kuanzia kwenye ngazi ya zahanati, ngazi ya vituo vya afya lakini hospitali za Wilaya na hospitali za Rufaa za Mikoa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mwanza Jimbo langu la Nyamagana ndipo ilipo hospitali ya Rufaa ya Mkoa hospitali ya Sekou Toure, lakini ndipo ambapo nina hospitali ya Wilaya ya Nyamagana ambayo iko Butimba. Nikianza na hospitali yetu ya Sekou Toure, hospitali hii imekuwa ni hospitali tegemeo lakini imekuwa ni hospitali kubwa ya muda mrefu na nimshukuru sana ameiangalia kwa muda mfupi aliokuwepo hospitali yetu kwa sasa imekuwa bora sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hospitali hizi haziwezi zikaboreka bila kuangalia umuhimu wa watu ambao wamefanya kazi kwenye maeneo haya. Nitumie nafasi hii nimpongeze sana ndugu yangu na rafiki yangu Dkt. Leonard Subi ambaye amekuwa *RMO* pale, lakini nimpongeze Katibu wake Ndugu Temba. Niwapongeze na Waganga wafawidhi mama yangu Onesmo ambaye leo ni mstaafu lakini dada yangu Bahati Msaki ambaye sasa anashikilia nafasi ile.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bila kuficha ni kwamba hospitali hizi pamoja na wataalam tulionao bila kutumia weledi wao na ubora na moyo wao wa dhati wa kujitoa

mazingira ya hospitali haya hayawezi kubadilika. Leo ukienda hospitali ya Sekou Toure ni sawa unazungumza hospitali tofauti kabisa na ilivyokuwa miaka mitatu huko nyuma iliyopita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ni pongezi kubwa kwa watumishi wote, lakini jitihada zinazofanywa na Serikali na utashi wa watu wenyewe waliopeva jukumu hili na nimeambia Dkt. Subi amepanda daraja kidogo. Nimpongeze sana kwa sababu jitihada alizozifanya Sekou Toure anastahili na sifa hiyo anastahili kwenda hapo alipo leo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na maboresho makubwa haya ya hospitali ya Sekou Toure ambayo kwa kweli ni hospitali ya Kanda ya Kimkoa, tunaitegema kwa nguvu nyingi, nimwombe sana liko jambo moja pamoja na ubora huu hospitali hii haina *CT Scan*. Sote tunafahamu tukiongeza *CT Scan* kwa sasa, mapato yaliyoongezeka kutoka shilingi milioni 30 kwa mwezi mpaka milioni 120, leo ukiongeza *CT Scan* utakuwa umeiongezea uwezo mkubwa lakini kingine tuongeze Madaktari bingwa kushughulika matatizo ya kibingwa ili wawepo kwa wingi waweze kusaidia umma wa watu zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ni sambamba na jengo tunalolijenga sasa hivi kwenye hospitali ya Sekou Toure, nimshukuru sana Mheshimiwa Waziri tumepata bilioni moja kwa mwaka huu, imefanya kazi kubwa na Mkoa wa Mwanza ni moja kati ya mikoa nane ambayo kwa kweli imetajwa katika matatizo ya vifo vya mama na mtoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kukamilika kwa jengo hili kwa wakati itakuwa imetusaidia sana kuhakikisha kwamba vifo vya mama na mtoto ambao ni sehemu ya kipaumbele cha Mheshimiwa Waziri, atakuwa ametusaidia lakini atakuwa amesaidia akinamama wa Mkoa wa Mwanza na wale wa mikoa ya jirani kuja kupata huduma hizi kwa kiwango cha hali ya juu, tukiadini mpango huu wa malipo kwa ufanisi utakuwa na tija na utatoa matunda ambayo ni stahiki sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumze juu ya habari ya uboreshaji wa huduma za afya kwenye hospitali zetu za Wilaya. Tunayo hospitali yetu ya Wilaya ya Nyamagana. Hospitali hii ilianza miaka mingi ikiwa kama zahanati ikapandishwa daraja kuwa kituo cha afya na sasa ni hospitali ya Wilaya. Ukweli usiofichika nirudie tena kusema Watumishi hawa Madaktari, Wauguzi na Wakunga wanafanya kazi kubwa sana. Hospitali hii miaka miwili iliyopita kabla hatujawa na dawa za uhakika, kabla hatujawa na uhakika wa kukabiliana na kushughulika na matatizo...

(Hapa kengele illia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante Mheshimiwa kwa mchango wako mzuri, muda wako umekwisha. Mheshimiwa Chatanda, ajiandae Mheshimiwa Mgumba.

MHE. MARY P. CHATANDA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii nami niweze kuchangia katika hotuba aliyotoa Mheshimiwa Waziri wa Afya, ndugu yangu, mdogo wangu Umy Mwalimu. Kwanza nianze kwa kuunga mkono hotuba hii ni nzuri, vilevile niunge mkono mapendekezo yaliyotolewa na Kamati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue nafasi ya kumpongeza Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kama ambavyo wenzangu wamezungumza kwamba anafanya kazi kubwa ya kuhakikisha Watanzania wanakuwa na afya bora. Nimpongeze Waziri, nimpongeze Naibu Waziri, nimpongeze Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu Ndugu yangu mpendwa Dkt. Chaula na Watendaji wote wa Wizara hii ya Afya kwa kazi kubwa na nzuri ambayo inaonekana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue nafasi hii Mheshimiwa Umy nimpe salamu za wanawake wa Mkoa wa Tanga wanasema kwamba wanashukuru kwelikweli kwamba Rais alimteua kuwa kwenye nafasi hii ameitendea haki, amewatoa aibu wanawake wa Mkoa wa Tanga. Kwa

hiyo, wanaendelea kumwombea kwa Mwenyezi Mungu aendelee kutimiza majukumu yake hayo vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitakuwa mchoyo wa fadhila kama sitashukuru kwa sababu sikuchangia katika ile Wizara ya TAMISEMI. Wizara ya TAMISEMI wamenipatia hospitali ya Wilaya ya Korogwe ambayo ilikuwa ni Korogwe Vijijini, nawashukuru sana. Wananchi wa Korogwe Mjini wanawashukuru kweli, lakini vile vile nitakuwa sijamtendea haki kaka yangu Profesa Maji Marefu kwa sababu sisi ni mapacha, kwa kumtengoa fedha bilioni 1.5 ili aweze kujenga hospitali katika Halmashauri yake ya Korogwe Vijijini, tunaishukuru sana Serikali kwa moyo huo wa upendo mliotuonesha katika Wilaya yetu hiyo ya Korogwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kwamba nimepewa hiyo hospitali naomba hospitali ile ni kuu kuu, nitaomba sasa nisaidiwe kupewa fedha kwa ajili ya ukarabati wa hospitali ile. Lile jengo la mbele Mheshimiwa Waziri Umyy Mwalimu analijua linavuwa. Kwa hiyo, naomba wanisaidie fedha kwa ajili ya ukarabati pale watakapokuwa wametukabidhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, matamshi ya humu ndani hayatoshi, niiombe TAMISEMI sasa ituandikie rasmi kutukabidhi ile hospitali ili kuanzia tarehe moja mwezi wa Saba tuweze kuanza kuisimamia Korogwe Mjini. Nitashukuru sana utekelezaji huo utakapokuwa umekamilika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niipongeze Serikali kwa kuweza kuipatia fedha hospitali ya Muhimbili ambapo sasa imeweza kuanza kufanya kazi ya kutoa huduma ya upandikizaji wa figo. Hii imesaidia sana kupunguza gharama za kwenda kutibiwa nje hasa ikizingatiwa hata kwenye taarifa ya CAG imeonesha kwamba tumepeleka wagonjwa wengi India kwenda kwenye matibabu na gharama imekuwa kubwa, lakini kwa utaratibu huu ambao sasa hospitali ya Muhimbili imeanza ya kupandikiza figo, itatupunguzia sana kupeleka wagonjwa nje na gharama zitapungua. *(Makofi)*

Mheshimishiwa Mwenyekiti, nimpungeze sana Dkt. Janabi kwa kazi kubwa anayoifanya na wenzake katika hospitali ile, kile kitengo cha Moyo cha Jakaya Kikwete. Niiombe Serikali, naungana na Kamati kwamba zile bilioni mbili walizokuwa wametengewa tunaomba wawape fedha hizo ili waweze kununua hivyo vifaa tiba, tusipofanya hivyo maana yake tunataka hawa watu sasa wasiendelee kufanya kazi nzuri ambayo tayari imeanza kufanyika. Shida iko wapi? (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hospitali ile inatusaidia kupunguza gharama za kwenda nje. Sasa kama waliomba bilioni mbili inashindikana kuwapa ni kwa nini? Naomba Serikali hebu iwatazameni katika hili, wapewe hizo bilioni mbili ili waweze kununua hivyo vifaa tiba waweze kufanya kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa nizungumzie suala la Chuo cha Uuguzi pale Korogwe. Jambo hili limechukua muda mrefu sana. Chuo cha Uuguzi Korogwe jengo hili limejengwa lina miaka sasa 15 halijawahi kutengewa fedha za kumaliza jengo lile. Mheshimiwa Waziri naomba mniambie leo, kulikoni jengo lile limejengwa mpaka kufikia ile hatua ya kutaka kuanza kupauliwa halitengewi fedha. Fedha na kodi za wananchi zimepotea pale maana yake lile jengo lisipomaliziwa, likianza kuchakaa tutaingia gharama nyingine ya kuanza kutenga fedha kwa ajili ya jengo lile pale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimwombe mdogo wangu Mheshimiwa Ummy alifika aliliona lile jengo, kile chuo kiko pale, watoto wako pale wanasoma, lakini kwa bahati mbaya sana majengo ya utawala hayapo, wamechukua madarasa ya wanafunzi wameweka *partition* zimekuwa ndio ofisi za Walimu, halafu watoto wanaenda kusomea kwenye bwalo la chakula, haiwezekani. Napata mashaka kwa nini fedha haitengwi, inawezekana kwa kipindi hicho ulikuwa ni uchochoro wa kupitisha fedha zile kwenda kuliwa, kama siyo kwa nini fedha hazitengwi kwa ajili ya jengo lile.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitaomba majibu ya kunitosheleza hapa kwa sababu nimeona kwenye kitabu hapa wamezungumzia mipango yao, wamesema wataboresha vyuo vya afya ili kuendeleza uzalishaji wa wataalam, wakavitaja hapo. Sijaona kuzungumzia Chuo cha Uuguzi Korogwe, kuna nini? Mheshimiwa Ummu mdogo wangu nampenda kweli kweli na mimi ndiye mpiganaji wake kwa kura za maoni Mkoa wa Tanga. Katika hili hatutaelewana. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru na naunga mkono hoja.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Mgumba jiandae Mheshimiwa Ngombale na Mheshimiwa Musa Mbarouk.

MHE. OMARY T. MGUMBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kunipa nafasi ili nami nichangie katika mjadala uliokuwa mbele yetu kuhusu hoja hii katika Wizara yetu hii ya Afya. Nimshukuru Mwenyezi Mungu aliyenipa afya na uzima tumeikuta jioni hii ya leo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze na pongezi na shukrani, Wizara ya Afya hii imefanya mambo makubwa sana, hasa katika uimarishaji wa upatikanaji dawa pamoja na uboreshaji wa vituo vya afya nchi nzima. Nitolee mfano kwangu nimepata kituo kimoja pale kwenye Kata yetu ya Mkuyuni, pia tumepata kituo kingine katika halmashauri hiyo hiyo katika eneo la Dutumi, niwapongeze sana kwa hayo yote. Pia tumepata katika mgao unaokuja katika bajeti hii tutengewa 1.5 bilioni kwa sababu ya hospitali ya wilaya, tunaishukuru sana Serikali hasa Wizara ya Afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na mambo mazuri hayo kuna ombi ambalo nataka niombe. Mheshimiwa Waziri wa Afya, pamoja na mambo mazuri anayotufanyia lakini tuna ahadi za Mheshimiwa Rais tangu 2010 kuhusu upatikanaji wa magari ya wagonjwa kwenye Kituo cha Afya Mkuyuni na Kituo cha Afya Kinole; ahadi hizi ni za muda mrefu,

namwomba sana ikiwezekana aziingize ili atupatie turahishe huduma ya afya katika jimbo letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia watumishi wa afya wako wachache; tuna zahanati ambazo tumeshazimaliza, kwa mfano Zahanati ya Bamba, tangu mwaka jana imekwisha, kuna Zahanati ya Tununguo, kuna Zahanati ya Kidugalo, zote hizi tunashindwa kuzifungua kwa sababu ya ukosefu wa watumishi wa afya. Nimwuombe sana atupatie hao watumishi ili tupeleke huduma karibu kwa wananchi wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimepitia kidogo kwa umbali ile ripoti ya *CAG*; nimegundua, kuwa pamoja na kwamba wanafanya juhudi kubwa katika upatikanaji wa dawa lakini Shirika la Dawa la *MSD* linadai zaidi ya bilioni sitini na moja. Niwaombe sana hizi pesa kwa sababu zilikuwa zitolewe na *global fund* na hazijatolewa mpaka leo niwaombe sana Serikali muisaidie *MSD* ili fedha hizi zipatikane ili tuweze kuongeza upatikanaji wa dawa katika hospitali zetu, zahanati na vituo vya afya ili tuweze kuwahudumia wananchi vizuri sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwaombe sana Serikali waisukume hii *MSD*, imekuwa ni msaada mkubwa sana na inatuletea sifa ndani ya nchi na nje ya nchi hasa baada ya kupata ule mkataba wa usambazaji dawa katika nchi za Afrika ya Mashariki pamoja na Kusini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hilo katika ripoti ya *CAG* tumegundua pia kwamba sasa hivi kuna upungufu wa zaidi ya 1.5 *trillion* kwenye ripoti ile. Kwanza lazima nikiri, maana tusije kupotosha kitu ambacho *CAG* amekiweka ni kweli kuna mapungufu ya 1.5 *trillion* haionekani. Hii ni Serikali ya kwetu na tusiposema ukweli tutakuwa hatujaitendea haki, tusipende kona kona wakati jambo ni kweli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kubwa kuliko chote *CAG* ndilo jicho la Wabunge na sisi Wabunge ni wawakilishi wa wananchi. Kwa hiyo anaposema *CAG* anatusemea sisi Wabunge na anawasemea wananchi wote wa Tanzania

kwa sababu ndio wenye mali. Sasa leo *CAG* amezungumza kwamba kuna pesa ambazo hazionekani 1.5 *trillion* halafu sisi wenye mali tukisema tukishabikia tunakosea sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niseme kwa kirefu katika hili kwa sababu ndio umekuwa mjadala kwenye mitandao ya kijamii na kuna upotoshaji mkubwa kwenye hili. Hii ripoti ya *CAG* imekuja hapa Bungeni baada kwanza kukabidhiwa Mheshimiwa Rais pale Ikulu kwa mujibu wa Katiba na Sheria inavyotaka. Kwa hiyo Mheshimiwa Rais kama angetaka isije au angetaka kufanya uchakachujaji wowote angeichakachua siku ile pale Ikulu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulimsikia kwa macho yetu Mheshimiwa Rais akimpongeza *CAG* mwenyewe Profesa kwamba wewe ni mtu mwema, ni mcha Mungu, naamini hukumwonea mtu katika ripoti hii na tutaifanyia kazi. Sasa akitokea mtu mwingine akianza kusema kwamba Rais anakumbatia haijulikani ni upotoshaji

T A A R I F A

MHE. CECIL D. MWAMBE: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

MWENYEKITI: Taarifa.

MHE. CECIL D. MWAMBE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninampa tu taarifa mzungumzaji anaeendelea kwamba, kwenye ripoti hii ukianza ukurasa wa mwanzo mpaka mwisho kabisa taarifa ya *ATCL* pamoja na *TANROADS* hazionekani kwa hiyo aone namna gani...

MWENYEKITI: Kaa chini.

MHE. OMARY T. MGUMBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba unilindie muda wangu na huyu ni ndugu yangu tunaheshimiana sana kwa sababu mimi naongelea taarifa ya 1.5 trilioni yeye anaongelea *ATC* ni vitu viwili tofauti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hilo nilikuwa nazungumza kwamba Mheshimiwa Rais mwenyewe alijipambanua katika vita vya ufasadi na rushwa na kwa namna yoyote ile hawezi kufumbia macho hili na ninavyomjua Mheshimiwa Dokta John Pombe Magufuli na ndio maana aliipokea na aliruhusu ile taarifa ije hapa Bungeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hili tulimwona Mheshimiwa Waziri Mkuu pia akipokea maelekezo kwa Mheshimiwa Rais baada ya kupokea taarifa hii kwamba wataifanyia kazi hasa pamoja na hayo mapungufu, maana yake ukisema unaifanyia kazi na huu upungufu upo lazima wamekubali kuifanyia kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niombe Serikali na niitake Serikali hili jambo si la kupuuza, ni jambo ambalo limezungumzwa na CAG katika ripoti yake ambayo sisi Wabunge na wananchi wa Tanzania ndio jicho letu. Kwa hiyo tunapona 1.5 *trillion* haina maelezo ya kutosha tunapata mashaka. Nimtake Waziri wa Fedha na Serikali kwa ujumla atuletee majibu ya kuridhisha katika hili sio kuanza kupiga kona kona ili kwamba kweli tuone Serikali hii na Mawaziri wanamuunga mkono Rais wetu, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli katika vita hii ya ufasadi na rushwa iliyokuwepo nchini kwetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hakuna namna yoyote lazima tupate majibu ya uhakika, Bunge hili ni moja, katika maendeleo hakuna vyama iwe CCM, iwe CHADEMA, iwe CUF, iwe ACT hakuna mtu anayetaka ufasadi wowote. Tunamtaka Waziri wa Fedha alete hapa majibu ili tuone namna gani na huu ubabaishaji uishe, tumechoka...

MWENYEKITI: Ahsante sana kwa mchango. Mheshimiwa Mbarouk na Mheshimiwa Ngombale kwa pamoja.

MHE. MUSSA B. MBAROUK: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kuniona. Naomba pia nami nichukue fursa hii kwanza kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha

kuchangia katika Wizara hii muhimu kwa maisha ya binadamu. Pia sichelewi kuwashukuru wapiga kura wangu wa Jiji la Tanga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naanza kuipongeza Serikali kwa kuweza kupokea bilioni moja na milioni mia nne kama mpango wa Serikali wa kuboresha vituo vya afya kwa ajili ya mama na mtoto. Labda katika hilo niseme tu kwamba nimepokea milioni mia tano kwa Kituo cha Afya cha Makorora, milioni mia tano kwa Kituo cha Afya cha Mikanjuni, lakini pia milioni mia nne kwa Kituo cha Afya cha Ngamiani, kwa hilo nashukuru. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na shukrani hizi naomba Waziri wa Afya anisikilize kwa makini. Tanga ni Manispaa ya kwanza Tanzania tangu mwaka 1951, lakini mpaka leo miaka 57 baada ya Uhuru hatuna hospitali ya wilaya. Halmashauri tumejitahidi kidogo tukaweza kujenga jengo la *administration block* katika Kata ya Masiwani Shamba, kata mpya ili tuweze angalau kujikongoja tuweze kupata hospitali ya wilaya, lakini bado haijatosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika bajeti ya halmashauri mwaka huu tumetenga takribani shilingi za kitanzania milioni mia tatu. Kwa hiyo namuomba Waziri wa Afya atutafutie angalau bilioni mbili, tukichanganya na milioni mia tatu hizi angalau tunaweza tukapata jengo la *OPD* ili wananchi wetu waweze kupata huduma za hospitali ya wilaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama hilo halitoshi, kuna upungufu mkubwa katika Jiji letu la Tanga katika sekta ya afya. Kuna upungufu wa watumishi, nikiwa na maana ya Wauguzi na Madaktari Bingwa. Kwa hiyo, Waziri napo kama wanavyosema wataalam *the good charity beginning at home*. Sasa naomba atupe upendeleo maalum ahakikishe katika hospitali yetu ya wilaya hiyo ambayo tunakusudia kuijenga tujiandae na Madaktari Bingwa na Wauguzi wa kutosha lakini hili la upungufu wa watumishi limepelekea sasa siku za *weekend* vituo vingi vya afya na zahanati kufungwa saa nane na nusu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili jambo nafikiri Wabunge wenzangu mtakuwa ni mashahidi; huu ni utaratibu ambao upo nchi nzima. Sasa inasababisha wananchi wetu kupata shida. Wananchi wanahoji sisi Watanzania tuna mkataba na Mungu? Kwamba kuumwa mwisho saa nane na nusu? Kama hatuna mkataba huo basi vituo vyetu vya afya na zahanati vifanye kazi masaa 24 ili wananchi wetu waweze kupata huduma bora na huduma ambazo zimekamilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile napenda kuizungumzia Hospitali yetu ya Rufaa ya Bombo. Bombo ni hospitali kongwe nchini Tanzania ambayo ilijengwa na wakoloni na ilikuwa hospitali iliyokamilika idara zote katika wodi na vifaa tiba; vile vile hata katika miundombinu ya lifti. Huu ni takribani mwaka wa nne Bombo hatuna lifti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo namwomba Mheshimiwa Waziri, najua nilifika kwake nikamweleza kwamba kuna utafiti mdogo niliufanya katika kampuni ya lifti inayoitwa *OTC* ya Ufaransa wameeleza kwamba ili tupate lifti mpya za kisasa wanahitaji *Euro* 126,000 ambazo ni takribani shilingi za kitanzania milioni mia nne.

Mheshimiwa Mwenyekiti, najua, kama Serikali itaamua kwa dhati tutaweza kuzipata milioni mia nne kama tulivyoweza kupata fedha za kununulia ndege na mambo mengine. Kwa hiyo, naomba kupitia Bunge hili Mheshimiwa Ummu hata kwa kutafuta wafadhili tuwe tayari kushirikiana lakini tuipe lifti ya Bombo, Tanga. Wananchi wanapata shida, wagonjwa wanaangushwa; mtu anatoka *operation* amebebwa na baunsa. Kuna utaratibu pale, kuna mabaunsa wako *special*, mtu akitoka *operation* kupandishwa ghorofani huko lazima abebwe na mabaunsa familia ilipe. Sasa hii ni aibu kwa nchi yenye rasilimali kama Tanzania kukosa lifti. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo napenda kuzungumzia, Tanga pia kuna ukosefu wa vitu kama *CT Scan*. Hospitali ya Rufaa ya Bombo haina vifaa hivyo; lakini kuna taarifa kwamba Watanzania wenzetu wenye asili

ya kiasia, Mabohora wametoa mashine ya *MRI* kama sikosei na *CT-Scan*, lakini Serikali imeshindwa kujenga jengo la kufitisha mitambo hii. Kwa hiyo nimwombe Mheshimiwa Waziri na Serikali, tusingoje mpaka wale Mabohora Watanzania wenye asili ya Kiasia wakaamua vinginevyo, mashine ile ikapelekwa mji mwingine. Tunaomba mashine ile Serikali iweze kujenga jengo pale ili tuweze kupata faida ya kutumia mashine ile.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ninalotaka kusema pia, nchi za wenzetu kama Kenya wameondoa ushuru katika mashine kama hizo za *MRI*, *CT Scan*, *Ultra Sound* na nyinginezo, hali inayopelekea hiyo huduma gharama yake kuwa ni ndogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitoa mfano mwaka jana na leo nautoa tena. Yupo mtu mmoja wa Tanga alikuwa na mke wake mgonjwa, alimpeleka Dar es Salaam kupata vipimo hivyo na aliambiwa ni laki nane. Jamaa yake wa Kenya alimwita, na alipofika Mombasa ikawa gharama ni sh 12,000 za Kenya, sawasawa na Sh.60,000/= za kitanzania. Kwa hiyo Serikali iondoe kodi katika vifaa tiba hivi kama *MRI*, *CT Scan* na nyinginezo ili gharama za matibabu ziwe nafuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama hilo halitoshi Madaktari Bingwa wa mifupa na vichwa kwa Tanga bado tuna tatizo kubwa. Kama tunavyojua kwamba watumiaji wa boda boda na vyombo vya usafiri wa miguu miwili ni wengi na kwa hiyo ajali ni nyingi. Anapoumia mtu lazima akimbizwe *MOI* Dar es Salaam au apelekwe *KCMC* Moshi na kwa sababu hiyo gharama zinakuwa kubwa. Hata hivyo, kama Serikali kupitia Wizara ya Afya itatuletea Madaktari Bingwa wa mifupa na vichwa pamoja na magonjwa ya akinamama tutaweza kuhudumia watu wetu pale Tanga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni kuhusu taulo za akinamama. Nilizungumza juzi kwamba juzi Rais Uhuru Kenyatta alisaini sheria kwamba Serikali ya Kenya itawapatia bure taulo za kike wanafunzi wote wa Kenya. Sasa nikitazama Kenya hawana rasilimali nyingi kama Tanzania, wao waweze

wana nini na sisi tushindwe tuna nini? Kama tumeweza kununua *Bombadier* tunawezaje kushindwa kugawa taulo za kike kwa wanafunzi wetu nchini Tanzania? Mheshimiwa Waziri naomba hili ulifanyie kazi, ikibidi na sisi Tanzania isainiwe sheria kwamba wanafunzi wote wa kike wapewe taulo za kike *free, no charge*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni wenzetu hawa wa Tanzania ambao wana upungufu wa akili au vichaa. Hawa nao katika maendeleo ya jamii ni jamii ya Watanzania, wao wananufaika vipi na pato la Taifa? Nashauri Serikali itenge fedha na kuipeleka katika kila halmashauri ili wenzetu hawa ambao wana upungufu wa akili waweze kusaidiwa. Leo mtu mzima mwenye upungufu wa akili anatembea uchi wa nyama *bus stand*, sokoni na watu hawajali, huu ni...

(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante Mheshimiwa Mbarouk. Mheshimiwa Ngombale, jiandae Mheshimiwa Tunza Malapa.

MHE. VEDASTUS E. NGOMBALE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi nami nitoe mchango wangu kwa Wizara hii ambayo inahusiana na afya ya Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote nianze kwa kutoa pongezi kwa Serikali kwa kutuwezesha kwa kutupa fedha katika Kituo cha Afya cha Kilwa Masoko shilingi milioni mia tano, Kituo cha Afya Pande, Kituo cha Afya Tindi shilingi milioni mia nne pamoja na *ambulance*. Tunashukuru sana kwa hilo, lakini pia tunaomba tupate pesa kwa ajili ya Kituo cha Afya Njinjo ili basi huduma ya afya iweze kwenda sawasawa katika Halmashauri ya Wilaya ya Kilwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze na suala zima la sera ya huduma bure kwa akinamama wajawazito pamoja na watoto walio chini ya miaka mitano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la sera ya huduma bure kwa akinamama wajawazito pamoja na watoto chini ya miaka mitano. Ni sera inatekelezwa, lakini bado ina changamoto kubwa. Kuna changamoto kubwa kwamba bado huduma hii haitolewi ipasavyo, bado akinamama wanahitajika wajandae kwa vifaa kwa ajili ya kwenda kujifungua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, limezungumzwa suala la *delivery kit*, naomba suala hili liwe wazi, elimu itolewe, wananchi wafahamu stahili yao kutokana na huduma hii, kama linachangiwa au linatolewa bure ili basi kila mwananchi aweze kupata huduma hii ipasavyo. Kwa hali iliyopo sasa suala hili ni kama limejifichaficha na akinamama wetu kule wanalazimika kuagizwa viwembe, mipira, wanaagizwa kanga; kumekuwa na vurugu na Serikali bado haijaweza kutatua tatizo hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia nizungumze, kwangu kuna hospitali ya *mission*. Serikali imeingia mkataba na Hospitali ya *St. Mark's* Kipatimu pale na kwa hivyo, akinamama wanatakiwa wapate huduma hii bure, lakini kumekuwa na changamoto katika hospitali hii na hasa pale Serikali inapochelewesha kupeleka pesa katika ule Mfuko wa *Basket Fund*. Uongozi wa hospitali ukiona Serikali imechelewa kupeleka fedha pale, wanachokifanya ni kuwatoza akinamama wajawazito gharama hizi za kujifungua. Kwa hiyo, hii sera ya utekelezaji huduma bure kwa akinamama wajawazito ni kama haieleweki kwetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kila nilipojaribu kuona sasa baada ya kuwa wamepata hizi pesa wanawezaje kuwarudishia wale akinamama pesa zao, inakuwa ngumu, nimefuatilia mara nyingi, lakini majibu hayajapatikana. Ninao ushahidi wa *receipts* ambazo wamelipa. Kwa hiyo, ninaomba ulisimamie hili, ili basi wananchi wapate haki zao, kwa sababu ni sera kwamba, huduma ya mama mjamzito na mtoto ni bure, lakini pale pana changamoto kubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia, katika ule mkataba tunaomba tupate maelekezo ya gharama za huduma zinazotolewa na hospitali hizi. Gharama zimekuwa za juu mno, tupate maelezo tufahamu sasa kwamba, gharama wanazotakiwa kutoa hospitali binafsi ni zipi; gharama zimekuwa juu mno kiasi kwamba wananchi wetu wanashindwa ku-*afford*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba Wizara ya Afya ilifuatilie hili kwa sababu, wananchi wanapata shida katika suala zima la gharama za matibabu katika eneo langu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala la tatizo la maji katika Hospitali ya Wilaya ya Kinyonga, pale Kivinje. Hospitali yetu ya Wilaya ya Kilwa ina tatizo la maji. Mpaka leo wagonjwa wakienda pale suala zima la maji ni kizungumkuti. Kwa hiyo, tunaomba Wizara iliangalie tatizo hili na ilitatue haraka iwezekanavyo kwa sababu, pamekuwa na mashaka ya upatikanaji wa maji katika Hospitali ya Kilwa Kivinje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala la ujenzi wa vituo vya afya pamoja na ujenzi wa zahanati. Wananchi katika jimbo langu wamejitahidi kujitolea kujenga zahanati, lakini mpaka sasa zile zahanati zimeisha, lakini bado hazijafunguliwa. Kuna Zahanati za Pungutini, Miyumbu, Marendego, Kipindimbi, Nambondo pamoja na Ongwe. Hizi zahanati zimekamilika kwa nguvu za wananchi lakini mpaka sasa hazijafunguliwa. Tuiombe Serikali ijitahidi kuhakikisha kwamba zahanati hizi zifunguliwe ili wananchi wetu waweze kupata huduma ipasavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala la huduma bure kwa wazee. Ni sera ya Serikali kwamba wazee sasa wapate huduma bure, lakini suala hili ni kama halijasimamiwa ipasavyo. Kule kwangu mpaka sasa haieleweki kuna taratibu gani kwa hawa wazee kupata ile huduma. Ilitokea mara moja tu Mkurugenzi alitoa tangazo kwamba wazee wajiandikishe ili waweze kupata utaratibu wa kuweza kupata hizo huduma bure. Hata hivyo, mpaka sasa ni wazee

wachache sana wamesajiliwa katika utaratibu ule. Tuombe Serikali itoe elimu zaidi ya namna gani wazee wetu watatibiwa bure, suala hili ni muhimu na ni suala la kiseru.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la walemavu. Ndugu yangu Mheshimiwa Mussa hapa amezungumza, nami nimekuwa nikilizungumza mara nyingi. Serikali bado haijaliona kwa kina suala la mahitaji maalum kwa walemavu. Kwa mfano katika Wilaya yangu ya Kilwa, katika Jimbo langu la Kilwa Kaskazini, takribani walemavu wa ngozi 15 tullazimika kuwapeleka *Ocean Road* kwa ajili ya kupata matibabu ya mionzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sababu ya kupata hayo matatizo ya ngozi ni kutokana na kukosa hitaji lao maalum la kupata mafuta ya kuwakinga dhidi ya athari ya miale ya mwanga. Tumekuwa tukisema mara nyingi, kama Serikali imeweza kuhudumia mama mjamzito na mtoto wa miaka mitano kwa nini isiweze kutoa mafuta bure kwa walemavu wa ngozi? Hawa walemavu wa ngozi wanaishi katika maisha ya kawaida kabisa na wakati mwingine hawajui hii bidhaa inapatikana wapi? Hili ni lazima lionwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini sio hilo tu, sisi sote ni walemavu watarajiwa, lakini mpaka leo Serikali bado hospitali zinazohusika na kutoa viungo bandia zinatoa kwa gharama ya juu mno. Leo ukitaka mguu bandia lazima uwe na milioni tatu, ni hela nyingi kwa mlemavu na hatuwezi kujua mlemavu ni nani? Sijui Serikali inalionaje suala hili? Suala la walemavu, ni asilimia ngapi walemavu katika nchi hii? Kwa nini mahitaji yao maalum yasitolewe bure? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuwa mlemavu si suala la kuchagua, kama tunatoa huduma kwa mama wajawazito, tutoe huduma kwa walemavu. Kuwa kipofu, kuwa kiziwi au kuwa mlemavu wa ngozi si suala la kuchagua. Mahitaji maalum kutokana na ulemavu wao ni suala ambalo Serikali inatakiwa ilianganalie, sasa nashangaa kwamba leo tuna walemavu wa ngozi tunawapeleka *Ocean Road* tena kwa

kuchangishana ilhali Serikali ipo. Serikali ifanye sensa ya walemavu wa ngozi, vile vile Serikali itoe huduma ya mafuta haya bure.

Mheshimiwa Mwenyekiti...

(Hapa kengele illia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante Mheshimiwa kwa mchango wako. Mheshimiwa Tunza, wajiandae Mheshimiwa Kunchela na Mheshimiwa Yosepha Komba.

MHE. TUNZA I. MALAPO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miongoni mwa pesa nyingi za dawa zinapotea kwa ajili ya kununulia dawa za malaria. Wakati tuko kwenye Kamati tumefika Kibaha kwenye kiwanda kinachozalisha dawa za viuadudu, viluilui wa mbu, lakini kusema ukweli tumekuta hakuna jitihada za makusudi za kutangaza dawa ile ili watu waweze kuitumia na kuua yale mazalia ya mbu, ili watu wasing'atwe na mbu na kupata ugonjwa wa malaria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo namshauri Mheshimiwa Waziri watilie maanani utumiaji wa dawa hii kwa ajili ya kuua hivi vimelea, ili pesa ya kununua dawa za malaria ipungue na tufanye mambo mengine katika sekta ya afya kwa sababu, ina mambo mengi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Hospitali ya Kanda ya Kusini, wenzangu wengi wameongea na mimi naomba niongee. Sisi tumechoka, tumechoka kwa sababu kila siku tunaongea. Safari hii imetengwa bilioni moja, bilioni moja ni pesa ndogo lakini tunaomba hiyo hiyo ndogo iende. Maana hapa tunaongea ndogo, lakini hatimaye hata hii ndogo haiendi. Mmetutengea bilioni moja kwa mwaka huu wa fedha unaokuja, tunaomba hii pesa iende, ili ikaweze kujenga hospitali ile na sisi tupate huduma za afya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Hospitali ya Rufaa ya Mkoa ya Ligula. Ukifika pale ni masikitiko makubwa, mvua hizi za masika zinaponyesha jengo la *OPD* linavuja. Vile vile *theatre* yetu ya Hospitali ya Mkoa wa Ligula inahitaji matengenezo makubwa. Kama mwenzangu alivyosema *X-Ray*mbovu, jengo lenyewe linahitaji ukarabati mkubwa. Kwa mwezi *OC* inakwenda shilingi milioni ishirini na tano, ni ndogo, hospitali ile inatoa huduma ya watu wengi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama hivi tunavyosema hatuna hospitali ya kanda, tunategemea hiyo hospitali ihudumie watu wengi, lakini mazingira yake ni magumu, mazingira yake ni duni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri Mkuu alikwenda pale Machi, 2016 palikuwa na matatizo. Madaktari 13 wakahamishwa, tangu Machi, 2016 mpaka leo ninapongea hata daktari mmoja hajaletwa. Tunatarajia hawa waliopo wafanye kazi kwa kiwango kipi? Hawa wahudumu wenyewe wa pale wana madeni, mpaka sasa hivi wanadai si chini ya milioni mia tano na kuendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo sisi watu wa Kusini, sisi watu wa Mkoa wa Mtwara pia tunahitaji huduma bora za afya. Tunaomba waone kwamba kule kuna watu ambao wanahitaji huduma bora. Tuna korosho tunachangia pato kubwa la Taifa hili; kwa hiyo nasi pia tunahitaji tupate huduma, si kwamba kila siku tukiingia humu tunaongea yanawekwa kwenye vitabu wanafunika, tukirudi kwenye bajeti nyingine mambo ni yaleyale, kitu kama hicho hatukipendi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye ile hospitali, tunaisemea hii hospitali kwa sababu kama unakuja Mkoa wa Mtwara huwezi kuacha kuongelea Hospitali ya Ligula. Ni hospitali tunayotaraji iwe na mazingira mazuri kwa ajili ya kuwahudumia watu. Tukienda kwenye wodi ya wazazi majanga, wodi ni ndogo, watu wanarundikana, hospitali mmesema ya rufaa ya mkoa, lakini inatoa huduma utasema

labda ni hospitali ya wilaya. Watumishi wana madai mengi, watumishi wako asilimia 39 tu, maana unapohitaji watumishi 10 wewe unao wanne tu, tunategemea watafanya kazi katika mazingira gani? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaposema Wizara inahusika na watoto pia tunajua ina wajibu wa kulinda haki zao. Leo watoto wanadhaliishwa kwenye vyombo vya habari, wanadhaliishwa kwenye mitandao ya kijamii; mtoto ametelekezwa na mzazi wake, pata picha kama ni mwanao wewe kesho anaambiwa na wenzie shuleni; wewe baba yako alikutelekeza; hivi kweli huyo mtoto ataweza kujifunza? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tusifanye vitu *just for* kwa ajili ya *show up*, tuonekane...

MHE. ALLY K. MOHAMED: Taarifa.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Kessy, muda wetu kusema kweli, umebaki muda mdogo sana.

MHE. ALLY K. MOHAMED: ... watu wanatelekeza watoto, kuna wengine wanawatupa mpaka chooni.

MWENYEKITI: Endelea.

MHE. TUNZA I. MALAPO: Mheshimiwa Mwenyekiti, mtoto yule tunampa athari ya kisaikolojia. Mimi ni Mwalimu najua mtoto hawezi kujifunza vizuri.

(Hapa kengele illia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante, Mheshimiwa Kunchela, Mheshimiwa Yosepher Komba.

MHE. RHODA E. KUNCHELA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi nami nichangie kidogo kwenye Wizara hii. Nataka niseme tu...

MWENYEKITI: Dakika tano.

MHE. RHODA E. KUNCHELA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Nataka niseme kwamba, bajeti ya dawa kwenye Wizara hii imechukua sehemu kubwa ya bajeti nzima. Kwa hiyo inaonesha kabisa kwamba kwa kuchukua bajeti hii kubwa ya dawa, kwamba Serikali hii imejipanga kutibu zaidi watu kuliko kuwapa kinga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini niongelee kidogo kuhusiana na Mkoa wangu wa Katavi. Mkoa wa Katavi sasa hivi sisi ni vinara kwa watoto wadogo wa kike wanapata mimba za utotoni kwa zaidi ya asilimia 36.8. Kwa hiyo ningeomba Mheshimiwa Waziri atakapokuja kuhitimisha atueleze kwamba, kama Wizara na Serikali kwa ujumla wana mkakati gani wa kuhakikisha hawa vijana au watoto wadogo wa kike wanapata elimu ya uzazi wa mpango, ili tupunguze hili janga katika Mkoa wetu wa Katavi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa takwimu tu, watoto wa kike wsichana 624 ambao wako chini ya umri wa miaka 18 kwa mwaka wanajifungua katika hospitali zile zile zilizopo katika Mkoa wetu wa Katavi, hatuna hospitali ya mkoa, tuna hospitali ya wilaya na hizi zahanati ndogo ndogo. Hata hivyo pia zahanati hizi pamoja na hospitali ya wilaya zimekuwa zikibeba mzigo mkubwa. Upungufu wa watumishi unasababisha watumishi hawa kufanya kazi wana-*over late*, wanafanya kazi na malipo yao pia, bado wanawacheleweshea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nimwombe Mheshimiwa Waziri kwa kuangalia uzito wa jambo hili, mimba za watoto katika Mkoa wetu wa Katavi limekuwa ni tatizo kubwa na watumishi pamoja na Madaktari, Wauguzi, pamoja na Manesi wanafanya kazi kubwa sana. Hakuna wodi za kutosha; akinamama wanalala wawili wawili kwenye vitanda. Kwa kupitia hii Serikali ya viwanda sasa wajipange na si kupeleka tu pesa kwenye mambo yasiyo na msingi, waangalie vipaumbele vya Watanzania kwa ujumla wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la ujenzi wa hospitali ya mkoa. Kama nilivyosema na nimekuwa nikiongelea sana jambo hili. Pesa ilitengwa zaidi ya bilioni moja, lakini mpaka sasa hivi haieleweki zile pesa ziko wapi. Kwa hiyo, tunaomba kupitia Wizara jambo hili hebu likae wazi, pesa hizi zirudishwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkurugenzi huyu, Mchina aliyehusika kupiga hizi pesa pamoja na Baraza la Madiwani lililopita waeleze pesa hizi ziko wapi, kwa sababu wanawapa mzigo watu wa Mkoa wa Katavi wanasafiri kutoka Mpanda kwenda Mbeya kufuata huduma kwenye hospitali za rufaa. Kwa hiyo, watu hawa wasiendeele kuwapa matatizo watu wa Mkoa wa Katavi, watu wanatumia gharama kubwa, wanasafiri siku nyingi kufuata huduma za rufaa katika Mkoa wa Mbeya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nijue tu Serikali wamejipangaje, kwa sababu takwimu zinaonesha kwamba afya ya akili kupitia Hospitali yetu ya Mileembe, wagonjwa wanaongezeka kwenye hospitali hiyo. Sasa kama Serikali wamefanya utafiti gani kuona kwamba kwa nini Watanzania wengi kupitia haya magonjwa ya akili wanaongezeka katika Hospitali ya Mileembe?

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini Tanzania pia, ni nchi ya tatu ambayo inaongoza kwa udumavu na ni nchi ya 10 inayoongoza kwa udumavu uliokithiri. Sasa ningeeomba tu, kwamba kwa takwimu hizi tukielekea kwenye Serikali ya viwanda na tunategemea kwamba hawa ni watoto, maana yake watakwenda shuleni tunakwenda kuzalisha watoto ambao watakuwa na utapiamlo, watoto ambao watakuwa na udumavu wa akili, hawatapata elimu ya kutosha. Sasa hiyo Serikali ya Viwanda bila kuwekeza kwenye elimu kupitia hawa watoto kupata lishe bora tunakwenda kutengeneza Taifa la namna gani? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini...

(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante, dakika tano zako zimekwisha. Mheshimiwa Yosepher Komba dakika tano.

MHE. YOSEPHER F. KOMBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Nami nianze kwa kumkumbusha dada yangu Mheshimiwa Umy Mwalimu, Mbunge mwenzangu wa Mkoa wa Tanga, mwaka 2016/2017 kwenye bajeti aliahidi katika Wilaya ya Muheza, Hospitali Teule ametenga milioni 20 kwa ajili ya gari la wagonjwa, lakini mpaka hivi ninavyoongea halijafika. Sasa ningepomba atakapokuwa anahitimisha atuambie hilo gari limekwamia wapi kwa sababu Wilaya ya Muheza Teule tuna shida kubwa sana ya gari la wagonjwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini si hilo tu kwenye Wilaya ya Muheza, kuna upungufu wa watumishi wasiopungua 117 katika Wilaya ya Muheza, lakini pia kuna upungufu mkubwa wa dawa na vifaa tiba. Tuna tatizo kubwa la dawa kuwa ghali, hasa dawa ya nyoka na dawa ya mbwa. Wananchi wanaopata matatizo haya wamekuwa wakitibiwa kwa sindano moja Sh.250,000 ya nyoka na inatakiwa sindano tatu na kama hauna kunakuwa hakuna msamaha katika hilo. Wameshapoteza maisha wananchi wasiopungua watano katika Hospitali Teule kwa sababu ya tatizo hili la kuumwa na nyoka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimwombe Mheshimiwa Waziri alione hili kama ni ajali kama ajali nyingine. Wananchi ambao wanapata tatizo la kuumwa na nyoka au na mbwa wawe wanatibiwa bure kwa sababu wanakuwa hawajajiandaa na hili tatizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine napenda kuongelea haki na maendeleo ya watoto. Tunajua watoto wana haki zao, tunajua watoto wanatakiwa watunzwe mpaka kufikia umri fulani ambao wanaweza kujitambua. Haki ya kwanza ni haki ya kiliniki. Tumeshuhudia na kama Waziri na Wizara yake wafanye utafiti waone, watoto wengi wanapoachishwa kunyonyeshwa kati ya miaka miwili mpaka miwili na nusu wanakosa haki ya kuendelea na kiliniki. Watoto wengi wanabaki nyumbani wakati Sheria ya Afya inataka

waende kiliniki mpaka miaka mitano. Kwa hiyo nimwombe Waziri kupitia Wizara yake waandae mkakati wa kufumbua hili suala. Watoto wengi wanabakia nyumbani kati ya miaka miwili na mitano wanapata magonjwa ambayo mwisho wa siku yanawasumbua kutibika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini haki nyingine ya watoto hawa ni makao na vituo kwa wale ambao wamekosa malezi ya wazazi wao. Nimeangalia takwimu za kwenye taarifa yako ya leo, kuna vituo 157, kituo kimoja tu ndicho kinamilikiwa na Serikali. Kwa hiyo wanataka kusema Serikali hawako *serious* na hili suala? Kama wanawaachia watu binafsi ndio wawe wanahangaika na watoto ambao wanatelekezwa, watoto wenye matatizo kwenye jamii, Serikali wana kituo kimoja tu kiko Kurasini, vituo 156 vinamilikiwa na watu binafsi. Hata hivyo, hawa watu binafsi hawawapi nafasi ya kutosha na kuwa-*support* ili waweze kuanzisha hivi vituo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, utaratibu wa kusajili vituo vya watoto yatima na watoto wenye mahitaji ni mgumu kwa watu binafsi, ni mgumu sana. Una mahitaji mengi sana kiasi kwamba mwenye nia anaishia njiani. Kwa hiyo niombe haki hizo za watoto zizingatiwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala lingine nataka kuongelea hapa. Sisi katika Wilaya ya Muheza tuna ujenzi wa hospitali ya wilaya katika Kata ya Lusanga, wananchi mpaka dakika hii wamejitoa kwa nguvu zao na mali zao kwa kiasi kikubwa, tuna michango ya kila kata kwa ajili ya hii hospitali. Tumeona imetengwa *1.5 billion, its ok*, tunaomba kutenga huku kusiishie kwenye kitabu. Tunaomba hizi hela zifike Muheza tukajenge hospitali ya wilaya kwa sababu hospitali tuliyokuwa nayo tunachangia na kanisa lakini pia bado haikidhi mahitaji. Kwa hiyo niombe 1.5 ifike kwa wakati isije ikapotelea njiani kama vile ambavyo tunatafuta *1.5 trillion* kwa sasa hivi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ninalotaka kuzungumzia, tunao ujenzi wa Chuo cha Utafiti kule Amani,

ilizungumzwa sana na viongozi wameahidi sana kipindi cha kampeni lakini mpaka sasa hivi na nimepitia humu sijaona chochote ambacho kimetengwa kwa ajili ya ujenzi wa hiki Chuo cha Utafiti wa Magonjwa ya Binadamu. Tunayo *NIMR* iko kule lakini bado inashindwa kufanya kazi inavyotakiwa kwa sababu ya ufinyu wa maeneo. Waliahidi watajenga chuo kingine, tunaomba hilo suala Mheshimiwa Waziri atakuja kuniambia ni lini wtaanzisha ujenzi wa hiki chuo kwa sababu tunakihitaji sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lipo suala lingine; kuna kituo cha wakoma narudi tena, Kituo cha Wakoma kule Tononoka Ngomeni. Ugonjwa ambao unaanza kuonekana kama vile haupo lakini unazidi kukithiri, ugonjwa ambao dalili zake zinaonekana kuanzia miaka mitatu mpaka thelathini, ugonjwa ambao ukikupata unapata ulemavu wa viungo unapata na upofu, ugonjwa ambao unaongoza kwa kutengwa na jamii. Tunacho kituo kule kina hali mbaya kina wazee, kina wanawake, kina watoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunamwomba Mheshimiwa Waziri na Wizara yake, kwanza, wale wanawake wanahitaji kuinuliwa kiuchumi, lakini pili, wale watoto wanahitaji kupata mahitaji yao ya muhimu ya afya, tatu, wale wagonjwa wanahitaji kupata tiba na huduma zingine za afya, kwa wakati na kwa usahihi, lakini lishe ni tatizo na matatizo mengine naomba ni...*(Makofi)*

(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante. Waheshimiwa tunaendelea na Mheshimiwa Benardetha Mushashu, wajiandae Mheshimiwa Sikudhani Chikambo, Mheshimiwa Esther Midimu na Mheshimiwa Hussein Nassor Amar.

MBUNGE FULANI: Mtoto wangu uko vizuri.

MHE. YOSEPHER F. KOMBA: Ahsante.

MHE. BENARDETHA K. MUSHASHU: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kunipa nafasi ili niweze kuchangia kwenye bajeti hii. Kwanza kabisa napenda nimpongeze Mheshimiwa Waziri, Ummu Mwalimu; Naibu Waziri, Dkt. Faustine Ndugulile; Katibu Mkuu, Dkt. Mpoki kwa hotuba nzuri ya bajeti, lakini vile vile kwa kazi nzuri wanayoifanya katika Wizara hii na katika sekta ya afya, kwa kweli nafasi walizopewa wanazitendea haki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile nampongeza Mheshimiwa Rais kwa kuonesha nia ya dhati ya kuiendeleza na kuiboresha sekta ya afya lakini pamoja na kazi zingine nzuri anazoendelea kufanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naendelea kupongeza kwa sababu kuna mambo makubwa yamefanyika katika Wizara hii. Kwanza, tumesikia hapa wanavyotuambia kwamba sasa hivi wanatoa chanjo dhidi ya kirusi cha *papilloma (papillomavirus)* ambacho kinasababisha saratani ya shingo ya kizazi kwa wasichana wa miaka 14. Hiki kitu kilikuwa hakijawahi kutokea Tanzania hongereni sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, nakumbuka mwaka jana kulikuwa na makelele mengi na hasa mwaka juu, juu ya kwamba hakuna dawa. Sasa hivi upatikanaji wa dawa umepanda mpaka asilimia 80 hadi asilimia 90, hongereni sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawapongeza kwa kusambaza *ambulance* nyingi katika vituo vingi kuliko miaka mingine yoyote ile. Nipende kuwapongeza sana Muhimbili, nampongeza Mkurugenzi wa Muhimbili, Dkt. Maseru kwa kazi nzuri ameirudisha Muhimbili kwenye *chart*, watu walikuwa wameshaikimbia, sasa hivi huduma zimekuwa nzuri kila mtu anataka kuja kutibiwa Muhimbili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nawapongeza watu wa *MOI*, Mkurugenzi wa *MOI* pamoja na watalaam wake wote. Sasa hivi wanafanya *operation* za magoti, za nyonga, lakini vile vile wameweza kufanya *operation* ya mgongo kwa njia

ya matundu (*laparoscopy*) kwa mara ya kwanza ndani ya Tanzania, hongereni sana kumbe wataalam wetu wanaweza. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nipende kumpongeza Mkurugenzi wa Taasisi ya Moyo, Profesa Janabi kwa kazi kubwa sana ambayo anaifanya. Tunakumbuka watoto wengi walikuwa wanapelekwa nje ili kuzibwa matundu yaliyo kwenye moyo, wao wanafanya sasa hivi. Betri maalum *pacemaker* zinawekwa kwenye moyo. Wameweza kufanya upasuaji wa mishipa kwa kutumia *lazer*, nilikuwa naisoma kwenye vitabu kumbe sasa hivi inafanyika Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile wameweza kufanya upasuaji wa moyo wakapandikiza mishipa bila kusimamisha moyo, kwa kweli wanastahili heko, hongereni sana. Mwisho wameweza kupandikiza hata na figo, kwa kufanya hivyo wameokoa pesa nyingi za kitanzania ambazo tungeweza kutumia kwa kwenda kutibiwa nje. Nipende kumkumbusha Mheshimiwa Waziri, kwamba watu wanaofanya vizuri namna hii haiwezekani bajeti yao ikapungua; sasa naomba waongezewe bajeti, waongezewe fedha, kusudi waweze kufanya makubwa zaidi ya hayo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na mambo mazuri yanayofanyika lakini bado kuna upungufu mkubwa wa watumishi na nafikiri huu umesababishwa kwa sababu utoaji wa huduma za afya umepanuka. Tumeongezea vituo vya afya, tumeongeza zahanati, tumeongeza hospitali, *obviously* lazima watumishi wapungue.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba sasa kwa kuwa kuna upungufu ni kilio cha kila mtu Serikali waliangalie kwa jicho la zaidi, kwa sababu hata kwenye hospitali tunazoiita hospitali maalum kama ya Benjamin Mkapa ambayo ina vifaa vingi vizuri vya kila aina lakini bado kuna upungufu wa watumishi. Ukienda kwenye hospitali za Kanda kama Bugando nayo unakuta kuna upungufu wa watumishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawashukuru sana Bugando ni Hospitali ya Rufaa kwa Kanda ya Ziwa. Mikoa yoyote ya kanda ya ziwa tunategemea Bugando. Tunawashukuru kwa kutuletea hata kituo cha kansa pale. Hata hivyo ukienda hasa upande wa *chemotherapy* unakuta kwamba hakuna wataalam. Tunaomba aidha wawapelekee wataalam wa kutosha au wale waliopo basi waweze kuwa-*train* kusudi watu wanaotoka Kanda ya Ziwa waweze kupata huduma za afya zilizoboreka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukienda kwenye Mkoa wa Kagera kuna upungufu mkubwa sana wa watumishi wa afya. Kati ya watumishi 6,245 wanaohitajika tuna 2,575 tu; kwa kweli ni upungufu mkubwa sana. Hata ukiangalia kitaifa upungufu wa watumishi ni asilimia 48; hii ni hatari kwa sababu pamoja na kupeleka dawa; tunasema dawa ziko kule kwa asilimia mpaka 90 kama hakuna daktari wa kuandika, hakuna muuguzi wa kuitoa hiyo dawa, kwa hiyo ina maana kwamba tutakuwa tumefanya kazi bure.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili tusije tukaharibu kazi nzuri tunayofanya basi naomba, kwa kuwa tunajua wapo Madaktari wengi mitaani ambao tayari wako *trained* lakini hawajaajiriwa na kwa kuwa juzi Mheshimiwa Mkuchika ametutangazia kwamba sasa kuna mafuriko ya ajira. Ajira zaidi ya elfu arobaini zitatolewa, tunaomba vibali vitolewe vingi kwa ajili ya sekta ya afya ili watu wetu waweze kunanii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini vile vile niwaombe waendeleo kuwa-*train* wale Madaktari Bingwa ili waweze kutoa tabibu za kibingwa katika hospitali zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkoa wa Kagera uko pembezoni...

(Hapa kengele ya kwanza ililia)

MHE. BENARDETHA K. MUSHASHU: Mheshimiwa Mwenyekiti, Hospitali ya Rufaa ya Bukoba ina Wataalam watatu tu, wa meno, akinamama na mama wajawazito.

Hata hivyo, kama mtu ni mahututi lazima akimbizwe kwenda mpaka Bugando Mwanza. Anatumia masaa nane mpaka 10 wakati *ambulance* waliyokuwa nayo ni mbovu, *spare* hamna. Mheshimiwa Ummy nimeshampelekea hilo tatizo, Mheshimiwa Waziri Mkuu nilishamwambia, naomba kujua je, katika hii bajeti wataweza kutupatia hii *ambulance* kusudi tuweze kuondoa hizo kero. (*Makofi/vicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkoa wa Kagera unahitaji hospitali nane za wilaya lakini tunazo mbili tu, kwa hiyo tulikuwa tunaomba, kwa sababu sasa hivi kila mtu anataka kwenda kutibiwa kwenye Hospitali ya Serikali.; tunaomba sasa tupatiwe Hospitali ya Serikali ya Wilaya ya Biharamulo, Hospitali ya Bukoba Vijijini, Hospitali ya Karagwe, Hospitali ya Wilaya ya Kyerwa, Hospitali ya Wilaya ya Missenyi na Hospitali ya Wilaya ya Muleba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza Serikali kwa kutoa hela za kukarabati vituo ambapo walikuwa wanatoa kati ya milioni mia nne mpaka mia tano. Kwa bahati mbaya Manispaa ya Bukoba hawajapata fedha hizo. Tunaomba na Manispaa ya Bukoba waweze kupatiwa hizo fedha milioni mia nne mpaka mia tano ili waweze kukarabati hivyo vituo vya afya na hii itawasaidia kutoa huduma bora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho ni bima ya afya. Bima ya afya ni muhimu sana ndugu zangu. Matibabu ni gharama mpende msipende, kuna siku utaugua huna hata senti tano ndani ya nyumba, lakini unaweza kwenda hospitali wakakwambia vipimo vinaenda mpaka laki nne mpaka laki tano. Unaweza ukaambiwa kuna *operation* ambapo inaenda mpaka milioni, huna hata senti tano utafanyaje. Kama tungekuwa kwenye mfumo wa bima ina maana tunabebana mchango wako, mchango wa huyu unampeleka yule na wewe ikiwa zamu yako unapelekwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia watu walio kwenye mfumo wa bima ya afya sasa hivi ni asilimia 32 tu, kwa hiyo napendekeza kwamba sasa Wizara ya Afya mfanye mtakachoweza kufanya, mfanye uhamasishaji mkubwa huko

vijijini watu wengi waweze kujua umuhimu wa bima ya afya kama walivyosema kwamba wanaleta *universal health coverage*; kusudi kila mtu aweze kuingia kwenye mfumo wa afya na tuweze kutoa afya bora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa, naendelea kuwapongeza kwa kazi nzuri wanayo... *(Makofi)*

(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MHE. BERNADETHA K. MUSHASHU: Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Chikambo, ajjandae Mheshimiwa Midimu.

MHE. SIKUDHANI Y. CHIKAMBO: Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote kwanza napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu aliyenijalia leo kusimama katika Bunge lako hili kupata fursa ya kuchangia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kumshukuru Mwenyezi Mungu naomba pia niwashukuru akinamama wenzangu walioniwezesha kuingia katika Bunge hili, naahidi kuendelea kushirikiana nao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri, dada yangu Umy, Naibu Waziri pamoja na watendaji wote wa Wizara. Nawapongeza hawa nafahamu sana umuhimu wa Wizara ya Afya kwa Watanzania. Kazi inayofanyika na dada yangu Umy na Naibu Waziri ni kazi nzuri sana inapashwa kupongezwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze moja kwa moja kwa kuzungumzia masuala muhimu ambayo nakusudia kuyasema kwa siku hii ya leo. Niendeleo kutoa pongezi. Katika Mwaka wa Fedha 2017/2018 mnamo tarehe 6 Agosti, nilitembelea Wilaya yangu ya Nyasa Mkoa wa Ruvuma. Nilishuhudia

tukiwa tunapokea vifaa mbalimbali ikiwemo vitanda na vifaa vya upasuaji. Naomba sana nipongeze jitihada za Serikali hii kwa kazi nzuri wanayoifanya. Imepelekea kufikia sasa kupata akina mama waliofanyiwa upasuaji kufikia 87.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ni jitihada nzuri ya kuonesha kwamba tunaokoa maisha ya akinamama na watoto. Hata hivyo, liko tatizo kubwa katika hospitali ile, tatizo la *X-ray*. Nimwombe dada yangu Ummy amefanya mambo mazuri sana, naamini *x-ray* ni jambo dogo tu atalikamilisha, atujalie tupate *x-ray* katika hospitali hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumzie suala la vifo vya akinamama wajawazito. Tunapozungumzia vifo vya akinamama wajawazito ziko changamoto nyingi ambazo zinapelekea kupatikana kwa vifo vya akinamama wajawazito. Mojawapo ya mambo ambayo yanayojitokeza ni umbali wa eneo la kujifungulia, vifaa tiba na wauguzi. Nafikiri hivyo ni miongoni mwa vitu ambavyo vinatakiwa viwepo kwenye hospitali zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikizungumzia suala la umbali wa eneo la kujifungulia kama nitakuwa na kumbukumbu nzuri kupitia ahadi za Serikali yetu ya Chama cha Mapinduzi tuliahidi kuwa na zahanati kila kijiji na kuwa na kituo cha afya kila kata. Niombe dada Ummy atakapofika basi atueleze, mimi kama mwakilishi wa akinamama wa Mkoa wa Ruvuma napenda kujua tumefikia hatua gani katika kuhakikisha ahadi hizi zinatekelezwa ipasavyo; na kupitia hivyo vijiji pia nitapata fursa ya kuona ni vijiji gani sasa kwenye Mkoa wangu wa Ruvuma tumefanya vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nije katika suala la wauguzi. Wachangiaji wengi wamesema kwamba tunalo tatizo la lkama ya watumishi. Ziko zahanati ambazo mpaka leo ukienda unaweza ukakuta mhudumu mmoja tu. Nesi afanye kazi ya kuandika huyo huyo, nesi aende akampime mama mjamzito, nesi aende akazalishe mama mjamzito, nesi aende akatoe dawa. Kwa hiyo jambo hili ni muhimu sana niombe

tuangalie sana katika suala hili la Ikama ya watumishi. Kwa bahati nzuri kupitia vitabu hivi wameeleza, kitabu cha Waziri amesema, kupitia zoezi lile la vyeti feki na mambo mengine ambayo yamejitokeza watumishi wengi sasa hawapo kwenye zahanati zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nafahamu kuna usemi unasema ukikata mti panda mti, kwa hiyo tumaini langu kwamba tumewatoa wale watumishi ambao tunafikiri kwamba wa likuwa na makosa kwa namna moja au nyingine, ni wajibu wetu sasa kuona nafasi zile tunazifidia katika kutoa huduma kwa wananchi wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumzie suala la upatikanaji wa dawa. Wamezungumza kupitia kwenye vitabu lakini nishukuru maoni ya Kamati ya Huduma za Maendeleo ya Jamii kupitia ukurasa wa 35, wamesema na wametoa mapendekezo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukija kwenye vitabu hivi unaona kabisa kwamba sasa suala la dawa si tatizo katika nchi yetu, lakini ukienda katika hali halisi yako maeneo mpaka hivi tunavyozungumza yana upungufu mkubwa sana. Wajumbe wa Kamati kupitia maoni ya Kamati wamesema ni vizuri sasa kama Wizara waweke utaratibu wa kuhakiki kuona hizi dawa zinaishia wapi kama kweli zinafika kwa watumiaji. Ni tatizo kubwa sana la upatikanaji wa dawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nalisema hili, Mheshimiwa Waziri Mkuu bahati nzuri alifanya ziara Mkoani kwetu Ruvuma, lakini miongoni mwa mambo ambayo alikumbana nayo ni upatikanaji wa dawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri Mkuu alipokuja kufanya mkutano katika Halmashauri ya Wilaya ya Tunduru ilisikitisha sana pale alipomwomba Daktari aeleze dawa zilizopo. Vile alivyojaribu kumweleza wananchi walimzomea sana. Hii ni kuonesha kwamba hizi dawa tunazozungumza kwenye makabrasha pengine sio zile zinazofika moja kwa moja kwa wananchi. Niombe sasa

Serikali yangu, naamini hii ni Serikali sikivu sana ione hivyo.
(Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hakuna njia nyingine yoyote, sisi uwepo wetu hapa umetegemea na afya zete; kama tusingekuwa na afya njema tusingekuwapo humu ndani leo. Sasa kuwepo na dawa itarahisisha sana kuona matibabu yanapatikana haraka sana. 0525

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie suala lingine la matibabu ya wazee. Naomba niseme; kwamba suala hili la matibabu ya wazee tumelisemea sana lakini mimi naweza nikaona halijasimamiwa ipasavyo. Hawa wazee tunaowazungumzia wanapokwenda kwenye hospitali si tu kuandikiwa dawa ni pamoja na kupata dawa. Kwa hiyo niombe huu mfumo ambao tunakusudia kutoa matibabu kwa wazee uzingatiwe vizuri ili wazee wale wafaidike.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nalisema hili kwa sababu naamini na sisi wote ni wazee watarajiwa. Kwa hiyo tukiweka misingi mizuri leo hata sisi Mwenyezi Mungu akitujalia tukafika huko uzeeni tutanufaika na hii mipango ambayo tumekuwa tukiiweka. Nimwombe sana dada Ummy kwa kazi nzuri anazozifanya anawapigania akinamama lakini anazungumza sana suala la wazee, basi tuhakikishe wazee hawa wanapata huduma ipasavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumzie suala la vituo vya afya. Sisi katika Halmashauri yetu ya Tunduru; naomba sana nimpongeze Mheshimiwa Mkuu wa Wilaya ya Tunduru kupitia wadau mbalimbali wakiwemo Waheshimiwa Wabunge; tumejitahidi pale katika kuhakikisha ujenzi wa kituo cha afya unaendelea. Hata hivyo, tuiombe sasa Serikali kuweka msukumo. Kama mnavyofahamu nguvu za wananchi peke yake zinaweza zisitoshe, kwa hiyo tunaiomba Serikali iangalie katika kuona tunaboresha kile kituo cha afya ili tuendeleo kupata huduma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na kituo hicho cha afya ambacho nimekizungumzia kilichopo Kata ya Nakayaya pia naomba kituo cha afya kilichopo Kata ya Narasi. Pale tuliahidiwa na Mheshimiwa Rais Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, naamini Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete hayupo lakini Serikali ya CCM ndiyo iliyopo madarakani. Tuliahidiwa pale kupata kituo cha afya; na kwa kweli ukiangalia na idadi ya watu waliopo pale tunastahili. Niombe sana katika kutekeleza jambo hili wakati utakapofika tunapoono umuhimu wa kuongeza vituo vya afya basi na kile kituo kipewe kipaumbele. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizingumzie suala la *CHF*; limezunguzwa kwenye vitabu na sisi sote tunalifahamu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumekuwa tukihimiza sana wananchi wetu kujiunga na *CHF*, na bahati nzuri dada Umyy amelizungumza kupitia kitabu chake; kwamba wanakusudia kuwa na *CHF* ya pamoja ambapo mgonjwa itamwazeshwa kutibiwa kutoka kwenye kituo cha afya, atatibiwa hospitali ya wilaya na vile vile atakwenda kutibiwa mkoani. Naomba katika kutekeleza hili tuangalie na changamoto zilizojitokeza. Inawezekana tukawa tunaangalia tulipoanguka lakini tukasahau tumejikwaa wapi, hatimaye tumeanguka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nalisema hili kwa sababu watu wengi wamekuwa wakisita kujiunga na *CHF* kutokana na huduma zinazotolewa. Mtu anajiunga kwenye *CHF* anapopata tatizo akienda kwenye zahanati hakuna dawa, hilo limekuwa tatizo. Sasa kwa kuwa tunakusudia kuwa na *CHF* ya pamoja, basi ni vizuri tukaangalia changamoto ambazo zimejitokeza katika mfumo huu tulipoanza nao ili tuboreshe ili wananchi wetu waweze kupata huduma zinazostahili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili ni jambo jema na wengi kwa kweli walikuwa wakikata tamaa. Kwa mfano sisi katika Halmashauri yetu ya Tunduru ni wakulima wa korosho. Mtu anaweza akatoka Nalasi anakuja Makao Makuu ya Wilaya

kuja kupokea pesa yake, lakini akiwa pale anapata tatizo la ugonjwa, CHF inafanya kazi katika zahanati yake, makao makuu ya wilaya haifanyi kazi. Kwa hiyo tukiweka mfumo mzuri itawasaidia, kwamba wanapopata matatizo hata kwenye hospitali za wilaya wanapata kutibiwa lakini watakwenda pia kutibiwa hospitali ya mkoa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niendeleo kuisitiza suala la upatikanaji wa dawa kama nilivyosema, ni kitu muhimu sana, naomba Mheshimiwa Waziri dada Umy akizingatie sana. Inawezekana pengine taarifa hizi wanazopata kupitia ngazi za mkoa zisiwe sahihi. Tukija kule kwenye maeneo yanayohusika pengine ile hali sivyo ilivyo, kwa hiyo nasisitiza jambo hili...

(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MHE. SIKUDHANI Y. CHIKAMBO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Midimu, jiandae na Mheshimiwa Nassor.

MHE. ESTHER L. MIDIMU: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia. Kwanza kabisa naipongeza Serikali yangu ya Chama cha Mapinduzi kwa kazi nzuri inazozifanya. Sisi Mkoa wa Simiyu katika majimbo yote tumeletewa gari za kubeba wagonjwa, hongera sana Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili nampongeza Mheshimiwa Umy kwa kazi nzuri anazozifanya pamoja na Naibu Waziri, kwa kweli wanafanya kazi nzuri. Waheshimiwa Wabunge juzi juzi tu tumeshuhudia Serikali inakabidhi magodoro, vitanda pamoja na mashuka, hongera sana kwa Serikali kwa kazi nzuri inazozifanya. Pia Serikali yetu inajitahidi sana dawa kwenye hospitali zetu, asilimia 85 mpaka asilimia 90 ya dawa zinapatikana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia naishukuru Serikali yangu kwa kutuletea pesa za ujenzi wa hospitali ya mkoa, naishukuru sana. Serikali imetuletea pesa tumemudu kulipa eneo la hospitali ya mkoa, ni ekari 121, fidia tumelipa zaidi ya milioni mia mbili, ujenzi wa *ground floor* tumelipa zaidi ya milioni mia tano, ujenzi wa kumaliza ghorofa moja tumelipa zaidi ya bilioni moja, jumla kuu ya pesa tulizolipa zaidi ya bilioni mbili tulizotumia kwenye ujenzi. Naishukuru sana Serikali yangu ya Chama cha Mapinduzi, sasa hivi jengo la *OPD* limekamilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana Serikali yangu; naiomba sasa iweze kutujengea wodi za wagonjwa. Wodi ya wazazi, wodi ya watoto na wodi ya akinamama. Hospitali ya mkoa bila wodi itakuwa bado haijakamilika, nashukuru sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hospitali teule ya mkoa haina gari la kubebea wagonjwa kuwapeleka Hospitali ya Rufaa ya Bugando. Tunaiomba Serikali itununulie gari la kubebea wagonjwa ituletee ili tuweze kupeleka wagonjwa katika Hospitali ya Rufaa Bugando na hospitali nyinginezo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia naiomba Serikali ituletee gari la mpango wa damu salama. Akinamama wengi wanapoteza damu kwa ajili ya kujifungua; inaweza ikanusuru akinamama pamoja na watoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hospitali yetu ya mkoa ina upungufu sana wa watumishi, tunaiomba Serikali ituletee watumishi. Watumishi waliopo katika hospitali ya mkoa ni watumishi asilimia 25, asilimia 75 hawapo. Tunaomba watuletee Madaktari Bingwa ili waweze kuhudumia na kukidhi mahitaji ya hospitali yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna jambo moja baya linajitokeza katika nchi yetu, halifai kuigwa katika jamii na linaleta taswira mbaya katika nchi yetu. Jambo hilo ni ubakaji wa watoto wadogo wa miaka miwili. Watoto

wadogo wanabakwa na baba zao, wajomba zao, pamoja na majirani kutokana na imani zao za kishirikina; inaumiza sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna kipindi nilikuwa ziara nilienda wilaya fulani ambayo sitaitaja; kuna mtoto mdogo wa miaka mitatu alikuwa amebakwa akaharibiwa sana na ikabidi wampeleke rufaa Bugando. Naiomba Serikali ikemee hilo kwa nguvu zote ikiwezekana wanaofanya hivyo wanyongwe, hiyo itasaidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni mimba za utotoni; sana sana zinatokea kwa maeneo ya wafugaji; naiomba Serikali iweze kudhibiti tatizo hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishukuru Serikali kwa kuanzisha Benki ya Wanawake, lengo ni kuwakomboa wanawake wote kiuchumi. Naiomba Serikali wakati Waziri anakuja kujibu hapa naomba aniambie benki hiyo ni lini itafika katika Mkoa wa Simiyu? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa ya Mwenyekiti wa Bodi kupitia vyombo vya habari alisema kuna madeni hayalipiki, ni bilioni nane. Naomba Mheshimiwa Waziri akisimama aje atueleze hiyo bilioni nane imekwenda wapi na ni akina nani waliokopa ambao hawarudishi? Naiomba Serikali yangu ijitahidi sasa kukusanya yale madeni ya bilioni nane ili hizo pesa ziwafikie wananchi wa Mkoa wa Simiyu. Akinamama wa Mkoa wa Simiyu nao wana hamu ya kupata zile pesa za Benki ya Maendeleo ya Wanawake halafu na wanawake wa mikoa mingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi, niendeleo kuipongeza Serikali yangu kwa kazi nzuri inazozifanya. Mwenyezi Mungu awabariki sana Mheshimiwa Rais na Waziri Mkuu kwa kazi nzuri wanayoifanya. Pia niwapongeze Mawaziri wote kwa ujumla wanajitahidi, wametembelea mikoa yetu pamoja na wilaya zetu wanafanya kazi nzuri, hongera sana, nawatia moyo, wachape kazi, wasonge mbele. Ahsanteni sana.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Hussein Nassor.

MHE. HUSSEIN N. AMAR: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ili nami niweze kuchangia. Kwanza napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu ambaye amenipa afya njema na kuweza kusimama Bungeni hapa leo na kuweza kuchangia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nianze kumpongeza Mheshimiwa Waziri Ummu na Naibu Waziri pamoja na watendaji wote wa Wizara kwa hotuba yao nzuri ambayo wameiwasilisha leo. Napenda pia nimpongeze Mheshimiwa Waziri kwa kutupatia gari la wagonjwa katika Kituo chetu cha Afya Nyang’hwale. Mwaka 2017 tulipata gari moja na nashukuru mwaka huu tumepata gari lingine, hongera sana kwa Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wilaya ya Nyang’hwale kituo cha Afya na Hospitali ya Wilaya ya Nyang’hwale, ama Wilaya ya Nyang’hwale kwa ujumla tuna upungufu mwingi katika vituo vyetu vya afya na hospitali. Upungufu wenyewe ni kama ufuatao:-

Tuna upungufu wa dawa, Wauguzi, Madaktari na vifaa tiba. Vifaa tiba kama vile *X-ray* na *Ultra Sound*. Upungufu huu unasababisha wananchi wetu kupata usumbufu mkubwa kufuata huduma hizi Mkoani Geita. Kwa hiyo tunamwomba Mheshimiwa Waziri ajaribu kuangalia upungufu huu ili kuwapunguzia adha wananchi wetu kufuata matibabu Mkoani Geita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bima ya afya. Watu wengi wamekuwa hawaoni faida ya bima ya afya sababu ni ipi. Sisi Wabunge tunajitahidi sana kuwahimiza wananchi wajiunge na bima ya afya, lakini wanashindwa kujiunga kwenye bima ya afya kwa sababu kwa wananchi ambao wameshajiunga na bima ya afya hawaoni faida yake. Vipi hawaoni faida yake? Ni kwamba wanapokwenda hospitali wanapata huduma, lakini huduma ya dawa wanakuwa hawaipati wanaambiwa waende wakanunue dawa

hakuna dawa. Kwa hiyo hii inawafanya wananchi wakate tamaa kubwa ya kujiunga na huduma hii ya bima ya afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rais wa Awamu ya Nne alifika katika jimbo letu na akaahidi Kituo cha Afya cha Kalumwa kiwe hospitali ya wilaya, lakini mpaka leo hii hatuoni mpango wowote wa Wizara kutupa hati ya kuipandisha hadhi kukipandisha hadhi kuwa Hospitali ya Wilaya ya Nyang'hwale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba sasa hospitali hii ipandishwe hadhi ili tuweze kupata dawa kulingana na wilaya; kwa sababu hospitali hiyo inahudumia vijiji zaidi ya 110, lakini pia wilaya za jirani zinakuja kupata huduma katika hospitali hiyo. Kwa hiyo kituo hicho kitakapopandishwa na kuwa hospitali ya wilaya naamini kabisa bajeti yake itakuwa ni kubwa na inaweza ikakidhi angalau kidogo kupunguza makali ya mahitaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba wizara ijaribu kuangalia. Tuna wodi moja pale ambayo ilijengwa mwaka 1958. Wodi ile inalaza wagonjwa 10 tu na leo hii hospitali ile inapokea wagonjwa wengi sana. Kwa hiyo tunaomba sasa tuweze kujengewa wodi ambayo ni ya kisasa na inaweza kubeba wagonjwa walio wengi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza Wizara kwa mikakati yake ya kupambana na ugonjwa wa saratani ya shingo ya uzazi. Ukweli ni kwamba naipongeza Serikali kwa kuanza kutoa chanjo kwa ajili ya kukinga tatizo hilo. Pia naomba sasa Wizara ishuke kule chini iende kutoa elimu ili kuondoa ile imani potofu waliyonayo wananchi wetu, kwamba tutakapochomwa sindano hiyo huwezi ukapata tena mimba, wengi wanaelewa hivyo, kwa hiyo naomba elimu hiyo iende ikatolewe kule chini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia Waswahili wanasema kinga ni bora kuliko kutibu. Kwa nini nasema hivyo; Wizara imeshagundua tatizo la chanzo cha ugonjwa wa saratani ya shingo ya uzazi. Jana nilisikia kwenye majibu ya

Mheshimiwa Waziri hapa alisema kwamba chanzo chake ni kwamba inatokana na kuambukizwa na wanaume ambao hawajakata govi zao. Kwa hiyo naiomba sasa Wizara iende ikatole elimu kwa walio na govi hizo ili waweze angalau zitolewe kuwakinga hawa. Kwa lugha nyingine wanaume ambao hawajafanyiwa tohara. Kwa hiyo naomba itolewe elimu kule ili kuweza kuwakinga hawa akinamama na maambukizi haya ambayo yanatoka kwa akinababa ambao hawajafanya tohara. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. Ahsante sana.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Flatei dakika tanona Mheshimiwa Sanga dakika tano.

MHE. FLATEI G. MASSAY: Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru sana kwa kunipa nafasi. Kwanza nianze kwa kweli kumpongeza sana Mheshimiwa Rais na Serikali yake kwa kufanya kazi kwa Awamu hii ya Tano, lakini pia nimpongeze sana Mheshimiwa Umyy Mwalimu pamoja na Naibu Waziri wake na Wizara kwa ujumla kwa kufanya kazi nzuri ambayo kwa kweli mimi nai-*admire*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nimshukuru sana Mheshimiwa Waziri amefika kwenye jimbo langu na kutembelea Hospitali ya Haydom na kwenda pia kwenye Kituo cha Afya cha Dongobesh na kutupatia fedha za kujenga kituo kile. Nakushukuru sana Mheshimiwa Umyy na kwa kweli kwa Serikali nzima pia naishukuru.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nishukuru ametuma tume ambayo imekwenda kwenye Hospitali ya Haydom na kuangalia Hospitali ya Haydom kama inakidhi kupandishwa hadhi kuwa hospitali ya kanda. Sasa niombe Mheshimiwa Umyy waone basi namna gani ya kuisaidia Hospitali ya Haydom ili iweze kupanda hadhi iwe hospitali ya kanda. Kwa nini nasema namna hii, Haydom ni hospitali inayohudumia Mikoa mitano, ikiwemo Singida, Dodoma, Manyara bila kusahau Arusha na Mara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa hospitali hii imeshakuwa katika eneo ambalo linafikika na pande zote hizi nilizozitaja ningeomba Serikali iangalie namna nzuri ya kuisaidia hospitali hii ili kupanda hadhi. Kwa mfano leo unaangalia Dar es Salaam kufikika kutokana na mafuriko imekuwa na shida; kwa hiyo angalia tungekuwa tumepandisha hospitali ya Haydom kuwa hospitali ya kanda tungekuwa tumepeleka huduma vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Serikali yetu inapenda kusaidia watu wa vijijini, basi tusaidieni kuifanya hospitali hii iwe hospitali ya kanda ili iweze kutoa huduma nzuri kuliko kwenda kwenye hospitali kubwa ya *KCMC*. Kutoka Haydom mpaka *KCMC* kuna kilometa 400, kutoka Haydom mpaka kule tunasema Jakaya Kikwete kilometa 700.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo niombe sana, kwa sababu tumeshaleta mapendekezo na ameshaikagua na Wizara yake tunahitaji Madaktari Bingwa sasa waliobobea waende vijijini ili wakawasaidie mama na mtoto kule vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na haya niombe sasa; maana unaposhukuru maana yake unaomba mara ya pili na hata kwenye Sala ya Baba Yetu ukiangalia sana kwa sisi Wakristo, sala nzima ya Baba Yetu inasema Baba yetu uliye mbinguni jina lako litukuzwe, yote haya ni kumsifu. Unapomsifu Baba yako aliye mbinguni maana yake baadaye unaweka ombi. Kwa sababu unaposema utuongeze mkate wetu wa kila siku maana yake unahitaji kuomba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo huwezi kuwa na *double standard*, ukawa unaomba wakati huo huo unatukana. Kwa hiyo niombe Serikali yangu ambayo inasikia, kwa kweli ahadi alizotoa Mheshimiwa Ummy ya gari ya wagonjwa pale Dongobesh mpaka leo inasubiriwa. Vile vile kubwa nishukuru pia kwa kutupatia hospitali ya wilaya ambayo itajengwa kwenye jimbo langu na nimeona kabisa kwenye bajeti hii ametutengea bilioni moja. Kwa hiyo nimshukuru sana yeye pamoja na Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kubwa ni kwamba ninao ushauri kwenye Serikali. Nimepata nafasi ya kutembelea katika kiwanda kile ambacho kinatengeneza dawa ya viuadudu. Mimi niombe, kama kweli Serikali inahitaji kumaliza Malaria au kupunguza Malaria tuweze kuhakikisha ya kwamba kile kiwanda kinakwenda kufanya kazi ya ku-*supply* ile dawa ili kuweza kuua vimelea vya mbu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu nimekwenda pale na hakika Mheshimiwa Rais alishaweza kuziagiza halmashauri zote nchini kuweza kununua zile dawa waka-*spray* kwenye maeneo yao ili kutokomeza vimelea vya mbu. Kwa msingi huo basi, siamini kama tuna dhamira ya dhati kumaliza tatizo hili la malaria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukitaka kumaliza malaria, niwashauri Wizara watafute namna, washauri hata hospitali zetu, kituo cha afya. Kwa mfano wakiviagiza au kuviomba hivi vituo vya afya, kwamba kila kituo cha afya kikanunua lita tano ya ile dawa, wakaagiza pia *dispensary* ikanunua kama lita tatu...

(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MHE. FLATEI G. MASSAY: ...ukaagiza maduka ya dawa yote nchini yakanunua ni rahisi kabisa kutokomeza malaria; lakini vinginevyo...

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Sanga.

MHE. DEO K. SANGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi niweze kuchangia. Kwanza niungane na wenzangu kuipongeza Serikali inayoongozwa na Dkt. John Pombe Joseph Magufuli pamoja na Mawaziri wote pamoja na Waziri mwenye dhamana ya Wizara ya Afya na watendaji wake wote, Makatibu Wakuu na kadhalika. Kazi ambayo inafanywa na Serikali hii hakuna mfano, ni kazi nzuri sana ukienda kwenye idara na wizara mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nichangie hii moja tu ya afya. Katika halmashauri yangu ya Mji wa Makambako tumepewa fedha shilingi bilioni moja milioni mia tano kwa ajili ya kujenga hospitali yetu ya Mji wa Makambako. Tumepewa shilingi milioni mia saba kwa ajili ya kuboresha kituo chetu cha afya katika Kata ya Lyamkena.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ombi langu kwa Serikali, naomba sana katika hospitali au kituo kilichopo Makambako pale; pale ni *centre*. Dawa tunazopata hazikidhi, tunahitaji tuongezewe dawa ili ziweze kuhudumia watu wetu; na ndiyo maana na mimi nimeunga mkono jitihada za Serikali zinazofanywa na nimejenga vyumba viwili vya Madaktari pale vitafunguliwa mwishoni mwa mwezi huu, vyumba viwili vya kutolea huduma vya Madaktari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna watu wanazungumza; Mheshimiwa Ali Hassan Mwinyi amewahi kusema kwamba Rais Dkt. John Pombe Joseph Magufuli kwa kazi kubwa aliyofanya kwa miaka miwili katika sekta mbalimbali ni sawa na miaka 10, hakuna mfano. Sasa kwa kazi hizo ambazo anazifanya; ukienda kule China Rais wa China amepewa kuwa ni Rais wa maisha kutokana na kazi anazofanya, kwa nini Magufuli asiwe Rais wa maisha kutokana na kazi anazofanya? (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa miaka miwili tu kazi ambayo amezifanya ni nzuri na kubwa. Kwa kweli lazima tumuombe kwa Mwenyezi Mungu aendelee kuishi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wako watu hapa kazi yao ni kubeza. Nilikuwa namsikia mtu mmoja akisema hizi hela ambazo zimewekwa hapa kwenye bajeti kama hazitaenda hizo hela basi nipeni mimi. Wako watu hapa wanabeza, jamani hii ni bajeti, ni mwelekeo wa bajeti, lazima tuishukuru Serikali kwa kazi inazofanya. Mnasema kama hizi hela zimewekwa tu, kama haziwezi kwenda; amesema mwenzangu mmoja kule kwa hata unapoamka unasema Mungu wangu tunakuomba na kadhalika; lakini yako mambo unamshukuru na kumwomba.

(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)

MHE. DEO K. SANGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hebu tamka unanijua? *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishukuru sana Serikali kwa kweli kwa kazi nzuri ambazo zinafanyika... *(Kicheko)*

MHE. CECILIA D. PARESO: Ongea taratibu.

MHE. DEO K. SANGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho nimalizie, pamoja na dakika chache hizi niombe sana Serikali; tumejenga zahanati 10, tumeshaezeka, tumepiga lipu, tuko hatua za mwisho. Tuiombe Serikali mtutengee fedha kwa ajili ya kumalizia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho, mimi pamoja na Wabunge wenzangu wa Mkoa wa Njombe, tunaipongeza Serikali kwa kutujengea Hospitali ya Mkoa wa Njombe. Jengo la *OPD* limeisha, ombi langu kuwa fedha zilizotengwa hapa tuone namna ya kumalizia hospitali ile ili ianze kufanya kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana na Mungu akubariki sana. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Waheshimiwa orodha iliyokuwa mezani kwangu ya Wabunge wote imekwisha, nawapongeza, lakini tunaendelea kumpongeza Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Mabingwa Hospitali ya Muhimbili na timu yao wote pamoja na Wauguzi, kazi nzuri mnaifanya na tunaiona.

Sasa naahirisha shughuli za Bunge mpaka kesho saa tatu asubuhi.

(Saa 1.45 Usiku Bunge liliahirishwa mpaka Siku ya Ijumaa Tarehe 20 Aprili, 2018, Saa 3.00 Asubuhi)